WILLIAM BRANHAM

Nabii
Azuru Afrika Kusini

kimeandikwa na

JULIUS STADSKLEV

Dibaji

Kuandikwa kwa kitabu hiki kuna kusudi lenye sehemu tatu. Kwanza, Daudi anatwambia katika Zaburi 105 kwamba tunapaswa "kuwajulisha watu matendo yake." Mungu alifanya matendo mengi makubwa mno na ya ajabu Afrika Kusini kupitia huduma ya Kikosi cha Branham. Jamani, laiti ningalipata maneno ya kuelezea yale Yeye aliyotenda kule Afrika Kusini miezi hiyo mitatu ya mwisho ya 1951. Lakini uwezo wa kibinadamu, hata katika upeo wake, usingeweza kabisa kuonyesha ishara na maajabu aliyoyafanya Mungu miongoni mwetu. Mwandishi mmoja, alipokuwa akitoa taarifa ya baadhi ya mikutano, alisema, "Mtu angetaka apate maneno ya kimbinguni kuelezea huduma ya kimbinguni ya Bwana miongoni mwa watu."

Ninapowaandikia kuhusu yale niliyoona Mungu akitenda Afrika Kusini, ninajisikia kama vile yule mwandishi hapana budi alijisikia hapo alipojaribu kuelezea upendo wa Mungu naye angeweza tu kusema,

> "Hata tungaliweza kujaza bahari kwa wino,
> Na mbingu ziwe zimetengenezwa kwa
> karatasi ya ngozi;
> Kama kila kikonyo duniani kingalikuwa ni
> kalamu ya unyoya,
> Na kila mtu awe kazi yake ni mwandishi;
> Kuandika upendo wa Mungu aliyeko juu
> Kungeikausha bahari;
> Wala hilo gombo lisingeweza kuenea hayo
> yote,
> Hata likitandazwa kutoka mbingu hata
> mbingu."

Daudi alikwisha kumwona Mungu akitenda kazi miongoni mwa watu Wake na wakati alipokuwa akitafakari jambo hili kila tamshi lake lililofuata lilikuwa "kwa maana fadhili zake ni za milele." (Zaburi 136). Hili "milele" lilihusisha siku zetu na wakati wetu. Naam, rehema Zake zinadumu milele. Zinadumu kwa ajili ya mfanyabiashara anayeongoza katika jiji linalostawi la Afrika Kusini. Zinadumu kwa ajili ya mwananchi duni kabisa katika himaya iliyobaguliwa ya Kiafrika.

Mara ya kwanza ambapo sauti ya kimbinguni ilinena na Ndugu Branham ilitokea kwenye upepo wa kisulisuli. Hivi ndivyo jinsi ile ile Bwana alivyonena na Ayubu, yule mzee wa kale wa zile nyakati za mwanzoni, kulingana na mlango wa thelathini na nane. Kuna kufanana kwingi sana kusiko kwa

kawaida kati ya maisha na huduma ya William Branham na ile ya manabii wa Agano la kale hivi kwamba hapawezi kuwapo na tashwishi yoyote kwenye moyo wa mtu yeyote mwaminifu ya kwamba yeye ni nabii wa Mungu kama tu vile Eliya, Elisha, Isaya, Yeremia na wengine wa hao ambao wametambulikana kama manabii wa Mungu.

Tukijua basi ya kwamba kwa kweli Mungu alifanya matendo ya ajabu sana Afrika Kusini, akithibitisha tena ya kwamba rehema zake zinadumu milele na akitenda kazi kupitia nabii katika siku zetu—haya yameandikwa—"kuwajulisha watu matendo yake."

Kikosi cha Branham kilipokuwa njiani kikielekea Klerksdorp kutoka Johannesburg kilisafiri katika magari mawili tofauti. Tulipofika mahali fulani tulisimama kufurahia uzuri wa mandhari isiyo ya kawaida. Nilipokuwa nikitoka kwenye gari Kasisi A. J. Schoeman, Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa, alinijia na kusema ya kwamba Ndugu Branham alitaka kuzungumza na mimi. Baada ya kubadilishana mawazo machache na watu mbalimbali hapo, Ndugu Branham alitugeukia mimi na Ndugu Bosworth. Akatwambia ya kwamba malaika wa Bwana alikuwa amemwambia ya kwamba inabidi taarifa iandikwe kuhusu mikutano ya Afrika Kusini na kwamba lilikuwa ni jukumu langu mimi kufanya jambo hili. Kwa hiyo, jambo la pili, taarifa hii inaandikwa kulingana na matakwa ya malaika wa Bwana.

Kusudi la tatu ambalo kwalo kitabu hiki kinaandikwa ni kwamba Mungu aweze kunena nawe kupitia kitabu hiki. Utakapokuwa ukisoma baadhi ya mambo muhimu sana ya maisha ya mwanzoni ya William Branham na karama inayotenda kazi kupitia kwake, naomba nawe pia utambue ya kwamba yeye ni nabii wa Mungu. Kwa hiyo, ujumbe anaouleta hautoki kwa mwanadamu bali unatoka kwa Mungu. "Akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote." (Zaburi 103:3).

Unaposoma ibada ya kawaida ilivyo naomba uweke kweli hizo moyoni mwako wewe mwenyewe na udai mambo ambayo kwa ajili ya hayo Mungu amelipia gharama iliyo kuu sana, mauti ya Mwanawe wa pekee.

Shuhuda hizi na ziwe mfano ulio hai na uvuvio kwako ili umwamini Mungu. Sheria za Mungu kwa dunia nzima huifanya imani katika Yeye kuwa nguvu zilizo kuu kuliko zote katika ulimwengu mzima.

Si suala la kuhudhuria ibada za Ndugu Branham, si suala la kupata kadi ya maombi kunakomwezesha mtu kuingia kwenye mstari wa maombi, si kuombewa na mtu yeyote kunakoleta uponyaji kwa nafsi yako ama uponyaji kwa mwili wako. Ni kumkubali Kristo tu na kazi yake iliyomalizika

pale Kalvari, kukubali ahadi Zake na kuzishikilia kwa imani isiyoyumbayumba. Ukiisha kufanya jambo hili—

> "Amini tu, amini tu,
> Yote yawezekana,
> Amini tu."

Yesu akamwambia, "Mimi sikukuambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?" (Yohana 11:40.)

Yaliyomo

UKURASA

Dibaji. iii

Sura ya 1

William Branham Ni Nani? 1

Sura ya 2

Karama Za Uponyaji Na Zaidi. 39

Sura ya 3

Ni Kwa Sababu Gani William Branham
Alizuru Afrika Kusini? 50

Sura ya 4

Mfano Wa Ibada Ya Kawaida 54

Sura ya 5

Taarifa Za Kutoka Afrika Kusini 73

Sura ya 6

Shuhuda 157





Kasisi William Branham Na Mkewe

William Branham Ni Nani?

William Branham alizaliwa kwenye shamba moja karibu na Berksville, Kentuky, si mbali na mahali ambapo Abraham Lincoln alizaliwa takriban miaka mia moja kabla yake. Hakuna mtu aliye na hakika ya tarehe hasa kwa kuwa kumbukumbu za kuzaliwa hazikuwa zikitunzwa huko Kentuky katika siku hizo. Hata hivyo, inaaminiwa alizaliwa tarehe sita Aprili 1909 na alikuwa na uzito wa ratili 5 tu. Mama yake alikuwa na umri wa miaka 15 na baba yake alikuwa na 18.

Siku ya kwanza ya maisha yake kitu cha ajabu sana kilitukia. Baada ya mkunga kumwosha na kumweka karibu na mama yake alienda dirishani kufungua kilango cha dirisha.

Hakukuwako na vioo kwenye madirisha ya nyumba ya Branham katika siku hizo na hewa na nuru vilirekebishwa kwa kufungua na kufunga vilango vya mbao. Mapambazuko yalikuwa tu yakianza makondeni, yakitupa miali midogo ya nuru kwenye hicho chumba. Pamoja na nuru hii kulikuja duara ndogo ya nuru yenye kipenyo cha kama futi moja ambayo iliwaka kwa mwangaza mkali juu ya kitanda ambamo mama na mtoto walilala.

Duara hii tangu wakati huo imeonekana na maelfu ya watu na hapana shaka ndiyo ile ile inayoonekana kwenye picha iliyopigwa huko Houston, Texas, kwenye uamsho wa Januari 1950. Taarifa ya picha hii pamoja na nakala ya fotostati ya matamshi yaliyotolewa na George Lacy, Mmarekani mchunguzi wa hati zinazoshukiwa, vitaonekana mwishoni mwa sura hii. Wakati huyo mkunga pamoja na wazazi wake walipoona duara hii walianza kulia; waliogopa wala hawakujua maana ya mambo hayo yote. Ni baada ya miaka mingi ambapo wale waliojua kuhusu duara hii walipofahamu ya kwamba Mungu alikuwa ameweka mkono Wake juu ya mtu huyu kwa ajili ya huduma kuu kwa watu wa duniani.

Dini katika hali yoyote haikuchukuliwa kuwa kitu cha maana katika familia ya Branham. Babu yake alikuwa ni Mkatoliki lakini baba na mama yake inaonekana hawakuwa na wazo lo lote kwa suala la Ukristo. Bali kwa sababu ya tukio hilo lisilo la kawaida lililotukia alipozaliwa, mama yake alimpeleka kwenye Kanisa la Kibaptisti lililoko jirani. Hii ilikuwa ndiyo mara yake ya kwanza kwenda kanisani na ya mwisho kwa kipindi cha miaka mingi.

Mwanzoni mwa msimu wa majani kupukutika wa 1909 Kentucky ilipatwa na moja ya dhoruba mbaya sana ya theluji. Wakati huu baba yake William Branham alikuwa

ameondoka kwenda kufanya kazi mbali kwenye kambi ya mbao ambako alikuwa amekwama kwa sababu ya tufani hii mbaya sana. Mara akiba ya chakula na kuni na makaa hapo nyumbani kwao vikaanza kwisha. Mama yake angetoka nje na kuleta chochote alichoweza kupata cha kuchoma kusudi amkinge mwanawe na yeye mwenyewe wasije wakafa kwa baridi. Hawakuwa kamwe na akiba ya kutosha ya chakula na wakati hicho kidogo kilipokwisha, aliweza kusikia kwamba nguvu zake zilikuwa zikimwishia. Ilibidi msaada uwafikie haraka endapo wangeishi. Hatimaye akawa mdhaifu sana hivi kwamba akaona kwamba kama akitoka nje akatafute kuni zingine huenda asingeweza kurudi.

Akamchukua mtoto na kumviringisha vizuri alivyoweza na akamlaza kitandani, akingojea kifo kije na kuwachukua wote wawili. Wangekufa kama isingekuwa mzee mmoja jirani yao mcha Mungu aliyehusika kiajabu kuhusu nyumba ya Branham. Alipochunguza, aliona hakukuwa na moshi uliotoka kwenye bomba la kutolea moshi. Ingawa theluji ilikuwa na kina kirefu, huyo mzee alienda zake kwenye kibanda hicho duni cha mbao kilichoezekwa kwa mbao na akakuta ya kwamba mlango ulikuwa umefungwa kwa ndani. Akatambua ya kwamba hapana budi kuna mtu ndani na akiwa haoni dalili yoyote ya joto ndani ya kile kibanda, akavunja mlango akaingia.

Alishtushwa sana na kile alichoona wakati alipoingia. Huyo mama alikuwa yuko karibu ya kufa kwa sababu ya baridi na kukosa chakula. Akaomba kwamba Mungu atayahifadhi maisha yao na asiruhusu mama huyu kijana na mtoto kuaga dunia namna hii. Haraka akakusanya kuni na kukaa pale mpaka akawa na moto mkali wa kutosha ambao mara ulipasha joto nyumba hiyo ndogo ya vyumba viwili. Halafu, akampatia huyo mama na mtoto chakula na mara walianza kupata nguvu.

Si muda mrefu baadaye, familia ya Branham ilihamia Utica, Indiana, na mwaka uliofuata wakahamia kwenye shamba moja maili tano nje ya Jeffersonville, Indiana, maili mbili kutoka mahali anapoishi sasa. Maisha yake ya mwanzoni yaliambatana na majanga, umaskini na kutoeleweka.

Baadhi ya kumbukumbu dhahiri sana za ujana wa William Branham zinahusu umaskini ambao walilazimishwa kuuishi. Baba yake alifanya kazi kwa mkulima mmoja tajiri kwa senti sabini na tano kwa siku. Anakumbuka akimwona akirudi nyumbani huku shati lake limegandamana na mgongo wake ulioungua kwa jua hivi kwamba ilimbidi mama yake kuchukua makasi na kulikata libanduke. Makazi yao duni yalikuwa ni kibanda kidogo cha vyumba viwili visivyosakafiwa na sinki la jikoni lililokuwa huko nje uani chini ya mtofaa.

Mara ya kwanza ambapo Mungu alinena kwa sauti ya kusikika na William Branham ilikuwa ni wakati alipokuwa

na umri wa kama miaka saba. Alikuwa ndiyo kwanza ajiandikishe kwenye shule ya kijijini maili chache kaskazini mwa Jeffersonville, Indiana. Alirudi nyumbani kutoka shuleni alasiri hiyo naye alikuwa anakusudia kujiunga na wavulana wengine kwenda kuvua samaki. Lakini wakati kijana Branham alipokuwa anakaribia kuondoka, baba yake alimwita na akamwambia kwamba itambidi kubeba maji kwa ajili ya mtambo wake wa kutengenezea gongo. Jambo hili kwa kweli lilikuwa ni jambo la kusikitisha kwake kwa kuwa kama mvulana alikuwa anapenda sana kuwinda na kuvua samaki. Bali aliona ya kwamba kwa kuwa baba yake alimwambia abebe maji, ingembidi kufanya kama alivyoambiwa.

Alipokuwa anabeba hayo maji, alisimama apumzike chini ya mti wa mpopula wa zamani sana kati ya nyumba na kibanda. Mara, akasikia sauti ya upepo ukivuma katika majani. Akaangalia pande zote na kutambua kwamba ilikuwa ni siku tulivu, yenye jua na joto. Aliposikiliza kwa makini zaidi, aliona ya kwamba kwenye sehemu fulani, kama ukubwa wa pipa, upepo ulionekana kama unavuma ukipitia kwenye miti. Mara hiyo tu sauti ikatokea kwenye hiyo miti ikisema, "Usinywe pombe kamwe, usivute sigara wala kuuchafua mwili wako kwa njia yoyote, kwa kuwa nina kazi kwa ajili yako utakayofanya utakapokuwa mtu mzima."

Jambo hili lilimshtusha naye akakimbilia nyumbani. Huku akilia, alijitupa kwenye mikono ya mama yake ambaye alifikiri ya kwamba alikuwa ameumwa na nyoka. Akamwambia mama yake kwamba alikuwa tu ameogopa wala hakumwambia juu ya kuvuma kwa ule upepo katika yale majani wala kuhusu ile sauti. Mamaye alimlaza kitandani akidhani alikuwa anaugua ugonjwa wa mshtuko wa neva. Kila ilipowezekana angeepuka kuukaribia mti huo, akiamua afadhali kuzunguka upande wa pili wa shamba.

Majuma mawili baadaye alipokuwa akicheza kingoni mwa Mto Ohio, aliona ono. Aliona kitu kilichoonekana kwake kuwa kama daraja lililotokea upande wa Kentucky wa huo mto, likielekea Indiana. Daraja hilo lilipokuwa linaendelea kuelekea Indiana, aliona watu kumi na sita wakianguka kutoka kwenye daraja hilo wakitumbukia majini. Alikwenda nyumbani na kumwambia mamaye jambo hili bali mama yake alisema ya kwamba alikuwa yuko usingizini akaota ndoto. Bali kijana William Branham alijua ya kwamba hakuwa amelala wala akiota. Hata hivyo hakuelewa na aliyokuwa ameona.

Miaka ishirini na miwili baadaye Daraja la Manispaa lilijengwa kati ya Louisville, Kentuky, na Jeffersonville, Indiana, kwenye mahali papo hapo hasa. Wakati wa kujengwa kwa daraja hilo, watu kumi na sita walipoteza maisha yao.

Mungu alikuwa akinena na kijana mwanamume huyo na akiwa anauweka msingi kwa ajili yake kusudi apate imani katika mambo ambayo Mungu angemwonyesha katika miaka ya usoni.

Alikuwa akihisi kuhusu jambo halisi ya kwamba kulikuwako na mtu fulani karibu naye ambaye daima alionekana anataka kuzungumza, bali yeye, akiisha kuwa ameonywa na mama yake juu ya mizimu na nguvu za pepo, aliogopa na daima alijaribu kupuuza jambo hilo.

Kuongezea mateso na huzuni juu ya umaskini, baba yake akawa mlevi. William anakumbuka jinsi ambavyo mwaka wote mzima alienda shuleni wala hakuwa na shati kabisa ambalo angeweza kuvaa. Anakumbuka jinsi alivyokaa shuleni na kuwaangalia watoto wengine waliokuwa na nguo na akaanza kutambua ya kwamba pombe ilikuwa imeinyang'anya familia yake mahitaji muhimu ya maisha.

Alisoma habari za Abraham Lincoln, ambaye akiwa kijana mwanamume alivyoshuka kutoka kwenye chombo cha mashua huko New Orleans na kuona wazungu wakimpiga mnada Mnegro mmoja mkubwa sana, wakimtenganisha na familia yake. Mkewe na mtoto wake walikuwa pale wakilia, wakati mtu huyo alipokuwa akiuzwa kana kwamba alikuwa ni farasi. Lincoln alitambua ya kwamba jambo hili lilikuwa ni baya na akaapa ya kwamba siku moja atafanya jambo fulani kuhusu jambo hilo hata likimgharimu maisha yake mwenyewe.

Vivyo hivyo kijana William Branham aliketi kule shuleni na akawazia juu ya umaskini ambao familia yake ilikuwa ikiuishi kwa sababu ya pombe. Alisema ya kwamba jambo hili lilikuwa ni baya naye atafanya jambo fulani kuhusu jambo hilo siku moja, hata likimgharimu maisha yake. Hajasahau kiapo chake, kwa kuwa mpaka leo hii yeye anafanya na ataendelea kufanya kila kitu awezacho ili kuwapa nuru watu juu ya madhara ya pombe na tumbaku.

William Branham anasimulia kuhusu wakati ambapo mwalimu wake, Bibi Temple, alipomwuliza kwa nini hakuvua koti lake alipokuwa darasani. Hakuweza kumwambia ya kwamba hakuwa na shati, kwa hiyo alimwambia kwamba alikuwa anasikia baridi. Mwalimu akasema, "Sawa basi, nenda pale uketi karibu na moto." Hapana budi ilibidi afanye vile mwalimu alivyomwambia, kwa hiyo akaenda hapo na akaketi karibu na jiko. Hapo akapata joto zaidi kuliko alivyowahi, na ingawa jasho lilikuwa linatiririka mgongoni mwake, bado asingeweza kuvua koti lake. Mwalimu asingeweza kuelewa na jambo hilo na akamwuliza iwapo hakuwa bado amepata joto, ndipo

akajibu, “Hapana, Mama.” Hatimaye mwalimu akasadiki ya kwamba alikuwa anashikwa na homa ya mafua, kwa hiyo akampa ruhusa aende nyumbani.

Ingawa hakujali kwenda nyumbani akiacha masomo shuleni, asingeweza kujizuia ila kulia. Kusudi afiche ukweli kwamba hakuwa na shati kama watoto wengine, alikuwa amemwambia uongo mwalimu wake kwa kumwambia alikuwa anasikia baridi. Hatimaye alipata shati. Shati lililotengenezwa kutoka kwenye gauni chakavu ambalo mmoja wa binamu zake alikuwa ameliacha nyumbani mwake. Alilikata sehemu yake ya sketi bali ingali haikufanana sana na shati. Hao watoto wengine walimcheka, wakisema alikuwa amevaa nguo ya msichana. Tena akadanganya akisema, “La, sijavaa nguo ya msichana. Hiyo ni suti yangu ya Kihindi.” Bali hawakumwamini na ndipo akaenda nyumbani akilia.

Lloyd, mwanafunzi mwenza wa darasa lake, aliuza Gazeti la Mtangulizi. Katika kuuza gazeti hili alijiunga na walichoita Maskauti Wapweke, naye akajipatia sare ya shirika hilo. Ilikuwa ni wakati wa Vita vya kwanza vya Dunia na sare zilikuwa zinapendwa sana. Kijana William Branham hapana budi aliipenda suti hiyo ya skauti kwa kuwa daima alitaka kuwa kama mwanajeshi. Kweli, hakuwa na shati, sembuse suti ya skauti. Kwa hiyo akamwomba rafiki yake, “Lloyd, utakapoichakaza hiyo, je, utanipa?” Akasema, “Hakika, nitakupa, Bill.”

Alingojea na kungojea, lakini ingawa mvulana huyo sikuzote alikuwa akiivaa suti hiyo, haikuonekana kamwe kuchakaa. Hatimaye akaona ya kwamba Lloyd hakuwa anavaa suti hiyo tena kwa hiyo akamwomba ampe. Kufikia wakati huu rafiki yake alikuwa amesahau ya kwamba alikuwa ameahidi kumpa suti hiyo na mama yake alikuwa ameikatakata kuitumia kutia viraka. Kitu tu ambacho angeweza kupata kilichobakia kwenye suti hiyo ya skauti kilikuwa ni soksi moja ndefu na basi kijana Branham akamwomba ampe hiyo.

Aliichukua akaenda nayo nyumbani akaivaa. Ilimfanya aone fahari kwa kuwa hiki ndicho kipande pekee cha nguo alichokuwa nacho kilichofanana angaa na zile za mwanajeshi. Akawazia moyoni ya kwamba hakika sasa alikuwa ni mwanajeshi wa kweli kwa maana alikuwa amevaa soksi moja ndefu. Alitaka kuivaa akienda shuleni bali hakujua jinsi gani angeweza kuivaa bila ya kuchekwa tena na watoto. Kwa hiyo akaamua kujitungia hadithi ya kwamba alikuwa amejeruhi mguu wake na alikuwa anatumia hiyo soksi kama bendeji. Hata hivyo, alipofika shuleni watoto wasingemwamini. Mara nyingine tena wakamtania; mara nyingine tena akaenda nyumbani akilia.

Jumamosi ilikuwa ndiyo siku muhimu sana nyumbani kwa Branham. Ilikuwa ndiyo siku wangemfungia Kootsie, yule nyumbu mzee, kwenye mkokoteni wa kubebea mbao na Bw. na Bibi Branham na watoto wote wa Branham wangepanda kwenye mkokoteni na waende zao mjini. Huko wangenunua vyakula vyao vya juma zima na mwenye duka sikuzote aliwapa watoto hao watano pakiti ya peremende kali.

Ilibidi baba yake kila mara awe mwangalifu kuwagawia peremende hizi kwa kila mmoja sawasawa kabisa, kuepuka shida, kwa maana macho kumi yenye njaa yalimwangalia kwa makini sana. William Branham, kifungua mimba kati ya hawa wana, alikuwa na tabia ya kutokula peremende zake zote Jumamosi bali aliweka baadhi yake mpaka juma lililofuata wakati ambapo angeweza kufanya mapatano na baadhi ya hao watoto wengine. Kwa kubadilishana na kuwapa wazirambe peremende zake mara chache aweze kuwafanya wamsaidie kazi za kuchosha za hapo nyumbani.

Baba yake William Branham alikuwa mwuza pombe haramu na alipika gongo hapo shambani. Jumapili moja asubuhi akiwa na umri wa miaka kumi William Branham alikuwa yuko pamoja na baba yake na jirani yake mmoja karibu na Mto Ohio. Walipokuwa wakitembea kuambaa kando ya mto, baba yake alitoa chupa kutoka kwenye mfuko wake wa nyuma na, baada ya kunywa, akampitishia jirani yake. Huyo jirani akanywa kisha akampitishia kijana William Branham ambaye alisema, “La, bwana, asante, sinywi pombe.” Huyo jirani akajibu kwa mshangao, “Ati u familia ya Branham na ni Mwairishi na hunywi pombe?” “Hapana, bwana!” bado alisisitiza. Baba yake akajibu kwa kusema, “Nina wavulana wanne na dondoandume moja,” huyo dondoandume akiwa ni William ambaye ndiyo tu alikuwa amekataa kunywa pombe.

Jambo hili liliuumiza sana moyo wake mwororo, kwa kuwa alikuwa mwangalifu sana na alipenda kufanya yale yaliyokuwa mema. Hapa baba yake mwenyewe alikuwa amemwita mwanamama wakati alipokataa kushiriki kunywa pombe, ambayo ilikuwa hasa ndicho chanzo kikubwa cha huzuni na umaskini mwingi nyumbani mwao. Jambo hili lilikuwa limezidi mno yale kijana Branham angaliweza kuvumilia na ndipo akasema, “Nipeni hiyo chupa nami nitawaonyesha ya kwamba mimi ni ukoo wa Branham na kwamba ninaweza kunywa pombe.”

Akaichukua ile chupa na akaanza kuiweka mdomoni mwake. Alipofanya hivyo, mara nyingine tena ile sauti aliyoijua ya upepo ikaja. Alikumbushwa wakati ule yule malaika aliponena naye kwa mara ya kwanza akimwambia asivute sigara hata kidogo, asinywe pombe, wala kuuchafua mwili wake kwa njia yoyote kwa kuwa alikuwa na kazi ya

kufanya atakapokuwa mtu mzima. Hakuwa akiwazia juu ya jambo hili na wakati alipoisikia, aliogopa, akaangusha ile chupa na akaanza kulia. Baba yake akasema, "Unaona, nilikwambia yuko kama mwanamke."

Huenda alikuwa ni kama mwanamke machoni pa ulimwengu bali Mungu alikuwa akinena na mvulana huyo. Mungu alikuwa akimlinda kwa ajili ya jambo fulani kubwa katika wakati ujao, jambo ambalo kwa hilo si kwamba tu atakuwa wa manufaa kwa jirani zake na kwa watu waliomfahamu bali msaada na baraka kwa mamilioni ya watu kote ulimwenguni. Tukio hili ni jaribu la kuvunja moyo kuliko yote na chungu sana katika maisha ya ujana wake.

Akiona ya kwamba watu hawakuwa wakimwelewa na akiwa anateseka na hali ya kujiona duni, hakuwa na marafiki wengi. Alikuwa na haya sana na wasichana na hakuwapenda. Ilionekana kana kwamba wavulana hawakumwelewa. Badala ya kushirikiana na watu, aliona ni afadhali kabisa achukue bunduki yake na mbwa wake na aende akawinde. Kwa mfano, vijana wa ujirani walikuwa wameamua kumfanyia karamu ya kushtukiza ya siku ya kuzaliwa kwake lakini akagundua jambo hilo. Mapema kipindi cha jioni kabla mtu yeyote hajakuja, alimchukua mbwa wake akaenda kuwinda rakuni wala hakurudi mpaka kama saa nne. Alifikiri karamu hiyo ingekuwa imeisha wakati huo na kila mtu amerudi nyumbani. Badala yake alikuta kwamba kila mtu alikuwa angali yupo hapo akicheza michezo na ilionekana wanajifurahisha. Alipoangalia dirishani na akawaona, aliamua ya kwamba hakutaka kuingia. Asingejisikia raha na amani; asingejifurahisha pale pamoja na watu hao. Kwa hiyo akaamua kwenda kwenye kibanda cha shambani na kulala huko usiku huo.

Alipokuwa na umri wa miaka kumi na minne alikuwa ametoka kwenda kuwinda ndipo akapata ajali ambayo ilimfanya alazwe hospitalini kwa miezi saba. Wakati huu ile sauti ilimrudia mara nyingi, bali aliiogopa kwa maana mama yake alikuwa amemwonya juu ya mizimu na pepo wachafu. Kwa kuwa alikuwa anaiogopa sauti hii sikuzote alikataa kusikiliza na akakataa kujibu. Lakini Mungu alimshughulikia katika miezi hiyo wakati akiwa hospitalini, hata ingawa wakati huu wote alikataa na kupuuza kumsikiliza Mungu.

Hao vijana wanaume wengine wangeshirikiana na wasichana na kwa kweli walifurahia hilo bali William Branham alionekana tu asingeweza kujifurahisha na yeyote wao. Hatimaye, wakati alipokuwa na umri wa karibu miaka kumi na nane, alishawishiwa kufanya miadi na mmoja wa hao

wasichana. Walipokuwa wametoka wakiwa kwenye matembezi ya gari, walisimama kwenye mkahawa mdogo kwenye viunga vya mji. Aliingia akanunue Koka-kola na sambusa.

Alipotoka alimkuta msichana huyu anavuta sigara, msichana ambaye alifikiri alikuwa ni msichana mzuri sana na mmoja ambaye angefurahia sana kuambatana pamoja naye. Kwake jambo hili lilikuwa ni la kushangaza sana. Asingeweza kuwazia kwa mwanamke kufanya jambo baya zaidi kuliko kuvuta sigara. Na basi alipoingia kwenye gari, huyo msichana akasema, "Utapenda kuvuta sigara, Billy?" Akasema, "La, Mama. Mimi sivuti sigara." Aliposikia hayo huyo msichana akajibu, "Ati huvuti sigara? Ulitwambia ya kwamba hunywi pombe, huchezi dansi na sasa unasema huvuti sigara. Ni kitu gani unachopenda kufanya?" "Vema," akasema, "ninafurahia kuwinda; ninafurahia kuvua samaki; ninafurahia kuwako tu huko nje msituni." Huyo msichana alimcheka na kumdhihaki. Mara hao wavulana wengine wakaungana na hao wasichana katika kuyadhalilisha mambo aliyoyapenda ndipo akakumbushwa tena kuhusu ukweli kwamba yeye hakuwa kama watu wengine. Hatimaye huyo msichana akasema, "Vema, sifurahii kufanya uchumba na dondoandume." Hili lilikuwa ni zaidi ya ambavyo angaliweza kuvumilia kwa maana jambo hili ndilo lile baba yake alilokuwa amemwita ile siku kule kando ya mto, wakati alipokuwa amekataa kunywa pombe ya gongo. Kwa hiyo akawaambia hao vijana, "Hakuna mtu atakayeniita mwanamama, nipeni hiyo sigara; nitaivuta."

Akaichukua ile sigara na alikuwa anakaribia kuiweka mdomoni mwake ndipo akasikia ile sauti aliyoijua kama upepo uvumao katika majani. Ndipo tena sauti hiyo ikamjia ikisema, "Usinywe pombe kamwe, usivute sigara wala kuuchafua mwili wako kwa njia yoyote, kwa kuwa nina kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima." Aliposikia haya akaogopa na asingeweza kabisa kuiweka hiyo sigara mdomoni mwake. Akijua ya kwamba kila mtu atamcheka endapo hakuvuta sigara, alivunjika moyo akalia. Akatoka kwenye gari na kuanza kukimbia barabarani akielekea nyumbani kwao. Wakaanza kumfuata kwa gari, wakimwashia taa, na kumcheka na kumdhihaki. Walipoendelea kumfuata, aliacha barabara na akaanza kuvuka shamba akielekea nyumbani kwao. Alikimbia umbali alioweza na kwa muda alioweza.

Hatimaye, akiwa amechoka, alilazimika kuketi chini. Hapa alilia kwa kuugua sana, na akatamani kwamba angekufa kwa maana hakuwa kama watu wengine. Watu hawakumwelewa wala hakuweza kujifurahisha pamoja nao. Alipokuwa ameketi pale juu ya mwamba akilia, alihisi uwepo wa mtu fulani karibu naye. Kwanza aliogopa sana hata asingeweza kugeuka na kuangalia. Hatimaye alipogeuka, hakuweza kumwona mtu

yeyote ingawa alihisi kwa hakika mtu fulani alikuwa yupo pale kwenye vichaka, karibu futi hamsini kutoka kwenye huo mwamba. Hakufahamu ilikuwa ni kitu gani wakati huo. Kwa hiyo basi hakuwa akitaka tu kwamba angekufa bali pia aliogopa. Mara nyingine tena akakimbia kuvuka shamba hilo, akilia na kukimbia alivyoweza.

Kama kijana mwanamume daima alikuwa akiwazia sana juu ya kwenda sehemu za magharibi. Daima alifurahia nchi ilivyo wazi yenye upeo mpana na huko ndiko kulivyo, huko nje makondeni akiishi kwenye maumbile asilia, ambapo aliishi muda wake wa furaha sana. Kwa hiyo, alipokuwa na umri wa miaka kumi na tisa aliamua ya kwamba atatoka aende huko magharibi ambako labda angeweza kupata kazi kwenye ranchi. Asubuhi moja ya Septemba alimwambia mama yake ya kwamba alikuwa anakwenda kwenye safari ya kupiga kambi huko Tunnell Mill, mahali ambapo ni kama maili 14 kutoka Jeffersonville, ambako alikwenda mara nyingi. Alimwambia jambo hili, akijua ya kwamba endapo angemwambia alikuwa anaenda magharibi, angemsihi na kumshawishi asiende.

Hakumwandikia mpaka alipokuwa Arizona na akiwa amepata kazi karibu na Phoenix. Kwa kweli alitambua ya kwamba alikuwa akimtoroka Mungu, bali hakutaka kukubali jambo hilo. Alifurahia maisha ya ranchi bali kama vile zilivyo furaha zingine kwake, shani hiyo mara ikaisha na alikuwa anatamani kwamba angalikuwa amerudi nyumbani.

Hakuwa amekaa sana huko magharibi ndipo alipopata barua kutoka kwa mama yake ikimjulisha ya kwamba ndugu yake Edward alikuwa ni mgonjwa sana. Hakulichukulia uzito sana kwa kuwa hadi kufikia wakati huu hakujatokea vifo vyovyote kwenye familia ya Branham naye aliona kwamba atapata nafuu tena karibuni. Hata hivyo, siku chache baadaye aliporudi kwenye ranchi kutoka mjini, alipewa ujumbe mfupi ulioandikwa, "Bill, njoo kwenye malisho ya kaskazini. Ni muhimu sana." Mara akaenda kwenye malisho hayo na mtu wa kwanza aliyekutana naye alikuwa ni mzee mwangalizi wa ranchi ambaye walimwita Pop. Pop alikuwa na uso wa huzuni alipokuwa akimwambia William Branham ya kwamba alikuwa ana habari za huzuni kwa ajili yake. Wakati huo huo mnyapara alikuja na akamwambia wakati huo huo ndio tu walikuwa wamepokea habari za kuhuzunisha ya kwamba ndugu yake Edward alikwishaaga dunia. Habari hii ilimfikia kama mshtuko wa kutisha sana hapo alipoanza kutambua kwamba hataweza tena kumwona ndugu yake akiwa hai.

Alipokuwa amesimama hapo, matukio yalipita mawazoni mwake. Alikuwa ameshindana na Mungu; alijua hilo. Hata hivyo Mungu alikuwa akizungumza naye hata kwa kupitia kwenye kifo cha ndugu yake. Wazo la kwanza lililomjia

William Branham mawazoni lilikuwa kwamba kama ndugu yake alikuwa yuko tayari kufa au hakuwa tayari. Alipogeuka na kuangalia hizo mbuga pana za majani, machozi yalimtiririka. Akakumbuka jinsi walivyokuwa wamefanya kazi pamoja kama watoto wadogo na jinsi maisha yalivyokuwa makatili na magumu kwao. Alikumbuka jinsi walivyokwenda shule bila chakula cha kutosha kwenye vyombo vyao vya chakula cha mchana, bila nguo za kutosha kufunika migongo yao, na huku vidole vimetokeza kwenye viatu vyao. Ilibidi wavae makoti yaliyochakaa yaliyofungwa kwa pini shingoni mwao kwa kuwa hawakuwa na mashati. Alikumbuka ya kwamba siku moja mama yake alikuwa amewapa bisi kwenye vyombo vyao vya chakula cha mchana na akataka kuhakikisha ya kwamba alipata sehemu yake, alikuwa ametoka nje na kuchota konzi ya bisi kabla ya saa ya chakula cha mchana.

Alipokuwa amesimama hapo akitazama kuelekea mashariki, ng'ambo ya hizo mbuga pana za nyasi, mara nyingine tena akashangaa. Je! ndugu yake alikuwa yuko tayari kufa? Vipi kama ingalikuwa ni yeye aliyekuwa amekufa, je! angekuwa yuko tayari? Na mara nyingine tena ilimbidi kukubali nafsini mwake ya kwamba hakuwa tayari wala hakutaka kukutana na Mungu wake.

Mara ya kwanza ambapo William Branham anakumbuka kusikia maombi ilikuwa ni wakati wa mazishi ya ndugu yake. Kasisi McKinney wa Kanisa la Port Fulton alikuwa akiongoza ibada ya mazishi. Wakati wa ibada hiyo alisema, "Huenda ikawa kuna wengine hapa wasiomjua Mungu. Kama ndivyo ilivyo, mbona usimkubali sasa?" Hili lilimgusa sana William Branham, ambaye alikuwa amerudi kwa ajili ya mazishi. Alitambua ya kwamba hakumjua Mungu.

Baada ya mazishi hakurudi magharibi bali alipata kazi katika Kampuni ya Shirika la Umma la Indiana. Baada ya kufanya kazi pamoja nao kwa muda wa miaka miwili, akicheki mita kwenye duka la mita za gesi mahali gesi za makaa zinapotengenezwa huko New Albany, aliathiriwa na gesi. Hiki kilikuwa ndicho chanzo cha ugonjwa wake uliomlazimisha kumkubali na kumsikiliza Mungu. Alikwenda kwa madaktari wote alioweza lakini hakuna hata mmoja aliyeweza kumtibu. Hatimaye alipelekwa kwa daktari bingwa mmoja huko Louisville, Kentuky, ambako aliambiwa ya kwamba itabidi kidole tumbo chake kitolewe. Kwa kuwa hakuwa na dalili za kidole tumbo, hakuweza kulielewa jambo hili, bali hata hivyo walisema ya kwamba ilibidi afanyiwe upasuaji apate kupona.

Aliamua mwishowe ya kwamba kama ilikuwa ni lazima kwake kufanyiwa upasuaji, labda basi alikuwa ni mgonjwa

kuliko alivyotambua. Hivyo basi alitaka awe pamoja na mtu aliyemjua Mungu. Kwa hiyo alimwita Mchungaji wa Kanisa la Awali la Kibaptisti aliyekaa pamoja naye hapo alipoingia kwenye chumba cha upasuaji. Kabla tu hawajaanza kumfanyia upasuaji, alijisikia ya kwamba alikuwa anakuwa mnyonge haraka sana. Hofu iliingia moyoni mwake ya kwamba kamwe hatazinduka aamke kwenye upasuaji huu bali kwamba ataitwa akakutane na Mungu wake, naye alitambua ya kwamba hakuwa tayari. Kwa mara ya kwanza maishani mwake alimwita Mungu amsaidie.

Mara baada ya huo upasuaji alipata ono lingine ambalo lilikuwa ndilo mahali pa kugeuka maishani mwake. Alijiona ametumbukia kwenye msitu mkubwa. Sauti ya upepo na ya kuchakarisha kwa majani ilikuwa inakaribia zaidi na zaidi. Akawazia moyoni kwamba ilikuwa ni mauti, ikija kumchukua. Loo, jinsi alivyomlilia Mungu kwa kuwa hakuwa tayari kukutana na Muumba wake. Huo upepo ulikuwa unakaribia zaidi na kuvuma kwa sauti kubwa zaidi. Ndipo ilionekana tena kana kwamba alikuwa amerudi kwenye siku za uvulana wake, akiwa amesimama pale kwenye kijia chini ya ule mti wa mpopula ambapo aliisikia ile sauti kwa mara ya kwanza ikimzungumzia alipokuwa na umri wa miaka saba. Mara nyingine tena ile sauti ikanena, "Usinywe pombe, usivute sigara wala kuuchafua mwili wako kwa njia yoyote... Nilikuita nawe usingeenda." Maneno haya yalirudiwa mara tatu. Ndipo Bw. Branham akasema kwa sauti kuu, "Bwana, kama huyo ni Wewe, naomba uniache nirudi duniani tena nami nitaihubiri Injili yako hadharani na kwenye pembe za barabara. Nitamwambia kila mtu habari zake."

Ono lilikuwa limekwisha. Alijisikia mwenye nguvu zaidi na akatambua ya kwamba mauti hayakuwa karibu bali kwamba angepona. Daktari hakuwa ameondoka hospitalini kwa sababu alikuwa akitaka kuchunguza maendeleo ya mgonjwa wake. Wakati alipomwona William Branham alisema, "Mimi si mtu anayeenda kanisani; kazi yangu ni kubwa sana sina nafasi. Bali ninajua ya kwamba Mungu amemtembelea mvulana huyu." Ni dhahiri kwamba huyo daktari alikuwa ameona ya kwamba William Branham asingeishi katika kufanyiwa upasuaji huo, bali si kwamba tu aliishi katika upasuaji huo bali alionekana mwenye nguvu zaidi na mzima akiendelea kupata nafuu. Si daktari wala William Branham walilielewa jambo hilo. Nina imani, hata hivyo, ya kwamba laiti wakati huo angejua anayojua sasa, asingekuwa amechanganyikiwa bali angaliweza kwa urahisi sana kuwaelezea daktari na wahusika wengine jambo hilo.

Baada ya siku chache alipewa ruksa akatoka hospitali na akarudi nyumbani. Ndipo akaanza kumtafuta Mungu.

Kufikia wakati huu hakuwa amepata mafundisho yo yote ya dini; hakujua jinsi ya kumpata Mungu, hakuwa amelihesabu Neno kwamba ni muhimu. Alikwenda toka kanisa hadi kanisa, akijaribu kupata mahali fulani ambapo Wakristo wangemsaidia na kumfundisha jinsi ya kuwasiliana na Mungu.

Usiku mmoja hapo nyumbani alimwonea njaa sana Mungu alihofu asingeweza kuishi isipokuwa ampate. Kwa kuwa hakutaka kumsumbua mtu yeyote hapo nyumbani, alitoka akaenda akaingia ndani ya banda moja la zamani la mbao nyuma ya nyumba na hapo akajaribu kuomba. Hakujua jinsi ya kuomba bali aliinua moyo wake kwa Mungu na kulia sana alivyoweza. Mara ikatokea nuru katika umbo la msalaba na sauti ikasema naye katika lugha asiyoielewa. Halafu ikatoweka. Aliogopa na kushangaa wakati aliposema, "Bwana, kama huyu ni Wewe, tafadhali rudi na uzungumze na mimi tena." Hiyo nuru ikaingia tena kwenye hicho kibanda. Alipokuwa akiomba ilijitokeza tena kwa mara ya tatu. Sasa akatambua ya kwamba alikuwa amekutana na Mungu. Alikuwa na furaha; akashukuru.

Akainua moyo wake kwa Mungu katika kutoa shukrani huku akiruka na akakimbia kuingia ndani ya nyumba kana kwamba alikuwa anakimbia hewani. Mama yake akasema, "Bill, umepatwa na kitu gani?" Akajibu, "Sijui, lakini kusema kweli ninaona raha." Badala ya kukaa nyumbani ambamo mlikuwa na watu, alitoka nje ambako angeweza kukaa peke yake pamoja na Rafiki yake mpya aliyempata.

Ikawa amefahamiana na Kasisi Ray Davis, Mchungaji wa Kanisa la Kibaptisti la Kimishenari, ambaye alikuwa ni baraka kubwa kwa Ndugu Branham katika maisha yake ya Kikristo ya mwanzoni. Moja ya mambo ya kwanza aliyotambua yalikuwa ni kwamba Mungu alimtaka kwenye huduma na kwa hiyo ingembidi kumponya. Akaenda kwenye kanisa linaloamini katika kutia mafuta na baada ya maombi aliponywa mara moja. Akitambua ya kwamba wale wanafunzi walikuwa na jambo fulani ambalo wahudumu wa kisasa hawakuwa nalo, alimwomba Mungu ampe kile wanafunzi wa mwanzoni walichokuwa nacho. Wanafunzi walibatizwa kwa Roho Mtakatifu, wakaponya wagonjwa, na wakafanya miujiza mikubwa katika Jina la Yesu. Akaanza kuomba apate ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yapata miezi sita baadaye wakati alipopata ubatizo huo, Mungu alinena naye akimwambia ahubiri Neno na kuwaombea wagonjwa.

Baada ya William Branham kumgeukia Mungu na kuitikia wito wa Mungu, kila kitu kilionekana kikimwendea vizuri sana. Alikuwa na furaha; alifurahia ushirika wa watu. Kwa mara ya kwanza maishani mwake alijisikia ya kwamba hakuwa mtu anayetia aibu, hakuwa mtu aliyetupwa na jamii

ya watu; na ya kwamba labda Mungu aliweza kuichukua hali hii ya kibinadamu isiyo na tumaini na kuifanya kitu fulani cha thamani.

Katika kipindi cha miezi sita baada ya kuongoka kwake, mipango ilikuwa ikifanywa kwa ajili ya ibada yake ya kwanza. Alianza mikutano ya hema katika mji wake mwenyewe wa Jeffersonville. Ilikadiriwa ya kwamba kadiri ya watu elfu tatu walihudhuria mkutano mmoja na watu wengi waliongoka. Hili lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida hata kwa mhudumu mashuhuri, na hapa huu ulikuwa ndio mkutano wake wa kwanza wa uamsho.

Kwenye ibada ya ubatizo iliyofuata mkutano huo wa uamsho, zaidi ya watu mia moja na thelathini walibatizwa katika maji. Ilikuwa ni kwenye wakati huu ambapo nuru ya mbinguni ilitokea juu yake alipokuwa akibatiza mtu wa kumi na saba. Nuru hii ilishuhudiwa na kusanyiko kubwa lililosimama kingoni mwa Mto Ohio na gazeti likaandika makala juu yake.

Watu waliokuwa wameokolewa katika mkutano wa hema wa Jeffersonville waliamua kujenga maskani, ambayo sasa inajulikana kama Maskani ya Branham.

Miaka michache iliyofuata ilikuwa yenye matokeo mazuri, katika wakati ambapo baraka za Mungu zilikuwa juu yake. Alipokea maono ya mambo ambayo yatakuja kutukia. Hakuweza kuyafahamu wakati huo bali yalipoanza kutimia, aliweza kuona ya kwamba Mungu alikuwa amempa picha sahihi.

Katika miaka ya mwanzoni ya huduma yake alikutana na Hope Brumback, msichana ambaye baadaye alimwoa. Baada ya miezi kama mitano ya uchumba, William Branham aliamua ya kwamba itambidi kumwomba kama alitaka kuolewa naye. Hata hivyo, alikuwa ni msichana mzuri na kama kamwe hatamwoa, asingepaswa kuwa akimpotezea wakati. Nitawasimulia hadithi ya haya zake, barua ya posa, ndoa yake na matukio mengine yaliyofuata ndoa yao ya furaha, kama ilivyosimuliwa na Ndugu Branham katika mtindo wake rahisi, lakini wa kuvutia.

Nilikuwa tu kijana mwanamume wa kijijini na mwenye soni sana. Mtu akiwazia jinsi nilivyokuwa mwenye soni sana, labda watu mtashangaa jinsi nilivyopata kuoa.

Nilikutana na msichana mzuri Mkristo. Niliona alikuwa ni mzuri sana. Nilimpenda msichana huyu na nilitaka kumwoa, bali sikuwa na ujasiri wa kutosha kumwambia. Alikuwa msichana mzuri mno kwa mimi kumpotezea muda wake—ingelifaa ampate mtu mwingine; kwa hiyo nilijua ilibidi nimwombe mapema. Nilipata senti ishirini kwa saa na babaye alipata dola mia tano kwa mwezi. Kila usiku nilipomwona

ningeamua ya kwamba usiku huo ningemwambia. Ndipo donge kubwa mno lingepanda kooni mwangu na nisingeweza kabisa kumwambia. Sikujua la kufanya. Unajua nilifanya nini hatimaye? Nilimwandikia barua.

Vema, barua hiyo ilikuwa na mapenzi zaidi ndani yake kuliko "Dada mpenzi." Nilijitahidi nilivyoweza kuandika barua nzuri, ingawa nina hakika ilikuwa dhaifu. Kwa hiyo asubuhi nikajiandaa kuitumbukiza kwenye sanduku la barua. Ndipo wazo likanijia juu ya yale ambayo yangetukia kama mama yake angeipata. Bado nilihofu kumpa kwa mkono. Hatimaye nikapata ujasiri wa kutosha kuitumbukiza kwenye sanduku la barua Jumatatu asubuhi. Jumatano usiku nilipaswa kukutana naye na kumpeleka kanisani. Juma zima mpaka Jumatano nilikuwa na wasiwasi sana. Jumatano usiku nilienda kumwona. Nilipokuwa nikienda niliwazia juu ya kile kingetukia kama mama yake angetoka nje na kusema, "William Branham!" Nilijua ningepatana vizuri na baba yake, bali sikuwa na hakika sana na mama yake.

Hatimaye nilienda hadi mlangoni na kumwita. Alitoka nje na kusema, "Aa, halo Billy, ingia." Nikasema, "Kama hujali nitaketi tu barazani." Nilihakikisha hawataniingiza ndani. Akasema, "Sawa, nitakuwa tayari mnamo dakika chache tu."

Ingawa nilikuwa na Ford ya zamani ya Mtindo wa "T", alisema, "Kanisani sio mbali; hebu na tutembee kwa miguu tu." Hili lilinishtusha sana na nilikuwa na hakika jambo fulani lilikuwa limetukia. Tulikwenda mpaka kanisani lakini hakusema jambo lolote. Nilikuwa na wasiwasi sana usiku huo sikusikia yale mhubiri aliyosema hata kidogo. Unajua mwanamke anaweza kukuweka katika hangaiko.

Baada ya kutoka kanisani, tulianza kutembea barabarani. Ulikuwa ni usiku wa mbalamwezi. Bado hakusema lolote. Hatimaye nikaamua kwamba hakuwa ameipata ile barua. Hili lilinifanya kujisikia vizuri zaidi. Nilifikiri ya kwamba labda barua ilikuwa imewekwa kwenye sanduku lingine la barua na mtu wa posta na punde si punde nilirudi kwenye hali yangu ya kawaida. Tukaendelea kutembea. Nikamtazama wakati tulipotoka nyuma ya miti. Macho yake meusi yalimetameta wakati miali ya mwezi ilipomwangazia. Nikawazia, Loo, jamani! Alionekana kama malaika.

Hatimaye akasema, "Billy?"

Nikasema, "Ndiyo."

Akasema, "Nilipata barua yako."

Loo, jamani! nikawazia, loo, loo. Yamenifika. Sasa, Bill, utakiona. Mambo yamekwisha sasa. Nikawaza alikuwa amengojea mpaka baada ya kutoka kanisani. Hakusema neno lingine. Ndipo nikasema, "Uliipata?"

Akasema, "Abee."

Nikawazia, endelea, fanya haraka. Nisingeweza kulivumilia jambo hilo. Mnajua jinsi wanawake walivyo; watakuweka kwenye wasiwasi. Tulikuwa tumetembea karibu urefu wa jengo la mji naye hakuwa amesema neno. Hatimaye nikasema, "Je! uliisoma?"

Akasema, "Abee."

Whiu! nikasema, "Ulifikiria nini juu yake? Je! ilikuwa ni sawa?"

Akasema, "Abee."

Nilitamani aseme jambo fulani. Ndipo nikasema, "Je! ulipenda mambo yaliyoandikwa humo ndani?"

Akasema, "Abee."

Nikasema, "Je! uliisoma yote?"

Akasema, "Abee."

Vema, tukafunga ndoa. Hatimaye tulifanikiwa. Kabla hatujafanya hivyo, hata hivyo, tuliamua ya kwamba itatubidi kuwaambia wazazi wake. Nilijua ningeelewana na baba yake vizuri sana, kwa hivyo nikakubali kumwambia. Yeye alikuwa aombe ruhusa kwa mama yake. Nilidumu kuliahirisha jambo hilo kwa muda mrefu nilivyoweza, kwa maana lilinifanya niwe na wasiwasi mara nilipowazia tu jambo hilo. Hatimaye, jioni moja nilikuwa nimewaaga usiku mwema na nilikuwa karibu na kuondoka wakati Hope aliponiashiria na kunielekezea kidole chake kwa baba yake. Loo, jamani! Nilijua hilo lilichomaanisha. Wakati ulikuwa umewadia; nisingeweza kuliahirisha tena. Kwa hiyo nikamwomba babaye kama ningeliweza kuzungumza naye hapo nje barazani kwa dakika moja. Akasema, "Hakika, Bill."

Tulipotoka kwenda hapo barazani nilisema, "Ni jioni njema, sivyo, Charlie?

Akasema, "Ni kweli, Bill."

Ndipo nikasema, "Vema—ee—ee,—."

Akasema, "Naam, Bill, unaweza kumchukua."

Nikasema, "Asante, Charlie." Loo jamani! Aliniondolea fadhaa nyingi sana. Ndipo nikasema, "Sasa angalia, Charlie, siwezi kumpa maisha mazuri kama unavyompa." Alikuwa mmoja wa viongozi kwenye Udugu wa Reli ya Pennsylvania. Loo, jamani; alipata fedha nyingi, nami huyo hapo nikipata senti ishirini kwa saa kwa sululu na beleshi. "Ila ninajua jambo hili moja," nikaendelea, "Sijaona kabisa mtu yeyote duniani ninayempenda kama yeye. Ninampenda kwa moyo wangu wote. Nitakuahidi jambo hili, Charlie, nitafanya kazi kadiri

niwezavyo kufanya kazi na nitafanya kila kitu niwezacho kufanya kuwa mwaminifu na mwema kwake. Nitafanya yote niwezayo kumpa maisha mema."

Akasema, "Naona bora wewe umchukue kuliko mtu yeyote nimjuaye kwa maana hilo ndilo jambo muhimu, Bill. Si fedha; ni jinsi mlivyo na furaha."

Nina furaha sana alijisikia hivyo juu ya jambo hilo. Furaha hailetwi na kiasi gani cha mali ya dunia uliyo nayo, bali ni vile mtu unavyoridhika na kiasi ulichopangiwa. Hiyo ni kweli. Kama una kingi au kama una kidogo, mshukuru tu Mungu kwa ajili ya hicho.

Tulifunga ndoa nami siamini ya kwamba kulikuwako na mahali popote duniani palipokuwa na furaha zaidi kuliko ilivyokuwa kwenye makazi yetu madogo. Ninakumbuka vitu tulivyokuwa navyo tulipoanza maisha kwenye vyumba viwili. Nilinunua jiko chakavu toka kwenye duka la vikorokoro kwa dola moja na nusu kisha nikatumia senti sabini na tano kutia jitometali ndani yake. Bibi mmoja alitupa kitanda cha kukunja cha zamani. Nikashuka kwenda kwa Sears na Roebucks na kununua moja ya zile seti za kiamshakinywa ambazo inakubidi uzipake rangi wewe mwenyewe.

Haikuwa na vitu vingi, lakini wapendwa wangu, palikuwa ni nyumbani; na ni afadhali niishi kwenye kibanda na nipendwe na Mungu kuliko niishi katika nyumba ambayo ni nzuri sana iliyopo bila kibali Chake. Hatukuwa na mali nyingi za ulimwengu huu. Ninakumbuka siku moja nilimwambia mke wangu ya kwamba itanibidi kuliomba kanisa linipe matoleo ili tuweze kulipia madeni yetu. Kabla ya wakati huu sijawahi kuchukua matoleo kamwe katika kanisa langu. Jumapili hiyo jioni nikamwomba mmoja wa wazee achukue kofia yake na achukue sadaka. Lakini baada ya kutangaza yale niliyokuwa nitafanya, nilimwona maskini mama mmoja mzee akifungua pochi yake na kuchukua sehemu ya fedha zake za pensheni. Loo, jamani! Sikuwa na ujasiri wa kuchukua pesa zake. Kwa hiyo nikasimama na kuwaambia nilikuwa nikiwatania tu na nikijiuliza kama wangeweza kufanya jambo hilo. Baadaye mfuasi mmoja wa kanisa alinipa baiskeli nzee ambayo niliipaka rangi na kuiuza.

Baada ya miaka miwili mvulana mdogo akaja nyumbani mwetu. Alipozaliwa jambo hilo lilitufunga tu pamoja vizuri zaidi. Wakati mara ya kwanza nilipomsikia akilia hospitalini kitu fulani kiliniambia ya kwamba alikuwa ni mvulana. Nikasema, "Bwana, huyo hapo mvulana wako. Nitamwita Billy kwa ajili ya baba yake na Paulo kutoka katika Biblia. Jina lake litakuwa ni Billy Paul."

Daktari akatoka na kusema, "Mvulana wako yuko hapo ndani."

Nikasema, "Naam. Jina lake ni Billy Paul."

Kwa hiyo basi tulikuwa na furaha. Ninakumbuka tulifanya kazi pamoja. Yeye angefanya kazi katika kiwanda cha mashati akijaribu kutusaidia kupata riziki. Ningehubiri kila usiku. Siku nzima ningefanya kazi kwenye mitaro. Mara nyingine wakati nilipokuja nyumbani usiku mikono yangu yenye sugu ingekufa ganzi kwa baridi, na mara nyingi inatoka damu. Hope angeketi na kufunga jeraha za mikono yangu usiku kabla sijaenda kanisani. Ndipo akasema alitaka nichukue likizo. Alikuwa ameweka akiba kama dola kumi na mbili, naye alitaka nifanye safari fupi ya kwenda kuvua samaki. Kwa hiyo nikasema, "Vema. Lakini je! hutaki kwenda kuvua samaki, na wewe pia?"

Akasema, "La. Afadhali niwepo hapa kwa ajili ya Shule ya Biblia ya Msimu wa Kiangazi."

Kwa hiyo nikaenda mpaka Ziwa Pawpaw huko Michigan, juu kidogo tu ya Indiana, pamoja na rafiki mhudumu wa siku nyingi. Fedha zangu hazikudumu muda mrefu sana na ilinibidi kurudi. Katika safari yangu ya kurudi nilipokuwa nikivuka Mto Mishawaka niliona watu wengi sana wakikusanyika kwa ajili ya mkutano. Nikishangaa ni mkutano wa aina gani, niliamua kusimama. Hapo ndipo nilipofahamiana na Wapentekoste.

Watu hao walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya mkutano. Walikuwa wakiimba "Ninajua ilikuwa ni damu, ninajua ilikuwa ni damu." Muda si muda askofu mmoja alisimama na akaanza kuhubiri juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nikaamua ya kwamba nitakaa mpaka kesho yake. Sikuwa na fedha za kuchukua chumba cha hoteli, kwa hiyo nilitoka nikaenda nje mashambani na kuegesha gari kwenye shamba la mahindi ambako nililala usiku huo. Kesho yake asubuhi niliamka mapema na nikarudi kanisani. Nilikuwa nimenunua chapati chache na maziwa kusudi fedha zangu zisiishe upesi. Niliporudi kanisani, kiasi kikubwa cha watu kilikuwa tayari kimekusanyika kwa ajili ya maombi ya asubuhi.

Usiku huo kulikuwako na wahubiri wengi sana wakiwa wameketi jukwaani. Kiongozi wao akasema, "Hatuna wakati wa kuwasikiliza ninyi nyote mkihubiri kwa hiyo tutaomba kila mmoja wenu kusimama tu na utwambie jina lako." Kwa hiyo waliponifikia nilisimama nikasema, "Kasisi William Branham," na kuketi chini.

Alasiri iliyafuata walikuwa na mzee mweusi aliyesimama akahubiri. Alikuwa kidogo mkongwe na nilishangaa kidogo kuwaona wakimchagua jamaa kama huyo kuhubiri mbele ya kusanyiko hilo kubwa. Alihubiri kutoka katika Ayubu 7. "Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya dunia, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja?" Vema, huyo mzee alichukua kama

miaka millioni kumi kabla hata ulimwengu haujaumbwa. Alikuwa karibu amenena juu ya kila kitu mbinguni, akashuka chini kwenye upinde wa mvua na akahubiri juu ya kila kitu duniani mpaka kufikia kuja kwa Kristo Mara ya Pili.

Usiku huo nilienda kwenye lile shamba la mahindi tena nikalala. Asubuhi, kwa kuwa nilidhani hakuna mtu anayenitambua, niliamua kwamba nitavaa suruali ndefu chakavu yenye milia. Suruali yangu ile nyingine ilikuwa imekunjamana kutokana na kuitumia kama mto. Hii ilikuwa ndiyo siku ya mwisho ambayo ningaliweza kukaa kwa maana nilikuwa tu na fedha za kutosha zilizobakia kununulia petroli ya kwendea nyumbani. Nilirudi kanisani na nilipofika hao watu walikuwa wanaimba.

Mhudumu kiongozi alisimama na kusema, "Ndio kwanza tuwe na ibada ya ushuhuda iliyoongozwa na mhubiri kijana kabisa kuliko wote hapa. Mhudumu kijana anayefuata ni William Branham wa Jeffersonville." Akasema, "Njoo hapa, Kasisi Branham, kama uko jengoni."

Unaweza kuwa na hakika jambo hili lilinishitusha sana. Niliangalia chini na nikaona suruali yangu ya milia. Kwa hiyo niliketi kimya kabisa. Kusema kweli, sikuwa nimewahi kamwe kuona vyombo vya mfumo wa kupaza sauti, na kwa kweli sikutaka kupanda kwenda pale na kuhubiri mbele ya wale wahubiri wote hodari.

Wakaita tena, "Je! kuna mtu ye yote anayejua mahali alipo Kasisi Branham?"

Niliinama tu kwenye kiti changu chini zaidi kuliko hapo awali. Huo wito ulirudiwa tena. Mtu mweusi aliyekuwa ameketi karibu yangu aligeuka na akasema, "Je! wewe unajua yeye ni nani?"

Nikasema, "Sikiliza, mimi ni Kasisi Branham, bali nimevaa suruali hii ya milia na siwezi kwenda kwenye lile jukwaa."

Huyo mtu mweusi akasema, "Watu hawa hawajali jinsi ulivyovaa. Wanajali kilicho moyoni mwako."

"Vema," nikasema, "tafadhali usiseme kitu cho chote kulihusu." Lakini huyo mtu mweusi hakungojea tena.

Akapaza sauti, "Huyu hapa! Huyu hapa!"

Moyo wangu ukavunjika; sikujua la kufanya. Usiku uliotangulia huko kwenye shamba la mahindi nilikuwa nimeomba, "Bwana, kama hawa ndio watu ambao daima nimetamani kukutana nao, wanaoonekana ni wenye furaha sana na walio huru, nipe kibali mbele zao." Vema, Bwana alinipa kibali kwao, bali nilijisikia vibaya kwenda juu pale mbele ya umati huo wa watu nikiwa nimevaa suruali hiyo

ya milia. Kila mtu alikuwa akiniangalia na ilinibidi nifanye jambo fulani. Kwa hiyo nikapanda kwenda hapo jukwaani. Uso wangu ulikuwa mwekundu, na nilipogeuka niliziona maikrofoni, na nikawaza moyoni, "Vitu vile ni nini?" Nikaomba, "Bwana, kama uliwahi kumsaidia mtu yeyote, nisaidie mimi sasa."

Nikafungua Biblia na macho yangu yakaangukia kwenye kile kifungu, "Yule tajiri akafungua macho yake katika kuzimu." Na ndipo akalia. Hakukuwa na Wakristo kule, na ndipo akalia. Hakukuwa na kanisa kule, na ndipo akalia. Hakukuwa na maua kule, na ndipo akalia. Hakukuwa na Mungu kule, naye akalia. Nilipokuwa nikihubiri, nililia. Kitu fulani kilinishika na nguvu za Mungu zikashuka juu ya kusanyiko.

Ibada iliendelea kwa kama saa mbili. Baada ya kumalizika, nilitoka nje. Jamaa mkubwa sana amevaa buti za kaoboi alikuja akajitambulisha kwangu. Akasema, "Mimi ninatoka Texas na nina kanisa zuri kule. Vipi kuhusu kuniendeshea mkutano wa majuma mawili?"

Mhubiri mwingine kutoka Florida akaja na kusema, "Vipi kama ukija ukanifanyie mikutano?"

Nikachukua kipande cha karatasi na nikaandika majina na anwani, na katika dakika chache nilikuwa na mlolongo wa miamsho ya kutosha kunichukua mwaka mzima. Vema, nilikuwa na furaha. Nikaruka na kuingia kwenye Fordi yangu ndogo muundo wa "T" nami huyo nikapitia Indiana, maili 30 kwa saa—maili 15 kwa saa kwenda mbele moja kwa moja na maili 15 kwa saa huku na huku.

Nilipofika nyumbani, mke wangu akaja mbio akanikumbatia. Aliponiangalia akauliza, "Kitu gani kimekufanya uwe na furaha hivi?"

Nikasema, "Nimekutana na kundi la watu walio na furaha sana niliopata kukutana nao maishani mwangu. Wao wana furaha kwelikweli, wala hawaionei haya dini yao. Watu hawa walinikamata nihubiri kwenye mkutano wao, na cha zaidi, nimepata mialiko kuhubiri makanisani mwao. Je! utaenda pamoja nami?"

Akajibu, "Mpenzi, nimeahidi kwenda pamoja nawe po pote hata kifo kitakapotutenganisha." Mungu na aubariki moyo wake mwaminifu.

Kwa hiyo nikaamua kwenda kumwambia mama yangu. Nilipofika kule, nilimwambia juu ya ile mialiko. Akauliza, "Utafanyaje kuhusu suala la pesa?" Tuliamini ya kwamba Bwana atatupa. Akanikumbatia na akanibariki na angali ananiombea. Akasema, "Mwanangu, walikuwa na aina hiyo ya dini katika kanisa fulani nililojua miaka kadhaa iliyopita, nami ninajua ni kitu cha kweli."

Basi enyi marafiki zangu, ninayosema sasa, na yawe fundisho kwenu. Makosa yangu na yawe ni fundisho kwenu. Marafiki na jamaa zangu walinionya nisikubali kile nilichojua kilikuwa ni wito wa Mungu kwangu. Wengine walisema ya kwamba watu niliokuwa nimekutana nao kwenye ule mkutano walikuwa ni takataka ya watu. Baadaye nilikuta kwamba, na ninasema hili kwa uchaji, ya kwamba wale walioitwa "takataka" walikuwa ndio "watu walio bora kabisa." Niliambiwa ya kwamba mke wangu angepata chakula cha kutosha siku moja kisha ashinde na njaa siku ya pili. Wengine waliniambia ya kwamba kazi yangu ilikuwa ni kukaa pale na kuangalia kazi ya Jefferssonville. Mke wangu alilizungumzia mama yake naye akasema angeingia kaburini mwake na moyo uliovunjika kama Hope akienda pamoja nami. Mke wangu alilia nami nikamwambia ya kwamba inatubdi twende nyumbani tukalizungumzie. Aliamua ya kwamba ataenda pamoja na mimi, bali nikasema ni afadhali tusiende. Marafiki wapendwa, hapa ndipo shida yangu ilipoanzia. Nilisikiliza yale mwanamke aliyokuwa aseme badala ya yale Mungu aliyokuwa aseme. Katika muda wa miezi kumi na nane nikampoteza baba yangu, ndugu yangu, shemeji yangu, mke wangu na mtoto wangu mchanga, na nusura nipoteze maisha yangu mwenyewe. Sitasahau jambo hilo kamwe.

Mnamo wakati huu nilikuwa nikifanya kazi kama msimamizi wa hifadhi za wanyama pori katika Mkoa wa Indiana. Mapato niliyopata kutokana na kazi hii yalitegemea watu niliowashika. Bali kamwe sikumshika mtu ye yote. Badala yake ningeketi chini na kuzungumza na wavunja sheria juu ya uwindaji halali, jambo ambalo niliona lilileta matokeo makubwa zaidi kuliko faini ambazo ningewatoza.

Kwa wakati huu msichana wetu mdogo alikuwa amezaliwa, kitoto Sharon Rose. Namtakia heri, leo yuko mbinguni. Alikuwa ni kipenzi changu. Ninawapenda sana watoto wadogo, na ninakumbuka jinsi tulivyokuwa na furaha pamoja. Nilitaka kumpa jina la Biblia. Nisingeweza kumwita Rose of Sharon kama Yesu kwa hiyo nilimwita Sharon Rose. Tuliishi kwenye nyumba ndogo ya zamani. Ninakumbuka nilikuwa nikija nyumbani kila jioni naye angekuwa ameketi pale nje kwenye uwanja akiwa amevaa aproni yake ya pembe nne na nilipopiga kona nilipiga honi ya gari niliyotumia kama msimamizi wa hifadhi za wanyama pori. Angejua kwamba nilikuwa ninakuja naye angesema, "goo goo goo." Ndipo angeinua maskini mikono yake midogo nami ningemchukua na kumkumbatia. Jamani, alikuwa anapendeza tu alivyoweza kuwa.

Muda si mrefu mke wangu akaugua ugonjwa wa kuambukiza mapafu. Kisha ndugu yangu akauawa papo hapo

karibu yangu. Unaona, njia ya mkosaji ni ngumu. Halafu baba yangu akiwa na umri wa miaka 52, alishikwa na ugonjwa mbaya wa moyo usiku mmoja na akafa akiwa mikononi mwangu saa moja baadaye. Siku chache tu kabla hajafa alikuwa kwenye baa na mtu fulani akamwambia anywe pombe. Alikunywa glasi hiyo lakini akaanza kutetemeka. Alipoiweka chini, alianza kulia na kuzungumza juu ya mwanawe aliyekuwa akihubiri. Akaendelea kusema ya kwamba miaka hii yote alikuwa amekosea na mwanawe alikuwa sahihi. Akasema, "Kwa kuwa mimi ni mlevi msiache hilo lirudi kwa wanangu. Hii ndiyo pombe yangu ya mwisho nitakayokunywa maishani mwangu mwote." Ndipo akachukua hiyo glasi na akajaribu kunywa kilichomo lakini akajimwagia uso mzima. Mara nyingine tena akalia, akachukua kofia yake na akatoka nje. Nilisimuliwa tukio hili na ajenti wa bima ambaye baadaye nilimwongoza kwa Bwana. Muda mfupi kabla ya kifo chake, alikuwa amempa Bwana moyo wake.

Mungu alikuwa bado anazungumza na moyo wangu. Ndipo shemeji yangu alikufa mumo humo nyumbani mwake mwenyewe. Wala kila kitu hakikuonekana kikienda sawa kanisani mwangu. Njia ya mkosaji ni ngumu. Unaona, niliendelea kushuka tu basi. Lakini wakati nilipokosea, ninaamini ya kwamba Mungu bado alilinda karama Yake. Ndipo nikasema, "Loo, nifanye nini; nilifanya kosa." Upako wa Mungu ulikuwa umeniacha wala haukurudi kabisa mpaka Malaika alipokutana nami katika mwaka wa 1946. Miaka hii ilikuwa ni kipindi cha giza cha maisha yangu. Haya yote yalikuwa ni matokeo ya kutofanya yale niliyojua Mungu alinitaka nifanye.

Baada ya muda mfupi mke wangu akashikwa na nimonia. Yale mafuriko ya 1937 yakaja ghafla naye alinaswa ndani yake. Ninakumbuka usiku huo. Kamwe sitausahau. Kuta za kuzuia maji zilikatika kule juu na mji huo ulikuwa unafutiliwa mbali kwenye ramani. Nikamchukua Hope na hao watoto wawili wachanga kwenye hospitali ya muda, iliyoanzishwa na serikali. Wote walikuwa kule juu wakiwa ni wagonjwa sana. Hope alikuwa na joto la 105°. Wakati nilipokuwa nimekwenda kuomba jioni hiyo alishikwa na ugonjwa, niliangalia juu na kusema, "Bwana, mrehemu mke wangu na umponye. Je! utamponya, Bwana? Kwa kuwa ninampenda." Ilionekana kana kwamba niliona kitu fulani kikianguka kama shuka nyeusi na ikashuka moja kwa moja namna hiyo. Basi nilijua tu wakati huo ya kwamba jambo fulani litatukia. Nilienda na kuwaambia watu wa kanisani mwangu. Wakasema ni kwa sababu nilikuwa ninahusika sana na nilikuwa ninamwonea huruma kwa kuwa alikuwa

ni mke wangu. Nikasema, "La, kuna pazia jeusi ambalo limekuja kati yangu na Mungu. Kitu fulani kimenitenganisha na Yeye wala Yeye hanisikii."

Loo, nilikuwa nimechoka. Ule usiku ambapo mafuriko yalitokea, nilikuwa kwenye kikosi cha doria mtoni. Nilikuwa nikiwaokoa watu kila mahali, nikiwavuta, nikiwalundika kama ng'ombe. Niliitwa wakati huo na nikaambiwa nishuke nifike mahali ambapo mafuriko yalitokea ng'ambo ya pili. Nilikwenda upesi sana kule. Niliweza kusikia watu wakilia. Nikamsikia mwanamke mmoja akipiga mayowe, "Nisaidieni! Nisaidieni!" Nikawazia kile ningeweza kufanya na ndipo nikakimbia na nikachukua mashua ya kasi. Nikaanza kupanda, bali nisingeweza kuyavuka hayo mawimbi. Kuta za kuzuia maji zilikuwa zimebomoka na nyumba hizo mbili za gorofa zilikuwa zimetikiswa kabisa kwenye misingi yao. Ingawa nilijaribu kuabiri kuyavuka hayo mawimbi, sikuweza kufanikiwa. Hatimaye nilienda upande mmoja na nikazolewa upande wa chini ili niweze kufunga kamba kwenye nguzo ya barazani wakati nikipitia hapo. Niliifunga hiyo mashua na kuacha mota ikinguruma ipate kustahimili mawimbi.

Nikakimbia kuingia ndani kwenye hiyo nyumba na nikakuta watoto watatu ama wanne wadogo, nikawachukua nikawaingiza kwenye ile mashua. Kisha nikamchukua mama yao, nikamwingiza kwenye hiyo mashua na nikaanza kuondoka. Ilikuwa kama saa saba ya usiku, mvua iliyochanganyika na theluji ilikuwa ikianguka, wakati niliporuka kuingia kwenye mashua na kuanza kurudi. Mara nilipofika kwenye nchi kavu ambako kundi la watu lilikuwa likingojea kuishika mashua hiyo tulipokuwa tunakaribia, yule mwanamke akaanza kulia, "Mtoto wangu mchanga, mtoto wangu mchanga!" Nilifikiri alikuwa amemwacha mtoto wake nyuma na kwa hiyo nikawaacha hapo nikarudi tena. Sehemu ya nyumba hiyo ilikuwa tayari imezama, wakati hatimaye nilipoifikia. Nikaingia ndani na nikaangalia kila mahali bila kumpata mtu yeyote. Baadaye nikaja kujua ya kwamba mtoto huyo alikuwa na umri wa miaka miwili hivi. Nilidhani alikuwa na mtoto mchanga kule ndani. Ndipo niliposikia upande mmoja wa nyumba ukiporomoka, nilikimbia nikarukia dirishani nikaangukia kwenye baraza. Nilipofanya hivyo, niliona mashua yangu ikiondoka. Nikainyakua ile kamba upesi na kuingia kwenye hiyo mashua nikiwa nimelowa kwelikweli. Nikajaribu kuiwasha, lakini kulikuwa na barafu kote kwenye kamba ya kuwashia. Nikaivuta tu na kuivuta, bali isingewaka.

Mkondo ukanisukumia mtoni na hiyo mashua ilikuwa tu karibu kupinduka; nisingeweza kuiwasha hiyo mota. Nilikuwa na mke mgonjwa na watoto wawili wagonjwa hospitalini. Ndiyo kwanza nimzike baba yangu majuma

machache kabla ya hapo. Nami huyo hapo. Nikapiga magoti ndani ya mashua hiyo na kusema, "Ee Mungu, nirehemu, mwenye dhambi. Ninajua nimefanya makosa, bali tafadhali, Mungu mpenzi, usiniache nimwache mke wangu na watoto na mimi nife maji katika mto huu." Nikavuta tena na tena. Mimi huyo hapo nikielekea moja kwa moja kwenye maporomoko. Nikavuta kamba bali haingewaka. Nikaomba tena na kusema, "Mungu, unirehemu." Nilikuwa na wakati wa kutafakari juu ya mambo mengi, enyi marafiki. Ninawaambia, wakati saa hiyo itakapowadia na mauti inasukuma moja kwa moja dhidi yako, utawazia juu ya mambo mengi sana ambayo huyawazii sasa. Nilivuta na kuvuta, na kwa neema ya Mungu hiyo mota ikawaka. Nikarudi na kuyapanda hayo mawimbi tena na nikatokezea kwenye Bustani ya Howard, huko chini ya Jeffersonville, kama saa tisa usiku.

Ndipo wakaniambia upande huo mwingine wa zile kuta ulikuwa umebomoka na yakaja kupitia kwenye Hori la Lanky Kank na kuikatilia mbali Bohari ya Serikali. Nikaenda kule upesi sana na nikakuta kwamba maji yalikuwa yameifikia ile hospitali ya muda. Nilimkuta kapteni mmoja amesimama pale na kusema, "Bwana, Kapteni, kuna mtu aliyekufa maji?"

Akasema, "La, hakuna aliyekufa maji."

Nikasema, "Nilikuwa na mke na watoto wawili wagonjwa humo ndani."

Akasema, "Vema, nafikiri kila mtu alitoka kadiri nijuavyo mimi."

Nikaendelea mbele kidogo na nikakutana na mchungaji wangu mwenzi. Akanishika kwa mikono yake na kunikumbatia na kusema, "Billy rafiki yangu, kama sitakuona tena, nitakuona kwenye ile asubuhi." Hiyo ndiyo mara ya mwisho niliyomwona. Aliuawa wakati wa hayo mafuriko.

Baadaye nilikutana na Meja Weekly ambaye alisema, "Kasisi Branham, mke wako na watoto walitoka kwa behewa la ng'ombe wakaelekea Charlestown, Indiana."

Mvua ya mawe na theluji ilikuwa inaanguka nilipokuwa nikikimbia kwenda kuchukua mashua yangu nianze kwenda kule ambako Kijito cha Lanky Kank kinapitia. Mtu fulani akasema, "Loo, behewa hilo la ng'ombe lilichukuliwa na maji kule juu na kila mtu aliyekuwamo ndani yake alikufa maji." Loo, jamani!

Kisha mtu fulani akasema, "Hapana, halikuzolewa; lilipita. Tulipata habari ya kwamba lilipita."

Vema, nikaingia kwenye mashua yangu nikaanza kwenda kule. Nikaona ule mkondo ukija; nisingeweza kuyapenya yale maji. Yalinizuia pale na hapo nikawa nimetelekezwa

mahali panapoitwa Port Fulton kwa karibu siku saba. Ndipo nilikuwa na wakati wa kuwazia jambo hilo lote tena. Ndipo nikaomba. Nililia na kuwazia moyoni iwapo mke wangu alikuwa amekufa ama yu hai. Watoto wangu walikuwa na hali gani, mama yangu? Hatimaye, maji yalipopungua nilivuka na nikaanza kutembea. Nilikuwa nikipanda kwenda barabarani na nikakutana na rafiki yangu wa siku nyingi, Bw. Hay, kutoka Charlestown. Nikamwuliza, "Je! mke wangu yuko kule?"

Akasema, "Hapana, Billy, Bibi Branham hayuko kule lakini tutampata mahali fulani."

Nikasema, "Kulikuwa na garimoshi lililokuwa likija na behewa la ng'ombe lililojaa wagonjwa."

Akasema, "Halikusimama kule."

Nikashuka nikaenda kwenye Ofisi ya Msimamizi wa Usafirishaji. Akasema, "Loo, dereva aliyeendesha behewa hilo la ng'ombe atakuwa hapa katika dakika chache. Alikuwa hapa kitambo kidogo kilichopita."

Aliporudi akaniambia, "Naam, bwana, ninamkumbuka mama mgonjwa na watoto wawili. Niliwaacha huko Columbus, Indiana. Walikuwa ni wagonjwa sana."

Hiyo ilikuwa ni kama siku saba ama nane zilizopita, nami nilijiuliza iwapo walikuwa wangali hai. Sikuwa na njia ya mkato, kwa hiyo nikaanza tu kupanda kwenda barabarani. Nilipokuwa nikienda huko huku nikilia, gari moja dogo lilikuja hapo nilipo. Ndani alikuwamo rafiki yangu ambaye alisema, "Bill, ninajua unachotafuta. Unamtafuta Hope, sivyo?"

Nikasema, "Ndiyo."

Akasema, "Vema, amelala karibu na mke wangu kwenye hospitali ya muda ya Baptisti huko Columbus, Indiana, akiugua Kifua Kikuu, anakaribia kufa." Akasema, "Sijui mahali watoto wako waliko. Sikuwaona kamwe, bali nilimwona Bibi Branham kule. Hutamjua utakapomwona. Amepoteza yapata ratili ishirini na tano za uzito. Anafikiri kwamba umekufa."

Loo jamani, enyi wapendwa, ninapowazia hilo kitu fulani kinachemka moyoni mwangu. Niliingia katika gari hilo na hatimaye nikafika kwenye Kanisa la Kibaptisti ambalo lilitumiwa kama hospitali ya dharura. Nikakimbia kuingia ndani; mahali hapo palijaa watu. Nikapiga makelele, "Hope! Hope!" kwa sauti kubwa tu nilivyoweza. Nikaangalia kwenye kitanda kidogo cha zamani pembeni na nikaona mkono mdogo uliokonda umeinuliwa ukinipungia. Ilikuwa ndiye. Uso wake ulikuwa umekonda sana na nikamkimbilia upesi na kuanguka chini karibu naye nikilia. Loo jamani! Alikuwa

karibu ameaga dunia. Macho yake meusi, yakionyesha maumivu makubwa sana aliyokuwa amepitia, yaliniangalia huku nikiukumbatia mkono wake uliopauka na kukonda nami nikaomba vizuri sana nilivyojua. Lakini ilionekana haikufaa kitu. Hakukuwa na jibu. Ndipo nikasikia mkono fulani umenigusa mgongoni. Ilikuwa ni daktari aliyesema, "Je! Wewe ni Kasisi Branham?"

Nikasema, "Naam bwana."

Akasema, "Naweza kuzungumza na wewe kwa dakika moja?"

Nami nikasema, "Naam bwana."

Nikasogea kando basi akasema, "Hivi wewe si rafiki msiri wa Daktari Sam Adair wa Jeffersonville?"

Nikasema, "Tumeishi pamoja, tukavua samaki pamoja, tukalala pamoja; tumekuwa kabisa tu marafiki wakubwa sana."

Akasema, "Vema, ninataka kukwambia, mke wako anakufa, Ndugu Branham."

Nikasema, "La, Daktari, Mungu hatamwacha afe."

"Vema," akasema, "kwa kadiri msaada wa tiba unavyohusika, amekwisha. Ana kifua kikuu kinachoenea mbio wala sidhani kitu cho chote kinaweza kukizuia, kwa kuwa sasa kimemshika vibaya kiasi."

"Je! Watoto wangu wachanga ni wazima?" Nikauliza.

Akasema, "Wako kwenye chumba kingine. Sababu ya kutowaruhusu kumkaribia ni kwa sababu yeye ana kifua kikuu. Mmoja wa watoto wako ni mzima sana, bali huyo mwingine ni mgonjwa sana."

"Je! utanipeleka waliko, Daktari?" Nikamwomba. Nilienda kule kuwaona maskini Billy wangu mdogo na Sharon wakiwa wamelala pale. Niliwaangalia kisha nikarudi mahali Hope alipokuwa. "Mpenzi," nikasema, "utapona. Utaweza kuja nyumbani, na kila kitu kitakuwa SAWA." Nililia na kumsihi Mungu kwa moyo wangu wote; nilifanya kila kitu nilichojua jinsi ya kufanya. Daktari Adair, namtakia heri, alifanya kazi kwa uaminifu kama vile mtu yeyote angaliweza kufanya kazi. Tulipiga simu Lousville daktari bingwa mmoja aje, Daktari fulani Miller, kutoka kwenye Sanatoriamu. Aliingia hapo chumbani siku hiyo, akamchunguza, na kutoa ushauri wa matibabu fulani.

Daktari Adair alimwambia, "Hayo ndiyo anayopata na hayo ndiyo tu tunayoweza kufanya."

Nami nikasema, "Daktari, hivi hakuna matumaini hata kidogo?"

Akasema, "Hakuna matumaini hata kidogo, bwana, isipokuwa Mungu amrehemu. Nadhani kwamba yeye ni Mkristo na wewe ni Mkristo."

Nikasema, "Ndiyo bwana. Yeye yuko tayari kwenda, lakini Daktari, ninampenda. Je! hakuna kitu fulani unachoweza kufanya?"

Akasema, "Kasisi Branham, nimeshindwa kabisa. Tumefanya yote tujuayo kutibu kifua kikuu."

Nikasema, "Loo jamani!" Nikamwangalia mke wangu na kuwazia, "Jamani, nifanye nini?"

Nikamwambia, "Nafikiri utakuwa sawa, sivyo?"

Akasema, "Sijui, mpenzi. Ni mamoja; jambo ni kwamba tu ninachukia kukuacha wewe na watoto."

Nikasema, "Vema, mpenzi, ninaamini utakuwa mzima."

Akasema, "Ninataka kuzungumza na wewe kidogo tu, mpenzi."

Nikasema, "Naam."

Akasema, "Je, yule daktari alikwambia lolote?"

Nikasema, "Usiniulize, mpenzi. Inanibidi kwenda kazini sasa lakini nitarudi kila baada ya saa chache." Ningemwangalia na kuomba na kulia na kusihi na kuomba sana. Ilionekana kana kwamba mbingu zilikuwa ni shaba mbele zangu. Nisingeweza kabisa kufika mahali popote.

Ninakumbuka nilikuwa huko Scottsberg, Indiana, nikitembea siku moja, wakati niliposikia tangazo la redio—"Tunamwita Bwana Nyama William Branham. Afike hospitalini. Mkewe anakufa. Njoo upesi. Mkeo anakufa." Loo jamani! Nikavua kofia yangu, nikaangalia juu na kusema, "Baba, nimefanya yote niwezayo kufanya. Unajua unairarua nafsi yenyewe ya mtumishi Wako, bali labda niliirarua nafsi Yako wakati niliposikiliza yale niliyosikiliza badala ya kukusikiliza Wewe. Nakusihi, usiurarue moyo wangu utoke ndani yangu. Je! hutamrehemu? Naomba nizungumze naye, je! utaniruhusu, Bwana?" Nikafungulia king'ora na nikaenda mbio nilivyoweza kwenye mji huo uliokuwa umbali wa kama maili thelathini kutoka hapo. Nilifika kule, nikaitupa bunduki kwenye gari, na nikakimbilia hospitalini. Nilipokuwa nikija mbio, huyo hapo maskini rafiki yangu wa zamani Dk. Adair akishuka kuja kwenye ukumbi. Yeye ni daktari halisi. Aliniona na akaanza kulia kama tu mtoto mchanga na akageuka kando. Nikasema, "Sammy, hali ikoje? "

Akasema, "Bill, ameaga dunia."

Nikasema, "Loo, la, daktari, haiwezekani. Twende."

Akaanza kulia na kusema, "Bill, siwezi kwenda pamoja na wewe, Hope ni kama dada kwangu. Siwezi kuingia kule na kumwangalia tena. Siwezi kabisa. Sasa, mwite mmoja wa manesi."

Nikasema, "La, nitaingia peke yangu." Niliingia hapo ndani na nikamwangalia. Kamwe sitasahau jambo hilo. Alikuwa amefunga macho yake na mdomo wake uko wazi. Nikaweka mkono wangu juu yake na alikuwa yuko baridi sana kwa jasho. Niliona ya kwamba hakuwa ameaga dunia bado. Nikamshika mkono wake na kusema, "Kipenzi, unanijua mimi? Angalia, kipenzi, unanifahamu?" Kamwe sitasahau hayo macho makubwa mno, ambayo sasa ni ya malaika, yalipofunguka na kuniangalia. Akatabasamu nami nisingeweza kujizuia.

Aliniashiria niiname kisha akasema, "Niko mnyonge sana. Kwa nini uliniita?"

Nikasema, "Kipenzi, ilinibidi nikuambie jambo fulani."

Akasema, "Ninaondoka, Bill."

Nikasema, "Jamani, kipenzi, huondoki, ni kweli, sivyo?"

Akasema, "Ndiyo ninaondoka." Nesi akaingia humo chumbani na huku Hope akipapasa shavu langu alimwangalia huyo nesi na kusema, "Ninatumaini utakapoolewa utapata mume kama wangu. Yeye ni mzuri sana kwangu." Loo, enyi marafiki, hilo lilinihuzunisha sana.

Nikasema, "Utapona, kipenzi." Huyo nesi asingeweza kabisa kuvumilia jambo hilo ndipo akatoka nje.

Hope akaanza kuniambia kuhusu Paradiso nilikomwita, jinsi kulivyoonekana kuzuri kukiwa na miti ya kupendeza na maua na ndege wakiimba. Kwa wakati huo huo nikafikiri ya kwamba pengine nisingemwita. Lakini namtakia heri, amekuwa akifurahia mahali hapo kwa muda mrefu sana sasa. Ilionekana kana kwamba amefufuka kwa muda kidogo na kusema, "Kuna mambo mawili ama matatu ninayokutaka ujue."

Nikauliza, "Ni mambo gani hayo?"

Akasema, "Je! Unakumbuka wakati mmoja ulipokuwa huko Louisville na ulitaka kununua ile bunduki ndogo ya .22?"

Nikasema, "Ndiyo."

Akasema, "Unakumbuka hukuwa na pesa za malipo ya kwanza?"

Nikasema, "Ndiyo, ninakumbuka."

Akasema, "Daima nilitaka uwe na bunduki. Nimekuwa nikiweka akiba chochote nilichoweza nikainunue. Siwezi

kuinunua, bali utakapofika nyumbani, angalia chini ya karatasi kwenye kile kitanda cha zamani cha kukunja na utakuta fedha hizo nilizoweka akiba hapo." Kamwe hamtajua jinsi nilivyojisikia nilipoenda nyumbani na nikakuta dola sita ama saba kule katika mapeni na mahela ambazo alikuwa ameweka akiba na kunyakua hapa na pale apate kuninunulia bunduki hiyo. Ndipo akasema, "Je! unaniahidi ya kwamba utanunua bunduki hiyo?"

Nikasema, "Nitainunua, kipenzi." Niliinunua na ningali ninayo. Ninakusudia kudumu nayo mradi niko hai. Baadaye, itakuwa ni ya Billy.

Akaendelea, "Ninataka uniahidi ya kwamba hutaishi peke yako."

Nikasema, "Jamani, kipenzi, usizungumze namna hiyo."

Akasema, "La, sitaki uwe pekee yako na watoto wetu waburuzwe huku na huko ovyo. Wewe pata msichana mzuri wa Kikristo ambaye atawatunza watoto vizuri, nami ninataka uoe tena."

Nikasema, "Mpenzi, siwezi kuahidi jambo hilo."

Akasema, "Niahidi. Usiniache niende hivi. Kitambo kidogo tu nilikuwa nikisafiri kwenye nchi nzuri sana ambako hakukuwa na magonjwa, wala huzuni. Ilikuwa ni ya raha tu wala hakukuwa na maumivu. Kulikuwa na viumbe weupe wakitembea kando yangu wakinipeleka nyumbani kwangu. Nilikusikia huko mbali sana njiani ukiniita ndipo nikarudi kuja kuona ulichotaka." Enyi marafiki, ninaamini Malango ya Paradiso yalikuwa yakifunguka naye alikuwa yuko tu tayari kuingia. Alizungumza na wapenzi wake na kuita baadhi ya majina yao. Mara nyingi nimeshangaa wakati mauti yajapo, kama Mungu hawaruhusu tu baadhi ya wapenzi wetu kuja mtoni wakati tunapovuka Yordani. Labda Mungu husema, sasa kwa kuwa mama anakuja nyumbani, shuka uende ukasimame karibu na lango na ungojee mpaka atakapovuka. Enyi marafiki, ipo nchi ng'ambo ya mto, mahali fulani huko ng'ambo ya mbali, labda umbali wa mamilioni ya miaka ya mwendo wa nuru. Bali ipo—na tunasafiri kuelekea huko.

Ndipo akasema, "Mpenzi, umehubiri habari zake, umezungumzia habari zake bali huwezi kujua jinsi kulivyo na fahari. Sasa ninaenda. Bill, nichukue unipeleke Walnut Ridge ukanizike kule. Sijali kwenda kwa maana niliona jinsi kulivyo kuzuri sana."

"Kweli unaenda sasa, mpenzi?" nikauliza kwa machozi.

"Ndiyo." Akaniangalia machoni kisha akasema, "Je! utaniahidi ya kwamba daima utahubiri Injili hii nzuri sana?" Nikaahidi. Akasema, "Bill, Mungu atakutumia." (Namtakia heri. Mara nyingi nimejiuliza kama Mungu huenda

atamruhusu kutuangalia tunapoenda mahali hadi mahali katika huduma yetu, tukijaribu kuutii ule wito aliojisikia ya kwamba Mungu atatutumia.)

Nikamwambia, "Mpenzi, nitazikwa karibu nawe, papo hapo kando yako. Vinginevyo, nitarudi mahali fulani hapa kwenye uwanja wa vita, kwa hiyo Mungu na anisaidie." Nikasema, "Sasa, kama ukinitangulia, wafu katika Kristo watatangulia, nenda upande wa mashariki wa lile lango ukaningojee hapo." Midomo yake ikaanza kutetemeka. Machozi yalikuwa yakitiririka machoni mwake.

Akasema, "Nina furaha sana." Nikamvuta karibu nami nikampa busu la kwaheri ya miadi yangu naye ya mwisho hata nitakapokutana naye upande wa Lango la Mashariki. Kwa neema ya Mungu na msaada Wake niko njiani leo. Nitakuwa huko moja ya siku hizi. Hiyo ni kweli.

Loo, ilikuwa ni vigumu kwenda nyumbani baada ya kuondoka kwake. Niliona maskini koti lake limening'inia pale. Kila kitu kilinikumbusha juu yake. Nilianza kulia nilipoangalia kila mahali. Mara mtu fulani akabisha mlango nami nikauliza ni nani. Ilikuwa ni mshiriki wa kanisa langu. Akasema, "Billy, ulisikia habari mbaya?"

Nikasema, "Ndiyo, nilikuwa na Hope hadi mwisho. Sasa hivi tu ndio kwanza niondoke hospitalini."

Akasema, "Mtoto wako mchanga yuko karibu na kufa, pia."

Nikasema, "Ati nini?"

Akasema, "Sharon Rose anakufa."

Nikasema, "Haiwezekani, Ndugu Brin."

Akasema, "Ndiyo, anakufa. Hivi sasa anakufa. Sasa hivi tu ndio kwanza Dr. Adair amfanyie uchunguzi kabla sijaondoka hospitalini."

"Kuna nini?"

"Ilitokea kwamba aliambukizwa kile kirusi kutoka kwa mama yake naye ana homa ya uti wa mgongo ya kifua kikuu."

Nikakimbilia hospitalini. Walinishikia mlangoni na kusema, "Huwezi kuingia hapo ndani." Nikaanza kuingia hata hivyo. Nesi akasema, "Angalia, Kasisi Branham, huna budi kumjali Billy Paul. Msichana huyo mchanga atakufa mnamo dakika chache."

Nikasema, "Hicho ni kipenzi changu kichanga. Sina budi kumwona." Nadhani nilimsikia huyo mtoto wangu mchanga akiniita nami nikasisitiza sina budi kwenda kumwona.

Akasema, "Huwezi kumwona, Kasisi Branham. Ametengwa." Akarudi ndani na kufunga mlango. Alipoufunga, nikaponyoka kwa upande mwingine na kushuka kwenda kwenye chumba cha chini ambako walimtenga. Ilikuwa ni hospitali duni sana. Alikuwa na chandarua kidogo

cha mbu juu ya uso wake, lakini nzi walikuwa wamepenya chini yake wakaandama macho yake. Nikawafukuza na kumwangalia. Namtakia heri. Alikuwa ameshikwa na degedege. Kwa sababu ya hayo maumivu makali, misuli yake yote ilikuwa imekakamaa. Nikasema, "Sharon, kipenzi, je! unamfahamu baba?" Midomo yake midogo ikaanza kutetemeka. Alijua nilikuwa nipo pale. Bali alikuwa na maumivu makali hivi kwamba wakati aliponiangalia macho yake ya mtoto mchanga ya bluu yalibenuka upande. Loo, jamani! Moyo wangu ulikuwa unachanguka. Nisingevumilia kuangalia macho yake yaliyobenuka upande. Hadi siku ya leo, ninamkumbuka maskini Sharon wangu kila ninapoona watoto wenye macho yenye makengeza. Nimeona zaidi ya watoto mia nne wenye macho yenye makengeza wakiponywa katika muda wa kama miezi mitatu ya mikutano yangu. Wakati mwingine inabidi Mungu akamue waridi apate kutoa manukato kwake. Mnajua hiyo ni kweli. Nikakiangalia maskini kitoto hicho chenye macho yaliyobenuka, kisha nikasema, "Ee, Mungu!" Nguvu zangu hazingeweza kabisa kustahimili tena. Nikainua mkono wangu na nikasema, "Ee Baba, ulimchukua mke wangu. Usimchukue mtoto wangu mchanga na kuniacha. Tafadhali, Mungu mpenzi, ninaomba msamaha kwa makosa yangu yote. Nitaenda kuhubiri. Nitafanya jambo lolote, lolote unalosema, Bwana mpenzi. Tafadhali usimchukue mtoto wangu mchanga, tafadhali, tafadhali." Ndipo likaja hilo pazia jeusi. Nilijua mambo yamekwisha. Nikasema, "Kwaheri, kipenzi. Malaika wa Mungu watakuja kukuchukua hivi karibuni. Utaenda kukaa na mama yako. Baba atauchukua maskini mwili wako mdogo na kukuweka kwenye mikono ya mama yako. Siku moja Baba atakuona tena." Niliweka mkono wangu juu ya moyo wake nikisema, "Ee, Mungu! Si mapenzi yangu, bali mapenzi Yako na yatimizwe."

Punde tu malaika wa Mungu wakashuka na kuichukua maskini nafsi yake na wakaenda Utukufuni nayo. Ndugu Smith, mchungaji wa Kimethodisti pale, alihubiri ibada ya mazishi. Wakati jeneza lilipokuwa likishushwa, alichukua mavumbi na kusema, "Majivu kwa majivu, mavumbi kwa mavumbi, udongo kwa udongo." Kupitia katika ule msonobari kulionekana kana kwamba kunatokea wimbo ulionong'onezwa.

"Kuna nchi iliyoko ng'ambo ya mto,
Tunayoiita nchi ya raha milele,
Na tunafikia tu nchi hiyo kwa shahada ya imani,
Mmoja mmoja tunaingia langoni,
Ambako tutaishi pamoja na wasiopatikana na mauti,

Siku moja watapiga kengele hizo za heri kwa ajili yako na yangu."

Loo jamani! Nilienda nyumbani nikiwa nimevunjika moyo. Nilijaribu kwenda kazini. Wakati huo nilikuwa nikifanya kazi ya umeme. Nilikuwa fundi umeme kishughuli. Asubuhi moja mapema sana nilipanda nguzo nipate kushusha mita ya nguzo. Nilikuwa nikiimba, "Kwenye kilima fulani mbali sana . . ." (Nilikuwa nikishusha waya wa pili. Kama wewe ni fundi umeme, unajua ninalozungumzia. Ule mkubwa unaukingama huu moja kwa moja.) "Palikuwapo na msalaba unaoparuza, ishara ya mateso na aibu. Nami ninaupenda msalaba huo wa kale . . ." Niliangalia chini ardhini na kulikuwako na kivuli cha mwili wangu na ile nguzo, vikifanya msalaba na kunikumbusha juu ya Msalaba ambao Kristo alikufa juu yake kwa ajili yangu.

Nikajifunga vizuri mshipi wangu wa usalama. Nilishikwa na wasiwasi sana. Nikavua glavu ili niushike huo waya mkubwa—ukiwa una nguvu ya volti 2,300. Ungaliweza kuvunja kila mfupa mwilini mwangu. Nikasema, "Mungu, mimi ni mwoga kufanya hili." "Bali," nikasema, "Sharon, kipenzi, baba anakuja nyumbani kukutana na wewe mnamo dakika chache. Siwezi kuvumilia jambo hilo tena."

Enyi marafiki, kamwe sitajua hadi leo hii yaliyotukia, bali ninaamini Mungu alikuwa akiilinda ile Karama. Jambo lililofuata nililojua nilikuwa nimeketi chini ya ile nguzo nimekumbatia magoti yangu, nikilia na kutokwa na jasho. Nikawaza moyoni, "Nimeharibikiwa; siwezi kufanya kazi." Nikapeleka zana zangu kwenye gari na kwenda nyumbani.

Nilikuwa nimetaka kuondoka na nikaishi na wapendwa wangu ambao wako pamoja na Bwana. Maisha ya duniani hayakuwa na thamani kwangu tena. Yote niliyoishia yalikuwa kwenye ulimwengu ujao; bila hao moyo wangu uliohuzunika sana usingeweza kupata ujasiri wa kustahimili mapambano. Bali yalikuwa ni mapenzi ya Mungu, nadhani, katika kuilinda Karama Yake. Yeye alikuwa na mpango fulani nao hauna budi kutekelezwa. Nina hakika ilihitaji kila maafa na huzuni kuu ambayo ilinilazimu kupitia kusudi kunifikisha mahali ambapo Yeye angeweza kunitumia. Mungu anajua yaliyo bora kabisa.

Mama yangu alikuwa amesema niende nikakae pamoja naye. Wengine walijitolea nyumba zao. Lakini angalia, nilitaka kukaa mahali ambapo mimi na Hope tulikuwa tumeishi. Hatukuwa na chochote ila fanicha chache za zamani bali zilikuwa ni zetu. Palikuwa ni nyumbani. Tulikuwa na furaha pamoja nami nilitaka kukaa nazo kwa sababu zilikuwa ni zake

na ni zangu. Jirani mmoja alikaa na Billy Paul na nilipokuwa niko nyumbani ningeenda kumchukua na kwenda naye nyumbani pamoja nami.

Siku hiyo nilipoingia nilichukua barua. Barua ya kwanza niliyoona ilisema, "Bi. Sharon Rose Branham." Ilikuwa ni akiba yake ya Krismasi—senti 80. Loo jamani! Nililala chini nikaanza kulia. Nikawazia moyoni kwamba ningechukua bunduki yangu na kuuondoa uhai wangu. Nilikuwa ninanaanza kuwa na kichaa, nikichanganyikiwa. Nilikuwa nina wasiwasi juu ya jambo hilo sana. Nilianza kulia na nikalia mpaka nikalala. Kamwe sitasahau jambo hilo. Niliota nilikuwa nikipitia kwenye mbuga pana za nyasi. Zamani nilikuwa nikifanya kazi huko Magharibi kwenye ranchi. Nilitembea katika hizo nikiimba, "Gurudumu la mkokoteni limevunjika." Mmeusikia. "Kule chini kwenye ranchi inayouzwa." Ilitokea niliangalia kando na kulikuwako na mkokoteni wa zamani wa magharibi wa mbuga pana za majani uliong'oka gurudumu. Gurudumu la mkokoteni lilikuwa limeng'oka. Nikasema, "Naam, hiyo ni kweli." Tokea upande wa nyuma, akatokea kijana mwanamke mrembo mwenye nywele za shaba akitembea, mwenye umri wa kama miaka 18 ama 20. Alikuwa ni msichana mrembo sana niliyepata kumwona. Nikavua kofia yangu na kusema, "U hali gani, Binti?" na nikaanza kuondoka.

Akasema, "Halo, baba."

Nikasema, "Samahani? Ati ulisema baba?"

Akasema, "Ndiyo. Hivi hunifahamu, baba?"

Nikasema, "La."

Akasema, "Unafundisha nini juu ya kutopatikana na mauti?" Ninafundisha ya kwamba hakutakuwako na wazee wo wote hasa mbinguni wala watoto wachanga. Sote tutakuwa ni wa rika moja, labda kama umri wa Yesu wakati alipokufa, kama umri wa miaka 30 hivi. Akasema, "Je! hujui unayofundisha juu ya kutokupatikana na mauti?"

Nikasema, "Ndiyo, lakini hilo lina uhusiano gani na wewe?"

Akasema, "Jamani, baba, hivi hunifahamu mimi? Huko duniani nilikuwa mtoto wako Sharon."

Nikasema, "Ati Sharon?"

Akasema, "Huzuni ni ya nini, baba?"

Nikasema, "Kipenzi, wewe siye Sharon?"

Akasema, "Ndiyo, yuko wapi Billy Paul?"

Nikasema, "Vema, kipenzi, sikuelewi."

Akasema, "Ninajua hunielewi. Mama anakutafuta."

Nikasema, "Ati mama! Mama yuko wapi?"

Akasema, "Baba, kwani hujui uko wapi?"

Nikasema, "La."

Akasema, "Huku ni mbinguni."

Nikasema, "Ati Mbinguni?"

Akasema, "Ndiyo, na mama yuko huko juu kwenye nyumba yetu mpya."

Nikasema, "Ati nyumba mpya?"

Akasema, "Ndiyo, nyumba yako mpya, baba."

Nikasema, "Kipenzi, sina nyumba mpya yo yote. Watu wetu wote ni wasokwao. Tunatangatanga tu, tunalipa kodi, hapa na pale. Kamwe hakuna Branham mmoja aliyewahi kuwa na nyumba yake mwenyewe. Mimi sina nyumba mpya yoyote."

Akasema, "Lakini, baba, unayo huku juu."

Nikaangalia kando. Ilionekana kana kwamba utukufu wa Mungu ulikuwa unakuja. Ndipo nikaona nyumba kubwa mno na nzuri sana ikiwa kule.

Akasema, 'Huko ndiko unakoishi sasa, baba. Mama yuko kule juu akikutafuta. Nitamngojea Billy Paul hapa. Hivi hutaenda kumwona?"

Nikasema, "Nitaenda, kipenzi."

Akasema, "Wewe kimbia nyumbani. Mimi nitamngojea Billy."

Nikapanda juu. Singeweza kuelewa na jambo hilo, bali nilipokuwa nikipanda vipandio Hope alikuwa yuko pale. Alikuwa mpenzi tu kama kawaida, kijana, nywele zake nyeusi zikining'inia begani mwake. Alikuwa amevaa mavazi meupe. Alipokuwa akininyooshea mikono, nilianguka tu miguuni pake.

Nikasema, "Kipenzi, sielewi na jambo hili. Nimemwona Sharon."

Akasema, "Ndiyo, alisema alikuwa anashuka kuja kukulaki."

Nikasema, "Kipenzi, hapana budi kuna kasoro mahali fulani hapa. Hivi yeye si ni kijana mwanamke mrembo? Hivi binti yetu si amekuwa ni msichana mrembo?"

Akasema, "Ndiyo, yeye anapendeza sana."

Nikasema, "Lo, kipenzi."

Akasema, "Una wasiwasi sana tu, sivyo?"

Nikasema, "Ndiyo."

Akasema, "Nimekuona. Umelia na kuwa na wasiwasi juu yangu na Sharon. Sisi tuko na hali bora zaidi ya wewe uliyo nayo. Usifadhaike tena."

Nikasema, "Hope, nitajaribu kutohofu, kipenzi."

Akasema, "Sasa hujapata kuniahidi jambo lolote maishani mwako, isipokuwa umelitimiza." Daima nimejaribu kushikilia ahadi yangu. Akasema, "Angalia, uniahidi ya kwamba hutafadhaika tena."

Basi nikasema, "Nitajitahidi kutofadhaika, kipenzi."

Akanikumbatia. Kisha akaangalia pande zote na kusema, "Mbona usiketi chini?" Nikaangalia na kulikuwako na kiti kikubwa mno pale. Nikageuka nimwangalie. Akasema, "Ninajua unalowazia, ni juu ya kile kiti cha zamani ambacho kilikulazimu kukiachilia."

Nikasema, "Ndiyo." Mawazo yangu yalirudi kule nyuma kwenye nyumba yetu ya zamani. Nilikuwa nimechoka sana na tulikuwa tu na vile viti vya zamani vyenye kitako cha nyororo, mnajua jinsi vilivyo; ingekubidi kuketi wima juu ya hivyo. Tulitaka kupata kiti cha Morris. Viligharimu zaidi ya dola kumi na tano wakati huo, na ninakumbuka ilitubidi kulipia dola mbili kwa malipo ya kwanza na dola moja kwa juma. Tulinunua kimoja na nilikilipia dola sita ama saba na nikafikia tu mahali ambapo nisingeweza kukilipia tena. Waliniambia ya kwamba watakuja kukichukua. Ninakumbuka siku hiyo. Hope alijua ninapenda sambusa ya cheri, ninamtakia heri, na kwa hiyo alikuwa amenitengenezea sambusa ya cheri. Ningerudi nyumbani usiku nimechoka sana baada ya kuhubiri na kuketi kwenye kiti hiki na kusoma Biblia kwa muda kidogo. Mara nyingi ningeshikwa na usingizi nikiwa nimeketi humo. Na usiku huo alijua kiti kimechukuliwa, kwa hiyo alitaka kunifariji. Huyo ni mke halisi; huyo ni mpenzi halisi. Nilijua alikuwa hana furaha kabisa kuhusu jambo fulani. Alitaka nishuke niende mtoni nikavue samaki kidogo usiku huo. Nikawazia kuna kasoro fulani. Nikasema, "Hebu na twende kwenye chumba cha mbele." Nikaona uso wake umebadilika. Nilijua tulipotembea kuingia kwenye chumba hicho kwamba kiti chetu kilikuwa kimechukuliwa. Akaniangalia akaanza kulia. Tukakumbatiana nami nikasema, "Jamani, mpenzi, hatungeweza kufanya lo lote juu ya jambo hilo. Hatungeweza kuzuia jambo hilo." Sasa, wakati akiniangalia pamoja na hicho kiti kikubwa, akasema, "Mpenzi, kamwe hawatakuja kukichukua hiki. Hicho tayari kimelipiwa." Tukaketi chini na kupumzika kidogo.

Lo, ndugu na dada, wakati mwingine ninachoka sana hapa duniani. Nimedhoofika. Hakuna mapumziko. Ninafanya shughuli mchana na usiku. Ninapoenda nyumbani kupumzika kuna watu kila mahali walio wahitaji sana. Ee, Mungu, nifanye

nini? Ila ninajua jambo moja, moja ya siku hizi nitauvuka ule mto. Nitakapofika ng'ambo ya pili nina nyumba kule. Nina kiti kimelipiwa tayari. Wapendwa wangu wananingojea. Na moja ya siku hizi nitavuka Yordani na ndipo ninaweza kupumzika.

Ilimbidi Mwenyezi Mungu kunipitisha kwenye matukio haya machungu sana kwa kuwa nilikuwa nimekataa kutii wito Wake. Karama na miito havina majuto. Laiti ningalimsikiliza Mungu badala ya mwanadamu huenda Karama hii ingalianza kutenda kazi mapema na hivyo basi huduma yangu huenda ingalikuwa mara mia moja zaidi ya vile imekuwa siku zilizopita. Isitoshe, ningalikwepa miaka kadhaa ya huzuni isiyoelezeka.

Kwa kuwa nilitubu na kila siku ninamruhusu Mungu kuongoza na kuyatumia maisha yangu, amenirudishia, kama alivyofanya kwa Ayubu wa kale, nami ninashukuru.

Mwingize moyoni mwako na uyaweke maisha yako wakfu Kwake, msomaji mpendwa. Kristo havunji matumaini. Kamwe hutalijutia jambo hilo. Mungu akubariki katika Jina la Yesu.

William Marrion Branham

PICHA YA MAMBO YA KIMBINGUNI

Picha hii ya ajabu sana ya Ndugu William Branham ilipigwa huko Houston, Texas, kwenye mwezi wa Januari ya 1950, na Studio za Douglas. Ilipigwa kwenye uamsho ule ule ambapo Ndugu Bosworth alimletea ombi la kuombewa kwa Florence Nightingale, ambaye hadithi yake imesimuliwa kwenye mlango unaoelezea jinsi William Branham alivyofanya uamuzi kuizuru Afrika Kusini.

Wakati wapiga picha, Bw. James Ayers na Bw. Theodore Kipperman, walipoisafisha picha hiyo walishangaa sana kupata thibitisho la nuru fulani juu ya kichwa cha Kasisi Branham. Kamwe hawajawahi kuona kitu kama hicho hapo awali wala hakuna mmoja wao angaliweza kufahamu kuwapo kwa duara hii ya nuru. Kesho yake waliwasiliana na Ndugu Branham na wengine kwenye kikosi chake. Ndipo basi walielezewa ya kwamba picha zingine kama hii zilikuwa zimepigwa hapo siku za nyuma bali nuru hiyo haikuwa wazi sana kama ilivyokuwa katika picha hii.

Negativu hiyo ilipelekewa George J. Lacy, Mchunguzi wa Hati Zinazoshukiwa, kusudi ahakikishe kama au la hiyo nuru iliyokuwa juu ya kichwa cha Ndugu Branham ingeweza kuwa ni matokeo ya kupigwa vibaya, kusafishwa ama kurekebishwa. Bw. Lacy alikubali kuichunguza negativu hiyo na kisha atoe maoni yake kuihusu. Kwenye wakati uliokusidiwa ambapo alikuwa amalize uchunguzi wake na uamuzi wake kutolewa, alitoka akaingia kwenye chumba chake cha kuongojea ambamo washiriki wa kikosi cha Branham, waandishi wa habari na wengine walikuwa wakingojea. Alipoingia chumbani aliuliza William Branham alikuwa ni yupi. Ndugu Branham alisimama kwa miguu yake na kujitambulisha. Bw. Lacy akasema, "Kasisi Branham, utakufa kama wanadamu wengine wote bali mradi kuna ustaarabu wa Kikristo, picha yako itadumu."

Picha hii sasa imepata hakinakili, picha ya kiumbe cha kimbinguni. Nakala yake imetundikwa kwenye mmoja wa kumbi za Washington, D.C.

Nakala ya picha ya maelezo ya George Lacy kuhusu picha ya Ndugu William Branham pamoja na duara ya nuru ya kimbinguni

George J. Lacy
Mchunguzi wa Hati Zenye Moshaka
Shell Building
Houston, Texas

Januari 29, 1950

RIPOTI NAMAONI

Yah. Negativu Iliyoshukiwa

Mnamo tarehe 28 Januari, 1950 kwa maombi ya Kasisi Gordon Lindsay, ambaye alikuwa akimwakilisha Kasisi William Branham wa Jeffersonville, Indiana, nilipokea kutoka kwa Studio ya Douglas iliyo kwenye Barabara Kuu ya 1610 Rusk katika jiji hili, filamu ya inchi 4x5 ya picha iliyoingizwa mwanga na kusafishwa. Filamu hii ilidaiwa kuwa ya Kasisi William Branham iliyochukuliwa na Studio za Douglas kwenye Jumba Kubwa la Mikutano la Sam Houston katika jiji hili, mnamo ziara yake ya hapa katika sehemu ya mwisho ya Januari, 1950.

OMBI

Kasisi Lindsay aliomba kwamba nifanye uchunguzi wa kisayansi wa negativu iliyotajwa hapo juu. Aliomba kwamba nifanye uamuzi, ikiwezekana, kama kwa maoni yangu hiyo negativu ilikuwa imerekebishwa, ama "kughushiwa" kwa njia yoyote au la, kabla ya kusafishwa kwa filamu hiyo, jambo ambalo lingesababisha mchirizi wa nuru kutokea mahali penye hiyo duara ya nuru juu ya kichwa cha Kasisi Branham.

UCHUNGUZI

Uchunguzi mkubwa na wa kihadubini na utafiti wa pande zote mbili za filamu hiyo ulifanywa ambayo ilikuwa ni Filamu ya Eastman Kodak Safety. Pande zote mbili za filamu hiyo zilichunguzwa katika nuru iliyochujwa ya urujuani na picha za miali isiyoonekana zilipigwa za filamu hiyo.

MEMBER AMERICAN SOCIETY OF QUESTIONED DOCUMENT EXAMINERS

Uchunguzi wa kihadubini ulishindwa kuonyesha kurekebishwa kwa filamu hiyo mahali popote pale kwa njia zozote zinazotumiwa katika urekebishaji wa kibiashara. Pia, uchunguzi wa darubini ulishindwa kuonyesha kuguswa kokote kwa emalshani ndani au kuuzunguka mwali wa nuru tunayonena habari zake.

Uchunguzi wa nuru ya urujuani ulishindwa kuonyesha kitu chochote cha kigeni, ama matokeo ya athari yoyote ya kemikali kwenye pande zote mbili za negativu hiyo, ambapo huenda ungaliufanya mwali wa nuru hiyo, baada ya kusafishwa kwa negativu hiyo.

Picha ya nuru isiyoonekana ilishindwa kuonyesha kitu chochote ambacho kingeonyesha ya kwamba kuna urekebishaji wowote uliofanyiwa filamu hiyo.

Uchunguzi pia ulishindwa kuonyesha kitu cho chote ambacho kingeonyesha ya kwamba negativu inayojadiliwa ni negativu yenye sehemu zaidi ya moja au ni negativu iliyofiduliwa maradufu.

Hakukuwa na kitu kilichoonekana ambacho kingeonyesha ya kwamba mwali wa nuru tunaonena habari zake ulikuwa umeelekezwa wakati wa kusafishwa kwake. Wala hakukuwa na kitu chochote kilichopatikana ambacho kingeonyesha ya kwamba haikusafishwa kwa njia ya kawaida na inayokubalika. Hakukuwa na kitu kilichopatikana katika densiti linganifu za vitu muhimu ambavyo havikuwa katika mwafaka.

MAONI

Kwa mujibu wa uchunguzi na utafiti ulioelezewa hapo juu maoni yangu dhahiri ni kwamba negativu iliyotolewa kwa ajili ya uchunguzi huu, haikurekebishwa wala haikuwa negativu yenye sehemu mbili wala iliyopigwa mara mbili.

Juu ya hayo, maoni yangu dhahiri ni kwamba mwali wa nuru unaoonekana juu ya kichwa katika duara ulisababishwa na nuru iliyoingia kwenye negativu.

Yamewasilishwa kwa heshima,

GJL/II

Karama Za Uponyaji Na Zaidi

Imeandikwa na F. F. Bosworth

Kwa zaidi ya miaka thelathini wakati wa miamsho mikubwa ya uinjilisti, nimefanya kazi kupita kiasi, nikiwaombea wagonjwa na walioteseka. Katika kipindi cha miaka kumi na minne ya wakati huu, tuliongoza Ufufuo wa Kitaifa wa Redio wakati ambapo tulipokea karibu robo milioni ya barua, karibu zote zikiwa zina haja za maombi toka kwa wagonjwa na watu wanaoteseka ambao wasingeweza kupona bila ya tendo la moja kwa moja la Roho Mtakatifu kujibu "maombi ya imani." Tumepokea maelfu mara elfu ya shuhuda tusizoomba ziandikwe kutoka kwa wale ambao wameponywa kimiujiza na kila aina ya mateso ya kimwili niyajuayo, pamoja na ukoma. Utukufu wote na apewe Mungu kwa maana matokeo haya yasingeweza kufanywa na mtu ye yote ila Yeye. Kutokana na miujiza hii, maelfu wameongoka kwa furaha sana, ambao tusingewapata kama tusingalihubiri sehemu ya uponyaji ya injili mara moja kwa juma katika miamsho yetu yote ya kiinjilisti.

Kwa kuwa huduma hii ya uponyaji imehitaji kufanyiwa kazi inayozidi nguvu za kibinadamu, tumeomba, loo kwa bidii sana, ili kwamba Mungu ainue wafanya kazi wengi zaidi kusaidia katika sehemu hii ya huduma iliyopuuzwa sana. Na katika kipindi cha miaka michache iliyopita, mara nyingi nimelia kwa furaha juu ya karama ya Mungu ya hivi karibuni kwa Kanisa ya ndugu yetu mpendwa, William Branham, na "Karama yake ya Uponyaji ya ajabu sana." Hii ni namna Mungu afanyavyo mambo ya ajabu mno "kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo" (Efe. 3:20), kwa maana sijapata kuona wala kusoma juu kitu cho chote kinacholingana na huduma ya uponyaji ya William Branham.

MALAIKA ANATOKEA

Mnamo Mei 7, 1946, Malaika aliyekuwa amesema na Ndugu Branham kwa sauti iliyosikika mara kwa mara tangu utoto wake hadi wakati huu, hatimaye alimtokea, na miongoni mwa mambo mengine akamwambia ya kwamba Kuja kwa Kristo kulikuwa kumekaribia. Na Mjumbe huyo wa Mbinguni akasema: *"Nimetumwa kutoka kwenye uwepo wa Mwenyezi Mungu kukwambia . . . ya kwamba Mungu amekutuma kuwapelekea watu wa ulimwengu karama ya uponyaji."*

Kwenye ukurasa wa 1291 wa Biblia ya Scofield, Dk. C. I. Scofield, D.D., katika maandiko yake ya pambizoni juu ya

Malaika anasema: "Ingawa malaika ni roho (Zab. 104:4; Ebr. 1:14), wamepewa uwezo wa kuweza kuonekana katika umbo la sura ya kibinadamu (Mwa. 19:1 na Maandiko mengine mengi katika Agano la Kale na Agano Jipya pia). Katika Kut. 23:20, Mungu alimwambia Musa: 'Tazama, mimi namtuma Malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengenezea.' Na katika Mwa. 24:40, tunasoma, 'Bwana. . . atapeleka Malaika Wake pamoja nawe, atafanikisha njia yako'."

Hivi ndivyo hasa Mungu amemfanyia Ndugu Branham. Yeye haanzi kuombea kuponywa kwa wanaoteseka katika mwili kwenye mstari wa maombi kila usiku, mpaka Mungu anapomtia mafuta kwa ajili ya kufanya kazi kwa ile Karama, na ni mpaka yeye anapohisi uwepo wa Malaika akiwa pamoja naye jukwaani. Bila ya kuhisi kuwepo huku, yeye anaonekana kuwa hoi kabisa.

KUPEWA ISHARA MBILI

Sasa angalia ya kwamba Mungu hakumtuma tu Malaika awe pamoja na Musa, Yeye pia alimpa miujiza miwili mikamilifu kama ishara na thibitisho kwa watu ya kwamba Mungu alikuwa amemtokea na kumwagiza, chini ya uongozi wa kiungu, kuwa mkombozi wao (Kut. 4:1-31). Ishara ya kwanza ilikuwa ni ile ya fimbo ya Musa kufanyika nyoka, na ishara ya pili ilikuwa ni ile ya kuweka mkono wake ubavuni mwake na kuufanya uwe "mweupe kama theluji kwa ukoma," nk. Mungu alimwambia Musa, "Basi itakuwa, wasipokusadiki, wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili" (Kut. 4:8). Katika vifungu vitatu vya mwisho vya mlango huu tunasoma ya kwamba wakati ishara hizi mbili ziliporudiwa "mbele ya watu, watu wakaamini. . .na wakainamisha vichwa vyao wakasujudu."

Ni hivyo tu, zaidi ya kumpeleka Malaika kuwa pamoja na Ndugu Branham na kumfanikisha, Yeye amempa pia ishara mbili za miujiza ya kweli kabisa ambazo zimetumika kuinua imani ya maelfu ya watu ambao kibinadamu wasingeweza kupona kufikia kiwango ambacho "Karama ya Uponyaji" hufanya kazi.

UBAINISHAJI WA KIMBINGUNI WA MAGONJWA

Ishara ya kwanza: Wakati Malaika alipomtokea Ndugu Branham, alimwambia jinsi ambavyo angeweza kujua na kutambua magonjwa yote na mateso; hivi kwamba wakati ile karama ilipokuwa ikifanya kazi, kwa kuuchukua mkono wa kulia wa mgonjwa huyo yeye angehisi mitetemeko mbalimbali

ya mwili ama kudunda ambako kungemwonyesha magonjwa mbalimbali ambayo kila mgonjwa alikuwa anaugua. Magonjwa ya viini, ambayo yanaonyesha kuwepo na kutenda kazi kwa pepo "mtesi" (Mdo. 10:38) kunaweza kusikiwa dhahiri. Wakati pepo wa kutesa anapokutana na karama hii hufanya vurugu kubwa sana ya kimwili hivi kwamba vurugu hiyo huonekana kwenye mkono wa Ndugu Branham, na ni halisi sana hata itasimamisha saa yake ya mkono mara moja. Hali hii kwa Ndugu Branham inasikika kama kushika waya wa umeme wenye moto mwingi mno. Wakati pepo huyo mtesi anapotolewa katika Jina la Yesu, unaweza kuuona mkono mwekundu na uliovimba wa Ndugu Branham ukirudia hali yake ya kawaida. Kama mateso hayo si ya ugonjwa wa viini, basi Mungu daima humfunulia Ndugu Branham mateso hayo kwa Roho. Ishara hii ya kwanza kwa kawaida huinua imani ya mtu huyo kufikia kwenye kiwango cha kuponywa; bali vinginevyo, ishara ya pili itafanya hivyo.

MWONAJI

Ishara ya pili: Huyo Malaika alimwambia ya kwamba huo upako ungemfanya kuona na kumwezesha kuwaambia wanaougua matukio mengi ya maisha yao tangu utoto wao hadi wakati wa sasa. Hata huwaambia baadhi yao mawazo yao wakati wakija jukwaani ama kabla hawajakuja mkutanoni. Hivi majuzi nilimsikia akimwambia mama mmoja aliyekuwa akimleta maskini msichana wake mdogo, "Mama, mtoto wako alizaliwa akiwa kiziwi na bubu; na mara ulipogundua ya kwamba hawezi kusikia, ulimpeleka kwa daktari." Na ndipo Ndugu Branham akamwambia mama huyo jinsi hasa daktari alivyosema. Huyo mama akasema, "Hiyo ni kweli kabisa." Umati mkubwa mno husikia haya yote kwenye vipaza sauti. Ndugu Branham kwa kweli huona jambo hilo likifanyika na huku akisogeza maikrofoni ili wasikilizaji wasisikie jambo hilo, yeye humwambia mgonjwa dhambi zozote ambazo hazijatubiwa wala kuachwa maishani mwao ambazo zinapaswa kuachwa kabla ya hicho Kipawa kutumika kwa ajili ya uponyaji wao. Mara watu kama hao wanapokubali na kuahidi kuacha hiyo dhambi ama hizo dhambi zilizofunulia namna hii, mara nyingi uponyaji wao unatukia mara moja kabla Ndugu Branham hajawa na wakati wa kuomba. Matamshi haya yaliyoletwa na Malaika yanathibitishwa kila usiku katika mikutano ya Branham mbele ya macho ya maelfu.

Hivyo basi huo umati wa wasikilizaji unashuhudia kila usiku tena na tena miujiza ya aina tatu mbalimbali. Hiyo miwili ya kwanza haiwaponyi wenye kuugua, bali hutumika tu kama ishara za kuinua imani ya wanaoteseka kufikia kiwango ambacho "karama ya uponyaji hutenda kazi kwa ajili

ya kuponywa kwao." Kwa kweli, ishara hizi mbili za kimiujiza zinawezekana tu wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa juu ya Ndugu Branham kwa ajili ya kusudi hili.

ZAIDI YA "KARAMA ZA UPONYAJI"

Hapana shaka Wakristo wachache hapa na pale, katika Wakati wa Kanisa, na wengine wakati huu wa sasa wametunukiwa "Karama ya Uponyaji" ambayo imeorodheshwa kati ya karama tisa za kiroho katika Mlango wa 12 wa I Wakorintho, kila moja ya hizo ikielezewa kama "Dhihirisho la Roho," (I Kor. 12:7-11). Inapaswa kuwepo na washiriki wa kawaida katika kila kanisa waliotunukiwa namna hii.

Lakini Ndugu Branham ni njia ambayo ni zaidi ya karama tu ya uponyaji; yeye pia ni Mwonaji kama vile walivyokuwa Manabii wa Agano la Kale. Yeye huona matukio kabla hayajatukia. Nilimwuliza, "Una maana gani? Unayaonaje?" Alijibu, "Ni kama tu vile ninavyokuona wewe; ni kwamba tu ninajua ni ono." Kwa udhahiri kabisa kama vile mtu anavyoona vitu vya kawaida vinavyowazunguka, Ndugu Branham, akiwa katika maombi mchana, anaona kwenye ono baadhi ya miujiza mikubwa kabla haijatukia. Anawaona wengine wamebebwa kwenye machela ya gari la wagonjwa, ama wameketi kwenye viti vya magurudumu, na anaweza kuelezea vile wanavyoonekana na vile walivyovaa, nk. Wakati akionyeshwa miujiza hii kabla haijatendeka, yeye huwa kwa kawaida, kwa wakati huo, hana habari na mambo yanayoendelea karibu yake. Hakuna hata mara moja kwa zaidi ya miaka sita tangu alipoipokea karama hiyo ambapo funuo hizi zilishindwa kuleta miujiza ya kweli jinsi ile ile hasa alivyokuwa ameiona tayari kwenye ono. Katika kila wasaa huo yeye anaweza kusema akiwa na yakini kabisa, "Bwana asema hivi," wala kamwe yeye hakosei. Aliniambia ya kwamba yeye hutekeleza tu yale aliyokwisha kujiona akifanya katika ono. Ufanisi wa sehemu hii ya huduma yake ni 100% barabara.

KUYATAZAMA YASIYOONEKANA

Wakati karama hii inapotenda kazi, Ndugu Branham anakuwa ndiye mtu mwepesi sana sana kutambua uwepo na kutenda kazi kwa Roho Mtakatifu na kwa mambo halisi ya kiroho kuliko mtu ye yote niliyepata kumjua. Akiwa chini ya upako ambao huendesha karama zake za kiroho na wakati anapohisi uwepo wa yule Malaika, anaonekana kwamba anapasua pazia la mwili na kuingia katika ulimwengu wa roho, na anaonekana kuwa anashukiwa na mfululizo wa mtiririko wa hisi ya mambo yasiyoonekana. Paulo aliandika (2 Kor. 4:18),

"Tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana: kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele."

Maneno ya Paulo hapa yanaonyesha ya kwamba sasa hivi tunaishi katika ulimwengu wenye sehemu mbili kwa wakati mmoja—ulimwengu wa hisi za mwili, na ulimwengu wa roho. Ulimwengu wa roho unauzunguka, na kufunika, na unapenya ndani na kuchaganyikana na ulimwengu wa hisi za mwili. Aina zote mbili za ulimwengu ziko kwenye nafasi ile ile moja kwa wakati mmoja. Vitu vya kawaida tunavyoona kwa macho yetu ya kawaida vipo katikati ya mambo halisi yaliyo bora zaidi yasioonekana kwa neva yetu ya jicho. Maandiko yanatufundisha ya kwamba kweli za "milele" zilizo bora zaidi zinatuzunguka hivi sasa. Ni vitu gani ambavyo kila mmoja wetu angeweza kuona kwa kila dakika ya maisha yetu, kwenye kila kona ya njia yetu, kama tungalikuwa na macho yenye upako wa kuyaona! "Yanayoonekana" yako katikati ya "yasiyoonekana," "yasiyodumu" katikati ya hayo ya "milele."

Paulo anasema, "Yeye aliyeunganishwa na Bwana ni roho moja naye." Tunapokuwa tumejazwa na Roho Mtakatifu, roho yetu na Roho ya Mungu zinaunganishwa pamoja zikawa moja kama jinsi vile bahari na ghuba vilivyo kitu kimoja kwa maana bahari humiminika ikaingia kwenye ghuba. Ndipo basi ni kwamba kweli tukufu za mambo halisi ya kiroho huchukua mamlaka na kutwaa utawala kabisa juu ya hayo yanayoonekana. Tunaona ukweli na hakika za kiroho kwa macho ya Mungu. Kwenye nyakati kama hizo matukio ya usoni yanaonekana kana kwamba yapo kama vile mvuto wa onyesho la awali la sinema inayokuja. Yesu alisema ya kwamba "Roho atawaonyesha mambo yajayo."

MIUJIZA KUONEKANA KABLA

Kwenye mkutano wa Fort Wayne mama mmoja aliingia kwenye mstari wa uponyaji akimbeba mtoto aliyezaliwa na mguu uliopindika ambao ulikuwa umefungwa piopi. Mara Ndugu Branham alipowaona, bila ya kuwasimamisha ili aombe kwa ajili ya uponyaji wa mtoto huyo, alimwambia huyo mama, "Loo, ndiyo, je! utafanya nitakalokwambia ufanye?" Huyo mama akajibu, "Nitafanya." Ndipo akamwambia, "Nenda nyumbani basi ukatoe piopi hiyo, na utakaporudi kesho usiku, umlete mtoto, na msichana atakuwa na mguu mzima kabisa." Maikrofoni iliyatangaza maneno haya kwa wote kwenye umati huo mkubwa sana. Iliwachukua zaidi ya saa nzima usiku huo kutoa piopi hiyo. Mama huyo alipomleta mtoto huyo usiku uliofuata, mtoto huyo alikuwa na mguu mzima kabisa na alikuwa amevaa jozi mpya ya viatu vidogo vyeupe na alikuwa akitembea. Daktari

aliupiga mguu huo Eksrei na akakuta kwamba uko mzima kabisa. Nilimwuliza Ndugu Branham kesho yake kwa nini alimpitisha huyo mama na mtoto wake kwenye mstari wa maombi bila ya kuombea kuponywa kwa mtoto huyo. Alijibu, "Halikuwa jambo la lazima, kwa kuwa katika ono alasiri nilimwona mtoto huyo ameponywa." Ingeyafanya makala haya yawe marefu mno kama ningesimulia visa vingine vingi vya ajabu zaidi katika utondoti kuliko kisa hiki. Sehemu hii ya huduma yake peke yake ingeweza kuleta matukio ya kujaza kitabu.

Katika Mlango wa 5 wa Yohana Mt., Yesu anasema, "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi... Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo Yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. Kwa kuwa Baba ampenda Mwana, Naye humwonyesha yote ayatendayo Mwenyewe." Yesu alikuwa na maana gani? Naam, Yesu alikuwa ni Mwonaji kama vile Manabii wa Agano la Kale walivyokuwa. Yeye aliona miujiza yake kabla haijatukia. Alimwona yule mtu aliyekuwa hawezi muda wa miaka 38 ambaye asingeweza kuingia kwenye lile birika wakati Malaika aliposhuka kuyatibua maji. Yesu akamjia na kusema, "Jitwike godoro lako, uende zako." Yesu alimwona Lazaro amefufuka kutoka kwa wafu kabla hajaufanya muujiza huo. Alimwambia Nathanaeli, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini, nilikuona." (Yohana1:48) Yeye aliona mahali mwana punda alipokuwa amefungwa bila ya Yeye kuwapo pale. Aliwaambia wanafunzi Wake wawili: "Nendeni zenu mjini; atakutana nanyi mwanamume amechukua mtungi wa maji; mfuateni..." (Marko 14:12-16). Na Kristo anayeishi ndani sasa anaendeleza kazi Zake kwa njia ya utumishi wa wanadamu kulingana na ahadi Yake kwa wakati huu: "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya...kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba, nanyi mkiomba lo lote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." (Yohana 14:12,13).

MVUTO WA IMANI UNASIKIWA

Kwa habari za yule mwanamke aliyegusa upindo wa vazi la Yesu na akaponywa, Yesu alisema, "Naona ya kuwa nguvu zimenitoka" (Luka 8:46). Jambo hili lilipojulikana, tunasoma katika Marko 6:55, 56, ya kwamba, "Na kila alikokwenda, akiingia vijijini, au mijini, au mashambani, wakawaweka wagonjwa sokoni, wakamsihi waguse angaa pindo la vazi Lake; nao wote waliomgusa wakapona." Mungu na ashukuriwe nguvu zizo hizo zingali zinatiririka kutoka kwa Kristo anayeishi ndani kuingia kwenye miili ya wagonjwa na wanaoteseka, nao wanaponywa.

Zile ishara mbili za miujiza ambazo Mungu huzidhihirisha kupitia kwa Ndugu Branham kuinua imani ya hao walio kwenye mstari wa maombi kufikia kiwango kinachofaa, zinatolewa pia kuinua imani ya wanaoteseka katika kusanyiko kufikia kiwango hicho hicho. Imani hii huvuta nguvu zile zile kutoka kwa Kristo anayekaa ndani ambaye anaendesha karama hiyo, na kuwaponya hao wanaoketi kwenye kusanyiko. Ni mamoja tu kama ni magonjwa yako yanayobainishwa kimuujiza, ama ni ya mtu aliye kwenye mstari wa uponyaji, ishara hizo ni zile zile, na zina matokeo yale yale juu ya wale wanaoketi kwenye kusanyiko hilo. Kwa nini ishara hizo zirudiwe kwa kila mtu ambaye ameishaziona tayari? Musa hakurudia zile ishara zake mbili kwa kila Mwisraeli binafsi. Elfu moja wangeshuhudia hilo thibitisho na kufanywa waamini wakati huo huo. Imani kwenye kiwango kinachofaa katika sehemu yo yote ya kusanyiko kubwa huvuta zile nguvu katika Kristo akaaye ndani, ambaye anaendesha hiyo karama; na jambo hili haliwezi kutukia bila ya Ndugu Branham kujua hilo. Analisikia dhahiri kama vile ambavyo wewe ungesikia kama ningevuta koti lako, na anajua mvuto huo unatoka upande gani; na hata anamtambulisha huyo mtu ambaye imani yake inamgusa Kristo.

Wakati mmoja kwenye mkutano wa Louisville, wakati alipokuwa akiwaombea wagonjwa jukwaani, alihisi mvuto thabiti wa imani ukitoka kwenye kusanyiko, na mara huo mvuto ulipokoma, alielekeza kidole upande huo na kusema, "Mama mmoja moja kwa moja kule nyuma ndio kwanza aponywe kansa." Naye aliponywa.

Wakati alipokuwa akisoma Maandiko kwa kusanyiko lingine, aliacha kusoma na akamwelekezea kidole mtu fulani ambaye hajawahi kumwona kabla ya hapo, na akamwambia, "Ndugu, imani yako sasa hivi imekuponya kansa hiyo inayosambaa upesi kati ya goti lako na kifundo cha mguu wako." Hiyo kansa ilikauka papo hapo.

Wakati alipokuwa akiwaombea hao waliokuwa kwenye mstari wa maombi kwenye mkutano wa Flint, alisimama kuomba naye akielekeza kidole kwenye roshani ya pili upande wake wa kuume, akasema, "Nimeona ono sasa hivi la mama aliyevaa suti ya bluu na vazi lenye milia kiunoni. Ndiyo kwanza aponywe kansa." Huyo mwanamke akaruka akasimama kwa miguu yake na kwa furaha kuu akasema, "Mimi ndiye huyo mama." Imani yake ilitenda kazi kwake akiwa kwenye roshani ya pili kama vile imani ilivyokuwa ikifanya kazi kwa hao waliokuwa jukwaani.

Msichana mmoja aliyezaliwa na macho yenye makengeza na ambaye alikuwa akihudhuria Shule ya Biblia huko Fort Wayne wakati wa mkutano kule alimwambia Bibi Bosworth ambaye alikuwa huko nyuma kwenye kibanda cha vitabu,

"Siwezi kuona jinsi nitakavyoweza kuingia kwenye ule mstari wa uponyaji, kuna watu wengi sana." Bibi Bosworth akamwambia, "Haitakubidi kufanya hivyo. Wewe simama tu hapa nyuma na umwombe Mungu aiinue imani yako kufikia kiwango cha uponyaji, nawe utavuta nguvu za uponyaji kutoka kwenye ile karama." Akafanya hivyo, na wakati wa ibada Ndugu Branham akasimama kidogo na kuelekeza upande alikokuwa na kusema, "Msichana mmoja huko nyuma ameponywa kabisa sasa hivi macho yenye makengeza." Macho yake yamekuwa sawa tangu wakati huo.

Msichana mmoja alibebwa akaletwa mkutanoni kwenye machela. Alikuwa anakufa kwa lukemia. Kwenye Johns Hopkins na kwenye Kliniki ya Mayo aliambiwa ya kwamba wamefanya kila kitu kilichowezekana kufanywa na kwamba hakukuwako na matumaini kwake kuishi. Akili zake zilikuwa zimeanza kuharibika. Niliondoka jukwaani pole pole nikaenda kwenye machela yake na kumwambia awe akiomba ya kwamba Mungu aiinue imani yake ifikie kiwango cha kuponywa na kwamba aidha itaendesha hiyo karama ama itamvuta Ndugu Branham ashuke aje kwake. Nikaangalia midomo yake ikitikisika katika kuomba na mara Ndugu Branham akausikia mvuto wa imani, akaruka kutoka jukwaani na akaenda kwenye machela yake, akamwombea, na kusema, "Katika jina la Yesu amka kutoka kwenye machela yako, pokea nguvu za kiungu na uwe mzima." Akatii na akiwa ameinua mikono na machozi ya furaha yakitiririka mashavuni mwake na huku anaabudu, alitembea huku na huku mbele ya watu wote na akashuka kwenda kwenye marefu ya kanisa. Dada yake aliniambia baadaye, "Dada yangu ni mzima kabisa."

Katika Ukumbi mkubwa wa Mikutano wa Fair Park huko Dallas, Texas, usiku mmoja wakati viti vya okestra vilikuwa vimejaa wagonjwa kwenye machela na kwenye viti vya magurudumu, wakati Ndugu Branham alikuwa anashughulika kuwaombea hao waliokuwa kwenye mstari wa uponyaji, wakati wote alikuwa akihisi mvuto wa imani kutoka upande wake wa kuume ambao hatimaye ulikoma. Wakati alipomalizana na wale aliokuwa akiwashughulikia, alimwelekezea kidole mtu fulani aliyekuwa kwenye machela kwenye viti vya okestra, naye akamwambia, "Ewe mtu, amka, ulikwisha kuponywa kama dakika tano zilizopita." Akaamka akimsifu Mungu. Mke wake akamjia nao wakakumbatiana na kulia pamoja kwa furaha. Mwanamume huyo alikuwa ameletwa kutoka Chicago katika hali ya kufa huku mapafu yake yakiwa yameliwa na kansa. Aliponywa na akaja kwenye mkutano mwingine huko Ft. Wayne siku chache baadaye kutoa ushuhuda wake. Amehudhuria mikutano mingine miwili tangu wakati huo. Ningeweza kuendelea na kuendelea kusimulia kurasa nyingi

za uponyaji kama huo wa hao walioponywa wakiwa wameketi ama kulala kwenye machela kwenye kusanyiko bila ya Ndugu Branham kuwagusa kamwe.

HAKUNA MAGONJWA MAGUMU

Hakuna kitu kama ugonjwa mgumu kwa Mungu. Mama mmoja kutoka Ugiriki aliyeziba koo aliingia kwenye mstari wa maombi. Hakuweza kumeza tone moja la maji wala aina yo yote ya chakula. Mara tu Ndugu Branham alipomwombea alikunywa glasi ya maji na akala kipingiti cha peremende. Siku moja ama mbili usiku baadaye katika mkutano uo huo viziwi tisa na bubu walikuja katika mstari wa maombi na wote tisa wakaponywa.

Wale waliozaliwa vipofu walipata kuona. Baada ya kumwombea mtu mmoja aliyekuwa kipofu kabisa, Ndugu Branham alimwambia, "Tembea uende mimbarani na uweke kidole chako kwenye pua ya yule mhubiri." Alienda moja kwa moja kwa yule mhudumu na akamvuta pua yake, akiwafanya wasikilizaji waangue kicheko.

Mmishenari mashuhuri sana kutoka Palestina akiwa kwenye hatua ya mwisho ya Kifua Kikuu aliletwa kutoka Yakima, Washington, katika gari la kubebea wagonjwa kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Jiji huko Seattle, Washington. Serikali ilimlipia nauli yake ya ndege ya kurudi nyumbani. Alipoamriwa, katika Jina la Yesu, kuamka na awe mzima alifanya hivyo, na siku mbili baadaye alikuwa akifanya kazi ya mikono nyumbani mwake.

UPONYAJI WA JUMLA

Kama tu vile ambavyo wito wa madhabahuni ama mwaliko wa wenye dhambi unavyofuata ibada ya kiinjilisti, hivyo basi baada ya utambuzi wa kiroho na uponyaji wa hao waliomo kwenye mstari wa maombi, mwaliko sasa unatolewa kwa wale walio kwenye kusanyiko ambao wako tayari kukubali uponyaji wao. Uponyaji wa mtu mmoja kwa zamu jukwaani ni utangulizi tu wa ibada kubwa ya uponyaji. Tuseme ni somo tu la kielelezo kwa wote walio mkutanoni ambao wanahitaji kufaidika na sehemu ya uponyaji wa Injili.

Kama tu vile ambavyo wenye dhambi mia moja wanavyoweza kuitikia wito wa mwinjilisti na bado wapate tukio kuu zaidi la muujiza wa kuzaliwa upya kwa kundi, vivyo hivyo imeonyeshwa kwa mshangao mkubwa ya kwamba wagonjwa wanaweza kuponywa kijumla na karama ya uponyaji. Ibada inapoelekea kwisha Ndugu Branham kwa kawaida huelekeza kidole kwa haraka sana kwa mtu mmoja baada ya mwingine akisema, "Kristo amekuponya." Watu wengine wanatupa kadi

zao za maombi hewani, wanatupa chini mikongojo yao na hao ambao wasingeweza kusimama wala kutembea wanasimama mara moja kwa miguu yao, baadhi yao wakiruka na kumsifu Mungu kwa furaha. Onyesho la namna hiyo halielezeki. Kwenye mkutano mmoja mvulana mmoja aliyekuwa kwenye kiti na ambaye hangeweza kusimama wala kutembea, aliruka mara moja kwa miguu yake akimsifu Mungu. Dakika chache baadaye, nilimwashiria na kuuomba umati wa watu wampishe njia aje jukwaani. Alienda kwenye maikrofoni na akawahubiria vizuri wasikilizaji waliokuwa wakilia. Karama hiyo ilitenda kazi kwa uponyaji wa jumla kama tu vile ilivyokuwa imekwisha kufanya kwenye mstari wa maombi ambapo waliponywa mtu mmoja mmoja kwa zamu.

UMATI WA WENYE DHAMBI WANAJITOA KWA PAMOJA

Na zaidi kabisa ya yote, kwa jinsi hii wenye dhambi wanashawishika juu ya dhambi zao na wanataka kuokolewa. Katika Warumi 15:18, 19, Paulo anazungumza juu ya kuwafanya "Mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo, kwa ishara kuu na maajabu, katika nguvu za Roho wa Mungu. . . tangu Yerusalemu, na kando kando yake, mpaka Iliriko." Nimeona idadi ipatayo wenye dhambi thelathini elfu katika siku moja wakisimama kwa miguu yao machozi yakiwatiririka kuitoa mioyo yao kwa Mungu. Si ajabu Yesu alisema, "Katika mji wo wote mtakaoingia—waponyeni wagonjwa waliomo."

Akinukuu Zaburi 68:18, Mtume Paulo alisema katika Efe. 4:8, "Alipopaa juu aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa." Habari za kipawa hiki cha kiungu kwa Kanisa imeenea kote ulimwenguni katika muda mfupi wa miaka sita, na simu nyingi za dharura zinaingia toka katika sehemu zote za dunia. Baadhi ya wanaoteseka wamerushwa kwa ndege juu ya bahari kutoka nchi zingine hadi Marekani wapate kuombewa.

Kabla ya kufunga, ninajisikia kwamba sina budi kuwaambia wale wanaosoma mistari hii lakini hawawezi kuhudhuria Mkutano wa Branham, ya kwamba jambo hili si lazima likuzuie kuponywa, na wewe pia. Maelfu wameponywa kimiujiza kwa maombi yao wenyewe. Mungu anatamani sana kuponywa kwako zaidi ya vile inavyowezekana kwako kukutamani. Yesu alikufa kusudi jambo hilo liwezekane. Kalvari inafanya kila kitu ambacho Mungu ameahidi kuwa mali yako binafsi. "Mzima kabisa" ndiyo mapenzi ya Mungu yaliyothibitishwa na kuonyeshwa kwa umati mkuu wa watu. Vitabu vyetu juu ya uponyaji pamoja na "maombi ya imani" vimeleta uponyaji kwa maelfu ya watu. Mtiririko unaoendelea wa shuhuda zisizoombwa zingali zinatufikia kutoka kwa wapendwa wetu redioni na jamaa zao pia. Kitabu changu,

"KRISTO ALIYE MPONYAJI", kikiwa sasa kwenye toleo lake la saba (kurasa 250), kinazo na kinazielezea dhahiri kweli za Biblia ambazo zimewaweka watu wengi mno huru kutokana na namna zote za mateso ya kimwili yasiyotibika kibinadamu wakati hapakuwapo na mtu mwenye karama ya uponyaji, si hata kuwapo kwa mzee wa kuomba maombi ya imani. Waliponywa kwa kuamini tu na kutekeleza Maandiko kuhusu kuponywa kwa mwili wao, kwa jinsi ile ile ambavyo wenye dhambi wanaamini na kutekeleza hayo Maandiko kuhusu kuponywa kwa nafsi yao. Kijitabu changu kinachoitwa "Ushuhuda wa Mkristo," kinachoonyesha jinsi imani yetu inavyopaswa kuwa kwa ajili ya kupokea baraka zote za ukombozi, kinatenda maajabu. Kweli zake, zikitekelezwa, zitaleta kutimizwa kwa ahadi ya Mungu kuponya ama kufanya kitu cho chote kile ambacho Yeye ameahidi katika Biblia.

Kasisi F. F. Bosworth

Ni Kwa Sababu Gani William Branham Alizuru Afrika Kusini?

Kila siku haja za maombi nyingi mno huja nyumbani kwa William Branham. Nyingi za hizi huambatana na tikiti ya ndege kumwomba aje awaombee wagonjwa. Ilikuwa ni moja ya haja hizi iliyomfanya Ndugu Branham kuifanya kuwa suala la maombi kabisa kuhusu ziara yake ya Afrika Kusini. Alikuwa ameifikiria Afrika Kusini hapo kabla, bali Bwana daima alikuwa amemwelekeza kwenda sehemu zingine. Mwaka huu alikuwa amewazia juu ya Australia na Japani, bali Bwana kwa udhahiri alimwongoza kwenda Afrika.

Mnamo mwezi wa Januari, 1950, Ndugu Branham na Ndugu F. F. Bosworth walikuwa wakiendesha mikutano huko Houston, Texas. Jioni hiyo hiyo ambapo ile picha ya Ndugu Branham ilipigwa, ambayo ilionyesha ile duara ya nuru juu ya kichwa chake, Ndugu Bosworth alimwonyesha Ndugu Branham picha ya mama mmoja. Ilikuwa imeambatanishwa na barua na tikiti ya ndege kutoka kwa Florence Nightingale wa Durban, Afrika Kusini, jamaa wa mbali wa Florence Nightingale yule aliyeanzisha Msalaba Mwekundu. Alikuwa ni mifupa mitupu kabisa na jambo hilo liliwakumbusha juu ya Georgia Carter, maskini msichana mdogo kutoka Milltown, Indiana, aliyekuwa katika hali ya aina hiyo hiyo kabla hajapokea kuponywa kwake. Kwa karibu miaka tisa alikuwa amelala kwa mgongo akiugua kifua kikuu na hakufikia angalau uzito wa ratili arobaini wakati Ndugu Branham alipomwombea.

Florence Nightingale huyu wa Durban alishikwa na kansa kwenye njia ya kuingilia tumboni jambo ambalo husababisha mtu afe kwa njaa. Alikuwa na uzito wa kama ratili hamsini tu. Alikuwa amelishwa glukosi kupitia kwenye mishipa ya damu mpaka njia hiyo haikuwezekana tena. Aliposikia habari za Ndugu Branham, alimlilia apate kuja amwombee. Hivyo basi akamwandikia aje, akimtumia picha yake pamoja na tikiti ya ndege.

Usiku huo huko Houston walimwombea Florence Nightingale, wakimwahidi Mungu ya kwamba kama Yeye angemponya na kumfanya mzima kabisa, wangelichukulia jambo hilo kama ni dalili kutoka kwa Mungu ya kwamba wanapaswa kwenda Afrika Kusini.

Majuma manane baadaye kikosi cha Branham kilitua Uingereza kikielekea Finland. Mfalme wa Uingereza alikuwa ametuma kebo akimwomba Ndugu Branham aje na amwombee. Wakati kikosi cha Branham kiliposhuka kutoka



Hii ni nakala ya picha iliyoambatanishwa na haja ya maombi ya Florence Nightingale.

kwenye ndege, jina la William Branham liliitwa kwa kipaza sauti. Florence Nightingale alikuwa amefika kwenye uwanja wa ndege dakika kumi na tano tu kabla hawajawasili na hao waliokuwa pamoja naye walitoa wito huu kwa Ndugu Branham aje upesi kwa kuwa walidhani mama huyo alikuwa anakufa. Mahali hapo palijaa umati wa watu hivi kwamba walipashwa habari wawasiliane naye kwenye Hoteli ya Picadilly. Jambo hili lilifanyika na yakafanywa matayarisho yeye apate kuja kwenye hoteli alipokuwa mama huyo.

Ilikuwa ni moja ya hizo siku zenye ukungu mwezi wa Aprili wakati walipopelekwa hotelini kwa gari ambako huyo mama alikuwa akikaa. Hakuna mtu kwenye kundi hilo aliyewahi kuona mwanadamu katika hali ya kusikitisha sana kama aliyokuwa nayo huyo mwanamke mle chumbani. Alikuwa amekonda sana hata ngozi ilishikamana na mifupa yake. Mioyo yao ilishikwa na huruma. Ilikuwa vigumu sana kwa Florence Nightingale kuzungumza huku machozi yakimtiririka mashavuni mwake kwa kuwa alikuwa akiteseka kwa maumivu makali mno.

Hao wote, pamoja na mhudumu wa Kanisa la Uingereza pamoja na manesi wake huyo mama, walipiga magoti wakaanza kumwombea. Walipoanza kuomba njiwa alikuja na akaketi kwenye kizingiti cha dirisha, akiangalia ndani akianza kulia kwa utulivu. Baada ya maombi, wakati Ndugu Branham aliposema, "Amina," huyo njiwa aliruka akaenda zake. Huyo mhudumu akaanza kunena akisema, "Je! mlimwona huyo njiwa?" Kabla hajamaliza swali hilo Roho wa Bwana akamvuvia Ndugu Branham kusema maneno haya—"Bwana asema hivi, utaishi, dada."

Miezi minane baada ya Ndugu Branham kumwombea Florence Nightingale huko Uingereza alipokea picha nyingine kutoka kwake. Wakati huu alikuwa ni mzima kabisa na mwenye afya na alikuwa na uzito wa ratili 155. Alikuwa ameweka nadhiri yake kwa Mungu na sasa akawa ameshawishika ya kwamba itabidi aende Afrika Kusini. Mungu alikuwa amemwita kwenda Afrika Kusini na sasa shauku yake ilikuwa kwamba aweze kuwa baraka kwa hao watu aliokuwa ameitwa kuwahudumia.

Tulipokuwa bado tungali tuko Johannesburg, na majuma kadhaa kabla hatujakuja Durban, Ndugu Branham alitwambia ya kwamba mikutano yetu iliyo mikubwa sana itakuwa huko Durban. Daima alizungumza juu ya Durban kwa matarajio ya mambo makubwa kutendeka kwa ajili ya Mungu. Baadaye katika kitabu hiki utakuta taarifa ya mikutano iliyofanyika kule, mikutano mikubwa kuliko yote iliyopata kufanywa Afrika Kusini. Hatukupata nafasi ya kukutana na Florence Nightingale tulipokuwa Afrika Kusini kwa kuwa tunafahamu yeye sasa anaishi Uingereza.

Picha hii inaambatana na
ushuhuda wa kuponywa kwake.

Mfano wa Ibada Ya Kawaida

Habari za jioni, wapendwa. Rehema kuu za Mungu na amani ziwe pamoja nanyi nyote. Kukaa kwangu hapa jijini kwenu ni kufupi, bali nimefurahia kila saa yake. Ninajisikia moyoni mwangu ya kwamba hii haitakuwa ndiyo ziara yangu ya mwisho ya kuja Afrika Kusini. Mungu akitujalia, tungefurahi kuja tena. Hapana shaka wakati huo hata mtakuwa na imani zaidi, kwa sababu ya yale mmekwishaona na mtakayoona usiku wa leo. Ninajua ya kwamba katika kusanyiko hili usiku wa leo kuna watu wengi ambao tayari wameponywa. Huenda msitambue jambo hili sasa hivi, bali shikeni ninayowaambia. Katika majuma yajayo mtaona watu waliokuwa wagonjwa wakati mmoja wakija kwa wachungaji wao na marafiki zao na kusema, "Ile shida ya tumbo imekwisha," "Ile kansa—sinayo tena," na "Hebu angalia mkono wangu; ninaweza kuutumia," na mambo mengine mengi sana kama hayo. Mtaona ya kwamba nimewaambia kweli.

Ningependa kuona uamsho katika makanisa yote ya Afrika Kusini. Sisi sote ni mmoja katika Kristo. Sisi ni Roho mmoja tulioounganishwa katika mwili mmoja. Hivi si litakuwa ni jambo zuri sana kuona kuta za madhehebu zimevunjwa hivi kwamba sisi sote tutatenda kama mtu mmoja katika Yesu Kristo? Hili litaleta uamsho.

Sasa ninataka kusoma sehemu tu ya Maandiko kwa maana ninafikiri ya kwamba hakuna ibada iliyo kamili bila ya kusomwa kwa Neno. Maneno yangu yatashindwa, kama ya mtu mwingine ye yote, bali Neno la Mungu halitashindwa kamwe. Kumbukeni, Neno la Mungu litamshinda Shetani mahali po pote, wakati wo wote na chini ya hali yo yote. Wakati Yesu alipokuwa hapa, Baba alikuwa ndani Yake Naye alikuwa sawa na Baba. Hata hivyo, wakati alipokutana na Shetani, hakutumia cho chote cha vipawa vyake. Yeye alisema tu, "Imeandikwa." Kila mara Yesu aliposema, "Imeandikwa," Yeye alimshinda Shetani. Wewe una ahadi hiyo katika Neno la Mungu, na kila wakati unapolitumia Neno katika imani, Shetani atakuacha. Hili ni Neno la Mungu na kama yale nisemayo hayakubaliani na hili, basi maneno yangu hayafai kitu. Lakini maneno yangu yakikubaliana na Neno la Mungu, basi Mungu atayaheshimu, jambo ambalo amelifanya tayari katika mikutano yetu.

Sasa nataka kusoma kutoka katika mlango wa pili wa Luka Mt., kuanzia kwenye kifungu cha ishirini na tano.

> "Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mweye haki,

mcha Mungu, akiitarajia faraja ya Israeli; na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana. Basi akaja hekaluni ameongozwa na Roho; na wale wazazi walipomleta mtoto Yesu ndani, ili wamfanyie kama ilivyokuwa desturi ya sheria, yeye mwenyewe alimpokea mikononi mwake, akamshukuru Mungu, akisema, Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, uliouweka tayari machoni pa watu wote; nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli. Naye Yusufu na mamaye walikuwa wakiyastaajabia hayo yaliyonenwa juu yake. Simeoni akawabariki, akamwambia Mariamu mama yake, Tazama, huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa vibaya. (Nawe mwenyewe, upanga utaingia moyoni mwako,) ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi. Palikuwa na nabii mke, jina lake Ana, binti Fanueli, wa kabila ya Asheri, na umri wake ulikuwa miaka mingi, alikuwa amekaa na mume miaka saba baada ya uanawali wake. Naye ni mjane wa miaka themanini na minne; haondoki katika hekalu, ila humwabudu Mungu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba. Huyu alitokea saa ile ile akamshukuru Bwana, na wote waliokuwa wakiutarajia ukombozi katika Yerusalemu akawatolea habari zake."

Bwana Yesu na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno.

Ninataka kuzungumza kwa muda mfupi tu juu ya matarajio. Kwa kawaida unapata unayotarajia. Sasa kama ulihudhuria mkutano upate kukosoa tu, Shetani hakika atakuonyesha jambo fulani la kukosoa. Kama umekuja kupata baraka, Mungu atahakikisha kwamba unapata baraka, kwa kuwa cho chote unachotarajia utakipata.

Hebu niwape mfano wa kile ninachomaanisha. Wakati mmoja mama yangu alinituma kwenda kwenye hafla na akaniambia kwamba ningekutana na dada yake. Akanielezea jinsi alivyo, akisema ya kwamba alikuwa ni wa umbo dogo, mwenye pua ndefu na kidevu kirefu, alikuwa na paji la uso pana, na alichana nywele zake kwa nyuma, na kuzisokota kwa nyuma. Nilienda kumtafuta. Nilikuwa na picha ya namna fulani ya sura yake.

Sasa, kama unakuja upate uponyaji wa Kiungu, inakubidi uwe na wazo fulani la Mungu ni nani. Unaamini jambo hilo? Sasa, Mungu ni Roho, bali unaweza kuangalia

jinsi anavyotenda kazi. Yesu alisema ya kwamba Yeye angemtuma Roho Mtakatifu Naye angeshuhudia habari za Kristo, na kutukumbusha mambo haya ambayo Yesu alikuwa amesema. Pia atatuonyesha mambo yajayo. Alisema, "Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya; na kubwa kuliko hizi atazifanya; kwa kuwa mimi ninaenda kwa Baba yangu." Alisema pia kwamba asingeweza kufanya neno mpaka Baba amwonyeshe, na halafu wakati Baba alipomwonyesha ono, alitenda jambo hilo. Sasa, Yesu ni yeye yule jana, leo na hata milele. Basi inatupasa kuwa na madhihirisho ya namna iyo hiyo kwenye mikutano yetu kama yale Yesu aliyokuwa nayo katika siku Zake.

Mara nyingi mmewasikia watu wakisema, "Kuona ni kuamini." Mmesikia msemo huo. Nitawathibitishia ya kwamba msemo huo ni kweli kwa sehemu tu. Papa hapa ninamwona mtu amesimama karibu na mimi amevaa suti nyeusi. Ana tai nyeupe yenye madoa mekundu. Ni wangapi wanaamini hiyo ni kweli? Hakika, mnaweza kumwona; mnajua ya kwamba yeye yupo hapa. Sasa nitageuka na kuangalia upande mwingine. Simwoni mtu huyo lakini hata hivyo yupo hapa. Ninajuaje? Kwa kuwa nina hisi nyingine. Kuna hisi tano katika mwili wa mwanadamu—kuona, kuonja, kugusa, kunusa na kusikia. Hizo zinatofautiana, moja kwa nyingine. Kwanza nilijua yeye yupo hapa kwa hisi ya kuona. Nikigeuka siwezi kumwona, lakini ninajua yupo hapa kwa sababu nimeweka mkono wangu juu yake na ninaweza kumgusa. Sasa hisi yangu ya kuona haifanyi kazi, lakini hisi yangu ya kugusa inafanya kazi. Nikimgeukia tena na kuondoa mkono wangu kutoka kwake, kugusa hakutamtangaza, bali kuona kutamtangaza. Una hisi nyingine. Sikilizeni, ninasikia muziki. Ni wangapi wanafikiri ninasema kweli? Je! mliuona? Mliugusa? Mliunusa? Mliuonja? La. Bali mna hisi ya kusikia. Sasa, kuona si kuamini. Kwa jambo hilo kusikia ni kuamini. Sasa, kuna hisi tano.

Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake—mtu roho. Ndipo akamwekea ndani yake hisi tano kusudi aweze kuwasiliana na mazingira yake ya duniani. Hazina uhusiano wo wote na Mungu. Hizo hisi tano zilitolewa zipate kuwasiliana na mazingira ya duniani. Bali nafsi ya mwanadamu, roho, ina hisi pia, ambayo ni imani. Kwa imani mwanadamu huwasiliana na Muumba wake. Hizo hisi tano hazina uhusiano wo wote na jambo hilo. Huwasiliana na mazingira ya duniani bali roho yako inawasiliana na mazingira ya kimbinguni. Kwa hiyo hisi ya kugusa, kama vile kumgusa kwangu mtu huyu, ni halisi kwa mwili. Kuona ni halisi kwa mwili. Ni kitu halisi. Lakini imani ni halisi zaidi kwa nafsi yako. Sasa sikilizeni, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo

usiyoyaona, usiyoyaonja, usiyoyagusa, usiyoyanusa wala kuyasikia. Hata hivyo ni halisi vile vile, halisi zaidi kuliko yo yote ya hisi hizo zingine tano.

Vipi kama hakuna mtu aliyepata kuona maishani mwake na kwa ghafla mtu fulani akapata macho na akaweza kuona. Tungalifikiri kwamba mtu huyo alikuwa ni mwendawazimu wakati aliposema ya kwamba angeweza kuona mambo na vitu pia na mwanga mkubwa wa jua, nk. Kama tungalikuwa na hisi nne pekee, tungalifikiri mtu huyo alikuwa ni mwenda wazimu. Lakini kwake yeye ni jambo halisi. Basi ndivyo ilivyo na imani. Je! ungeweza kusema shati hilo ni jeupe? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba shati hilo ni jeupe? Hiyo inaonyesha ya kwamba mnaweza kuona. Sasa, kama imani yako ikisema utaponywa, na ni halisi tu kwako kama macho yako ambayo yanasema ya kwamba shati lile ni jeupe, umeponywa. Imani huliarifu jambo hilo. Ni kamilifu.

Sasa hebu na twende kwenye somo letu kwa muda mfupi. Simeoni alikuwa ni mzee aliyeishi hekaluni. Kulingana na wanathiolojia tunaambiwa ya kwamba alikuwa kwenye umri wa miaka themanini na kitu. Siku moja alipewa ahadi na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti hata atakapomwona Kristo wa Bwana. Alizunguka akimwambia kila mtu, "Mimi sitakufa mpaka nimemwona Kristo." Wao wakasema alikuwa na kichaa. Wakasema, "Daudi na manabii wote walimtarajia Kristo, na sasa hebu mwangalieni mtu huyo, akiwa mzee kama hivi alivyo, hata hivyo anafikiri atamwona Kristo." Alikuwa na haki ya kuamini jambo hilo kwa kuwa Roho Mtakatifu hawezi kusema uongo. Sasa angalia, yeye hakuona aibu. Haikuwa kitu kwake alikuwa na sifa njema sana jinsi gani, kwamba historia yake ya ukoo ilikuwa ikoje, wala jinsi alivyokuwa mtu wa kuheshimika. Alikuwa na ahadi kwa Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti hata atakapomwona Kristo wa Bwana. Hakuona haya kushuhudia jambo hilo, kwa maana Roho Mtakatifu alikuwa amemwambia hivyo.

Sasa, Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa na Simeoni yupo hapa usiku wa leo. Ni wangapi wanaoamini katika kuponya Kiungu? Vema, kama unaamini jambo hilo, kumbuka Daudi alisema, "Kilindi kinapoita kilindi." Kwa maneno mengine, kama kuna kilindi ndani hapa kinachoita, kuna kilindi huko nje kuwasiliana nacho. Ni kama hivi: kabla hapajakuwapo na pezi kwenye mgongo wa samaki ilibidi kuwe kwanza na maji apate kuogelea. Vinginevyo, asingalikuwa na pezi hilo. Kabla hakujakuwapo na mti kuota katika nchi ilibidi kwanza kuwe na nchi, la sivyo kusingekuwako na mti wo wote wa kukua nchini. Unaona ninalomaanisha?

Sasa, muda mrefu uliopita nilisoma kwenye gazeti juu ya mtoto mchanga aliyekula mpira wa pedali ya baisikeli

na mpira kutoka kwenye penseli. Wakampeleka kwa daktari ambaye alimfanyia uchunguzi naye akasema maskini mtoto huyo hakuwa na salfa kabisa mwilini mwake. Mpira una salfa ndani yake, kwa hiyo alikuwa akila mpira ili apate salfa. Kama kulikuwako na kitu fulani ndani yako chenye shauku kuu ya salfa, hapana budi kuwe na salfa mahali fulani itakayoitikia shauku hiyo. Kukiwa kuna maumbile ndani ya moyo wa mwanadamu, hapana budi kuwe na muumba wa kuumba maumbile hayo.

Kama ukiomba kumpata Mungu zaidi, hapana budi kuwe na mambo zaidi ya Mungu ya kupokewa. Ulipokuwa u mwenye dhambi, nafsi yako ililia kumpata Mungu. Makafiri wanalia wampate Mungu. Kuna kitu fulani ndani yao kinachotamani sana kuabudu. Hawakujua waabudu kitu gani, kwa hiyo walijitengenezea sanamu na kuiabudu hiyo. Ilikuwa ni ujinga wa kutomjua Mungu, lakini inaonyesha ya kwamba kulikuwako na kitu fulani kilichokuwa kikimlilia Mungu, kikililia kuabudu. Ilibidi kuwepo na Mungu mahali fulani kuumba kiumbe hicho, la sivyo shauku hiyo isingalikuwamo ndani yao. Sasa ninyi watu hapa mlioinua mikono yenu na kusema mliamini ya kwamba uponyaji wa Kiungu upo, na kwamba mliutamani, hapana budi kuwe na chemchemi ya uponyaji iliyofunguliwa mahali fulani vinginevyo msingekuwa na shauku hiyo. Mnaona, ni kilindi kikiita kilindi.

Simeoni alikuwa ameahidiwa kumwona Kristo. Hebu na tuseme ilikuwa ni Jumatatu asubuhi wakati Yesu alipozaliwa. Hawakuwa na magazeti na redio tulivyo navyo siku hizi, bali njia pekee waliyokuwa nayo kutuma ujumbe fulani ilikuwa ni mdomo kwa sikio. Kulikuwako na wanajimu wachache wa nyota waliokuja kule na wakamtambua Yeye kwa ishara. Malaika walishuka na kutangaza kuzaliwa Kwake. Wachungaji wachache walikuja kumwabudu, bali waliojua si wengi. Kulikuwa na watu yapata milioni mbili katika Israeli wakati huo, na labda kwa usiku mmoja kulikuwa na watoto wengi waliozaliwa. Kama ilivyokuwa desturi ya Wayahudi, kwenye siku ya nane ilibidi mama aje na kutoa dhabihu kwa ajili ya utakaso na kumtahiri mtoto. Wazia tu hao watu wengi hapo hekaluni asubuhi hiyo, kila mtu akijishughulisha na mambo fulani. Safu ndefu ya akina mama ilisimama pamoja na watoto wao wachanga, na huko chini barabarani alisimama maskini bikira mmoja akiwa amejifunika shela usoni mwake akiwa ameshika hua wawili kama sadaka ya utakaso. Watoto tajiri wangeweza kutoa mwana-kondoo bali hii ilikuwa ni sadaka ya mkulima mdogo wa kijijini, hua wawili wadogo au njiwa wawili. Na halafu maskini mtoto huyo mchanga alikuwa amefungwa nguo za kitoto.

Mariamu kwanza alikuwa na jina baya. Walimwambia ya kwamba huyo alikuwa ni mtoto wa Yusufu, kwamba Yusufu alikuwa ndiye baba yake. Kwa hiyo, ninaweza tu kuona hao wanawake wakirudi nyuma kumkwepa yeye na mtoto wake, aliyezaliwa nje ya ndoa takatifu. Lakini katika maskini moyo wa yule bikira alijua mtoto mchanga huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu, ingawa alikuwa amefunikwa katika nguo za kitoto. Huyo hapo, Imanueli, akikaa katika mwili. Alimpembeza mtoto huyo mchanga, kila mtu anarudi nyuma kumkwepa.

Huko mbali ndani hekaluni Simeoni aliketi akiandika. Yeye alikuwa na ahadi ya kwamba angemwona Kristo. Ninaweza kuwazia nikimwona Roho Mtakatifu akishuka na kusema, "Simeoni, amka. Toka nje, Simeoni." Hakujua mahali alikokuwa anaenda lakini huyo akatoka hekaluni. Huyo akaenda kupitia kwenye safu hiyo ya akina mama, akisimama mbele ya maskini mama huyo aliyekuwa na jina hilo baya. Akamchukua mtoto huyo mchanga mikononi mwake, huku machozi yakitiririka ndevuni mwake. Akaomba, "Bwana, sasa mruhusu mtumishi wako aondoke kwa amani, kulingana na Neno lako: Kwa maana macho yangu yameuona wokovu wako. . . "

Huko nyuma kabisa pembeni kulikuwako na mama kizee akiomba. Kwa miaka mingi alikuwa akiitarajia faraja ya Israeli. Alikuwa ni kipofu na alikuwa ni nabii mke. Wakati uu huu Roho Mtakatifu akasema, "Ana, simama kwa miguu yako." Huyo hapo anakuja, kipofu, akitembea miongoni mwa watu, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Akaja karibu na Mariamu, akamchukua huyo mtoto mchanga mikononi mwake, na akamtukuza Mungu.

Na Roho Mtakatifu yuyo huyo aliyemwongoza kipofu Ana kwa Mwokozi yupo hapa usiku wa leo kukuongoza kwa Mwokozi, Kristo wa Mungu, Yeye aliyekufa pale Kalvari na akamtuma Roho Mtakatifu. Na je! linaonekana ni jambo geni kwenu wakati ninapowaambia jambo hili, ya kwamba ninyi watu mlio na njaa ya kuponywa na Mungu mmeumbiwa shauku hiyo moyoni mwenu na Roho Mtakatifu. Kama alivyowaongoza Simeoni na Ana wa kale, vivyo hivyo amewaongoza ninyi kuja hapa usiku wa leo. Mmekuwa mkitarajia jambo hilo. Sasa lipo hapa kwa ajili yenu. Kwa kuwa kuna chemchemi iliyojaa damu, inayotiririka kutoka ubavuni mwa Imanueli, ambamo kila mmoja anaweza kujitumbukiza ndani ya mafuriko hayo kuondolea mbali mawaa yake ya hatia na kila mgonjwa anaweza kuondolewa ugonjwa wake.

"Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu: adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa kupigwa

Kwake sisi tumeponywa." Kila mmoja wetu. Nanyi, enyi watu wapendwa, mnaoamini ya kwamba kuna chemchemi mahali fulani, hii hapa—imefunguliwa mbele zenu, bure. Kila atakaye, na aje na apokee kuponywa kwake. Roho Mtakatifu yeye yule aliyempa Simeoni ahadi hiyo, anawapa ninyi ahadi hiyo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyemwongoza Simeoni kwa Kristo amewaongoza kwenye chemchemi ya uponyaji. Ni Roho yeye yule jana, leo na hata milele. Je! mnaamini jambo hili? Ni kweli. Wao walio wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu. Je! mnaamini jambo hilo?

Mimi ni mwanadamu tu ila nilizaliwa nabii, kuona maono. Yapata miaka mitano iliyopita malaika alinitokea. Alikuwa amevaa nguo nyeupe, na juu yake kulikuwa kuna nuru inayong'aa. Alikuwa na uzito wa kama ratili mia mbili, amenyoa ndevu kabisa, hana viatu, na nywele zake zilifika mabegani mwake. Alinijia na kusema ya kwamba nilizaliwa ulimwenguni nipate kuwaombea wagonjwa. Aliniambia ya kwamba alitumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuniambia jambo hili. Alisema, "Kama utakuwa mwaminifu na uwafanye watu wakuamini wewe, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako, si hata kansa." Ndipo nikamwambia nisingeweza kwenda; sina elimu. Akasema ya kwamba kama vile nabii Musa alivyopewa ishara mbili, vivyo hivyo ningepokea ishara mbili ambazo zingekuwa ni ushahidi wa yale ninayowaambia. Ningemshika mtu mkono naye akasema angesema nami, akinifunulia shida ya mtu huyo. Mambo mengi yangetimia na ningeona maono. Ningejua siri za mioyo ya watu, nikitambua mambo yao yaliyopita na pia mambo ya usoni.

Kabla hajaondoka nilimwuliza mambo haya yangewezekanaje. Akasema ya kwamba wakati Yesu alipokuwa hapa hakuweza kamwe kufanya jambo lo lote Yeye Mwenyewe, ila lile Baba alilomwonyesha. Ni watu wangapi wanajua hilo ni kweli? Biblia inasema nini? "Yesu Kristo yeye yule jana, na leo, na hata milele." Kama ni yeye yule leo kama alivyokuwa wakati ule, basi Yeye ataponya vile vile leo kama alivyofanya wakati huo. "Bado, kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mnaniona . . . " Hiyo si ni kweli?

Sasa, nina muda mfupi tu wa kuwapa ushuhuda kabla hatujaanza kuwaombea wagonjwa. Wakati mmoja huko Marekani, nilipokuwa kwenye gari moshi nikienda Kusini kukutana na Ndugu Bosworth, nilipata ono. Nilimwona mvulana mdogo amelala sakafuni na nguo zake zote zimeraruliwa. Niliona miamba na miti; ilikuwa ni nchi ya ugenini. Mwili wake mdogo wote ulikuwa umevunjwavunjwa, naye huyo hapo amekufa. Usiku huo mkutanoni niliwaambia watu kuhusu ono hili. Nikasema, "Liandike kwenye Biblia yako na uone kama halitatimia."

Siku chache baadaye walinipeleka kwa mvulana mdogo ambaye alikuwa amekufa maji katika handaki la umwagiliaji. Bali huyo hakuwa ndiye huyo mvulana niliyemwona kwenye ono, ambaye alikuwa na umri wa yapata miaka minane ama kumi na alikuwa ameuawa kwa ajali. Mvulana huyu aliyekufa maji alikuwa ni jamaa mdogo, mwenye nywele nyeusi, amevaa vizuri. Hakuwa ndiye mtoto huyo. Kote Marekani na Canada nilishuhudia na kuwaambia, "Liandike hilo kwenye Biblia yako." Iliandikwa kwenye maelfu ya Biblia. Niliwaambia ya kwamba hapo ono hilo litakapotimizwa na mvulana huyo awe amefufuka, itatokea katika "Sauti ya Uponyaji."

Mnamo Aprili, 1950, tulipokuwa huko Ufini, tulitoka Helsinki na tukaenda mpaka Kuopio. Baadhi yetu tulikuwa tumetoka kwenda kupanda mnara wa ulinzi ambapo tungeweza kuona nchi ya Urusi. Nilikuwa nikifunga sana na nikawaambia mameneja wangu, "Jambo fulani litatukia." Tulipokuwa tukirudi tulifika mahali palipotokea ajali. Gari lilikuwa limewagonga wavulana wawili. Mmoja alikuwa amegongwa ubavuni na kutupwa kwenye mti, kichwa chake pamoja na mbavu zake zimevunjwavunjwa. Gari hilo, lililokuwa likiendeshwa kwa mwendo wa maili sabini kwa saa, lilimgonga huyo mvulana mwingine likamrusha mbele kabisa, likamvingirisha chini ya gari na kumtupa nje nyuma ya gurudumu la nyuma likamtupa hewani. Yapata dakika ishirini baadaye sisi tukawasili. Kulikuwa na kundi kubwa la watu. Walikuwa wamemlaza chini na kumfunika usoni kwa koti lake.

Bw. Lindsay na hao wengine walitoka nje na kumwangalia, bali mimi nisingeweza kwenda. Niliwazia juu ya mwanangu na moyo wangu ukahuzunika. Hatimaye wakauliza, "Mbona huendi?" Kwa hiyo nikaenda. Nilipomwangalia maskini mvulana huyo, walikuwa wameliondoa hilo koti usoni mwake, nusura moyo wangu uzimie. Nilimwazia maskini Billy Paul maelfu ya maili toka nilipokuwa. Wote walikuwa wanalia. Nikaanza kugeuka, ndipo nikasikia mkono juu yangu. Nikasema, "Sielewi jambo hili ni nini." (Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama pale wakasema, "Yule pale yule mtu wa miujiza kutoka Marekani. Hebu tuone atafanya nini." Unaona jinsi vile watu wasivyoelewa.) Nikageuka na kusema, "Inaonekana kana kwamba nimemwona mvulana yule mahali fulani. Hebu na tuangalie tena." Ndipo wakalifunua koti lake tena. Nikasema, "Nimemwona mvulana yule." Nilikuwa nimevuviwa sana, nisingeweza kumkumbuka mara ya kwanza. Nikawaambia hao wahudumu, "Je! huyu ni mfuasi wa makanisa yenu?" "La," wakasema. Ndipo nikatambua yeye alikuwa ndiye yule mvulana niliyekuwa nimemwona katika ono siku za nyuma huko Marekani kama mwaka mmoja na nusu hapo kabla.

Kamwe hamtajua jinsi nilivyojisikia. Hapakuwapo na pepo wa kutosha huko kuzimu ambao wangeweza kumshikilia. Nikasema, "Karibieni nanyi mtauona utukufu wa Bwana." Nikapiga magoti jinsi vile tu nilivyoonyeshwa katika lile ono nikaomba: "Mwenyezi Mungu, katika nchi ya uenyeji wangu yapata mwaka mmoja na nusu uliopita, Wewe ulinionyesha mvulana huyu na ukaniambia ya kwamba angefufuka." Huyo hapo amelala, amevunjikavunjika kabisa, ndipo nikasema, "Ee, Bwana, yasikie maombi ya mtumishi Wako. Na sasa ewe mauti—huwezi kumshikilia tena, kwa maana Yesu Kristo alitoa ahadi ya kwamba mvulana huyu ataishi." Mvulana huyo akasimama kwa miguu yake, akiwa hai na mzima. Hao hapo wafanyabiashara wamesimama, watu mashuhuri wa jiji. Nina matamshi kutoka kwao wakithibitisha jambo hili, yametiwa sahihi na mthibitishaji rasmi.

Ningeweza kuendelea kwa saa nyingi nikiwapa shuhuda za jinsi ambavyo Mungu ameponya kimiujiza, bali hatuwezi kuchukua wakati zaidi kwa kuwa hatuna budi kuingia kwenye ibada ya kuponya. Laiti ningaliweza kumwombea kila mmoja wenu mmoja mmoja, bali hilo haliwezekani. Nitaliombea kusanyiko lote nanyi nyote mnaweza kuponywa, kama tu vile mwenye dhambi akilichukua Neno na kuliamini anavyoweza kufanywa kiumbe kipya. Sina budi kuwafanya kuamini. Unapokea uponyaji wako kwa imani ile ile inayookoa ama kuponya nafsi yako.

Usiku wa leo tena kama kawaida tunataka kuwaita jukwaani watu kama kumi ama kumi na watano kati yenu ninyi watu hapo chini mlio na kadi za maombi. Hii si ibada ya kuponya bali ni onyesho la yale yanayoweza kutukia kwenu ninyi nyote huko mliko. Mwanangu Billy alisambaza kadi za maombi mapema jioni hii. Billy Paul, ulisambaza namba zipi usiku wa leo? L-50 hadi L-100." Vema, alisambaza kadi hamsini usiku wa leo nami ninaamini tutaita kumi na tano za kwanza, kutoka L-50 hadi L-65. Angalia namba iliyoko nyuma ya kadi yako na uone kama una yoyote ya namba hizo kutoka L-50 mpaka L-65. Kama unayo, njoo hapa upesi sana uwezavyo ili tuweze kuwapanga mstarini na kuanza ibada ya maombi.

Usifikiri ati kwa sababu hujapokea kadi ya maombi ya kwamba hutaponywa. Ninataka mwone kwamba haina uhusiano wo wote na kadi za maombi. Ninawaita watu wachache hapa ili kwamba mweze kuona ile Karama ikitenda kazi na hapo mwamini. Pia inasaidia kuleta Upako juu yangu.

Wakati wakiutayarisha mstari wa maombi ninataka kusema, enyi Wakristo wapendwa, ya kwamba siwajii ninyi kama mponyaji wa kiungu. Ninakuja kama ndugu

yenu. Siji kupachukua mahali pa daktari wenu. Ninakuja kuwaombea ninyi kwa ufunuo wa Kiungu, kanuni ya Kiungu ya Mungu. Karama na miito ya Mungu haina majuto. Madakatari ni watumishi wa Mungu nao wanafanya yote wawezayo kwa ajili yetu. Bali nguvu zao na maarifa vina kikomo. Nguvu za Mungu hazina kikomo. Kama madaktari na manesi hawakuhitajika, wasingekuwapo hapa. Wao ni msaada mkubwa kwetu. Hakika ninathamini yale manesi wamefanya kwa ajili ya wagonjwa na walio dhaifu katika mikutano hii. Mungu na awabariki ninyi nyote, madaktari na manesi pia. Msichana wangu mdogo, ambaye nilimwacha nyumbani nipate kuja kwenu, anataka kuwa nesi, na endapo mwanangu hatakuwa mhudumu ningependa awe daktari.

Watu wengi wanasema wanajua Mungu anaweza, bali je! Yeye yuko radhi? Katika Zaburi 103, kuponywa kwa magonjwa kumewekwa katika daraja lile lile kama msamaha wa maovu ama dhambi. Na kwa hiyo kama ni mapenzi ya Mungu kusamehe dhambi, ni mapenzi Yake kuponya magonjwa.

Ninataka kuombea leso hizi. Hizi hapa mamia ya barua. Kila mwezi ninapokea maelfu ya hizo kutoka kote duniani na mambo makubwa yametukia. Hii ni kulingana na Biblia, Matendo 19. Paulo alijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani yake, na laiti tu ungalitambua Mungu yuko ndani yako. Sasa, iweni na kicho ninapoomba.

Baba mwenye rehema, leso hizi zilizopo hapa kwenye makasha haya na viti, ninakuomba katika jina la Mwanao Yesu, uzibariki. Huko kote nchini kuna akina mama na akina baba na watoto, wakingojea leso hizi zirudishwe. Wengi ni wagonjwa sana, nami ninawaombea, Baba mpenzi. Kuna maskini baba fulani mzee anayeketi nyumbani ambaye ni kipofu, mama fulani aliyelala kitandani akiugua, akingojea leso hizi zirudi. Imeandikwa katika Maandiko ya kwamba leso na aproni zilitolewa kwenye mwili uliotiwa mafuta wa Mt. Paulo, na magonjwa na pepo wachafu wakawatoka hao watu. Baba, tunajua sisi si Mt. Paulo bali Wewe ungali ni Yesu yeye yule, uliyekuwa pamoja na Mt. Paulo na watu Wako wote. Ee, Mungu, wafanyie hivyo tena, ili watu wapate kujua Wewe ni Yesu, Mwana wa Mungu, yeye yule jana, leo na hata milele.

Umekuwa mwema sana kwetu, Baba wa Mbinguni, na wakati unapita upesi sana wakati tukizungumza habari za Yesu, tukizungumza habari za kazi Zake za ajabu. Wakati alipokuwa hapa duniani Yeye alisema bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Bali ulimwengu haufahamu. Wamepofushwa na mungu wa dunia hii, wakitembea katika giza katika njia yao wenyewe na katika tamaa zao wenyewe

chafu za dhambi. Lakini tunakushukuru, Wewe umesema ya kwamba utakuwa pamoja nasi, hata kukaa ndani yetu hadi ukamilifu wa dahari.

Usiku wa leo, po pote unapoweza kupata moyo mnyenyekevu, Wewe utawaongoza kwa Roho Wako. Ee, Mungu, Jumamosi hii usiku wakati watu wengi wako madukani wakinunua bidhaa, wengi wako kwenye baa mitaani na nyumba za ufisadi, na vijana wanaume wamelala sakafuni kwenye baa, na vijana wanawake wakifuata njia ya upotovu—wakicheza dansi linalowaelekeza kwenye kaburi lisilo na Kristo, ee, Bwana, kwa namna fulani waongoze watu hao. Nena nao usiku wa leo na ujalie wapate nafasi kwenye madhabahu ya haki ya mtindo wa kale na wawe watumishi Wako, Bwana.

Kuna wengi hapa usiku wa leo, Baba, ambao ni wagonjwa na ni wahitaji. Ninamhisi Roho Wako sasa na sisi sote tunajua ya kwamba Wewe upo hapa. Ulisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao." Tunakuhisi, halisi kwa hisi ya kiroho, nasi tunajua ya kwamba Wewe upo hapa.

Na sasa, Baba, kama nilivyoshuhudia kwa watu hawa kuhusu karama Yako ya Kiungu, wao watakuwa wanalo neno langu tu Wewe usiponena, Bwana. Bali ninajua ya kwamba Wewe utanena, utathibitisha, utashuhudia, na sifa zote na utukufu ziwe Kwako, Ee Mwana wa Mungu uliye wa ajabu sana. Wewe u mwema sana kutukomboa sisi maskini wenye dhambi tuliopotea, tunaostahili kufa na kutengwa, tunaostahili kwenda kuzimu, lakini Wewe umetukomboa. Loo, jinsi moyo wangu unavyoruka ninapofikiri kwamba nimekombolewa na kwa hakika tu kama Wewe ulivyofufuka kutoka kaburini, siku moja tutafufuka tukiwa na mwili mpya na hatutakuwa wagonjwa wala kuteseka tena.

Sasa, Mungu mpenzi, wabariki usiku wa leo wale waliopo hapa. Jalia Roho Mtakatifu atende kazi tu moja kwa moja huku kwa wasikilizaji hawa sasa. Jalia wakukubali Wewe kwa furaha na waokolewe na kuponywa usiku wa leo, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Mwanao, Yesu. Amina.

Nileteeni mgonjwa wa kwanza.

Habari za jioni, mama. Sasa, dada, je! unaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu amenituma kukusaidia? Sina kitu cha kuponya nacho. Kama ningalikuwa daktari, ningekupa dawa. Mimi ni mtumishi wa Mungu na kwa njia hiyo ninaweza tu kuvuvia imani yako ili kwamba Mungu aweze kukusaidia. Mimi siwezi kufanya yale ambayo Mungu amekwisha kufanya. Mimi ni nabii na ninaweza tu kukwambia kwa ono kwamba una shida gani. Kama ninaweza kukwambia sasa una shida gani, je! utaamini ya kwamba Mungu alinituma?

Kabla hujakuja kwenye mkutano usiku wa leo ulikuwa kwenye maombi. Hilo ni kweli? Uliomba ya kwamba upate kuitwa usiku wa leo. Umekuwa na maumivu makali ya kichwa kwa muda mrefu. Je! unaamini kwa moyo wako wote? Basi, nenda zako nyumbani na ukubali kuponywa kwako.

Njoo, kijana. Je! unampenda Yesu? Roho wa Mungu tayari yuko juu ya mtoto huyu. Kama Yesu angalikuwa amesimama kwenye jukwaa hili na angelikwambia, ewe mvulana mdogo, kwamba una shida ya mambo fulani machache, je! ungemwamini? Sasa, kama nikikwambia, je! utaamini ya kwamba Mungu alinituma? Mimi ni chombo tu cha Mungu. Ninaona ono la maskini mvulana huyu mbele yangu. Unaumwa na vidonda vya mdomo. Ni kweli? Kama ni kweli, inua mkono wako. Nenda nyumbani ukifurahi, kwa kuwa Mungu amekuponya.

U hali gani, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Una kasichana kazuri sana. Nina msichana mdogo nyumbani, mdogo tu kidogo kuliko wewe. Jina lake ni Rebeka. Bali ilinibidi nimwache maskini Rebeka kusudi nije hapa kukuombea.

Kama Yesu, Mwana wa Mungu, angalikuwapo hapa, unajua Yeye anawapenda tu watoto wadogo, angewachukua mikononi Mwake na kuwabariki. Yeye alisema, "Waacheni watoto wadogo, wala msiwazuie; kuja kwangu: kwa maana watoto kama hao ufalme wa mbinguni ni wao." Kama Yesu angalikuwa yupo hapa usiku wa leo, Yeye angekubariki. Angeweka mikono Yake juu yako na angejua shida yako ni nini. Unaamini hilo? Unaamini ya kwamba Yesu anaweza kumwonyesha Ndugu Branham kwamba una shida gani? Ninafikiri wewe ni msichana mdogo mzuri sana.

Mama, mtoto wako amezaliwa katika hali hii. Ni ugonjwa wa neva. Ugonjwa huo umemfanya mtoto wako kuwa mnyonge na kukosa nguvu. Hali ya mwili wake mzima ni mbaya sana. Zaidi sana si matatizo ya sehemu za mwili bali ni hali ya kudhoofika kwa jumla kwa mtoto huyu. Msichana huyu ni mlegevu, hali vizuri na sikuzote ana mafua makali, sivyo? Hilo si ni kweli?

Sasa, unajua ya kwamba mambo yote hutenda kazi kwa manufaa ya wale wampendao Mungu. Ninataka kukuuliza jambo fulani. Unampenda sana msichana huyu kuliko maisha yenyewe. Je! utaahidi ya kwamba kama Mungu atamponya mtoto huyu na kumpa afya, utamlea, si kama msichana wa kisasa, bali utamlea kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwamba Mungu ataweka maisha yake mikononi Mwake? Je! utamfundisha kuifuata njia hiyo na wewe

mwenyewe uishi vivyo hivyo na uwe mfano mbele yake wa mwaminio wa kweli kabisa, aliyejazwa na Roho wa Mungu? Je! utafanya hivyo? Yale niliyokwambia juu ya mtoto huyu, hayo ni kweli? Sasa, ninaamini kuna matumaini kwa mtoto huyu. Mungu ananena nyumbani mwenu. Unafahamu ninalomaanisha, sivyo? Hata kabla sijasema jambo hilo, ulijua. Nililihisi likijidhihirisha, kwa hiyo sina haja ya kulisema. Nenda ukamtumikie Mungu maishani mwako mwote. Ninataka kumbariki maskini mtoto wako. Njoo hapa, kipenzi. Nikumbatie kwa mikono yako.

Mwenyezi Mungu, Mwanzilishi wa uhai, Mpaji wa kila kipawa chema. Maskini msichana huyu mdogo, anayesimama hapa akiniangalia kwa macho yake bluu ya kitoto kichanga, ananifanya nimkumbuke maskini Rebeka wangu, maili elfu nyingi ng'ambo ya bahari.

Mungu, mrehemu maskini mtoto huyu. Yasikie maombi ya mtumishi Wako, Baba. Ulisikia ahadi ya mpendwa huyu. Umeonyesha ono, Nawe unajua mambo yote. Na anaposimama usiku wa leo huku mwili wake mdogo umeegemezwa kwangu, jalia iwe kama katika siku ya Eliya wakati alipoulaza mwili wake juu ya mtoto aliyekufa na akafufuka. Jalia afya na nguvu zimjie msichana huyu mdogo. Jalia mafua na magonjwa yaishe katika mwili wa mtoto huyu na jalia asije akasahau usiku huu kamwe. Jalia hii iwe ndiyo siku muhimu ya mabadiliko ambapo baraka za Mungu zitakuwa juu ya mtoto huyu. Jalia akutumikie siku zake zote, na wapendwa wake vivyo hivyo. Ninambariki mtoto huyu mdogo mimi kama nabii Wako, katika Jina la Mwanao mbarikiwa, Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Kipenzi, usiogope sasa. Utakuwa mzima. Hizo homa na mambo mengine yatakoma. Mungu akubariki, mpenzi.

Huyu hapa mama mmoja amesimama nisiyejua lo lote kumhusu, bali Baba yangu anamjua Naye anaweza kunishushia sehemu yo yote ya maarifa Yake. Amini kwa moyo wako wote nawe umeponywa. Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

(Aliwageukia wasikilizaji.) Ninamwona mwanamume mmoja amesimama pale akiwa anaumwa. Ninaona una shida gani, bali siwezi kukuponya, bwana. Je! unaamini ya kwamba Yesu Kristo anaweza kukuponya? Kama nitaweza kusema shida yako ni nini, basi unapaswa kuamini. Sivyo? Una shida ya henia mbili. Kama hiyo ni kweli, inua tu mkono wako. Sasa, kama unaamini, unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Mungu akubariki. Mwamini Mungu. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

Ni jambo la fahari kusimama hapa na kuona jinsi Bwana wetu anavyotembea katika kusanyiko hili. Kuna

mwanamume mwingine aliye na henia. Angependa kuponywa, pia. Sivyo, bwana? Kama ukiamini, unaweza kuponywa. Uwe tu na imani kwa Mungu. Endelea kuamini. Yeye anaweza kukuponya.

Huyo ni mke wako anayeketi karibu na wewe, huyo mama hapo. Unaamini ninaweza kukwambia una shida gani, mama? Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Unaamini? Vema, una presha ya juu ya damu, sivyo? Hilo si ni kweli? Kama utaamini kwa moyo wako wote unaweza kwenda nyumbani ukawe mzima. Mungu akubariki.

(Aliwageukia watu walio kwenye mstari wa maombi.) Vema, mama, njoo. Unaamini kwa moyo wako wote? Je! unaamini ya kwamba Yesu Kristo yupo hapa kukufanya mzima? Ninaona shida yako ni nini na ni jambo ambalo laiti lisingalitukia. Lakini hicho ndicho kitu cha kwanza ambacho Mungu aliahidi kuponya, kifua kikuu. Sivyo? Hebu njoo hapa dakika moja. Ugonjwa huu mbaya sana, yapata miaka kumi na tano iliyopita, ulimwondoa mama yake Billy duniani. Hiyo ilikuwa ni kabla ya karama hii kudhihirishwa kwangu. Sikuzote nimeidharau T.B. Mungu na anipe nguvu usiku wa leo kukuweka huru kutokana na huu.

Ee, Baba, turehemu, Mungu. Baba, kama ninajua jinsi ya kuwa mwaminifu, niko hivyo sasa. Baba, ninakuomba kwa moyo wangu wote, yasikie maombi yangu na unipe imani ninapoingia kwenye mkondo huu kukabiliana na pepo huyu, ambaye vinginevyo atampeleka maskini mwanamke huyu kaburini mapema. Turehemu, Mungu, na umtoe kwake. Mpe mtumishi Wako nguvu na neema na imani sasa hivi, ninapokwenda kukabiliana na adui huyu mbaya sana.

Sasa, ewe pepo unayeitwa kifua kikuu, ninakuja katika vita hivi vya imani ya watu wawili na kukupa changamoto, nikidai karama ya uponyaji wa Kiungu niliyopewa na malaika. Unajua jambo hilo. Toka kwa mwanamke huyu. Mwache katika jina la Yesu Kristo. Mtoke apate kuishi.

Dada yangu, mimi ni mgeni tu kwako bali wewe fanya kama ninavyokwambia. Je! utafanya hivyo? Siku moja barua ya kutoka ng'ambo ya bahari itakuja kwangu ikisema, "Ndugu Branham, niko huru sasa na kifua kikuu." Nenda zako toka hapa ukiwa na furaha, ukishangilia, ukila cho chote uwezacho kula, nawe utaanza kuongezeka uzito na kupata afya. Mungu akubariki. Niandikie ushuhuda wako uutume Marekani.

Mgonjwa mwingine, tafadhali.

Yupo malaika wa Bwana aliyepo hapa pamoja nasi. Shetani atajaribu kukufanya usiamini, bali malaika

wa Bwana anataka wewe uamini. Msimamo wako ndio utakaokuwa ni njia yako ya kuikabili shida hii. Endelea kuamini.

Uko tayari kwa kufanyiwa upasuaji. Kunapaswa kuwe na upasuaji unaoendelea sasa hivi. Shida iko kwenye tumbo lako, uvimbe ambao wanajiandaa kuuondoa. Je! nimesema kweli? Basi inua mkono wako. Je! unaamini ya kwamba utakuwa mzima? Mungu akubariki. Nenda ukishangilia, imani yako imekuponya. Bwana asifiwe.

Mama huyu anaumwa na kitu kile kile. Wewe amini kwa moyo wako wote. Mungu amekuponya. Nenda sasa. Hivyo ndivyo inapasa kuamini.

Una vidonda tumboni. Hiyo ni kweli? Unaweza kwenda nyumbani, utapona.

Kama Mungu atasema na mimi na kuniambia shida yako ni nini, je! utakubali uponyaji wako? Kisukari. Hilo ni kweli? Basi umefanya nini? Umekubali uponyaji wako, sivyo? Mungu akubariki. Hebu na tuseme Bwana asifiwe. Sasa, ndugu, nenda zako, na baada ya kitambo kidogo unapoendelea kwenda kwa daktari wako, atakupa ruhusa. Unaweza kutuandikia ushuhuda wako. Mungu akubariki.

U hali gani, bwana. Je! unaamini ya kwamba umepona sasa? Unaamini? Hakika, nenda nyumbani na ule cho chote unachotaka. Shida yako ya tumbo imekuacha. Mungu akubariki. Nenda zako nyumbani na ukale. Imekuwa muda mrefu tangu umeweza kula kile ulichotaka.

(Tena aliwageukia wasikilizaji.) Ninaona kitu fulani kikitembea moja kwa moja pale. Siwezi kufahamu ni kitu gani. Amini sasa kwa moyo wako wote. Loo, ingekuwaje kama sote tungeliamini!

Ewe mama unayeketi pale, ulikuwa na shida ya kike. Imekuacha. Hebu na tuseme Bwana asifiwe.

Ungetaka kuponywa uvimbe huo, sivyo, dada? Nenda zako nyumbani na uwe mzima. Mungu akubariki. Loo, Yeye si ni wa ajabu!

Nina hakika mnaweza kuthamini jambo hili kwa maana kuna karibu nafsi elfu tano zinazojaribu kuivuta Karama hii. Ni kama makasia, kupiga huku na huku. Ni vigumu kwangu kuchagua ipi, lakini ninajua ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo hapa kuwaponya. Aminini kwa moyo wenu wote.

Ewe kijana mwanamume, wewe uliyepo hapo karibu na ukuta, je! unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Je! unaamini ya kwamba tunasimama katika uwepo Wake

sasa? Sisomi mawazo yako. Unajua shida yako ni nini. Daima chakula ulacho kinapanda kooni. Unachoka sana, ni vigumu kwako kusimama. Una njaa moyoni mwako. Unataka kumtumikia Mungu. Hujapata kabisa kumtumikia jinsi ulivyotaka kumtumikia. Sivyo? Mkubali sasa kama Mwokozi wako, batizwa katika Roho Mtakatifu pia upate kuponywa.

Wewe pale, kwenye kile kiti chenye magurudumu. Mungu ameiponya hali yako ya ulemavu. Nenda zako nyumbani ukiamini na ukikiri yale Kristo amekutendea, nawe utaponywa kabisa. Utafurahia afya kamili.

Vema, mlete mgonjwa mwingine.

Njoo, mama. Je! unaamini kwa moyo wako wote? Yeye hajui Kiingereza. Mwambie tu ameponywa. Alikuwa na ugonjwa wa moyo. Mwambie aende zake nyumbani na kushangilia. Hawezi kuzungumza Kiingereza bali hakika anajua jinsi ya kuwa na imani.

Sogea hapa, bwana. Je! utanitii mimi kama nabii wa Mungu? Vema, umekuwa na yabisi kavu kwa muda mrefu, sivyo? Inua mikono yako hewani, chapua miguu yako. Ondoka jukwaani ukitembea. Yesu Kristo amekuponya. Mungu akubariki. Hebu na tuseme Bwana asifiwe.

Naam, dada, una wasiwasi kuhusu mgongo wako, sivyo? Vema, simama. Nyonganyonga mgongo wako huku na huko, inama. Yesu amekuponya shida hiyo ya mgongo. Hunayo tena. Amina!

Kwa ajili ya huyo mtoto mchanga?

Mungu, katika Jina la Bwana Yesu ninakuomba kwa ajili ya uponyaji huu. Jalia macho yake madogo yawe ya kawaida. Mwache, ewe Shetani. Ninakuapiza umwache mtoto huyu.

Amekuwa na makengeza kwa muda gani? Vema, hana makengeza sasa. Hayo macho yemenyoka kikamilifu na yako kawaida. Unaweza kwenda nyumbani sasa ukishangilia, bwana. Mtoto huyu mchanga amepona kabisa. Hebu na tuseme Mungu ashukuriwe. Mwangalieni mtoto huyu mchanga. Macho yake yamenyoka sawasawa kabisa. Semeni Bwana asifiwe.

(Aliwageukia wasikilizaji.) Ninawatakeni mwamini kwa moyo wenu wote na mwangalie upande huu. Mungu anataka kuwaponya na yote yawapasayo kufanya ni kulikubali jambo hilo, liaminini na Mungu anawajibika kulitimiza. Mnaweza kuona jinsi ilivyo rahisi?

Ninamwona mwanamume mmoja pale aliye na kansa ya tumbo. Amini kwa moyo wako wote. Amini tu.

Kila mtu aangalie upande huu na uamini kwa moyo wako wote. Yesu Kristo yupo hapa kuwaponya. Iweni tu na imani. Naam, dada, wewe unayeketi pale pembeni. Una wasiwasi, sivyo, jakamoyo, umejaa wasiwasi, sivyo? Simama kwa miguu yako. Yesu Kristo amekuponya. Amina! Haleluya!

Mtoto wako mchanga ana nafuu, sivyo, ndugu? Tayari anafanya tofauti na alivyokuwa, sivyo? Yesu alimponya usiku wa leo ibadani. Hebu na tuseme Bwana asifiwe.

Kila mtu anaweza kusikia vizuri huko nyuma? Mara nyingine wakati Upako unaposhuka juu yangu unaufanya uso wangu kufa ganzi kabisa. Msifikiri ya kwamba nina wasiwasi ninapousugua uso wangu, lakini mdomo wangu unahisi kana kwamba umenenepa sana. Ni hisi takatifu sana. Siwezi kuelezea jambo hilo. Ninampenda, ninajua jambo hilo. Ninampenda kwa moyo wangu wote.

Yupo mama mmoja anayeketi pale akiomba, akijitahidi tu kwa bidii zote. Wewe, dada, wewe hapo uliyevaa koti hilo jeusi. Angalia upande huu na uniamini kwa moyo wako wote. Unaamini? Unanikubali kama nabii wa Mungu? Vema, hii hapa shida yako, dada. Ninaona sasa. Kwa kweli huna shida sana. Umepagawa na pepo mtesi, hiyo ndiyo shida. Sivyo? Unahofu na kuchoka. Umejaa wasiwasi tu. Kama hilo ni kweli, inua mkono wako. Mungu ameyasikia maombi yako. Shetani hawezi kukushikilia. Sasa, inua tu mkono wako juu ninapoomba.

Bwana Mungu, tunapoona shida yake na nikijua ya kwamba maskini mwanamke huyu amefungwa, Shetani akijaribu kumwambia kwamba ameshindwa, ninakuja Kwako kuomba rehema. Kwa dakika chache zilizopita amekuwa akijaribu sana kuwasiliana na Wewe. Sasa, Baba, ninaomba roho huyo amwache mwanamke huyo katika Jina la Yesu Kristo. Jalia aondoke hapa akishangilia na mwenye furaha na akiwa mzima tena, kwa jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, dada, umemalizana na huo. Uko huru sasa. Uwe tu na imani na uamini kwa moyo wako wote.

Sasa, je! mnataka kuponywa huko mliko, ninyi nyote? Mnaamini kwa moyo wenu wote? Enyi marafiki, ningependa kukaa hapa saa moja zaidi ila nguvu zangu zinaisha upesi. Ni haya maono nami siwezi kuelezea. Tafadhali niaminini sasa. Kama mtafanya nitakavyowaomba mfanye, mtaenda zenu nyumbani usiku huu mkiwa wazima. Kama nikimchukua mmoja baada ya mwingine litakuwa ni jambo lile lile. Hakika, marafiki, mnajua nimesema kweli, na Mungu amethibitisha ya kwamba nimesema kweli. Yesu Kristo alimponya kila mtu yapata miaka 1900 iliyopita.

Ni wangapi wenu sasa walio na imani kumkubali Yeye kama Mponya wenu? Inueni mikono yenu. Hiyo ni kweli, hao walio kwenye vitanda hivyo vya wagonjwa na ninyi mnaoketi kwenye viti vyenu na kadhalika. Mnaweza kuponywa. Nimefanya yale malaika aliyoniambia nifanye. Alisema nifanye ishara kama vile nabii Musa alivyofanya. Kisha uombe na uwe mwaminifu unapoomba, wala hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako. Mnaamini jambo hilo? Basi inamisheni vichwa vyenu kwa muda kidogo tu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninakuomba kwa ajili ya rehema kwenye saa hii, rehema kwa ajili ya binadamu wote, na zaidi sana kwa ajili ya watu hawa waliopo hapa. Nimeshuhudia habari Zako, ee, Yehova mkuu, na za Mwanao mpendwa, Yesu, na Roho Mtakatifu amethibitisha ushuhuda wangu kwamba ni wa kweli. Na sasa, Baba, nimewaambia ya kwamba Mwanao alikufa kwa ajili ya uponyaji wao na malaika wa Bwana alikutana na mimi na kumtia mafuta mtumishi Wako aende na ujumbe huu. Shuka kwenye kusanyiko hili sasa. Jalia nguvu za uponyaji kutoka Kalvari, kutoka kwenye ile damu ya sadaka, mwili na mauti ya Bwana wetu Yesu, zimjie kila mgonjwa anayeisikia sauti yangu. Baba mpenzi, mbariki kila mmoja aliye katika maombi sasa, kila mmoja anayeamini ujumbe huu. Tujalie, Bwana. Sikia kilio changu kinyenyekevu kinachokujia Wewe. Ninaomba ya kwamba utajalia maombi yangu yajibiwe.

Katika jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninakemea kila pepo wa magonjwa, kila nguvu za pepo, kila nguvu zilizowafunga watu, viwete, wenye makengeza, vipofu, na wanaoteseka. Ewe Shetani, umeanikwa hadharani. Huwezi kuwashikilia watu hawa. Nguvu zako zimevunjwa. Yesu Kristo alikushinda pale Kalvari. Ninamwakilisha sasa katika karama ya Kiungu nawe umeanikwa hadharani na kuitwa utoke. Ninakuapisha kwa jina la Bwana wangu Yesu Kristo, ambaye itakulazimu kumtii, kwa kuwa ninaliitia Jina Lake kwa kicho na utakatifu juu ya watu hawa walio wagonjwa. Watoke wapate kuponywa kupitia Yesu Kristo, Mwana mpendwa wa Mungu. Amina.

Sasa, mnapoinamisha vichwa vyenu ninawatakeni mwamini tu ninaposema maneno haya. Ninajua kinachohitajika kumshinda Shetani nami nitasema maneno haya. Ninawataka myakariri kwa kuomba kutoka moyoni mwenu ninapoyanena. Hebu watu walio wagonjwa po pote katika kusanyiko hili sasa, wayakariri maneno haya kwa kuomba kutoka moyoni mwenu, nikiisha kuyasema.

Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa uzima wa milele, Mpaji wa kila kipawa chema, tuma baraka Zako za uponyaji juu yangu, maskini

mwanadamu anayeugua. Sasa ninakubali mauti ya Mwanao pale Kalvari, aliyekufa kwa ajili ya kuponywa kwangu. Kwa neema yako, Bwana, tangu usiku huu na kuendelea, nitashuhudia kuponywa kwangu. Imeandikwa ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu wa maungamo yangu, nami nitakiri uponyaji wangu mpaka nimekuwa mzima kabisa. Nisikie, ee, Bwana, kwa maana ninajikabidhi Kwako kwa ajili ya uponyaji wa mwili wangu, kukupa Wewe sifa katika jina la Mwanao mtakatifu, Yesu Kristo. Amina.

Taarifa Za Kutoka Afrika Kusini

Katika milango iliyotangulia mmetambulishwa kwa William Branham, huduma yake na karama ya uponyaji ambayo hutenda kazi kupitia kwake. Mmeambiwa jinsi ambavyo alielekezwa na Bwana kwenda Afrika Kusini. Kusudi mpate kuifahamu vizuri zaidi huduma yake, nimewapa ujumbe wake ulionakiliwa kwa umeme neno kwa neno katika ibada ya kweli ya kawaida ambapo anawaombea wagonjwa. Katika mlango huu ningependa kukupa taarifa fupi ya majuma kumi tuliyokaa huko Afrika Kusini.

Mikutano ya kidini iliyo mikubwa kuliko yote iliyopata kufanywa Afrika Kusini ilifanywa na William Branham na kikosi chake kwenye miezi ya Oktoba, Novemba na Desemba, 1951. Haya yalikuwa ni maoni ya pamoja ya kila mtu niliyezungumza naye kuhusu mikutano hii. Katika kuzungumza na wahudumu, wamishenari, maafisa wa serikali na watu wengine waliokuwa na shauku ya usitawi wa kiroho, kijamii na uadilifu wa watu, tulihakikishiwa ya kwamba matokeo ya mikutano hii yatadumu kwa miaka mingi ijayo.

Mamia ya maelfu walikusanyika pamoja huko nje, katika kumbi, viwanja vya maonyesho, uwanja wa ndege na hata kwenye uwanja wa mbio za farasi wakimtafuta Mungu. Makumi elfu wamemshukuru Mungu kwa ajili ya uponyaji wao. Baadhi yao waliponywa papo hapo, wengine walipokea uponyaji wao polepole. Wengine, baada ya kuhisi mguso wa Mungu, wangeweza kushuhudia ni wakati gani na ni mahali gani. Haiwezekani kuorodhesha njia mbalimbali ambazo watu walipokea uponyaji wao. Kulikuwa na mathalani wale walioondoka kwenda nyumbani na wakakuta magonjwa yao yametoweka. Kwa wengine, uponyaji wao ulikamilika barabarani, kwenye magari, kwenye mabasi na teksi. Na halafu kulikuwa na wale waliokwenda nyumbani wakiamini na wakatambua, walipofanyiwa uchunguzi na daktari, kwamba imani yao haikuwa bure.

Wale walioambatana na William Branham kwenda Afrika Kusini walikuwa ni W. J. Ern Baxter, meneja wa kikosi hicho, F. F. Bosworth, mkongwe katika huduma ya uponyaji wa Kiungu, Billy Paul, mwana wa William Branham, na mimi mwenyewe. Katika kipindi hicho cha majuma kumi ya kukaa huko, mikutano iliendeshwa kwenye miji kumi na moja iliyo mikubwa sana kukiweko na jumla ya ibada zaidi ya mia moja na ishirini na jumla ya watu wote waliohudhuria kwa pamoja ikiwa nusu milioni. Hakuna njia ya kujua ni makumi elfu wangapi waliosimama na kutia sahihi kadi za kukata shauri

kwa ajili ya wokovu wa mtu binafsi wala kujua ni elfu ngapi walioko ambao leo hii wanafurahia afya njema kwa sababu ya uamsho huu.



Picha imepigwa na J. J. Wesselo, Johannesburg

Hii ni picha ya Kikosi cha Branham na wanachama wa Komiti ya Taifa iliyohusika na matayarisho yote kuhusu ule uamsho.
Safu ya mbele: *A. W. Preller, F. F. Bosworth, A. J. Schoeman, William Branham, W. F. Mullan na W. J. Ern Baxter.*
Safu ya kati: *H. C. Phillips, D. Freeman, G. Vermeulen, J. H. Saayman na Billy Paul Branham.*
Safu ya nyuma: *ED Pettenger, E. King, J.W. Gillingham na Julius Stadsklev.*

Kikosi cha Branham kilifanya ibada katika miji kumi na moja. Taarifa ndefu ingeweza kuandikwa juu ya mikutano hiyo katika mji wo wote kati ya miji hii, bali haiwezekani kuelezea kwa utondoti. Si jambo la lazima, kwa sababu mengi ya mambo ya ajabu yaliyofanyika yalitukia tena na tena katika mikutano mbalimbali kote katika Muungano huu.

Tumejaribu kuandika ripoti zote kwa usahihi iwezekanavyo. Kama kumekuwako na sababu yo yote ya kutilia shaka kuhusiana na usahihi wa taarifa yo yote, hiyo imeondolewa. Ni afadhali tufanye makadirio ya chini kuliko kukadiria kupita kiasi umati wa watu, idadi ya wanaopokea wokovu, uponyaji, na mahudhurio ya mikutano hiyo kwa jumla. Hesabu hiyo imetolewa tu ili kwamba uweze kuelewa vizuri zaidi na kukisia matokeo yaliyoletwa na mikutano hii kwa Afrika Kusini. Katika nafasi ya kurasa hizi chache sitaweza hata kidogo kuingiza ndani shuhuda zote, taarifa za kuvutia na kila kitu. Nitaweza tu kuwapa taarifa za

mikutano hii kwa uwakilishi, kuwasaidia kufahamu yale yaliyotukia katika uponyaji wa kimiujiza wa mwili na nafsi kulikoshuhudiwa usiku baada ya usiku.

Isingewezekana kutoa taarifa kamili juu ya mikutano hii huko Afrika Kusini bila kwanza kutaja ushirika mzuri sana wa kusifika tuliopokea kutoka kwa Jeshi la Polisi la Afrika Kusini, wafanya kazi wa Msalaba Mwekundu, wafanyakazi wa Gari la Wagonjwa wa St. Johns na manesi. Kamwe hatujapata kuona kundi la watu walioshirikiana sana kwa moyo na walikuwa ni wenye msaada sana. Ibada baada ya ibada wengi wao walifanya kazi bila malipo yo yote ya kifedha. Ingawa hatukupata nafasi ya kuwashukuru wote mmoja mmoja, hata hivyo tulithamini kila kitu walichotenda na tunataka sasa kuwashukuru kwa moyo.

Ni wazi kwamba, ufanisi mkubwa wa mikutano hiyo ulikuwa kwa sehemu kubwa ni kwa sababu ya uaminifu wa wakristo—wachungaji, wamishenari, wafanyakazi, na walei—waliosimama nyuma ya Kikosi cha Branham katika maombi na imani. Uamsho wa Afrika Kusini ulidhaminiwa na Apostolic Faith Mission, Assemblies of God, Pentecostal Holiness, na Full Gospel Church of God. Kasisi A. J. Schoeman alikuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa na Kasisi W. F. Mullan alikuwa ndiye Katibu wa Taifa. Wakristo wengi na wachungaji wa madhehebu mengine walihudhuria mikutano hiyo, wakashirikiana, na wakashiriki katika baraka ambazo Mungu alizitoa bure kwa wale walioamini.

Afrika Kusini ni nchi inayopendeza sana, nchi yenye tofauti zinazoshangaza. Kwa mfano, jiji la Johannesburg ni jiji la kisasa tu kama miji mingi ya Marekani. Kadiri ya maili sabini ama themanini kutoka nje ya jiji hili na kuingia vijijini unaweza kuingia kwa gari katika maeneo ya wananchi ambako wananchi wanaishi vile wamekuwa wakiishi kwa vizazi na vizazi, kwenye vibanda vyao vidogo.

Masetla wa kwanza Wazungu wa Afrika Kusini, Waholanzi wafanyabiashara, walilowea kwenye Ghuba ya Tumaini Jema. Mapambano yao hayakukabiliwa na mazingira ya maumbile bali na Bushmen na Wahotentoti. Baadaye wakimbizi wa Huguenots wa Kifaransa wakawasili wakitafuta usalama. Katika mwaka wa 1688 mia mbili wao ambao walikuwa wamefukuzwa kwa nguvu kuingia Uholanzi, walihamia Afrika Kusini. Hadi kufikia mwaka wa 1795, Waingereza walianza kulowea kule. Hivyo basi, kulikuwa na mapambano kati ya Wazungu na pia vita vya umwagikaji mwingi wa damu walivyopigana na makabila ya wenyeji. Ndipo ikaanza ile "safari kuu ya kuhamia kaskazini," ambayo iliwaleta masetla kwenye eneo la kaskazini mwa Afrika Kusini. Haya yote yanaifanya historia ya Afrika Kusini ya kuvutia. Afrika Kusini iliendelea kuwa koloni la Uholanzi hadi mwaka wa 1902, wakati ilipokabidhiwa kwa Waingereza kutokana na Vita vya Makaburu.

Huku kuielewa picha ya nyuma ya Afrika Kusini kunamwezesha mtu kuwafahamu watu wake na kutambua ya kwamba Afrika Kusini si mfano halisi wa bara la giza, ambayo ni sehemu ya bara hilo. Shirikisho la Afrika Kusini lina idadi ya Wazungu zaidi ya 3,000,000 na wasio Wazungu ni 10,000,000. Ilisimama kwenye nafasi muhimu katika vile Vita viwili vya Dunia.

Tulikuwa kabisa tumepanga kuondoka Uwanja wa Kimataifa wa New York tarehe moja Oktoba, 1951, tufike Johannesburg tarehe tatu. Tulipokuwa kwenye uwanja wa ndege tukiwa tayari kupanda ndege, tulisikia ya kwamba William Branham na Billy Paul wasingeweza kwenda, kwa sababu ya ushauri mpotovu, viza zao hazikuwa zimekamilika. Hivyo basi, W. J. Ern Baxter, F. F. Bosworth na mimi mwenyewe tukaondoka bila wao.



W. J. Ern Baxter, William Branham,
Billy Paul Branham, F. F. Bosworth na Julius Stadsklev

Watu wa Afrika Kusini walivunjika moyo pakubwa sana tulipofika Johannesburg nao wakasikia kwamba Ndugu Branham na mwanawe Billy hawakuja. Magazeti ya Johannesburg yalitangaza ya kwamba watu zaidi ya 4,000 tayari walikuwa wameanza kumiminika Johannesburg ili wamwone. Mamia ya watu walikuwa wamesongamana kwenye Uwanja wa Ndege wa Palmietfontein ngaa wapate kumtupia jicho, huyu Mwinjilisti wa Marekani ambaye alikuwa amemwona malaika kwenye mwaka wa 1946 na ambaye alitarajiwa kuwasili humo kwa ziara ya miezi miwili kote katika Shirikisho hili.

Tulipokuwa tunaingia Johannesburg mara moja tulitambua kile hao abiria wengine waliokuwa kwenye ndege walichomaanisha walipolitaja kama "Jiji la Dhahabu," kwa maana karibu na jiji hilo na chini yake ilikuwako migodi ya dhahabu iliyo mikubwa kuliko yote duniani. Si Johannesburg

peke yake tu bali uchumi wa Afrika Kusini nzima umesimama juu ya mwamba wa dhahabu. Katika muda wa zaidi kidogo ya nusu karne, Johannesburg likiwa na idadi ya watu 603,470, limekuwa ndilo jiji kubwa kuliko yote katika Afrika Kusini.

Mikutano ya kwanza ya uamsho wa Afrika Kusini ilifanyikia katika Maskani ya Kati huko Johannesburg. Ingawa hili ni moja ya makanisa yaliyo makubwa kuliko yote jijini, watu walianza kukusanyika saa moja asubuhi kwa ajili ya ibada ya alasiri. Muda mrefu kabla ya wakati wa ibada ya alasiri, jengo hilo lilikuwa limejaa watu. Mikutano ya jioni ilifanyikia kwenye Maskani ya Uwanja wa Maranatha kwa sababu hapakuwapo na jumba la mikutano katika jiji la Johannesburg lililokuwa kubwa kutosha kuuchukua umati wa watu, ambao ulikuwa ni zaidi ya watu elfu kumi kwa wastani kila jioni.

Ibada ya jioni katika Bustani ya Maskani ya Maranatha iliyo kwenye maeneo ya Misheni ya Imani ya Mitume

Katika mkutano wa kwanza wa alasiri, Ndugu Baxter alileta ujumbe juu ya kweli za uponyaji wa Kiungu. Aliwaelezea vifungu vya Maandiko ambavyo vilimwonyesha mtu ye yote mwaminifu ya kwamba Kristo hakufa tu kwa ajili ya dhambi zetu bali pia alilipia kuponywa kwa miili yetu.

Mtu mmoja kutoka Pretoria kwenye ibada hii ya kwanza alifikia uamuzi ya kwamba kama mambo haya yalikuwa ni ya kweli, ambayo hayana budi kuwa kwa kuwa yalitoka moja kwa moja kwenye Neno la Mungu, yeye angeenda nyumbani na kudai kuponywa kwa mwili wake kama jinsi alivyokuwa amedai kuponywa kwa nafsi yake, kulingana na ahadi za Mungu. Alifanya jambo hilo. Baada ya siku kadhaa alienda kwa daktari akafanyiwe uchunguzi, ambao ulionyesha ya kwamba hapakuwapo na dalili ya kansa iliyoonekana ambayo alikuwa nayo.

Ukweli wa kuponya Kiungu ulipata ardhi yenye rotuba katika mioyo ya watu wa Afrika Kusini. Ukweli huu haukuwa mgeni kwao. Andrew Murray, mmoja wa waandishi mashuhuri

sana juu ya suala la uponyaji wa Kiungu, alikuwa ni Mwafrika Kusini na katika wakati wa maisha yake alikuwa ndiye kiongozi wa Dutch Reformed Church. Kanisa la Kiingereza pia linaamini na kufanya huduma hiyo kwa kiwango fulani, ya kuombea wagonjwa. Misheni ya Imani ya Kimitume, huduma ya Kipentekoste iliyo kubwa sana katika Afrika Kusini, ilianzishwa na John G. Lake, ambaye maisha yake yalipata ushawishi mkubwa sana kutokana na huduma ya Ndugu F. F. Bosworth. Pamoja na msingi huu wa dini shamba lilikuwa tayari kwa ajili ya kuvunwa.



Sanamu ya ukumbusho wa Andrew Murray, mbele ya kanisa ambamo aliwahudumia watu wake.

Ndugu Baxter na Ndugu Bosworth waliendesha mikutano mpaka Oktoba 6, ambapo Ndugu Branham na Billy Paul waliwasili kutoka Marekani. Walitarajiwa kufika saa kumi na moja lakini ndege yao ilichelewa wala haikuwasili mpaka saa tatu na dakika chache.

Walipitishwa haraka kwenye ofisi ya forodha, na kupelekwa kwenye Maskani huko kwenye Bustani ya Maranatha kusudi wafunge mkutano wa jioni hiyo. Ndugu Branham alizungumza kwa dakika chache tu halafu akafunga mkutano kwa maombi kwa ajili ya wote wale waliohitaji uponyaji. Tuna shuhuda za watu waliopokea uponyaji wao usiku huo wa kwanza. Miongoni mwao ni Ernest Blom aliyekuwa ametoka Durban kwa gari apate kuhudhuria mikutano hiyo huko Johannesburg. Majuma kadhaa baada ya kurudi nyumbani alihojiwa na ripota wa gazeti la Durban Sunday Tribune, ambalo liliripoti habari hizo katika makala ya tarehe 11 Novemba, mwaka wa 1951.

Siku zilizofuata zilikuwa ni siku za matarajio makuu nasi tuliona mambo ambayo Afrika Kusini haijapata kuona hapo kabla. Kama ilivyokwisha kutajwa, haiwezekani kuorodhesha uponyaji wote na matukio ya ajabu sana yaliyotukia kwenye mikutano hii, lakini ningetaka kuwasimulia baadhi ya matukio ambayo ninayakumbuka vizuri sana.

'MIRACLE' SETS BOY WALKING NORMALLY

(Sunday Tribune Reporter)

A FAITH cure, described by his mother as a "miracle," has enabled 16-year-old Ernest Blom, of Eastview Road, Red Hill, Durban, formerly a cripple, to walk normally for the first time in his life.

Last Sunday evening, Ernest astounded a packed congregation of more than 500 people at the Full Gospel Church in Beatrice Street, Durban, by rising from his seat and walking without the slightest difficulty to the pulpit to testify that "a miracle happened and I am now completely cured."

Excited groups of people gathered outside the church later to watch Ernest walking and to congratulate him on his recovery.

His mother, Mrs. Mary S. Blom, said: "Ernest is the youngest of my family of 10. When he started to walk, I noticed that his left leg was shorter than his right. He could only walk on the tips of his toes, and had to drag his left foot.

WENT TO HEALER

"From the age of four until a month ago, he was under the care of a specialist. For two years he wore a leg iron without any noticeable improvement. The specialist latterly suggested an operation, but said he could not guarantee that it would be a success, so I gave up the idea.

"I heard of Pastor William Branham's remarkable faith-healing successes in the States. When my daughter and a friend heard he was to visit Johannesburg they motored from Durban three weeks ago and took Ernest along. They attended his opening meeting in the Mafanatha Park Hall, at which 15,000 people were present."

Ernest himself here took up his story. He said: "I was right at the back of the hall. Pastor Branham asked all the people wanting to be cured to lay hands on each other. I laid my hands on those of a man sitting beside me. Pastor Branham said, 'I will pray for you.'

"WEIRD SENSATION"

"I experienced a weird sensation. It was just like cold water running through my body. I began to cry. My sister said, 'Are you healed, Ernest?' I replied, 'Yes, I am sure I am healed.'

"Because of the huge crowd I could not move, but as I was being helped from the back of the hall I kept repeating, 'I am sure I am healed.'

"Pastor Branham said: 'All you people who are healed, will you come forward.' I was assisted to the sick bay by others. He told me to walk up and down the platform on which he was standing.

"URGED ON"

"I broke into a sweat but something urged me on, and I managed to walk normally across the platform and back.

"When I got back to Durban and my school friends at Hunt Road School saw me walking into the classroom, they were flabbergasted.

"My left leg is getting stronger every day. I can now play cricket and other games."

Jioni moja hapo Johannesburg wakati Ndugu Branham alipokuwa akizungumza na mtu fulani jukwaani kwenye mstari wa maombi, upesi aliwageukia wasikilizaji na akaelekeza kidole kwa mama mmoja kijana aliyekuwa amelala kwenye kitanda cha wagonjwa. Akasema, "Mama, mgongo wako umevunjika kwenye sehemu tatu mbalimbali kutokana na kuanguka. Yesu Kristo amekufanya mzima. Simama na ukubali uponyaji wako." Bibi huyo alipigwa na bumbuazi, lakini kwa imani akasimama na kumsifu Mungu kwa ajili ya uponyaji aliokuwa ameupokea mara moja. Kesho yake jioni aliitwa aje ashuhudie kuhusu kuponywa kwake na wakati huo tukampiga picha, Bibi Ann Weiblen, pamoja na Ndugu Branham, Kasisi A. J. Schoeman na Billy Paul.

Jioni hiyo hiyo msichana mdogo mwenye umri wa kama miaka kumi na minne alibebwa kwenye kitanda cha wagonjwa na wafanyakazi wa Msalaba Mwekundu. Yeye pia mgongo wake ulikuwa umevunjika na alikuwa analia kwa sababu ya

Picha imepigwa na Wesselo

maumivu makali aliyokuwa akisikia. Mkutano ulipokuwa ukiendelea, Ndugu Branham alimwelekezea kidole na kusema, "Mgongo wako umevunjika. Yesu Kristo ndio kwanza akuponye. Simama na ukubali uponyaji wako." Mwanzoni msichana huyo hakuweza kuamini yale aliyokuwa amesikia. Akasema, "Ati nani, mimi?" Ndugu Branham akasema, "Ndio, wewe." Aliposikia hayo, akasimama. Mama yake alikuwa ameketi kwenye kiti karibu na hicho kitanda cha wagonjwa na wakati huyo msichana alipoamka mama yake akasimama pia. Alikuwa amejaa furaha sana hata akazimia na kuanguka kwenye kitanda ambacho msichana huyo ndio kwanza aamke. Tuna picha yao pia ambayo ilipigwa sekunde chache tu kabla mama huyo hajazirai.

Baada ya ibada msichana huyo alitembea-tembea akishangilia uponyaji huo ambao ndio kwanza apokee. Nilimwuliza jinsi mgongo wake ulivyokuwa umevunjika naye akasema ilitukia katika ajali ya gari yapata mwaka mmoja uliopita. Nilipomwuliza alikuwa ametembea kiasi gani tangu alipopata ajali hiyo alijibu ya kwamba hajasimama kwa miguu yake tangu wakati wa ajali hiyo mpaka usiku ambao Ndugu Branham alimwelekezea kidole na kumwambia aamke na kudai uponyaji wake.

Matukio haya mawili ya kuponya yalikuwa ni ya kuvutia sana kwa sababu yalionyesha usahihi wa maneno ya Ndugu Branham yaliyonenwa chini ya upako. Kama Ndugu Branham angalifanya kosa na kuwaambia ya kwamba Kristo alikuwa amewaponya wakati hawakuwa wamepona, ingekuwa ni balaa. Hakuna mtu aliyevunjika mgongo angeweza kuamka kwenye kitanda chake na kutembea isipokuwa awe alikuwa

Picha imepigwa na Wesselo

ameponywa. Kwanza huenda asingeweza kusogea na kama alisogea, huenda angekatika baadhi ya neva jambo ambalo lingeweza kusababisha kifo cha mara moja.

Tukio lingine lisilo la kawaida kabisa liliwapata Wazee wawili kutoka Kanisa la Dutch Reformed. Walikuwa wamekuja kwenye mikutano hiyo na kuchunguza. Mmoja wao, wakati alipomsikia Ndugu Branham akibaini magonjwa, akiwaambia watu shida yao ilikuwa ni nini, na halafu wakati akiwa anashuhudia miujiza ikifanyika, alishawishika ya kwamba ilikuwa ni ya Mungu. Huyo Mzee mwingine aliketi pale na pia akamchunguza Ndugu Branham akifichua magonjwa, akiwaambia watu mambo ya siri za moyo wao na kwamba katika jina la Yesu walikuwa wameponywa na wangeweza kuamka na kwenda nyumbani wakidai na kufurahi katika kuponywa kwao. Yeye alishawishika kwamba ilitokana na nguvu za pepo. Watu hao wawili walikuwa waaminifu bali walifikia maamuzi tofauti. Mzee wa kwanza alienda zake nyumbani; huyo wa pili akaenda chini ya mti kuomba. Alipokuwa hapo anaomba alimwomba Mungu amwonyeshe kama mambo haya aliyokuwa ameona yalikuwa ni ya Mungu

ama ni ya Shetani. Alikuwa ni mwaminifu na akakubali kuamini lo lote atakalofunuliwa na Mungu. Alipokuwa akiomba, alisikia mkono kwenye bega lake. Akageuka aone ilikuwa ni nani, bali hapakuwa na mtu. Badala ya kuona mtu, yeye aliona ono. Aliona mawingu mawili, na kati ya mawingu hayo aliketi yule Mzee rafiki yake jinsi vile hasa alivyokuwa ameketi muda kidogo uliopita wakati walipokuwa wakizungumza juu ya huduma ya Ndugu Branham. Mwisho wa hilo ono alikwenda haraka alivyoweza nyumbani kwa yule Mzee kumwambia yale yaliyokuwa yametukia. Wakati alipokuwa akimwelezea lile ono, watu wengine wa familia hiyo waliokuwa hapo wakaona chapa ya mkono juu ya shati lake. Walipoliangalia hilo shati kwa makini, waliona lilikuwa limetiwa alama kwa moto, waziwazi ikiacha alama ya mkono wa kushoto. Habari hizo zikamfikia Ndugu Branham juu ya jambo lililotukia naye akasema, "Ninajua habari zote hizo. Nililiona jambo hilo kwenye ono alasiri ya leo. Nileteeni shati hilo na mkono wangu wa kushoto utaenea kikamilifu kwenye chapa hiyo ya moto iliyoachwa juu ya shati hilo." Jambo hili lilitekelezwa na ilikuwa kama vile Ndugu Branham alivyokuwa amesema. Jioni hiyo hilo shati lililetwa mkutanoni na mamia wakaona chapa ya mkono iliyochapwa kwa moto kwenye shati.

Jioni moja wakati Ndugu Branham alipoagiza mstari wa maombi upangwe, tuliona kwamba moja ya namba zilizoitwa haikuwako. Billy Paul alikuwa amesambaza kadi za maombi mapema kwenye ibada hiyo hiyo kwa hiyo tukaona hakika kwamba mtu yule aliyekuwa na namba hiyo alikuwa yuko. Ndugu Branham aliwaomba watu wote waliokuwa na kadi kuchunguza namba zao tena na kama walikuwa na namba hiyo inayokosekana waje mbele tafadhali. Basi mama mmoja alisimama akaeleza kwamba alikuwa na namba hiyo. Lakini, hapo kwanza alipoipokea kadi ya maombi alisikia kitu fulani kikipita mwilini mwake. Ilikuwa ni kama mshtuo wa umeme, ila tu ni mdogo kidogo bali ni wa kudumu muda mrefu zaidi. Alikuwa na kansa mdomoni mwake ambayo daima ilikuwa ikimuuma. Baada ya mhemuko huu kama mshtuo, yale maumivu yalikuwa yameondoka. Alijisikia ameponywa na kwa hiyo hapakuwapo na haja ya yeye kwenda kwenye mstari wa maombi.

Mzee mmoja wa Dutch Reformed aliingia kwenye mstari kusudi aombewe. Baada ya kumwombea, Ndugu Branham alimwambia ya kwamba alikuwa amekwisha pokea uponyaji wake na angeweza kwenda nyumbani akimsifu Mungu. Akasema pia, "Una mke nyumbani anayeugua kansa. Unaweza kufurahia kwa maana yeye pia amepona." Baadaye wakati mtu huyu alipokaribia nyumbani kwake aliona ya kwamba taa zote nyumbani zilikuwa zinawaka na magari machache yalikuwa hapo nje. Kwa namna fulani alichanganyikiwa,



Kasisi William Branham pamoja na Kasisi A. J. Schoeman, Mwenyekiti wa Taifa, ambaye alikuwa akitafsiri ujumbe katika lugha ya Kiafrikana.

Picha imepigwa na J.J. Wesselo

akishangaa ni kitu gani kilichokuwa kinatendeka. Alipoingia nyumbani alimwona mkewe ametoka kitandani, akijisikia vizuri, na akimshukuru Mungu kwa kumponya mwili wake. Alikuwa amewaita baadhi ya marafiki zake wakati aliposikia alikuwa ameponywa, nao walikuwa wamekuja. Wote pamoja wakashangilia katika uponyaji ambao hao wawili walikuwa wameupata.

Katika mkutano mwingine huko Johannesburg mvulana mmoja mdogo mwenye umri wa miaka kama saba ama nane aliitwa kwenye mstari wa maombi. Ndugu Branham aliongea na mvulana huyo kwa muda wa dakika chache akielezea ya kwamba huo moyo mdhaifu aliokuwa nao ulisababishwa na mateso ya pepo. Akamwambia ya kwamba atawekwa huru na siku moja atakuwa akihubiri Injili ile ile iliyokuwa wakati huu inaletewa watu wa Afrika Kusini. Mara Ndugu Branham akawageukia wasikilizaji na katika kipindi cha dakika chache zilizofuata za kimya ilikuwa ni dhahiri ya kwamba alikuwa akiona ono la kitu fulani juu ya wasikilizaji. Ndipo akaelekeza kidole chake moja kwa moja juu ya mimbara na kusema ya kwamba kulikuwako pia na msichana mdogo na mvulana mwingine huko kati yao waliokuwa wana ugonjwa ule ule. Kila mtu aliona wasiwasi wakati alipokuwa akielekeza kidole chake mahali alipojua walikokuwa, bali asingeweza kuwapata. Dakika zilipokuwa zinapita, alisisitiza ya kwamba walikuwako. Alisema ya kwamba roho huyo aliyekuwa akimfunga mvulana huyu alikuwa akiomba msaada toka kwa pepo wengine kama yeye katika kusanyiko hilo. Aliendelea kuangalia bali asingeweza kuwapata. Ndugu Baxter akajitokeza toka nyuma yake na kwa kuweka mkono wake juu ya mgongo wa Ndugu Branham alimfanya asogee mbele. Alipofanya hivi, Ndugu Branham alisogea karibu zaidi na mimbara na hapo aliweza kuwaona hao ambao walikuwa kidogo tu mbele yake. Hao hapo wale wawili aliokuwa akiwatafuta, mvulana mwenye umri wa miaka kama kumi na

miwili na msichana mwenye umri mdogo kwa miaka michache kuliko wake. Wote wawili walikuwa wamelala kwenye vitanda vya wagonjwa nao walikuwa wamekingwa asiwaone kwa sababu ya mimbara. Akawaombea na kuwaambia ya kwamba walikuwa wamekombolewa kutokana na pepo ambaye alikuwa akiufanya moyo wao kuwa mdhaifu. Alikuwa ameona ono la hao wote watatu wakipona. Baadaye nilimhoji mama wa huyo mvulana aliyekuwa amelala kitandani. Akaniambia ya kwamba mvulana wake alikuwa katika hali ambayo asingeweza kuketi kwa zaidi ya dakika kumi kwa siku moja.



Ndugu Baxer pamoja na Justus du Plesis ambaye alikuwa mkalimani wa mara kwa mara wa lugha ya Kiafrikana.

Huduma ya Ndugu Branham siyo ya kawaida kabisa na kama vile Ndugu Bosworth alivyotukumbusha mara nyingi hapajakuwapo na kitu cho chote cha kufanana nayo tangu wakati Kristo alipokuwa hapa duniani. Mungu amekuwa mwema kwa watu Wake na mara kwa mara ametupa waonaji na manabii, lakini kadiri tunavyoweza kuona katika kumbukumbu za historia hapajakuwapo na mtu mwingine ye yote aliye na huduma kama ya Ndugu Branham. Mara nyingi angeona kati ya maono thelathini na arobaini kwa siku na wala kamwe hapajakuwapo na lo lote la hayo lililokosea. Mara nyingi angeshuhudia maono ya ibada zijazo kabla ya wakati wake ama matukio yatakayotukia siku za usoni. Mara nyingine angetwambia habari za matukio haya kabla kwa kweli hayajatukia na ndipo tulipoyaona tungekumbushwa yale aliyokuwa ametwambia.

Baadaye kidogo baada ya sisi kuwasili Johannesburg, Ndugu Branham aliona ono ya kwamba kesho yake yeye, Ndugu Schoeman na baadhi ya wengineo wangeshuka mjini. Wangemwona mwenyeji mmoja amesimama pembeni amevaa shati la bluu na surali nyeupe. Ndugu Branham alimwelezea alivyokuwa huyo mwananchi, hata akaelezea hiyo kona na majengo ambapo huyo mwananchi alikuwa amesimama karibu nayo. Kesho yake walishuka wakaenda mjini na Ndugu Branham akawaelezea ono hilo wale waliokuwa pamoja naye. Walipokuwa wakitembea katikati ya mji, walipiga kona fulani na hapo moja kwa moja mbele yao alisimama mwananchi

huyo, amevaa jinsi ile ile hasa Ndugu Branham aliyokuwa amemwelezea habari zake. Mazingira, pia, yalikuwa vile vile hasa alivyokuwa amesema.

F. F. Bosworth, mzee wa siku nyingi katika huduma ya uponyaji wa Kiungu.

Siku moja Ndugu Branham aliona katika ono msichana mwananchi aliyekuwa na paji pana sana la uso lenye kovu. Alikuwa ameketi chini akiangalia ardhini kana kwamba alikuwa akifanya kitu fulani kwa mikono yake. Ndugu Branham akasimulia ono hili kwa wengine na siku chache baadaye walikuwa wametoka matembezini wakiendesha gari na mara huyo hapo yule msichana ameketi kando ya barabara akiuza shanga. Hakuna mtu mwingine kwenye gari kwa mara ya kwanza aliyemtambua huyo msichana kuwa ndiye ambaye Ndugu Branham alikuwa amemwona katika ono. Baada ya wao kuendesha gari kwa kama nusu maili, Ndugu Branham aliwaomba kama wangesimama na kugeuka kwa sababu alikuwa anataka kumwona msichana huyu aliyekuwa ameketi hapo kando ya barabara, akitengeneza na kuuza hizi shanga. Walirudi nyuma wakasimama kuangalia baadhi ya hizo shanga. Mara tu walipokuwa wako tayari kwenda Ndugu Branham akasema, "Je! hakuna mtu anayemtambua msichana huyu?" Walipomwangalia walimtambua kuwa ni yule msichana ambaye Ndugu Branham alikuwa amewaambia habari zake, akiwa ameketi ardhini, akiangalia chini kana kwamba alikuwa akifanya jambo fulani kwa mikono yake. Huyo msichana alipoangalia juu wao pia waliona uso wake mpana na lile kovu.

Ndugu Branham akiwahudumia wananchi akiwa na wakalimani watatu.

Jioni ya kwanza Ndugu Branham aliyokuwa katika nyumba ya Ndugu Schoeman, Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa, alipata ono la kitu kilichokuwa kimempata binti wa Ndugu Schoeman. Alikuwa amefanyiwa upasuaji kwenye jicho lake. Ndugu Branham akaelezea huo upasuaji kama vile ulivyotukia hasa. Ndugu Schoeman akathibitisha kila kitu kilichokuwa kimesemwa; ilikuwa tu ni vivyo hivyo kabisa kama ilivyokuwa imetukia.

Baada ya kumalizia juma zima la mikutano huko Johannesburg, tulisafiri kwenda Klerksdorp kwa magari. Huu ni mji mwingine wa uchimbaji wa madini yapata maili mia moja kusini magharibi mwa Johannesburg. Ibada ya kwanza kule ilisitishwa kwa sababu ya mvua na ya pili ilisimamishwa kwa sababu ya dhoruba ya upepo mwingi na baridi. Jumapili asubuhi Mungu alinena na Ndugu Branham kwa ono, akimhakikishia ya kwamba tungekuwa na hali nzuri ya hewa katika vipindi vya mikutano iliyosalia ya Afrika Kusini. Mikutano hii miwili ndiyo tu iliyositishwa kwa sababu ya hali ya hewa kote katika ziara hiyo yote ya Afrika Kusini, hata ingawa baadhi ya mikutano ilifanyika katika miji iliyokuwa na misimu yao ya mvua.

Jumapili, tarehe 14 Oktoba, ilikuwa ni siku ya kupendeza. Watu walisafiri kwa magari kutoka mania ya maili kuja mikutanoni. Niliambiwa na watu wengi wa mijini ya kwamba hilo lilikuwa ndilo kundi kubwa kupita yote lililopata kukusanyika kwenye jiji la Klerksdorp. Ndugu Baxter alileta ujumbe wa Injili jioni hiyo na wakati alipowaomba hao ambao wangependa kusimama na kwa jinsi hiyo basi kuonyesha kumkubali kwao Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana

wao, takriban watu elfu tatu walisimama kujibu wito huo. Kwa kuwa watu katika mji huu pia walishuhudia nguvu za Bwana za kutenda maajabu, kupitia Ndugu Branham, wao pia walikubali ya kwamba nabii kutoka katika nchi nyingine alikuwa akiwazuru. Walitambua ya kwamba labda hawataona tena kitu cho chote kama hiki maishani mwao. Jumapili ilikuwa ni moja ya siku kuu kuliko zote ambazo Klerksdorp uliwahi kuona. Kulikuwa na watu wengi waliopokea uponyaji kwa ajli ya mwili wao na nafsi pia.

Ninamwazia yule mvulana mdogo aliyekuwa na umri wa miaka kumi na moja ama kumi na mbili aliyekuwa amepokea kadi ya maombi na ambaye namba yake ilikuwa imeitwa. Alipokuwa anakuja jukwaani niliona ya kwamba macho yake yalikuwa na makengeza mabaya sana. Mara Ndugu Branham alipomwona, alisimulia hadithi ya maskini mtoto wake wa kike ambaye macho yake yalikuwa na makengeza kwa sababu ya maumivu makali aliyoumwa muda mfupi kabla ya kufa kwake. Ndugu Branham kamwe hakosi kuingiwa na huruma anapoona mtoto mdogo mwenye macho yenye makengeza. Alimwombea mvulana huyo na kisha akamwambia aangalie juu. Alipofanya hivyo, macho yake yakanyoka. Huyo mvulana aliwageukia wasikilizaji na hao watu wakashangilia kwa kuwa macho yaliyokuwa na makengeza sasa yalikuwa ni mazuri kabisa. Daktari wa sehemu hiyo alimfanyia huyo mvulana uchunguzi na kusema kwamba macho yake yamerudi kuwa kawaida. Baada ya ibada nilipata picha ya mvulana huyo ambayo tunayo hapa.

Jioni moja baada ya ibada baadhi yetu tulikuwa tumeketi kwenye meza ya chumba cha kulia chakula nyumbani kwa Mchungaji P. F. Fourie, mmoja wa wachungaji wa mahali hapo. Tulikuwa tukifurahia vinywaji naye Ndugu Branham alikuwa akituzungumzia juu ya kweli za kiroho. Baada ya Bibi Fourie kuja na kujiunga nasi mezani, niliona ya kwamba Ndugu Branham alikuwa akimwangalia kila mmoja wetu kwa makini sana, kana kwamba alikuwa akitafuta kitu fulani. Mnamo dakika chache akaketi kwenye kiti chake na kutwambia ya kwamba alikuwa ameona ono alasiri hiyo. Sasa tulikuwa tumeketi mezani kama tu alivyokuwa ametuona. Ndugu Bosworth aliketi mwishoni mwa meza, Mchungaji na Bibi Fourie upande wa pili wa meza kuelekeana, na mimi pamoja na Sidney Smith tulikuwa upande wa pili kutoka kwa Ndugu Branham. Kila mmoja wetu alikuwa kwenye sehemu na mahali hasa ambapo alikuwa ametuona katika ono alasiri hiyo. Sasa angeweza kutuambia yale ambayo Mungu alikuwa amemfunulia. Akamgeukia Bibi Fourie na kumwelezea matukio fulani tangu ujana wake. Alipoelezea kwa utondoti, Bibi Fourie aliketi pale amechangamka kuwazia ya kwamba Mungu alikuwa amesema na nabii Wake kumhusu yeye. Pia



Wakati mmoja macho yake yalikuwa na makengeza, sasa yamepona.

alimwambia ya kwamba alikuwa na ugonjwa wa moyo na maumivu ya tumbo ambayo yalisababishwa na wasiwasi. Baada ya kuzungumza zaidi kuhusu ono hilo na kumfariji, aliomba ruhusa aondoke mezani akapumzike usiku huo.

Kituo chetu kilichofuata kilikuwa toka tarehe 17 hadi 21 Oktoba, huko Kimberley, mji mkuu wa almasi ulimwenguni. Mikutano kule ilipangiwa kufanyikia kwenye Ukumbi wa Mji, lakini wakati wa ibada ya kwanza ya jioni jengo hilo lilijaa watu na hata kulikuwako na watu wengi zaidi waliokuwa huko nje kuliko waliokuwa ndani. Kamati ya mahali hapo iliona kwamba jambo fulani linapaswa kufanyika kusudi maelfu ya watu waliotaka kuhudhuria mikutano hiyo washughulikiwe. Kwa ushirikiano mzuri wa viwanda vya kuchimba madini tulipata ruhusa ya kutumia Uwanja wa Michezo wa De Beers, ambao uliweza kuketi kama watu elfu sita na unahesabiwa kama mmoja wa viwanja vizuri sana vya michezo Afrika Kusini. Umilele tu ndio utakaoonyesha yale yaliyofanikishwa kwa sababu ya vifaa vilivyoongezewa.

Wakati Ndugu Bosworth alipokuwa anakula kwenye mgahawa mmoja wa mahali hapo, kijana mmoja mwanamume alikuja na kumwuliza kama yeye alikuwa ni mmoja wa washiriki wa Kikosi cha Branham. Alimwambia ya kwamba alikuwa ametoka Kusini-magharibi ya Afrika na ya kwamba binti yake mwenye umri wa miaka mitano alikuwa anakufa kwa kansa. Alimwuliza Ndugu Bosworth

kitu gani kingewezekana kufanyika ili mtoto wake aweze kupata uponyaji ambao alitambua kwamba Kristo alikuwa ameununua. Ndugu Bosworth akamwelezea ya kwamba ingawa huenda asiweze kupata kadi ya maombi, bado angeweza kupata uponyaji. Alimshauri adumu katika maombi kwamba Mungu angempa Ndugu Branham ono la mtoto wake aliyekuwa akiugua kansa. Mtu huyo akaja mkutanoni akimwamini Mungu. Wakati alipokuwa amesimama kando, akiomba, Ndugu Branham alimgeukia na kusema, "Nenda zako nyumbani; kama unaweza kuamini, mtoto wako ambaye yuko nyumbani akiwa anaumwa na kansa atakuwa mzima." Baadaye, nilimwuliza Ndugu Branham alichokuwa ameona kumhusu mtu huyu, naye akaniambia alikuwa ameona ono la msichana mmoja mdogo amelala kitandani, anaumwa kansa. Duara ya nuru iliyokuwa ikining'inia papo hapo juu ya mtu huyu ilionyesha ya kwamba huyo alikuwa ni mtoto wa mtu huyo.

Sidney Smith wa Durban, aliyekuwa akisafiri pamoja nasi wakati huu, alinisimulia tukio la kuvutia sana. Bw. Smith alikuwa ndio kwanza apaki kwenye nyumba alimokuwa akikaa Ndugu Branham apate kumleta kwenye ibada. Alipotoka kwenye lango aingie barabarani, alikutana na mtu aliyekonda sana ambaye alimtambua Ndugu Branham naye akamsihi amwombee. Mtu huyo alikunja mikono yake ya shati kuonyesha jinsi mikono yake ilivyokuwa myembamba; haikuwa mikubwa zaidi ya ukubwa wa kifundo cha mkono wa mtu. Ndugu Branham alimwangalia na kusema, "Unaugua TB. Je! unamwamini Mungu?" Mtu huyo akasema, "Ninamwamini Mungu." Ndugu Branham akamwombea na akazungumza naye kwa dakika



Picha ilipigwa na Howard Shaw

Mungu anamfunulia mtumishi Wake mambo ya siri za mioyo ya wanadamu.

chache, baada ya hapo akasema, "Hebu tuone mkono wako tena." Wakati huu wakati mtu huyo alipokunja mikono yake ya shati, alishangaa sana kuona ya kwamba mkono wake ulikuwa umekuwa mkubwa na sasa ulionekana una nguvu kuliko ulivyokuwa dakika chache kabla. Hiki kilikuwa ni kisa ambapo Mungu hakumponya tu mtu huyo papo hapo, bali alimpa nguvu za kimwili kimiujiza ambazo kwa kawaida zingemrudia polepole.

Katika kila mji ambako tulifanya mikutano, watu wangetusimamisha mitaani kutwambia matukio ya uponyaji ambao walikuwa wamepata ama wamesikia. Sikumbuki mji wo wote ambao tulikutana na watu wengi sana wakitutolea taarifa za mambo ambayo Mungu alikuwa amewatendea kupitia huduma ya Ndugu Branham kama ilivyokuwa huko Kimberley.

Tulipata changamsho nyingi za furaha katika ziara yetu ya Afrika Kusini. Tuliona watu wakisimama kwa maelfu kumkubali Kristo kama Mwokozi wao. Viwete waliponywa, vipofu waliona, viziwi walisikia, bubu waliongea, mlemavu aliinuliwa kutoka kwenye kitanda chake cha wagonjwa, na wale waliokuwa wakisikia maumivu waliwekwa huru. Bali kamwe hatutasahau ile furaha ya kuwasikia wananchi na machotara wakiimba. Huenda sauti zao hazikuwa zimefunzwa bali ilionekana kwamba yote iliyowabidi kufanya ni kufungua vinywa vyao na muziki ungetoka. Mtetemo wa ajabu jinsi gani wa mfululizo wa sauti, mrekebisho wa uzito wa sauti kama huo ulikuwa unafurahisha kusikia. Ninakumbuka huko Kimberley zaidi ya sauti 6,000 zilichanganyika pamoja na kutoa muziki kama wa kinanda kikubwa mno, zikivumisha nyimbo za waliowekwa huru.

Kuimba huku kungemvuvia mtu ye yote na kumfanya ainue moyo wake katika kumwabudu Mungu. Wakati sifa kwa Mungu zilipokuwa zinaimbwa na Neno likaletwa kwenye mioyo ya watu, wanaume na wanawake walizishika ahadi za Mungu. Wengine walifanyika viumbe vipya katika Kristo Yesu. Wengine waliohitaji uponyaji wa kimwili waliinuka katika imani wakimwamini Mungu, na wakapokea uponyaji kwa ajili ya miili yao.

Baada ya moja ya ibada hizo mtu mmoja alinijia na kusema ya kwamba alikuwa amemwona malaika wa Bwana amesimama jukwaani kando ya Ndugu Branham. Nilimwambia atoe maelezo ya sifa za malaika huyo kwa maana wengine walikuwa wamemwona na kutoa sifa zake nami nilitaka kujua kama sifa hizo zilikuwa ndio zizo hizo ama zinatofautiana. Alisema ya kwamba alikuwa ni mtu mkubwa, karibu ukubwa wa Ndugu Baxter, amenyoa ndevu na amevaa vazi jeupe likiwa na matamvua ya dhahabu upindoni. Alisimama moja kwa moja nyuma ya Ndugu Branham alipokuwa akiwaangalia wasikilizaji, akiona maono ya watu wakiponywa na kuwaelekezea kidole, akiwatia moyo kusimama na kukubali uponyaji wao.

Kwenye mmoja wa mikutano iliyofanywa kwa wasio Wazungu, Mhindi mmoja alikuja kwenye mstari wa maombi. Ndugu Branham alimwangalia na kusema, "Wewe si Mkristo. Unaumwa kansa na vidonda. Hujawahi kamwe kumkubali Kristo kama Mwokozi wako. Kristo atakuponya, bali inakubidi kwanza umkubali kama Mwokozi na Bwana wako. Kisha uondoke uende ukawaambie watu wako yale aliyokufanyia na ndipo uponyaji wako utakamilika." Akasema, "Kama utafanya hivyo, inua mkono wako wa kuume." Akainua mkono wake wa kuume. Akamwita mmoja wa wafanyakazi wake akamchukue bibi huyu na kumwongoza kwa Kristo ili kwamba apate kutimiza nadhiri aliyokuwa ametoa.

Mfululizo wa mikutano iliyofuata ilifanywa huko Bloemfontein, Oktoba 24 mpaka 28. Neno Bloemfontein linamaanisha chemchemi ya maua. Ni mji wa kupendeza sana pamoja na bustani zake, maua na barabara pana. Tulipowasili mjini hapo, Kikosi cha Branham kilikaribishwa na kundi kubwa la watu na kwaya mchanganyiko ikiimba "Amini Tu." Ndugu Bosworth aliwaambia watu ya kwamba wangeona kitu ambacho hakuna mtu aliyewahi kukiona tangu wakati ambao Kristo alikuwapo hapa duniani. Hakuna wakati kamwe hapo nyuma katika historia ya kanisa ambapo Mungu amekuja kutenda kazi kwa njia hii. Jinsi hili lilivyokuwa ni la kweli kwa maana Mungu kweli alitenda kazi katika jiji la Bloemfontein kuliko alivyowahi kutenda wakati uliopita. Maelfu ya watu walikuwa wamekuja toka maili nyingi. Nilimhoji mtu mmoja ambaye alikuwa ameruka kwa ndege kutoka Afrika ya Kaskazini, karibu maili elfu nne. Niliambiwa na afisa wa polisi ya kwamba walikisia zaidi ya magari elfu moja yaliyotokea nje ya mji yalikuwa yamo humo Bloemfontein. Pia hapakuwapo na jumba la mikutano

Kwaya ya Kamati Karibishi ambayo ilitulaki kwenye vitongoji vya hilo jiji.

kubwa la kutosha kukaa umati wa watu uliotarajiwa. Kamati ya mjini hapo ilikuwa imefanya matayarisho ya kutumia Viwanja vya Fair, ambavyo viliketi watu 6,000. Usiku huo wa kwanza kabisa viwanja hivyo vilijaa maelfu waliokalia viti na mabenchi karibu sana na jukwaa ilivyowezekana.

Ndugu Bosworth alihubiri jumbe juu ya uponyaji wa Kiungu. Kwa kuwa maelfu wangekusanyika hapo kwenye Viwanja vya Fair kabla ya saa kumi na mbili, mara nyingi ibada zingeanza wakati huo. Yeye angeelezea kweli za uponyaji wa Kiungu kama zilivyoelezewa kwenye Biblia na kuelezea jinsi ambavyo Mungu alikuwa akitenda kazi kupitia Ndugu Branham. Ndugu Baxter angeleta jumbe za wokovu wa mtu binafsi. Kila wakati kulikuwako na mtokeo wa watu wengi sana kwa wito huu kwa wale waliotaka kuukubali wokovu ambao walinunuliwa huo pale Kalvari. Kulikuwa na jioni kadhaa ambapo zaidi ya kadi elfu mbili za kukata shauri zilijazwa na kurudishwa. Wanaume na wanawake wasingeweza kuitikia kwa wingi kama huo, au kwa idadi yoyote, isipokuwa Roho wa Mungu alikuwapo na akasema nao. Je! Bloemfontein ama wo wote wa miji hiyo mingine ya Afrika Kusini ambayo ilipata baraka za huduma ya Ndugu Branham unaweza kuendelea vivyo hivyo ulivyokuwa?



Kundi dogo la mahema yaliyopigwa kukalia baadhi ya watu waliotoka nje ya mji waliokuwa wamekuja kuhudhuria mikutano.

Kwenye mkutano wa Ijumaa jioni huko Bloemfontein, Ndugu Branham aliona ono la tofauti na lo lote alilopata kuona siku zilizopita. Alikuwa akiwaombea watu na wakati huo alikuwa akiwatia moyo kumwamini Mungu, kukubali uponyaji ambao Mungu alikuwa amewanunulia. Kristo alikuwa amekwisha kulipia uponyaji wao bali hakukuwako na njia ambapo Yeye angeweza kuwapa huo wasipouamini na kuukubali. Ndipo Ndugu Branham alipokuwa amesimama nyuma, akali akiwatia moyo kuamini, aliona ukuta mkubwa ukiinuka juu nyuma ya uwanja wa michezo, ukienea kukingama urefu wake wote. Ukuta huu ulipoendelea kuinuka ulikuja juu ya watu na matone makubwa ya maji yalionekana kama yanaudondokea. Matone haya ya maji yalipokuwa yakidondoka, daima yaligonga moja kwa moja juu ya kichwa cha mtu fulani. Ndugu Branham alikadiria ya

kwamba kulikuwako na matone kama 1500 kama hayo naye alishawishika ya kwamba watu hawa walikuwa wameponywa tayari, bali ilikuwa ni juu yao kuendelea katika imani yao kusudi wadumishe uponyaji huo. Alikadiria ya kwamba hakuna mkutano hata mmoja katika ile iliyotangulia ambapo watu wengi sana waliponywa kama walioponywa usiku huo hapo Bloemfontein.

Mara nyingi Ndugu Branham huwakumbusha watu ya kwamba hawezi kusema jambo lo lote ila lile alilofunuliwa na Bwana. Jioni moja bibi mmoja alikuja kwenye mstari wa maombi na baada ya Ndugu Branham kuona ono kumhusu huyo mama alimwambia awe na hakika kwamba amejiandaa kukutana na Mungu wake. Baada ya kuzungumza maneno ya kumfariji alimwambia amtumikie Mungu kwa moyo wake wote. Hakuna neno lililosemwa juu ya ugonjwa wake wala habari za kuponywa kwake.

Baada ya ibada tulimwuliza Ndugu Branham kwa nini alikuwa amezungumza na bibi huyo jinsi alivyozungumza. Alitwambia ya kwamba alikuwa ameona ono la mlolongo wa mazishi na kwamba mwanamke huyo angekufa muda si muda. Haidhuru angetaka jinsi gani kumwambia huyo bibi jambo lingine asingeweza kusema zaidi ya vile Bwana alivyokuwa amemwonyesha.

Kesho yake asubuhi tuliarifiwa ya kwamba bibi huyo alikuwa ameaga dunia usiku.

Sura nyingi kama hii zilikuwa ni za kawaida na mara nyingi ambalanzi zingerudi zikiwa ni tupu.

Ingawa karibu mikutano yote ilifanywa kwa ajili ya Wazungu, hata hivyo mikutano mitatu ilikuwa imepangwa kwa ajili ya wananchi. Mara kwa mara tuliweza kupenyeza kwa shida mikutano mingine michache ya wananchi kwenye ratiba iliyojaa tayari. Jumamosi alasiri Ndugu Bosworth alizungumza kwenye mkutano mmoja kama huo. Baada ya ujumbe wake aliwaita jukwaani watu kama kumi na wawili waliokuwa wamefanyiwa upasuaji hatari wa mfupa wa nyuma ya sikio. Watu hawa

walikuwa wameondolewa kiwambo kimoja cha sikio. Kusudi wao waweze kusikia kupitia kwenye sikio hilo, ingembidi Mungu awaumbie kiwambo kipya cha sikio. Hivyo Ndugu Bosworth aliwaita watu waliokuwa na sikio moja zuri ikiwa wao watakuwa wamekwisha kusikia Neno la Mungu na kwa hiyo walikuwa na imani ya kuamini kwa ajili ya uponyaji mkamilifu. Aliwatumia kama onyesho, kielezo cha ujumbe wake. Alikuwa amewaambia ya kwamba Mungu atawaponya kama wangeamini na sasa alikuwa amewaita watu kama kumi na wawili kuthibitisha jambo alilokuwa amesema. Aliwatumia wale waliokuwa na kasoro ya kusikia, hasa badala ya maradhi mengine, kwa sababu hicho kilikuwa ni kitu kilichokuwa kinaweza kusikika na kuonekana kwa wasikilizaji. Alijaribu kusikia kwao kwa kuwafanya waweke kidole chao kwenye sikio lao zuri na halafu kuwanong'oneza kwenye sikio ambalo limeondolewa kiwambo. Kila mmoja wao aliyemwombea aliweza kusikia. Baada ya onyesho hili aliwaongoza watu kwenye maombi ya jumla, akiwaambia waombe wakimfuatisha neno kwa neno. Walifanya jambo hili, na mamia walipokea uponyaji wao alasiri hiyo.

Hivyo msingi mzuri sana uliwekwa kwa ajili ya ibada Ndugu Branham alizofanya Jumapili asubuhi. Kwenye ibada hiyo ilikisiwa kulikuwa na umati wa watu wapatao 15,000 wasio Wazungu. Ulikuwa ni mkutano mkubwa kuliko yote wa ibada ya wasio Wazungu tulioshuhudia Afrika Kusini. Wananchi hao walitoka Basuto na bila shaka ufanisi mkubwa wa mkutano huo ulikuwa ni matokeo ya kupandwa kuzuri kwa Neno na wamishenari waliowahudumia wananchi hawa. Vilema wengi waliokuwa wamebebwa mkutanoni wakati wa kuingia walitoka wakitembea. Ninakumbuka kiwete mmoja aliyetembea kwa mikono yake na kukokota miguu yake lakini aliweza kutembea wima katika muda wa siku mbili. Kulikuwako na mtoto aliye na kichwa chenye maji aliyepona katika muda wa siku nne pamoja na uponyaji mwingine mwingi wa ajabu sana. Wamishenari kadhaa walinipa taarifa ya kwamba waliamini ya kwamba kulikuwako na kama watu elfu moja ambao walikuwa wameponywa katika ibada hii moja. Rafiki yetu mmoja mzuri, Mmishenari Kast, aliandika taarifa ya mikutano ya wananchi huko Bloemfontein nami nitanukuu taarifa hiyo kama alivyonipelekea.

MIKUTANO YA BRANHAM KWA AJILI YA WENYEJI HUKO BLOEMFONTEIN, TAREHE 27-28 OKTOBA, 1951

Imeandikwa na Mmishenari A. Kast

Kupitia gazeti la "Sauti ya Uponyaji," huduma ya Ndugu Branham na ya Ndugu Bosworth zilijulikana vizuri sana hapa

Picha Ilipigwa na Studio ya Oliver

Sehemu ya ibada ya Jumapili asubuhi ya wananchi huko Bloemfontein.

na kila jitihada ilifanywa kutangaza mikutano hii miwili muhimu kote katika Freestate na Basuto. Mabasi mengi yalikodishwa na pia mabehewa maalum kwenye njia zote za reli yalichukuliwa kuwaleta watu wengi wenye njaa na wanaoteseka kuja Bloemfontein. Kanisa la pili kwa ukubwa la Eneo hilo lilikodishwa kwa ajili ya mikutano hiyo wakati kumbi zingine sita kubwa zilitumika kwa malazi. Kwa miezi kadhaa, maombi mengi yalitumwa kwenye kiti cha enzi cha Mungu, ya kwamba mikutano hiyo ipate kuwa dhihirisho kubwa mno la nguvu za Mungu.

Mkutano wa kwanza ulikuwa uwe ni wa Jumamosi saa 8:30 alasiri, bali wengi waliwasili tayari siku mbili kabla, na Jumamosi yote asubuhi watu walilizunguka Kanisa hilo wakingojea kwa shauku kuingia jengoni. Kwa kuwa Kanisa hilo lingeweza tu kukaa watu 800, ni vipofu tu, viziwi, viwete, na wagonjwa kwenye machela waliruhusiwa kuingia ndani; ambapo maelfu mengi ilibidi wabaki nje. Milango ilifungwa, bali licha ya hilo wengine walijaribu kuingia Kanisani kupitia madirishani. Ndugu F. F. Bosworth alifika na alifurahiwa kuona kundi kubwa kama hilo likimsifu Mungu kwa nyimbo zao. Neno la Mungu lilihubiriwa na imani ilikuwa ikikua kufikia kiwango ambacho kila mtu alitarajia mambo makuu. Karibu watu thelathini waliokuwa wamepoteza kusikia kwao kwenye sikio moja kwa kufanyiwa upasuaji ama kwa maradhi waliitwa jukwaani nao waliombewa kibinafsi na Ndugu Bosworth. Katika kila kisa kusikia kulirejeshwa mara moja na wasikilizaji walishangazwa na mambo ambayo Mungu alikuwa amefanya kupitia mtumishi Wake mnyenyekevu. Wengine wengi walikuwa wametamani kuitwa jukwaani kusudi wapate kuombewa kwa kuwekewa mikono, bali Ndugu Bosworth alitoa tangazo hili thabiti: "Kila mmoja wenu anaweza kuponywa ugonjwa wo wote, kama tu mnaweza kuamini Neno la Mungu!" Aliahidi kuwaombea wote kwa wakati mmoja, akiwaomba wasikilizaji kurudia maombi yake. Hili lilifanyika na Mungu akatenda miujiza mikuu. Mara baada ya maombi, Ndugu Bosworth aliomba apewe shuhuda, na wengi walikuja kwenye maikrofoni kushuhudia juu ya nguvu za Mungu za uponyaji. Kila mtu alimsifu Mungu wakati mwanamke mmoja mzee aliposema: "Nilikuja mkutanoni nikiwa kipofu na kiziwi, bali sasa ninaweza kuona na kusikia." Walipoulizwa ni wangapi waliopokea uponyaji wa sikio, kulikuwako na 67 ndani ya Kanisa hilo na huko nje kulikuwako na wengi sana walioponywa hata wasingeweza kuhesabiwa. Kila mtu alimshukuru Mungu kwa yale yaliyofanywa, bado wakitarajia mambo mengi zaidi kesho yake wakati Ndugu Branham na Ndugu Baxter walipotarajiwa kuja.

Jumapili, Tarehe 28 Oktoba.

Siku ya kutosahaulika kamwe! Ikieleweka kwamba hakuna kanisa wala ukumbi wa umma ungaliweza kuenea umati uliotarajiwa, iliamuliwa mkutano ufanyike kwenye viwanja vya mpira. Asubuhi na mapema kazi ikaanza ya kuweka vipaza sauti na kutayarisha mahali pa kuhubiria. Mara nyingine tena saa nyingi kabla ya wakati wa ibada kuanza, maelfu yalitiririka kwenye viwanja hivyo. Wamishenari na wafanyakazi wa taifa

Billy Paul akigawa kadi ya maombi kwenye ibada ya wenyeji.

mara walipanga utaratibu wa kuuketisha umati wa watu sehemu sehemu na kuwaleta wagonjwa wote mbele. Mnamo saa 3:30 asubuhi tayari kulikuwa na watu wapatao 5,000 waliokusanyika. Tulianza kuimba na wale waliosikia upatano mtamu wa sauti hawatasahau kamwe sauti hiyo ya kimbinguni. Muda wa maombi ulipowadia, wanaume wote, wanawake, na watoto walipiga magoti chini wakiomba kwa pamoja wapate kuzuru kukuu kwa Mungu. Ilikuwa ni kilio Kwake na machozi yetu yalitiririka kwa urahisi, tukiona njaa ya kila moyo. Baada ya mahubiri mazuri ya injili yaliyoletwa na mmishenari mmoja, watu walihamasishwa kutarajia mambo makuu kutoka kwa Mungu. Waliambiwa ya kwamba halikuwa ni jambo la lazima kuombewa kibinafsi, bali mtu angeweza kupokea uponyaji akiwapo mahali po pote katika wasikilizaji. Ushuhuda wa yale Mungu aliyokwisha kufanya tayari katika vituo vingine ulitia nguvu imani ya hao waaminio.

Mnamo saa 4:30 asubuhi Ndugu Baxter na baadhi ya wengine waliwasili na ujumbe mfupi wa injili ulifuata

ukihubiriwa na mtumishi Wake aliyetiwa mafuta. Wakati wito ulipotolewa wa kujisalimisha kwa Kristo, maelfu ya mikono iliinuliwa na Mungu aliona kila mmoja wa hiyo. Ni wokovu mkuu jinsi gani! Hadi wakati huu, wote walikuwa wakimngojea Ndugu William Branham kwa shauku. Wakati mtumishi huyu mnyenyekevu wa Mungu alipofika, alijawa na huruma alipowaona viwete wengi wako mbele zake, lakini kwa uhakika wa imani alisema ya kwamba wengi wa hawa waliopatwa na balaa watakuwa wakitembea. Wananchi kumi waliitwa mbele na Ndugu Branham, kwa Roho wa Mungu, akamwambia kila mmoja maradhi yake na kisha akaomba kwa ajili ya uponyaji wao, ambao walipewa. Kufikia wakati huu idadi ya wasikilizaji ilikuwa imeongezeka ikafikia 12,000 na Ndugu Branham aliomba kwa bidii kwa ajili ya uponyaji wa kila mtu, akimwamuru Shetani awaache wanaoteseka katika Jina la Yesu Kristo. Mungu alisikia maombi hayo na akawaokoa wagonjwa. "Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa na Bwana atamwinua" (Yakobo 5:15).

Hakuna jicho lingeweza kuona yale Mungu aliyotenda katika muda huo mfupi sana mtakatifu. Hakukuwa na wakati wa kutoa shuhuda wakati wa ibada, lakini mtu mmoja alimwambia tu mwenziwe: "Nimeponywa. Ninaweza kuona. Ninaweza kutembea. Sina maumivu tena. Haleluya!" Hiyo ibada kuu ilifikia mwisho kwa wimbo wenye nguvu wa sifa.

Katika majuma yaliyotangulia mikutano hiyo, zaidi ya majina 4,000 ya watu yalipokelewa wakiomba waombewe. Vikapu viwili vilivyojaa barua vilipelekwa mikutanoni ambako Ndugu Branham aliziwekea mikono yake, akiomba uponyaji kwa ajili ya wagonjwa wasiojulikana. Majuma yaliyofuata tulisikia shuhuda nyingi kutoka kila sehemu ya nchi hii.



Ndugu Branham akizungumza na Albert Mokoma, mwananchi wa Basuto aliyeponywa TB huko Bloemfontein na sasa anahubiri Injili.

Kutoka kwenye Kituo hiki cha Misheni, "Mlima Tabor," Basuto, watu hamsini walihudhuria mikutano (maili 115) na isipokuwa kwa wachache, wote walirudi wakiwa wameponywa. Kutoka kwenye kijiji kingine, Thaba Tsoeu, watu ishirini na tatu walikwenda Bloemfontein na wakati tulipopatembelea mahali hapo, kumi na tano walishuhudia kupokea uponyaji. Tukienda kwenye kituo cha mbali zaidi, Mohaleshoek, tajiri wa basi, aliniambia: "Nilimbeba kiwete nikamwingiza kwenye basi, lakini aliporudi kutoka kwenye hiyo mikutano, aliweza kutembea mwenyewe." Wengine wengi waliponywa kiajabu kule. Mwinjilisti mmoja kutoka milima ya Basuto alituletea taarifa: "Karibu wote waliokwenda Bloemfontein wameponywa, mvulana mmoja bubu anazungumza sasa, mkono uliolemaa umeponywa, nk."

Tulipokuwa tunawasili huko Zastron, O.F.S., mamia walikuja hapo kwenye kanisa letu la mtaa kwa sababu ya yale Mungu aliyofanya huko Bloemfontein. Mtu mmoja kipofu alishuhudia ya kwamba anaona sasa na akasoma Biblia mbele zetu. Mwanamke aliyekuwa ameteseka kwa zaidi ya miaka ishirini wala asingeweza kufanya kazi yo yote ameponywa kabisa na anafanya kazi tangu siku hiyo. Wanawake wawili walishuhudia ya kwamba wasingeweza kutembea, bali sasa wanatembea. Karibu nusu ya wale waliohudhuria mikutano ya Branham kutoka kwenye mji huo waliponywa. Po pote tulipozuru, watu walitoa taarifa za uponyaji wa ajabu. Wengine waliandika barua wakisimulia juu ya kazi kuu za Mungu. Mwanamke mmoja aliyesafirishwa kwa ndege kutoka kwenye milima ya Basuto aliponywa kabisa kutokana na ugonjwa wa pumu na shinikizo kubwa la damu, na magonjwa mengine mengi. Hakuweza kufanya kazi yoyote kwa muda wa miaka kumi na miwili na sasa ni mzima. Mhudumu aliyepooza kutoka Kroonstad aliandika ya kwamba anaweza kutembea sasa bila ya mikongojo, na kwamba wafuasi wengine sita wa kanisa lake pia waliponywa.

Tunaamini ya kwamba watu wasiopungua elfu moja waliponywa wakati wa mikutano hiyo miwili, ambayo kwayo tunamsifu Mungu. Ingawa miezi mitatu imepita tangu wakati huo, haja za maombi zinatufikia kila juma. Zote zinazungumzia juu ya yale yaliyofanyika huko Bloemfontein nao wanaamini wao pia wanaweza kuponywa. Melfu hapa wanangojea kwa shauku na kuomba kwamba Kikosi cha Branham kirudi mapema Afrika Kusini.

****

Kutoka Bloemfontein tulisafiri pande za kusini magharibi kwa kama maili mia tisa mpaka Capetown. Capetown mara nyingi unachukuliwa kama Lango la Kuingilia Afrika. Kuanzishwa kwa ustaarabu wa kisasa katika Afrika Kusini

msingi wake ni Capetown ambao umejengwa chini ya Table Mountain. Palikuwa ndipo mahali hapo ambapo mwaka wa 1652 Jan van Riedeeck alianzisha kituo cha mbali cha kwanza kwenye njia ya biashara ya kwenda Indies ya Mashariki. Siku hizi ni jiji la kisasa lenye watu nusu milioni, bandari maarufu sana ulimwenguni, mji mkuu wa bunge la Jamhuri, na ulio maarufu sana kwa mandhari yake nzuri.

Mikutano kule ilifanyikia kwenye Uwanja wa Ndege wa Wingfield, unaoendeshwa shughuli zake na Shirika la Ndege la Afrika Kusini ambalo lilijitolea moja ya mabanda yake ya ndege bure. Kila ibada ilikuwa na watu elfu tano hadi elfu kumi waliohudhuria. Hapa tena kama kawaida viti vilijazwa

Picha ilipigwa na Staples

Banda la ndege No. 3 kwenye Uwanja wa Ndege wa Wingfield.

tele kwenye saa kumi na mbili jioni. Kwa hiyo, ibada mara nyingi zingeanza wakati huo, ikiwapa watu nafasi ya kusikia ujumbe kutoka kwa Ndugu Bosworth na Ndugu Baxter pia, pamoja na dhihirisho la Karama inayotenda kazi kupitia kwa William Branham.

Mikutano ya wasio Wazungu ilifanyikia kwenye Ukumbi wa Drill huko Capetown. Kwenye ibada moja iliyofanyika huko, watu hamsini na watatu walidai uwezo wao wa kuona uliongezeka sana ama ilithibitika wamerudia hali ya kawaida kabisa. Wengi wa hawa walikuwa hapo kabla ni vipofu kabisa.

Ibada ya Jumapili asubuhi, iliyofanywa kwa ajili ya wasio Wazungu, ilikuwa ianze saa 4, lakini watu walianza kukusanyika saa 7:30 usiku. Waliketi kwa saa kadhaa wakingojea ibada ianze. Ndipo wakati milango ilipofunguliwa sehemu ndogo tu ya hao

waliokuwa wamekusanyika huko nje waliweza kuingia ndani ya huo ukumbi ambao ulienea idadi ya watu chini ya elfu tatu. Kwenye ibada ya alasiri nilizungumza na maafisa kadhaa wa polisi ambao waliniambia ya kwamba kwa makadirio ya chini kabisa watu hamsini walikuwa wamezimia mchana wakingojea wapate kuingia kwenye ukumbi huo.

Baada ya mahubiri yaliyopewa kichwa cha habari "Jukumu na Kutiwa Moyo" maombi ya jumla yalifanyika kwa ajili ya wote wale waliohitaji uponyaji. Baada ya maombi tuliomba



Ukumbi wa Drill, Capetown, Africa Kusini.

tupewe shuhuda. Wengi walikuja mbele na kutoa ushuhuda kuhusu uponyaji waliokuwa wameupokea. Msichana mmoja aliyekuwa amebebwa akaingizwa humo Ukumbini alikuwa na kifundo cha mguu kilichovunjika ambacho kisingeweza kupona. Alipokea uponyaji wake, akatembea kuelekea jukwaani akiwa mzima kabisa, na akatoa ushuhuda wake.

Sehemu ndogo ya umati ambao haukuweza kuingia kwenye Ukumbi wa Drill.

Wengine walielezea jinsi walivyoweza kusikia vizuri zaidi. Wawili waliokuwa vipofu walishuhudia ya kwamba waliweza sasa kuona. Imani yao ilikuwa kubwa.

Ninakumbuka wakati wa kipindi cha ujumbe huo nilipokuwa nimeketi jukwaani nikiwaangalia watu na jinsi walivyoupokea ujumbe huo wa imani waliokuwa wakiletewa, nilimwona mama mmoja ambaye alikuwa ameketi kama futi thelathini ama arobaini mbele ya jukwaa. Alikuwa akiangalia mikono yake. Ungeweza kuona kwa hizo konzi kubwa na kilichoonekana kama kukakamaa kwa vidole kwamba alikuwa na ugonjwa wa yabisi kavu. Alikuwa hawezi kusogeza vidole vyake lakini kwa kuwa amelisikia Neno la Bwana likifafanuliwa, imani yake ilikuwa imeongezeka naye akaangalia vidole hivyo vilivyolemaa na kujaribu kuvisogeza. Mwanzoni hapakuwapo na msogeo wo wote kamwe. Aliendelea kuifanyia zoezi imani yake na alipofanya hivyo ikawa ni dhahiri kwamba aliweza kuvichezesha zaidi ya alivyoweza hapo kabla. Baada ya dakika chache tena, alikunjua na kukunja mikono yake kwa urahisi kabisa. Tabasamu likatokeza usoni mwake wakati alipotambua ya kwamba alikuwa sasa yuko huru kutokana na ulemavu wake uliosababishwa na yabisi kavu.

Ndugu Branham, chini ya Upako, akiombea leso kulingana na Matendo 19:11-12.

Picha ilipigwa na Staples

Siku moja wakati Ndugu Bosworth alipokuwa akitembea barabarani, aliendewa na bibi mmoja aliyemchukulia kwamba ni Mmarekani na akamwuliza kama alikuwa na uhusiano wo wote na mikutano hiyo ya uponyaji wa Kiungu. Mama huyo alielezea ya kwamba yeye alikuwa si mwaminio na hivyo basi hakujihusisha sana na hiyo mikutano, lakini

daktari wake alikuwa amemwambia juu ya wagonjwa wake watatu ama wanne waliokuwa kwenye mikutano hiyo nao walipokea uponyaji. Alikuwa amesikia habari za Mizimu na Ukristo wa Kisayansi na alijiuliza kama mikutano hii ilikuwa imedhaminiwa na mojawapo ya hayo. Kwa kuwa daktari wake alikuwa amemwambia juu ya mikutano hiyo na akamshauri ya kwamba labda angepata manufaa kutokana nayo, aliona kwamba labda ingefaa kwake aihudhurie.

Wakati Ndugu Branham akiwa yuko chini ya upako, ni jambo la muhimu sana kwamba mtu afanye vile hasa anavyomtaka afanye. Maneno yake wakati huo si yake tena, bali ni maneno ya Roho Mtakatifu, akitamka mapenzi ya Kiungu na ya Mwenyezi Mungu. Ningetaka kunukuu kutoka kwenye barua ambayo inaonyesha umuhimu wa jambo hili. "Mama aliyetoka Wingfield aliyekuwa ameponywa kansa na akaambiwa na Ndugu Branham abatizwe alihudhuria ibada ya ubatizo Alhamisi iliyopita jioni, bali hakubatizwa. Alimwambia mchungaji, 'Kuwazia ya kwamba miaka hii yote nimekuwa mfuasi wa kanisa na kamwe sikuwa nimeokoka hata ingawa nilikuwa ni mwalimu wa Shule ya Jumapili. Lakini sasa nimeokoka na nimeponywa.' Alifurahia wokovu wake na uponyaji, bali alisahau yale Ndugu Branham aliyokuwa amemwambia afanye. Hakubatizwa. Jumamosi iliyofuata, akafa. Alilipia gharama ya kutotii kwake."

Wakati Ndugu Bosworth alipokuwa akiwahubiria wenyeji Jumapili moja alasiri huko Capetown alisema jambo hili, "Kama ninyi wahudumu wenyeji mtamwamini Mungu, Mungu atawapa baadhi yenu karama ya uponyaji alasiri ya leo." Ndugu Bosworth kwa namna fulani alifadhaishwa sana na maneno ambayo yeye mwenyewe alinena, akiwa aliyasema kabla hajatambua yale aliyokuwa akisema. Baada ya ibada aliniambia, "Ninaamini Mungu aliniongoza kusema maneno yale. Kama una nafasi ya kufuatilia jambo hili, ninaamini tutakuta kwamba kulikuwa na mchungaji fulani mwenyeji pale alasiri ya leo ambaye amepokea karama ya kuponya."

Niliulizia baadhi ya wamishenari kama walikuwa wamesikia juu ya mchungaji ye yote mwenyeji kule ambaye alikuwa amepokea karama ya uponyaji kama Ndugu Bosworth alivyokuwa ametamka kwenye ibada. Mmoja wao aliniambia juu ya mchungaji mmoja mwenyeji aliyekuwa ameamini katika uponyaji wa Kiungu, lakini kwa sababu ya ukosefu wa imani katika maombi yake mwenyewe hakuwa amemwombea mgonjwa kamwe. Lakini, baada ya ibada hii, alizunguka kwa watu mbalimbali waliokuwa wagonjwa na kuwaombea, na wengi walipokea uponyaji wao. Baadaye mmishenari yuyu huyu aliniandikia barua ambamo alisema hivi, "Yule mwenyeji ambaye amepokea kipawa cha uponyaji alikuwa ni mwananchi wa Angola, Afrika, ya Kireno. Yeye hajui kusoma wala kuandika

hivi kwamba mara nyingi hawezi kujielezea mwenyewe. Yeye ni mvulana mdogo tu bali Mungu amemwinua mtumishi Wake na sasa anahitajika sana. Malori (magari ya mizigo) yaliyojaa wagonjwa yanawaleta wagonjwa kutoka mbali wapate kuombewa naye. Jana nilipitia mahali hapo ambapo tulifanyia mikutano kwa ajili ya machotara na wenyeji, na alikuwa ndiye huyo hapo akifanya mkutano wa nje."

Taarifa zingine za mwenyeji huyu zinathibitisha ukweli ya kwamba Mungu alimpa mchungaji mwenyeji karama ya kuponya pale ambaye angethubutu kumwamini Mungu na kupiga hatua ya imani.

Mara nyingine tena nitawanukulia ripoti iliyoandikwa juu ya mikutano ya huko Capetown iliyochapishwa huko kwenye Visiwa vya Uingereza na gazeti la *Habari za Ukombozi* na baadaye na gazeti la *Mbiu za Imani* huko Marekani.

HABARI MOTOMOTO ZA UFUFUO KUTOKA CAPETOWN

Na Frank G. Holder

Haijawahi kutokea katika historia ya usafiri wa ndege za kimataifa banda lake lilipowekwa kwenye matumizi yenye manufaa ya namna hiyo, likiwa na matokeo mazuri hivi kati ya wenyeji wa mahali hapo. Banda ambalo kwa kawaida hutumiwa na wasafiri wa ndege, Banda Namba 3 ghafla lilibadilishwa likawa "Ukumbi wa Injili" likiketisha watu elfu nne ndani na karibu elfu mbili nje.

Ujenzi wake wa chuma kitupu na mazingira yake yasiyovutia ukumbi huu haukuwa na mengi sana ya kuvutia katika uzuri wa ujenzi, lakini shauku iliyokuwapo miongoni mwa msongamano wa watu waliokuwa wakikusanyika kwenye ukumbi huo mara ilisababisha mazingira ya matarajio yasiyo ya kawaida. Mahali hapa pakiwa pako maili nyingi nje ya mji, huenda mtu anaweza kuwazia Yohana Mbatizaji wa kisasa alikuwa akiliita kusanyiko lake litoke liende nyikani likasikie ujumbe wake kutoka kwa Mungu.

Pamoja na mpangilio huu wa kidini wa mtindo usiovutia, kulikuwako na mlolongo wa magari ya wagonjwa yakiwashusha wagonjwa wao waliokuwa kwenye machela kwenye sakafu baridi ya saruji mbele ya jukwaa la muda. Vilema, viwete, vipofu, na wagonjwa wa kila namna walimiminika kuchukua nafasi zao katika Zahanati ya Wagonjwa iliyokuwa ikiendelea daima kufurika.

Ndugu William Branham na kikosi chake kutoka Marekani walikuwa wamekwisha wasili Capetown wakiwa na ujumbe ambao unaweza kutangazwa na thibitisho lile

lile la nguvu za kimbinguni kwa ishara za ajabu sana na maajabu, kwenye majumba mazuri sana ya mikutano ya kisasa, ama katika mabanda ya viwanja vya ndege. Tayari habari zilikuwa zimepachangamsha mahali hapo, kwani wale ambao wameitikisa Johannesburg, Kimberley, Bloemfontein na miji mingine mingi ya Afrika Kusini wamewasili Capetown.

Tangu siku ya kwanza miujiza ilianza kufanyika wakati nguvu za kipentekoste na utukufu wake zilipotangazwa kila mahali. Makusanyiko yaliongezeka mpaka kupata viti ikawa ni jambo la anasa, na miujiza ikawa ni mingi mno kuweza kuandikwa. Viwete waliruka na kutembea; viziwi walisikia vizuri, kansa zilikauka, pepo walikimbia, na mioyo dhaifu ilitiwa nguvu mara moja. Ndugu Branham alipokuwa akinena kwa ufunuo aina ya ugonjwa wa mtu, hakuna kamwe hata wakati mmoja ilipoonekana kuwa ni makosa hata kwa sehemu, imani iliongezeka na watu wakaponywa. Nguvu za uponyaji zingeshuka juu ya kusanyiko na ilihitaji tu imani mtu kuchukua lililohitajika, na jambo hilo lilipokelewa. Mamia ya wasioamini walishawishika kuhusu ukweli wa Injili nao wakamkubali Kristo kama Mwokozi wao.

Capetown imekwisha tikiswa na nguvu za Mungu, na yote yalitukia katika siku tano. Iwe mtu yuko kwenye basi ama anatembea barabarani, mtu daima alisikia tu watu wakizungumza juu ya mkutano wa Uwanja wa Ndege wa Wingfield na miujiza ya ajabu sana.

Mikutano maalum iliendeshwa kwa ajili ya watu weusi peke yao, na miongoni mwao hata mambo makubwa zaidi yalifanyika. Nguvu za Mungu zilikuwapo kuponya, hivi kwamba walikuwa wakiwekeana mikono na kupokea ukombozi. Mtu mmoja ambaye alikuwa kilema kwa miaka mingi aliamua kujaribu miguu yake ambayo iliponywa. Alikimbia kwenye barabara huku akifukuzwa na polisi aliyetaka maelezo. Ni wazi kwamba aliyapata! Nje ya mkutano kwenye Uwanja wa Gwaride mjini, watu weusi walikuwa wakipokea uponyaji wa kila namna ya magonjwa.

Kamwe hatujawahi kushuhudia wingi wa ishara na maajabu kama huo, ama shuhuda kama hizo za ufunuo wa kiungu na nguvu. Huku ni kuzuriwa na Mungu, na katikati ya hayo yote, mioyo yetu ilikuwa na shauku sana ya Nchi ya Uenyeji wetu. Tunaomba impendeze Bwana kutuma kwa haraka wimbi la baraka katika Visiwa vya Uingereza. Mpaka zitakapokuja, hebu na tuombe, tuamini, na kuitayarisha mioyo yetu kwa yote hayo ambayo Mungu atatupa!—*Habari Njema za Ukombozi*

—*Mbiu ya Imani*

Matokeo ya mikutano hii si wokovu peke yake wa nafsi na kuponywa kwa miili bali pia imani iliyovuviwa na nabii

wa Mungu. Na imani hii inatoa matokeo yake katika huduma ya wafanyakazi wengine kwenye maeneo ya Afrika Kusini. Wachungaji wengi na wamishenari wametoa taarifa ya kwamba huduma yao wenyewe imepanuka kutokana na mikutano ya Branham. Jambo hili ni wazi kulingana na barua ifuatayo iliyopokelewa na Ndugu Bosworth kutoka kwa mmishenari mmoja anayetoa taarifa juu ya mkutano uliofanywa baada ya Kikosi cha Branham kurudi Marekani.

"Nina hakika mtafurahi pamoja nasi kwa nguvu za ajabu za Bwana Yesu zinazoendelea pamoja nasi hapa Afrika Kusini. Jinsi nilivyothamini kitabu chako na zile jumbe kwenye ile miamsho ya kule kwa wenyeji huko Pretoria na Orlando. Zaidi sana nimerejea kwenye mazungumzo ya mtu binafsi na msaada katika mikutano hiyo. Sasa katika mkutano wa Moroka—karibu na Orlando—ishara zimekuwa zikifuatana na kuhubiriwa kwa Neno katika njia ya upendo sana. Wagonjwa waliponywa, viziwi walisikia, na vipofu waliona, na viwete walitembea. Utukufu wote kwa Bwana wetu mtukufu! Hayo yalikuwa ni majuma mawili tu yaliyopita.



Ndugu Branham akiwa pamoja na mchungaji mwenyeji.

Halafu jana jioni tulikuwa na vita vikali nyumbani. Mama, aliyekujua katika siku za mwanzoni za Sayuni, alishikwa na ugonjwa wa pepopunda kwa hakika kabisa. Huku mataya yake yamejifunga kabisa tuliomba kwa bidii sana mpaka yeye mwenyewe akaweza kuomba pamoja nasi apate kufunguliwa kikamilifu kutoka kwenye maumivu makali sana. Ndipo adui akaingia kwa ukatili mno kuliko ilivyowahi kuwa. Macho yake yakabingirika, taya zake zikajifunga vibaya zaidi kuliko ilivyowahi kuwa na akashikwa na mishtuko ya maumivu, hatimaye akazirai. Upesi nilimtuma binti yetu Eunice akampigie simu Ndugu W. F. Mullan. Akiacha chakula chake cha jioni mezani alikuja mara moja. Baada ya maombi mafupi alimkemea adui katika Jina lenye mamlaka la Bwana Yesu, ndipo ushindi ukapatikana! Muda mfupi sana baadaye

akalipuka katika kusifu kwa furaha isiyo na kifani, huku akinena kwa lugha zingine; akararua bendeji toka kwenye sehemu iliyoathiriwa na mara moja akaamka yu mzima na yeye mwenyewe akahudumia chakula cha jioni, amini usiamini! Hakika tulikuwa na wakati wa furaha kuu wa kusifu na kutoa shukrani kwa kumponya huyu shujaa wa msalaba mwenye umri wa miaka sitini na tisa, ambaye kwa muda wa miaka thelathini na miwili amekuwa daima kwenye mstari wa mbele wa vita bila kupumzika. Tunamtazamia Mungu amruhusu kupumzika sasa ili kwamba apate kuwa baraka kwa makanisa ya nyumbani. Amekuwa mnara wa ukumbusho maishani mwake mwote wa nguvu za Bwana za uponyaji bila kugusa dawa tangu mwaka wa 1907, ingawa alikuwa na vita vikali sana na adui. Akiwa anakaribia kuwa kipofu, naye ni kilema kwa ajali ya kupanda farasi, nimonia mara nne, sumu ya chakula kilichoharibika akiwa na kipimo cha juu sana cha joto kilichopata kurekodiwa hapa naye akaishi, na sasa ushindi huu mkuu na wa haraka. Yote ninayoweza kusema ni haleluya.

Moja ya mambo ya ajabu sana ya uponyaji kwenye mkutano wa Moroka lilikuwa ni lile la mwanamke mwenye umri wa miaka themanini aliyekuwa karibu kuwa kiziwi na karibu kuwa kipofu, pamoja na kupooza kwenye upande wake wa kushoto. Bwana kwanza aliponya maskio yake, kisha macho yake, na imani ilipoongezeka aliamriwa katika Jina la Bwana kuinua mkono wake. Huo ukainuka haraka bila matatizo yo yote na punde si punde alikuwa akitembea bila msaada wa aina yo yote. Utukufu!

Mwingine aliyeleta baraka maalum kwa wenyeji ambao wanapenda watoto sana alikuwa ni mwanamke aliyevalia vizuri aliyekuwa kiziwi kwenye sikio moja na akiwa amembeba mtoto aliye kiziwi kwenye maskio yote mawili. Tulimwombea mama kwanza tukapata ushindi kamili na kisha tukamwombea mtoto. Wakati aliposhtuka nilipodata vidole vyangu nyuma ya kichwa chake watu waliguswa sana kuona macho yake madogo yakiangalia kwanza upande huu halafu tena yakiangalia upande mwingine wa pili akijaribu kuielewa kelele hiyo. Bwana asifiwe!

Msichana mmoja mwenye umri wa miaka kama kumi na sita alikuwa kiziwi kwenye maskio yote mawili naye aliponywa. Ndipo adui akarudi na akafunga sikio moja. Alirudi kwenye mstari wa maombi na baada ya kumkemea adui yeye alisikia mapigo madogo sana ya saa yangu ya mkononi. Hii ilikuwa ni baraka kuu kwa watu ambao walikuwa wamekuja kutoka Shule ya Biblia ya Witbank kusaidia katika mikutano hiyo.

Huku nikihisi imani katika mvulana mwenye umri wa miaka minane hivi ambaye alikuwa kiziwi kwenye sikio moja, niliona Mungu angetenda kazi kwa njia ambayo angeitia moyo imani ya watu, kwa hiyo niliziba tu sikio hilo lililokuwa zima

na nikamwuliza, 'Je! unaweza kunisikia?' Kutikisa kwake kichwa na kuitikia 'Ndio' kwa haraka kulikuwa ni baraka kweli kweli kwa watu. Asifiwe Bwana wetu Yesu mtukufu.

Kati ya mikutano ya alasiri na ya jioni ya siku ya mwisho, nilikuwa nikipumzika nyumbani kwa mchungaji (David Mzolo) ndipo akaja mwanamke aliyeinama kwa maumivu ya siku nyingi, akiwa ameegemea kabisa kwenye fimbo yake. Nilipogundua imani katika mazungumzo yake tulimtegemea Mungu kwa ajili ya maombi ya imani, tukimwomba Bwana amponye toka kichwani hadi mguuni. Yeye akafanya hivyo hasa! Akirukaruka kila mahali kama msichana wa shule na kumsifu Mungu kwa uponyaji wake, mara alisimama na kupiga makele, 'Ninaweza kuona kwa jicho langu lisiloona.' Hata hatukujua ya kwamba alikuwa na jicho lisiloona.

Lakini haya ni machache tu kati ya mambo mengi ambayo yametendwa na nguvu za Bwana wetu Yesu mtukufu aliyefufuka. Na atukuzwe kwa njia kuu zaidi tena katika mikutano ijayo.

Wengi walikuja mbele kwa ajili ya wokovu kila usiku—mara nyingine kadiri ya watu hamsini na sitini walikuwa wamepiga magoti wakitafuta wokovu. Mwanamume mmoja alishuhudia kwamba ameishi maisha ya dhambi, lakini hayo yote sasa yalikuwa yamebadilika. Mwingine akasema, 'Sasa nina moyo mpya na maskio mapya.' Alikuwa ameokolewa na kuponywa. Kwa kweli mioyo yetu inafurika."

J. S. R.

Wakati huu tulisafiri kwa magari mpaka Port Elizabeth kupitia njia iitwayo Barabara ya Bustani. Hii inahesabiwa na wengi kama barabara ya kupendeza sana kati ya pwani kubwa mno ya Afrika Kusini. Kuambaa kandoni mwa barabara hii kuna baadhi ya miti yenye umri wa zaidi ya miaka elfu moja na inayokua ikafikia urefu wa futi mia moja na ishirini. Zipo sehemu chache sana katika Afrika ambako maua hustawi kwa wingi sana hivyo kama yanavyostawi kwenye barabara hii. Upande mmoja wa barabara hii kuu kuna pwani zinazopendeza sana za Bahari ya Hindi yenye joto la kadiri na upande wa pili wake kuna Safu ya Mlima Outeaiqua inayopendeza sana. Kuna zaidi ya aina elfu mbili za maua mwitu katika eneo hili. Ni jambo la kawaida kukuta mayungiyungi ya kala yenye kipimo cha upana wa inchi nane.

Uamsho wa Port Elizabeth ulifanyika tangu tarehe 7 Novemba hadi tarehe 11. Mara ya kwanza mikutano hiyo ilifanyikia kwenye Ukumbi wa Soko la Unyoya lakini baadaye ilihamishiwa kwenye Uwanja wa Michezo wa Davis. Hapa tena umati wa watu ulikuwa ndio mkubwa sana uliopata kuonekana katika jiji la Port Elizabeth. Jioni moja Ndugu Branham alimwelekezea kidole mzee mmoja aliyekuwa amelala kwenye



Ukumbi wa Soko la Unyoya

kitanda cha wagonjwa. Akamwambia, "Bwana atakuponya. Unaweza sasa kuinuka, kunja blanketi lako na kitanda chako na utembee." Huyo mzee akasimama na akaanza kukunja blanketi lake ambapo wanaume kadhaa wa Msalaba Mwekundu, ambao daima walikuwa hapo kwenye mikutano nao walikuwa tayari kuwasaidia wagonjwa, walikuja kumsaidia. Akanena kwa sauti kuu na kwa mkazo aliposema, "Ndugu Branham aliniambia nikunje blanketi langu na kitanda changu na hiyo haimaanishi ya kwamba mnapaswa kunisaidia. Kwa hiyo ondokeni na msinisumbue."

Lilikuwa kidogo ni tukio la kuchekesha hata hivyo linaleta ukweli unaotakiwa uuone. Wakati nabii wa Mungu, akinena chini ya Upako, akitoa amri, ni jambo muhimu sana ya kwamba litekelezwe juu ya alama. Kama Naamani angelijitumbukiza mara sita tu kwenye Mto Yordani asingepokea uponyaji wake. Ilikuwa ni kutimizwa kikamilifu kwa maagizo aliyopewa na mtumishi wa Mungu ambako kulimwezesha kuona dhihirisho linaloonekana la kuponywa kwake. Kwa hiyo ndivyo ilivyokuwa kwa mtu huyu kule Port Elizabeth. Alidhamiria kufanya kila kitu ambacho Ndugu Branham alikuwa amemwambia afanye kusudi aweze kupokea uponyaji alioahidiwa.

Jioni nyingine Ndugu Branham alimwelekezea mwanamume mmoja kidole ambaye alikuwa na bendeji kubwa sana usoni mwake, na akamwambia, "Je! ungependa kumkubali Kristo kama mponya wako, kama atanifunulia shida yako?" Mtu huyo akatikisa kichwa, "Naam." Ndugu Branham akasema, "Una kansa. Simama, nenda zako nyumbani nawe utakuwa mzima." Mwanamume huyo alipokuwa amekuja humo ukumbini jioni hiyo, uso wake ulikuwa umevimba hivi kwamba mdomo wake wa juu ulikuwa unaning'inia juu ya wa chini. Alipoondoka humo ukumbini jioni hiyo, karibu kuvimba kote kulikuwa kumeondoka naye akatoa taarifa kwetu siku kadhaa baadaye ya kwamba hiyo kansa ilikuwa imedondoka kutoka usoni mwake, bila kuacha dalili yake yoyote mwilini mwake.

Ndugu Branham pia alielekeza kidole chake kwa mmoja wa manesi waliokuwa kwenye safu ya mbele na kusema, "Mama, unahangaika juu ya mtu fulani. Si wewe mwenyewe wala mtu aliyepo hapa usiku wa leo. Ni juu ya mama yako ambaye yuko nyumbani akiwa na hali mbaya sana ya moyo. Nesi, unaweza kwenda zako nyumbani sasa, kwa maana mama yako amekwisha kupona."

Kwenye ibada ya Jumapili asubuhi kwenye Ukumbi wa Soko la Unyoya, Mhindi mmoja alikuwa kwenye mstari wa maombi. Wakati alipofika kwa Ndugu Branham aliambiwa, "Wewe si Mkristo lakini umeamini zaidi dakika hizi tano za mwisho kwa sababu ya yale yaliyotukia humu jukwaani kuliko vile ulivyopata kuamini katika maisha yako yote ya nyuma." Mwanamume huyo akatikisa kichwa chake. Ndugu Branham akasema, "Siwezi kumwomba Kristo awe Mponya wako usipomchukua kama Mwokozi wako na Mfalme. Kama nikiweza kukwambia unachoumwa, je! utamchukua Kristo kama Mwokozi na Mfalme wako?" Mwanamume huyo akasema, "Ndio." Ndugu Branham akasema, "Una ugonjwa wa kisukari. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako." Mtu huyo akainua mkono wake na halafu akaambiwa aende na kwa kuamini angepata uponyaji wake.

Jioni hiyo nilizungumza na mama mmoja wa Msalaba Mwekundu aliyetoa ushuhuda wa uponyaji wa mama yake. Halafu aliniuliza kama nilimkumbuka yule Mhindi aliyeponywa kwenye ibada ya asuhubi. Huyo mama alikuwa ni katibu wake myeka na alikuwa amemtia moyo kuja mkutanoni. Aliponiambia jambo hili, nilikumbuka yale Ndugu Branham aliyokuwa amesema kwenye chakula cha mchana. Alikuwa ametwambia ya kwamba alipoona ono la yule Mhindi mwenye kisukari alimwona pia mama mmoja Mzungu. Ingawa ilionekana kana kwamba alikuwa amekwisha kumwona mama huyo kabla, hakumtambua wala asingeweza kutambua alikuwa na uhusiano gani na mtu huyu au kuponywa kwake. Kwa

kuwa sehemu hiyo ya ono haikuwa dhahiri sana, hakusema lo lote kulihusu wakati huo. Alhamisi iliyopita Ndugu Branham alikuwa amemwelekezea kidole bibi huyu ambaye niliongea naye na kuzungumza naye juu ya mama yake, aliyekuwa nyumbani akiumwa na moyo. Wakati huo alikuwa amevaa yunifomu yake ya kazi. Lakini wakati alipofanya kazi kwa huyo Mhindi na kuzungumza naye kuhusu mikutano, alikuwa amevaa nguo za kiraia. Huyu alikuwa ndiye yule mama ambaye Ndugu Branham alikuwa amemwona katika ono lililomhusu yule Mhindi, bali hakumtambua, labda ni kwa sababu alikuwa tu amemwona katika yunifomu.

Baada ya moja ya ibada hizo mtu mmoja alikuja kwangu na akaniambia ya kwamba alikuwa amemwona malaika wa Bwana akiwa amesimama moja kwa moja nyuma ya Ndugu Branham. Nilimwambia mtu huyo kumwelezea alivyo ili kwamba nijue kama sifa zake zilikuwa kama za hao wengine waliokuwa wametoa taarifa ya hadithi hiyo hiyo ama hapana. Mtu huyo aliniambia ya kwamba huyo aliyemwona alikuwa mkubwa zaidi kuliko Ndugu Branham, amenyoa ndevu na amevaa vazi jeupe. Maelezo haya yalifanana na yale yale niliyokuwa nimepokea kutoka kwa watu wengine watatu kuhusu malaika ambaye walikuwa wamemwona jukwaani akiwa pamoja na Ndugu Branham. Mtu huyu pia alielezea kwamba wakati Ndugu Branham aliponyosha mikono yake na kuwaombea watu kwa pamoja kitu fulani kilidondoka kutoka mikononi mwake kama madini ya fosforasi. Kilionekana karibu kama maji yanayometameta daima yakitiririka kutoka kwenye vitengele vyake na mikononi mwake. Justus duPlessis, mkalimani mkuu wakati wa ziara ya Ndugu Branham huko Afrika Kusini, aliniambia ya kwamba mara nyingi wakati Ndugu Branham alipokuwa akiwaombea wagonjwa aliona kivuli sakafuni. Alipochunguza kwa taa hakukuwako kabisa na kitu chochote kilichoonekana kati ya taa na sakafu, hata hivyo hiki kivuli kilikuwapo. Alishawishika kabisa ya kwamba hiki hakikuwa ni kitu cho chote ila ni kivuli cha huyo malaika wa Bwana.

Baada ya ibada moja nilimwona mtu mmoja akichechemea na mikongojo yake kwa njia ya dhiki sana. Alipotoka nje ya mlango alisimama kwa muda kidogo, akainamisha kichwa chake, akaangusha mikongojo yake na akaanza kutembea vizuri kabisa.

Ilikuwa ni kule Port Elizabeth ambapo mtu mmoja alikuja na akaniambia ya kwamba usiku uliotangulia alikuwa amesafiri kwenda nyumbani kwa teksi, kwa kweli amesikitika kwa maana hakuwa amepokea uponyaji wake. Moyo wake ulikuwa na huzuni na mzito kwa sababu alikuwa na hakika ya kwamba angepokea uponyaji wake jioni hiyo. Wakati alipotoka kwenye teksi hiyo alitambua ya kwamba hali yake ya ulemavu mwilini mwake ilikuwa imetoweka naye aliweza kutembea vizuri kabisa.

Asubuhi tuliyoondokea Port Elizabeth, Ndugu Baxter, Ndugu Branham na Billy Paul walishuka kwenda mjini. Walipokuwa wakirudi kwenye basi, Ndugu Branham aliwaambia hao wengine ya kwamba kulikuwako na mama mmoja humo kwenye basi aliyekuwa akijaribu kuwasiliana naye. Alimwelekezea kidole bibi mmoja aliyekuwa na nguo ya hudhurungi aliyekuwa ameketi mbele ya hilo basi. Ndugu Baxter akamfahamisha ya kwamba bibi huyo asingeweza kamwe kujua ya kwamba walikuwa humo kwenye basi kwa kuwa alikuwa ameketi mbele nao walikuwa wameingia kwa nyuma na pia walikuwa wameketi kwa nyuma ya basi. Hakuna la zaidi lililozungumzwa kuhusu jambo hilo mpaka mama huyo alipoamka na akatembea kuelekea nyuma ya basi hilo. Mwanamke huyu akamjia Ndugu Branham na kumwuliza kama alikuwa ndiye Kasisi William Branham. Akasema, "Ndio, mama, nawe una shida ya kike na usaha. Pia una mtoto nyumbani ambaye ni mgonjwa sana. Unaweza sasa kwenda zako nyumbani na uwe mzima, kwa maana imani yako imekuponya." Baada ya haya mama huyo aligeuka na akaanza kulia kwa furaha.

Billy Paul Branham, ambaye uungwana wake na huruma kwa wengine kulimfanya apendwe sana na watu.

Kutoka Port Elizabeth tulisafiri kwa magari mpaka Grahamstown, mji wa kupendeza sana na wa kuvutia wa Kiingereza. Kamati ya mahali hapo ilikuwa imekodisha kwa ajili yetu Ukumbi wa Jiji unaoweza kuketi watu 1200. Watu walianza kukusanyika kwenye saa 1:30 asubuhi kwa ajili ya ibada ya alasiri ambayo ilifanyika kwenye saa 8:30. Kabla ya kuwasili kwa Kikosi cha Branham kamati ya mahali hapo ilitaka kuweka kipaza sauti nje ya Ukumbi huo wa Jiji wapate kuwahudumia watu ambao wasingeweza kuingia humo jengoni. Bawabu akasema hili halikuwa ni la lazima kwa sababu kamwe katika historia ya Grahamstown hapajawahi kuwa na ibada yo yote ya kidini kwenye Ukumbi huo wa Jiji, wala mahali pengine po pote mjini, ambako mfumo wa vipaza sauti ulihitajika. Walishangaa sana walipoona umati ukilijaza jengo hilo na mamia wakiwa wamesimama nje.

Kulikuwako na uponyaji mwingi katika mikutano hii miwili iliyofanyiwa huko Grahamstown lakini kulikuwako na matukio matatu ambayo ningetaka kuwaletea mzingatie. Moja lilihusu mzee mmoja aliyelazwa kwenye kiti cha magurudumu hawezi. Ushuhuda wake umewekwa katika mlango uliotengwa kwa shuhuda. Ndugu Branham alimwelekezea kidole na kumwambia ya kwamba alikuwa amepona na ya kwamba anapaswa kuamka. Mtu huyo akaamka. Baadaye nilizungumza naye na kumwuliza kwamba ilikuwa ni muda gani tangu alipotembea. Akajibu ya kwamba hakuwa ametembea kwa miaka miwili hadi jioni hiyo.

Ndugu Branham pia alimwelekezea kidole mama mmoja. Akasema, "Una TB. Amka na ukubali uponyaji wako." Bibi huyo hakusogea. Akasema, "Simama. Kristo anaweza kukufanya mzima. Simama na ukubali uponyaji wako." Bado hakukuwako na jibu. Ndipo Ndugu Branham basi akamgeukia mtu mwingine ambaye alikuwa amemwona kwenye ono. Ilikuwa ni mama mwingine aliyekuwa amelala kwenye kitanda cha wagonjwa. Akamwambia, "Mama, umekuwa na hali mbaya sana ya moyo. Haiwezekani kwako kuishi muda mrefu zaidi Kristo asipokuponya. Ikiwa utasimama na kukubali jambo hilo, Kristo atakuponya." Mama huyo alisimama na baadaye tulipokea ushuhuda ya kwamba alikuwa amepata kuwa mzima. Ningetaka kuwarudisha kwa yule mama wa kwanza, ambaye hakusimama wakati Ndugu Branham alipomtia moyo kusimama. Hatujasikia kamwe kwamba alipokea uponyaji wake. Hakuna hakika kwamba alipona kwa maana hakufanya kama nabii wa Mungu alivyokuwa amemwelekeza kufanya.

Ndugu Bosworth kingoni mwa Mto Vaal.

Ilikuwa ni baada ya ibada ya jioni wakati Ndugu Branham, Ndugu Baxter na Billy Paul walipokuwa wameondoka kwenye jumba la mikutano ambapo mama mmoja alinijia mimi na Ndugu Bosworth tuliokuwa nyuma ya jukwaa. Alikuwa akimwongoza mvulana mwenye umri wa kama miaka sita. Akamwambia Ndugu Bosworth, "Ninajua

ya kwamba huwezi kumwombea kila mtu, lakini hivi huwezi kumwombea mvulana wangu?" Alieleza ya kwamba tangu kuzaliwa mwanawe hajaweza kuona vizuri sana. Angeweza kutambua umbile la mwanadamu kama ingekuwa ni umbali wa futi tatu kutoka kwake. Cho chote kilicho kwenye umbali wa zaidi ya futi nne ama tano toka alipo hakuweza kukitambua. Ndugu Bosworth alimwombea mvulana huyo na kisha akamwambia mama huyo aende kwenye kona ya mbali, yapata futi thelathini kutoka tulipokuwa. Alimwambia asimame hapo wala asitoe sauti yo yote wakati tukitafuta kuona kama kuona kwa mvulana huyo kulikuwa kumekuwa kuzuri zaidi. Ndugu Bosworth basi akamwambia mvulana huyo aende kwa mama yake. Mara akaanza kutembea kutoka nyuma ya jukwaa akielekea moja kwa moja kwa mama yake. Mama aliangua kilio cha furaha, kwa kuwa kamwe mvulana huyo hajawahi hapo nyuma kumtambua yeye wala mtu ye yote yule kwa umbali wo wote wa zaidi ya futi tatu ama nne. Jaribio hili lilirudiwa mara nyingi. Mvulana huyo alithibitisha ukweli kwamba macho yake yalikuwa yamekuwa mazuri zaidi kwa kusema ya kwamba aliweza kumwona mama yake akiwa upande mwingine wa kile chumba. Mtoto huyo akiwa na furaha na tabasamu usoni mwake alisema, "Ninaweza kukuona, mama." Lilikuwa ni dhihirisho lingine la nguvu za imani.

Mikutano huko East London iliendeshwa kutoka tarehe 14 Novemba mpaka 18, kwenye Uwanja wa Shirika la Ragbi la Mpakani, mahali pekee katika East London palipoweza kutoshea umati huo. Kwa wastani karibu watu 6,000 walihudhuria na jioni ya mwisho tulipokuwa huko umati ulikadiriwa kuwa karibu 15,000. East London ndio makao makuu ya Ndugu Bhengu, mmoja wa wahudumu mashuhuri sana wa wenyeji wa Afrika Kusini. Ana ushawishi mkubwa mno kwa wasio Wazungu katika sehemu hii ya Afrika Kusini. Niliambiwa na baadhi ya maafisa wa polisi ya kwamba baada ya Ndugu Bhengu kuja kwenye mji wao, uhalifu miongoni mwa wasio Wazungu ulishuka kwa asilimia 30 katika miezi sita ya kwanza.

Jioni ya kwanza tulipokuwa huko East London kulikuwa na upepo mwingi sana mwanzoni mwa ibada. Mara tu Ndugu Branham alipokuja jukwaani, upepo ulitulia na kukawa shwari. Haya yaliripotiwa kwenye *Gazeti la Daily Dispatch* kesho yake na nakala ya sehemu iliyokatwa imetolewa hapa.

Ijumaa iliyofuata tulikuwa na tukio lilo hilo la mvua. Ilionekana kana kwamba ingebidi mkutano uvunjwe. Lakini Ndugu Branham alipofika kwenye viwanja hivyo, mvua ilikoma kunyesha na baada ya dakika chache mbingu zilikuwa nyeupe. Ndipo tena Jumapili usiku tulikuwa na dhihirisho lingine kama lile lililotukia Jumatano jioni.

MAELFU WAKUSANYIKA KUMSIKIA BRANHAM AKIZUNGUMZA

Hakuna Uponyaji Katika Mkutano wa Kwanza

Dharuba za ghafla za baridi za upepo mkali zilishambulia vibaya sana Uwanja wa Shirika la Ragbi la Mpakani ambapo umati ulikuwa umekusanyika jana usiku kungojea kuja kwa William Branham, kiongozi wa Kamati ya Uinjilisti wa Branham na Mkutano wa Uponyaji wa Kiungu.

Miali michache ya nuru katika umbo la duara ilipenya gizani ikisaidia kutupa mwanga kwenye machela zilizobeba miili iliyofunikwa vizuri sana na mablanketi. Kulikuwako na vitanda vya safari, pia. Ndani ya kimoja cha hivyo alilala mtoto mwenye uso mwembamba na macho makubwa na kwenye kingine mlikuwamo na msichana ambaye vidole vyake vilivyo mifupa mitupu vilitutumuatutumua mablanketi bila kukoma. Kati ya safu ndefu moja na nyingine ya viti kulikuwako na korija kwa korija ya viti vya walemavu.

Jukwaa la muda, lisilo la kudumu, lililofunikwa kwa turubai, lilikuwa na safu ya viti, maikrofoni na mimbara. Mkutano ulifunguliwa na mmoja wa ndugu waliokuwa wakiongoza kusanyiko katika kuimba wimbo wa sifa, "Loo Salama Kwenye Mwamba," ambao uliimbwa kwa sauti kuu sana kisha ukaishia kwenye hewa nzito iliyolowa umande. Mtoto mchanga alilia kwa sauti ndogo, na sauti kubwa ya king'ora cha ambalanzi kikasikika kwa mbali. Ndugu Baxter, mhubiri wa Canada, aliingia mimbarani na matarajio yaliuhamasisha umati wa watu waliokuwa wakingoja. Aliwaambia juu ya kazi ya Uamsho huo, akawaambia kitu fulani juu ya Misheni ya Imani ya Mitume, akazungumzia juu ya mafanikio ya William Branham, na "Kipawa chake cha Uponyaji" wa kiungu.

BRANHAM ANAFIKA

Kulikuwa na kutulia kidogo, na ndipo ikasikika tetesi ya kwamba mtu huyu, ambaye inasemekana alijiliwa na malaika miaka mitano iliyopita na kuagizwa apeleke karama ya uponyaji kwa watu wa ulimwengu, alikuwa amewasili kwenye uwanja huo, na punde si punde atakuja mimbarani.

Alikuja. Upepo ukakoma. Ukimya mkubwa ukatanda juu ya kusanyiko hilo. Yeye ni mtu mdogo. Si mnenaji mzuri, ila kwa kweli, ni mnenaji aliyevuviwa. Yeye anazungumza kutoka kwenye kilindi cha nafsi yake na kwa uaminifu ambao hauwezi kukanushwa. Na kilindi cha uaminifu wake kingeonekana kwamba ndicho utimilifu wa nguvu zake.

Ndugu Branham hakutoa madai yo yote ya kwamba angeweza kufanya huduma na ustadi wa uponyaji. Hasa, yeye alisema, alikuwa ni chombo ambacho kwa hicho Mungu alichagua kuponya nacho. Lakini ni wale tu waliomwamini Yesu Kristo, ambao waliamini ya kwamba Yeye alikuwa amekufa wapate kuishi, ambao kweli na kwa uaminifu wote waliamini, wakakubali, ya kwamba miaka 1,900 iliyopita waliponywa kweli, ya kwamba iliandikwa ya kwamba waliponywa, hawa tu ndio wangaliweza kuponywa.

Asingefanya uponyaji kwenye mkutano huu wa kwanza, alisema, ila angewapa wale waliokusanyika kwenye uwanja huo muda wa kuangalia ndani ya mioyo yao, kulikubali neno, kisha warudi kesho yake ambapo alijisikia hakika ya kwamba rehema ya Mungu ingetolewa, na wengi wa hao waliokuwa viwete, vilema na vipofu, wangetembea na kuona, bali ni kama tu walilikubali neno. Mkutano ulifungwa kwa maombi yaliyoongozwa na Ndugu Branham.

Imechapishwa tena kutoka kwenye Daily Dispatch, 5 Novemba, 1951



Picha imepigwa na Howard Shaw



Picha imepigwa na Howard Shaw

Wakati mmoja macho yake yalikuwa na makengeza, lakini sasa ni manyofu.

Kidole gumba cha msichana huyu kilikuwa kimeshikamana na kiganja cha mkono wake. Tuliambiwa ya kwamba wasingeweza kumfanyia upasuaji kukisahihisha kwa sababu neva na vena za damu zilivuka kutoka kidole gumba chake mpaka kwenye kiganja cha mkono wake. Hiyo ni kusema, kidole gumba kilikuwa ni sehemu ya kiganja chake. Wakati Ndugu Branham alipokuwa akiendesha ibada ya uponyaji jioni moja huko East London yeye alishika imani papo hapo alipokuwa ameketi, na akadai uponyaji wake. Baada ya ibada, yeye alituonyesha mkono wake ambao ulikuwa mzima kabisa.

Kwenye mkutano uliofanyika kwa ajili ya wenyeji, Ndugu Branham alimwelekezea kidole mvulana mmoja na kumwambia alikuwa ametoka hospitalini na alikuwa anaugua TB. Kisha akazungumza na mwanamume aliyekuwa ameketi karibu yake na kusema ya kwamba yeye naye pia alikuwa na TB. Ikawa kwamba Ndugu Branham aliwaelekezea kidole watu watano wao moja kwa moja kwenye safu, kila mmoja akiugua ugonjwa mbaya wa TB. Aliwaambia ya kwamba kama wangeendelea kuamini, Mungu angewaponya kabisa. Baada ya ibada nilizungumza nao na nikawapiga picha. Waliniambia wote walikuwa wametoka kwenye Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza huko East London.

Walipokuwa wakisafiri kwa magari kutoka East London kwenda Durban, Ndugu Branham alipata ono la nyumba ya kienyeji iliyokuwa juu ya kilima fulani. Walipokuwa wakiendelea na safari yao, aliona kilima hiki na nyumba hii ya kienyeji. Alimwomba dereva asimame. Walipokuwa wakienda kule kwa miguu, Ndugu Branham alionyesha kile



Picha imepigwa na Howard Shaw

Ndugu Branham akiwahudumia wenyeji.



Ibada ya wananchi huko East London.

kibanda, kilichokuwa miongoni mwa vingine vilivyofanana kabisa nacho. Alisema ya kwamba ndani yake wangemkuta mwanamke mwenyeji amelala kitandani akiwa mahututi kwa TB. Mama huyu atakuwa ni Mkristo na angeweza kuzungumza Kiingereza. Walipoingia ndani ya kile kibanda, kulikuwa na huyo bibi mwananchi amelala kwenye kitanda kidogo kama tu vile Ndugu Branham alivyokuwa ameelezea. Akasema alikuwa akiomba kwa ajili ya uponyaji na kwamba Bwana alikuwa amemwahidi ya kwamba Yeye angemtuma nabii kutoka katika nchi nyingine kumwombea naye angepokea uponyaji wake.

Matangazo yalizaa matokeo mazuri.

Tulipokuwa tukisafiri kuambaa pwani ya kusini-mashariki mwa Afrika Kusini tulipata nafasi ya kupitia na kuzuru baadhi ya vijiji vya wenyeji. Kila mahali tuliposimama na kuzungumza na wenyeji tuliwaona kuwa ni wachangamfu sana na wakaribishaji. Wengi wa hao wenyeji waliweza kuzungumza lugha nne ama tano za kikabila na halikuwa ni jambo lisilo la kawaida sana kumpata mmoja aliyeweza kuzungumza Kiingereza. Tulivutiwa sana na ukweli kwamba watu hawa daima walionekana kuwa wenye furaha. Kamwe hawakuwa na haraka na daima walikuwa tayari kutupa tabasamu tulipokuwa tukiwapiga picha. Hatukupata kamwe hata mtu mmoja aliyesita kuungana nasi katika kupiga picha ama kutwambia juu ya shanga zao, kazi nyingi za sanaa ama maisha wanayoishi.

Durban ni jiji linalopendeza. Hewa yake imejaa manukato ya aina mbalimbali za maua mwitu na ya nyumbani yanayouzwa kwenye masoko ya maua. Kuna fuko zinazojulikana ulimwenguni kote. Pia ndio makazi ya vijana wachangamfu wa riksho. Halafu, pia, kuna Soko la Kihindi, mahali ambapo Mashariki inakutana na Magharibi. Mtu hujikuta katika mazingira ya kinyumbani ya Mashariki, kwa kuwa ndani na kwenye vitongoji vya Durban kuna karibu Wahindi 200,000, ambao kwanza waliletwa kutoka Asia kama watumwa wapate kufanya kazi katika migodi ya madini. Juhudi zote za kuingiza mawazo ya kimagharibi kwa watu hawa zimeshindikana nao

Wale wanaume watano Ndugu Branham aliwatambua ambao walitoka kwenye Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza.

wanaishi kama wahenga wao walivyoishi kwa mamia ya miaka. Kuna michongo ya nakshi ya zamani za kale inayovutia ya kimashariki na kazi nyingine za sanaa. Wanawake wa Kihindi huvaa sari za hariri, ambapo wengi wa wanaume wa Kihindi hufunika vichwa vyao na tarbushi nyekundu. Jiji la Durban linakaliwa pia na idadi ya Wazungu ipatayo watu 130,000 na idadi ya wenyeji wapatao 110,000.

Mikutano ya kufana sana ya uamsho mzima wa Afrika Kusini ilifanyikia Durban, Pwani ya Miami ya Afrika Kusini, ambako ibada ziliendeshwa kutoka tarehe 21 mpaka 25 Novemba. Baadhi ya mikutano hiyo ilifanyikia kwenye Ukumbi wa Jiji, mingine ilifanyikia Kwenye Uwanja wa Mbio za Farasi wa Greyville.

Ndugu Branham na wenyeji wawili karibu na East London.

Picha ilipigwa na Lynn Acutt

Watu, baada ya kushindwa kupata nafasi ya kuingia katika Ukumbi wa Jiji la Durban, walisimama katika Bustani za Jiji na kusikiliza ibada kutoka kwenye vipazasauti.

Kwenye ibada ya ufunguzi Jumatano jioni, iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Jiji, mama mmoja alimleta mwanawe mwenye umri wa miaka kumi na moja kwenye kiti cha magurudumu. Alimwacha mvulana wake akiwa kwenye kiti chake cha magurudumu huko mbele ambako wagonjwa wengine walikuwa wamekusanyika kisha akaenda kuketi kwenye kiti huko nyuma mbali. Wakati Ndugu Branham alipoomba kwa ajili ya wagonjwa wote mwishoni mwa ibada, mvulana huyo alisimama. Mama yake alidhani mtu fulani alikuwa anamshikilia. Walipotoka nje, alimwuuliza naye akakuta kwamba mvulana huyo alikuwa amesimama bila msaada wo wote. Akamwambia kwamba kwa kuwa alikuwa ameweza kusimama mwenyewe, labda angeweza kutembea. Akamwambia atoke kwenye hicho kiti cha magurudumu na ajaribu. Alifanya hivyo naye aliweza kutembea, mara ya kwanza kwa miaka kadhaa.

Karibu watu 20,000 walikuwa mkutanoni Alhamisi jioni kwenye Uwanja wa Mbio za Farasi wa Greyville. Ndugu Bosworth alileta ujumbe wa wokovu wa mtu binafsi. Maelfu walisimama kuonyesha shauku yao ya kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana wao.

Baada ya kutoa ujumbe wake juu ya wokovu wa mtu binafsi, Ndugu Bosworth aliwazungumzia kwa dakika chache juu ya kweli za uponyaji wa Kiungu. Kisha akawaombea

Baadhi ya wafanyakazi wa Kikosi cha St. John Ambulance ambao walijitolea kuwahudumia watu.

na kuwatia moyo wadai uponyaji ambao Kristo alikuwa ameununua wakati alipoilipia adhabu ya dhambi. Katika dakika chache watu watano mbalimbali, ambao wote hawakuwa wameweza kutembea kwa miaka mingi, walikuja mbele na wakashuhudia kuponywa kwao. Baadhi yao walikuwa ni watoto ambao hawajawahi kuweza kutembea vizuri, mwingine alikuwa ni mama mmoja aliyekuwa kwenye kiti cha magurudumu kwa miaka mitano. Mmishenari aliyeitwa Mchungaji Brown aliripoti ya kwamba papo hapo mbele yake kabisa waliketi viziwi na bubu wanne. Hawakuwa wameweza kusikia cho chote ibadani bali walipoona watu hawa watano wakisimama kutoka katika viti vyao vya magurudumu na kutembea, wengine wao wakiwa wazima kabisa, wengine wao wakiyumbayumba bali wakimwamini Mungu watapata ukombozi mkamilifu, hapana budi walitambua ya kwamba Mungu alikuwa akiwaponya watu na kwa hiyo wakati wao wa kudai uponyaji wao ulikuwa umewadia. Hata hivyo, maamuzi yo yote waliyofikia walipokuwa wameketi pale, wakiwa hawasikii bali wakiona yale Mungu aliyokuwa anafanya, Mungu alirejesha kusikia kwao. Kwa mara ya kwanza maishani mwao waliweza kusikia sauti. Mchungaji Brown alinielezea ya kwamba hajawahi kumwona mtu ye yote mwenye furaha kama wanaume hawa wanne wakati walipotambua ya kwamba waliweza kusikia.

Ijumaa Ndugu Branham alienda katikati ya mji kununua jozi ya ndara. Alipoingia kwenye Duka la Viatu la Cuthberts, karani mmoja aliyemtambua alimkaribia. Karani huyo akamwonyesha mtu fulani, aliyekuwa wakati huo akitoka

humo dukani, aliyekuwa ameingia na kununua jozi yake ya kwanza ya viatu katika muda wa miaka ishirini. Miguu yake ilikuwa imeumbuka sana hivi kwamba asingeweza kuvaa viatu. Katika ibada ya kwanza ya jioni kule Durban wakati Ndugu Branham alipowaombea watu kwa jumla, mtu huyu alipokea uponyaji wake na sasa miguu yake ilikuwa mizima.

Nimewaambia hapo nyuma kuhusu watu kutuletea taarifa ya kwamba walimwona malaika wa Bwana jukwaani pamoja na Ndugu Branham. Tulipokuwa huko Durban nilipokea barua nami ningetaka kuwanukulia sehemu yake.

"Nimekuwa nikiomba kwa muda fulani ya kwamba Mungu angeniruhusu kumwona malaika wa Bwana, wakati Ndugu Branham alipozuru Durban. Alhamisi usiku, tarehe 22 Novemba, nilihudhuria ule mkutano mkubwa, uliofanyika maalum kwa wasio Wazungu, hapo katika Uwanja wa Mbio za Farasi wa Greyville. Baada ya Ndugu Branham kuwapo jukwaani kwa muda mfupi, mara niliona kiwiliwili dhahiri cha mtu mwingine aliyekuwa amesimama moja kwa moja nyuma ya Ndugu Branham. Kiwiliwili hicho kilikuwa mfano wa nuru iliyong'aa. Mtu huyu alikuwa na umbo refu sana kuliko la Ndugu Branham. Nilitaka kuwa na uhakika ya kwamba haya hayakuwa ni mawazo tu ya akili kwa hiyo nikaendelea kumkazia Ndugu Branham macho. Kiwiliwili hiki kingine kilifunuliwa kwangu mara tatu. Mbali na jambo hili, pia nilijaliwa kuona, wakati Ndugu Branham alipoinua mkono wake wakati akihubiri, kitu fulani cha majimaji kilichoonekana kama fosiforasi (inayong'aa sana), kikitiririka kutoka kwenye mkono wake na kiganja chake cha mkono. Niliridhika ya kwamba Mungu alikuwa ameyajibu maombi yangu. Mungu apewe sifa kwa ajili ya Ndugu Branham, nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu."

O. C.

Siku yetu ya mwisho huko Durban ilikuwa ni Jumapili, tarehe 25 Novemba, siku ambayo hatutaisahau kamwe. Tarehe hii inapaswa kuandikwa katika herufi nyekundu, kwa sababu ilikuwa ni siku ya barua ya herufi nyekundu kwa maelfu ya watu wa Durban pamoja na vitongoji vyake na pia kwa washiriki wote wa Kikosi cha Branham.

Shughuli za siku hiyo zilianza kwenye saa 12 asubuhi wakati mabawabu walipofika kazini kwenye Uwanja wa Mbio za Farasi wa Greyville. Watu walikuwa wakikusanyika kwenye lango lake tangu saa kumi usiku na wakati mabawabu walipofika walikuta watu wengi sana hata ilikuwa ni vigumu kuuongoza umati huo. Mchana kulikuwa na zaidi ya maafisa wa polisi sabini na tano kwenye doria nao waliomba msaada wapate kuuelekeza umati kwa kuliita Jeshi Tendaji la Mgambo. Kama nilivyogusia hapo awali, Polisi wa Afrika Kusini walikuwa na adabu, watenda kazi hodari, wachangamfu na daima wanapenda kusaidia.



Picha ilipigwa na Lynn Acutt

Wawili wa kikosi cha watu sabini na tano wa Jeshi la Polisi la Afrika Kusini waliouongoza umati kwenye Uwanja wa Mbio za Farasi wa Greyville.

Ndugu F. F. Bosworth, kiongozi wa siku nyingi katika huduma ya uponyaji wa Kiungu, aliongoza ibada ya asubuhi. Alipofika aliona umati mkubwa sana aliopata kuona umekusanyika pamoja kwa ajili ya ibada ya dini katika muda wa miaka arobaini na kitu ya huduma yake. Aliwaletea watu ujumbe uliovuviwa wenye upako wa Mungu juu ya kweli za uponyaji wa Kiungu na akaelezea karama ambayo Mungu amempa William Branham. Kiwango kikubwa cha ufanisi wa mikutano hiyo kilikuwa ni kutokana na msingi uliowekwa na ustadi wa kuhudumu wa F. F. Bosworth katika mioyo na nia za watu kuhusu kweli za Biblia za uponyaji wa Kiungu na karama isiyo ya kawaida ambayo inafanya kazi kupitia kwa Ndugu William Branham.

Baada ya mafundisho ya Biblia juu ya somo hilo, yeye aliwaita watu kadhaa kuja jukwaani kusudi adhihirishe yale aliyokuwa akiwafundisha. Aliwaita wale waliokuwa wafanyiwe upasuaji mkubwa wa mfupa wa nyuma ya sikio kwenye sikio moja; sikio hilo lingine lilipaswa kuwa zima, hivi kwamba mtu huyo awe alisikia Neno la Mungu, na kwa kusikia Neno la Mungu alipata imani. "Imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa Neno la Mungu," Warumi 10:17. Kusudi mtu upate imani, hapana budi kuwe na mahali pa kuweka imani yako. Baada ya kujaribu kusikia kwa wagonjwa watatu wa kwanza ambao Ndugu Bosworth aliwaombea, tulikuta ya kwamba kila mmoja wao aliweza kusikia kwa sikio lao ambalo lilikuwa halisikii. Walikuwa wamepokea kiwambo

MRS. J. A. NAUDE, of Blythswood Road, Durban, was brought in to the Durban City Hall on this stretcher which she is holding. She picked it up after the American evangelist, the Rev. William Branham, told her last night that she was cured after she had been bedridden for 10 months with internal trouble.

Bedridden Woman Walks At Evangelist's Command

A DURBAN woman who had been bedridden for the past 10 months, rose up from a camp bed in the Durban City Hall last night where she had been taken to hear the American evangelist, the Rev. William Branham, and declared: "I feel as if I were two years old."

The Rev. Mr. Bhanham after a succession of people had come on to the stage to receive God's blessing suddenly turned to Mrs. J. A. Naude, of Blythswood Road and said: "You, Madam, have been suffering from internal trouble, but you are now cured—get up off that bed."

Mrs. Naude immediately rose to her feet, swayed a little and then walked to the end of the bed where her husband and daughter looked on in amazement.

Mr. Naude told a "Mercury" reporter that he had had a succession of doctors attending to his wife and they had told him that nothing could be done for her. He had spent his savings trying to make her well.

Pastor J. F. Wooderson, of Durban, said he had visited Mrs. Naude about a month ago at her home in response to Mr. Naude's request that he should go and pray for his wife.

TOLD SHE WAS CURED

Another woman from Sydenham who admitted that she had cancer and only a short time to live was told by the Rev. Mr. Branham that she had been cured.

First of all the evangelist diagnosed her complaint after she had confirmed that they were complete strangers and then, taking her hand in his, he pointed out to her that her disease had manifested itself in his own hand, which had become swollen.

He told her that if her disease could be cured his hand would become normal. There was a hushed silence as the Rev. Mr. Branham prayed fervently for several minutes and the woman closed her eyes. When they both looked at his hand it was normal; the woman left the stage sobbing with relief.

Another young man was told that he had been cured of tuberculosis and he admitted that he felt much better after he had received the evangelist's blessing.

The City Hall was packed, while thousands more people stood outside in the pouring rain listening to the service which was relayed through loudspeakers.

People came on stretchers, in wheel-chairs and on foot. Some blind, others crippled and some mentally ill, all hoping that something in the nature of a miracle might be achieved.

ANXIOUS RELATIVES

Nurses and first-aid men and anxious relatives ministered to their charges while the four-hour service was in progress.

All over the hall, as the tension mounted, women and even some men broke down and wept.

Early yesterday morning people were queueing outside the City Hall in the hope of obtaining seats. In the afternoon there was a service at which the Rev. W. J. Ern Baxter was the principal speaker, as he was again in the evening.

Mikato hii ya nakala za gazeti kuhusu mikutano ya huko Durban imetolewa kwenye gazeti la Natal Mercury, Durban.

Bibi J. A. NAUDE, wa Mtaa wa Blythswood, Durban, alipitisha siku tulivu jana, zaidi sana akipumzika, baada ya kuponywa kwake Jumatano usiku na mwinjilisti Mmarekani, Kasisi William Branham. Baada ya kulazwa kitandani kwa miezi 10, alimwambia atoke kwenye kitanda chake cha kambi na atembee. Wakati mpiga picha wa "Mercury" alipomtembelea jana alimkuta Bibi Naude akipanga maua, huku binti yake, Anne, mwenye umri wa miaka tisa, akimwangalia, amefurahia mama yake kupata afya tena.

Rises From Spinal Cast At Words Of Evangelist

A DURBAN woman who had not walked for four months rose from a plaster spinal cast and, supported by helpers, walked shakily across the City Hall stage last night after the Rev. William Branham had weakly spoken the words: "I have prayed for you. Go — you are cured." The woman, Mrs. M. M. van Niekerk, of Wentworth, has been in hospital for more than four months with spinal tuberculosis.

The City Hall was packed, and an overflow estimated at 3,000 people crowded the city gardens to hear Mr. Branham's words through loudspeakers.

An elderly man in the audience, whose disease Mr. Branham diagnosed as arthritis, was told to rise. He did—and the pain he once felt he felt no more.

"The lady next to you," Mr. Branham went on, "is your wife. And you, Madam, also suffer with arthritis. Rise—you are healed."

Another woman, Mrs. E. Raath, of Fynnland, rushed to the stage with an eight-year-old girl, who, she claimed, had had a squint. Her eyes had become perfectly normal.

Scores of people whom, it is said, doctors had given up for lost clambered on to the stage, declaring that they were no longer ill. "I lost my job because I had tuberculosis," said one. "Tomorrow I shall look for another job."

Imechapishwa tena kutoka katika gazeti la Natal Mercury, Durban.

Cripples Rise From Wheel-Chairs And Walk

SCENES of mass-healing, of cripples and stretcher cases getting up from wheel-chairs and beds and walking, followed a prayer by an American evangelist, the Rev. William Branham, before many thousands at the Greyville Racecourse, Durban, last night.

Mr. Branham, who exhorted all cripples, sick, deaf and dumb people to be healed, was led from the platform sobbing and supported by two helpers.

After he made his appeal one small boy, sitting in a wheel-chair, staggered to his feet and, with the support of two men, walked towards the platform. One after another others followed until a huge crowd surged forward; crippled women and children threw down crutches and leg-irons; mothers wept as children took a few steps, for some the first in their lives.

A Native rushed forward with his boy, who, he said, had had a twisted foot and body. "I was crying," he told "The Natal Mercury," "when I saw my boy's foot was straight; it was flat. He is whole."

An Indian boy went up to the stage and gave up his crutches and leg-irons. He walked up and down the steps. A club-footed Indian girl took up her discarded club boot.

One Indian girl, a tuberculosis and meningitis case, had been let out of hospital yesterday morning to attend the service. She was supposed to have gone back but she had not. Instead she went away, healed (she said) with her parents.

A cancer case who had not walked for nine months came to the service on a stretcher, got up on Mr. Branham's exhortation, and took away her stretcher. An Indian who had had a "locked" ankle for six months told "The Natal Mercury" that he was healed. He had come in the afternoon, he said, with his ankle stiff and immovable. He could now move it easily.

Men were praying over stretchers in cases where patients had not been healed. They prayed and urged the cripples to walk and the sick to be healed. On the other hand scores of people, mostly non-Europeans, flocked to the platform to testify cures.

In the background stood little Native girls on crutches, people with twisted bodies—smiling for the recovery of others, yet weeping because they had not been so fortunate.

Earlier Mr. Branham dealt with a 17-year-old Indian boy who had been deaf and dumb from birth. He clapped his hands and the boy smiled. The first words that came from his mouth were "Mama" and "Papa."

"I AM HEALED"

Mr. E. C. Dennis (45), of 365a Flower Road, Clairwood, stood on the platform at Greyville, blocking his left ear. He had not heard with his right ear since he was seven.

Another Evangelist, the Rev. F. F. Bosworth, whispered into his right ear, and Mr. Dennis repeated combinations of numbers over a microphone. The crowd, mostly Natives and Indians, cheered as they heard him say: "I am healed."

Imechapishwa tena kutoka kwenye gazeti la Natal Mercury, Durban, Ijumaa, 23 Novemba, 1951.

kipya cha sikio kwa nguvu za Mungu za uumbaji. Alipomaliza kumwombea mtu wa nne, vile vile tulijaribu kusikia kwake lakini tukakuta ya kwamba hakuweza kusikia. Tuligundua ya kwamba mtu huyo hakuwa amesikia ujumbe wala ahadi za Mungu, na kwa hiyo hakuwa na imani. Hili lilikuwa ni onyesho la umuhimu wa kusikia na kuliamini Neno.

Kabla Ndugu Branham hajakuja kwenye ibada ya alasiri, Ndugu Ern Baxter alihubiri ujumbe, kwa mtindo wake unaoeleweka kwa urahisi wenye kutia moyo, akielezea mpango wa Mungu wa ajabu wa wokovu wa mtu binafsi. Baada ya kutilia mkazo ya kwamba wokovu huu ulinunuliwa kwa gharama kubwa na kama walikuwa wapokee manufaa makamilifu ya huo ingewabidi wao kuyatoa maisha yao Kwake kama tu vile Kristo alivyokuwa ameyatoa maisha Yake kwa ajili yao, aliwaomba wale waliotaka kuwa Wakristo wasimame. Walisimama kwa maelfu. Kila mahali watu walisimama kwa miguu yao. Wale waliokuwa kwenye sehemu za Wazungu na za wasio Wazungu vivyo hivyo walionyesha shauku kubwa ya kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana wao. Ndugu Baxter alitugeukia sisi tuliokuwa tumeketi jukwaani kana kwamba kusema, "Hapana budi wamenielewa vibaya. Haingewezekana maelfu haya yote yawe ni ambao wanataka kuwa Wakristo." Baada ya kuelezea umuhimu wa hatua yao aliwaomba hao waliotaka kuwa Wakristo wapunge mikono yao. Tamasha kama hilo ambalo hatujawahi kabisa kuona. Katika zile ibada tatu za siku hiyo ilikadiriwa na wachungaji wa mahali hapo ya kwamba zaidi ya watu elfu thelathini walisimama kama ushuhuda wa shauku yao ya kumkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao.

Kabla ibada ya alasiri haijaanza, ripoti zilikuwa zikija za wale waliokuwa wamepokea uponyaji wao katika ibada ya asubuhi. Isingewezekana kusimulia matukio mengi ya uponyaji halisi uliotukia huko Durban siku hiyo. Ndugu Branham alipoona maono ya uponyaji aliwaelekezea watu kidole na kuwaambia ya kwamba walikuwa wameponywa. Kulikuwapo na wale waliotoka kwenye viti vyao vya magurudumu na kutembea, wengine kwa mara ya kwanza katika miaka mingi. Kulikuwako na viziwi na bubu waliotabasamu na kutoa sauti kwa kuwa waliweza kusikia kwa mara ya kwanza maishani mwao. Kulikuwa na watoto wadogo ambao wasingeweza kufahamu yote hayo lakini ambao sasa waliweza kutembea kwani hawakuweza kufanya hivyo hapo awali.

Kwa kweli hii ilikuwa ni siku kuu ya uamsho wa kiroho katika jiji la Durban. Kwa mujibu wa jeshi la polisi watu elfu hamsini na tano hadi elfu sitini walikuwa wamekuja kusikiliza Injili na wengine zaidi ya elfu kumi na tano waliorudishwa kutoka malangoni kwa ajili ya ukosefu wa

nafasi katika uwanja ulio mkubwa sana na mzuri sana wa mashindano ya farasi katika Afrika Kusini. Mungu alikuwa amenena na mioyo ya maelfu na alikuwa amewafanya wajitokeze wakasikilize Injili na wapokee uponyaji kwa ajili ya nafsi na mwili pia.

Katika toleo la Januari-Machi la "Mshika Bendera," lililochapishiwa Durban, tuna taarifa kutoka kwa wachungaji watatu wa mahali pale. Ripoti hizi hazitoi tu picha nzuri sana ya mikutano katika Durban bali muhtasari wa uamsho wote kwa jumla.

KUZURIWA KUKUU KWA AFRIKA KUSINI

Imeandikwa na Mchungaji A. H. Cooper, Mwenyekiti,

Kamati ya Branham ya Durban

Wakati Kasisi Wm. Branham na wafanyakazi wenzake, Kasisi W. J. Ern Baxter na Kasisi F. F. Bosworth, walipoanza ibada zao za Mikutano ya Uponyaji wa Kiungu Afrika Kusini, tarehe 4 Oktoba, si watu wengi waliotarajia mabadiliko makubwa ya kiroho yaliyofuata huduma yao. Hakika, Bwana amefanya mambo mengi sana zaidi ya yale tuliyoomba na kuwazia.

Kamwe kabla ya hapo mikutano kama hiyo haijawahi kufanyika katika nchi hii. Kamwe watu wengi hivi hawajawahi kuelekezwa kwa Mungu ama kubadilishwa katika wakati mfupi kama huo. Kamwe madhihirisho kama hayo ya wokovu wa Mungu na nguvu Zake za uponyaji hayajashuhudiwa, na ni imani ya wengi kwamba ushawishi mkubwa wa kiroho wa mikutano yao utaendelea sikuzote.

Katika miamsho hiyo yote huduma ya kimiujiza ilikuwa dhahiri. Kuweka kumbukumbu ya hao walioponywa hakungewezekana, bali mamia juu ya mamia walipokea nguvu za uponyaji wa Kristo, na walitutumia shuhuda zao. Idadi kubwa ilipokea uponyaji bila kuguswa na mwanadamu.

Kila mkutano, ambao ulihudhuriwa na maelfu na maelfu, ulipita kwa mbali matarajio ya watu katika miji mbalimbali iliyozuriwa. Watu 10,000 kamili ama zaidi walihudhuria kila usiku ibada za Johannesburg kwenye Uwanja wa Marantha. Katika kila mji kumbi zilizo kubwa kuliko zote zilionekana kwamba hazitoshi kabisa kuyakalisha makusanyiko hayo makubwa mno.

Siku baada ya siku, mamia ya wanaume na wanawake katika mikutano mbalimbali walimkubali Kristo kama Bwana na Mwokozi wao kutokana na mahubiri yanayoamsha nafsi na ya kweli ya Mwinjilisti Baxter; jumbe zake zenye upako kwa Wakristo hatutazisahau kamwe.



Picha imepigwa na Lynn Acutt

Moja ya picha za mkutano wa Durban ambao ulivunja rekodi zote za kuhudhuria zilizopita.

Picha imepigwa na Gorven

Sehemu ya wasio-Wazungu kwenye ibada ya Jumapili alasiri huko Durban.

Wala kamwe hatutasahau mafundisho ya thamani ya yule Mtume wa Imani, Kasisi Bosworth, ambayo yalichukua mahali muhimu katika kila mkutano, katika kuumba na kuchochea imani katika yule Mponyaji Mkuu. Tena na tena, chini ya huduma yake, tuliona roho za uziwi zikitolewa na viwambo vya masikio vikiumbwa tena. Hakuna kisa cha ugonjwa kilichoikatisha tamaa shauku ya imani ya shujaa huyu wa vita wa siku nyingi. Alitumika mfululizo na sisi kwa kweli tulijifunza kumpenda.

HUDUMA YA NDUGU BRANHAM

Imenenwa vizuri ya kwamba jambo la kipekee katika huduma ya Ndugu Branham ni ile karama yake ya ajabu sana ambayo humwezesha kugundua na kutambua magonjwa waliyo nayo watu. Dhihirisho hili ni kamilifu asilimia mia moja. Ni kitu kidumucho wakati wote na cha kushangaza sana. Kwa kuwa Ndugu Branham, kwa Roho wa Mungu, anaweza kujua katika sekunde chache, bila kosa, kile ambacho wakati mwingine ni majuma kadhaa ya uchunguzi kwenye kliniki unaweza kwa shida kugundua. Hii ni ishara kubwa sana, ikithibitisha ya kwamba Mungu anawazuru watu Wake.

Dhihirisho ambalo ni kubwa zaidi na la ajabu zaidi na la karibuni sana katika huduma ya Ndugu Branham ni karama yake ya Utambuzi na Neno la Maarifa, vipawa ambavyo humwezesha wakati akiwa chini ya upako kuwaambia watu mara moja siri za mioyo yao. Wakati mwingine kuna dhambi ambazo watu wameficha na ambazo hazijatubiwa, ambazo huwazuia kupokea uponyaji wao. Utambuzi huu wa kushangaza, uliodhihirishwa wakati mmoja katika huduma ya Kristo na ya Elisha, ni usioweza kupimwa kina, wa kipekee, na wenye utukufu; kutumika kwake huleta roho ya uchaji juu ya mkutano, na kwa kweli inawapeleka wenye kuiona kwenye siku za nyuma za miujiza za Biblia.

Akikanusha nguvu zo zote zake binafsi za kuponya, yeye hakukosa hata mara moja kuwaelekeza wanaume na wanawake kwa Bwana Yesu. Wahudumu wa madhehebu mbalimbali walihudhuria ibada hizo — baadhi yao waliamini na wakabarikiwa sana, na wengine tena hawakuamini na sasa wanapinga.

MKUTANO WA KIHISTORIA WA DURBAN

Historia ya kanisa ilifanyika kwenye siku ya mwisho ya uamsho huo wakati karibu watu 45,000, Wahindi, wenyeji na Wazungu walipokusanyika pamoja kwa ajili ya ibada ya alasiri kwenye Uwanja wa Mashindano ya Mbio za Farasi. Baadhi walikisia idadi ya juu zaidi. Mapema zaidi kabla ya

mkutano kuanza malango yalifungwa na maelfu waliachwa nje barabarani. Kwenye ibada ya asubuhi takriban watu 25,000 walikuwa wamehudhuria na jioni 23,000—kulingana na makadirio ya chini sana ya magazeti. Na idadi hii ya kushangaza sana ilivumilia—kwa saa nyingi—joto kali sana, lililofuatana na pepo za vimbunga na baadaye na mvua. Kamwe, kamwe hao waliojaliwa kuhudhuria ibada hizi hawatasahau tamasha la uchaji, wala matokeo yenye utukufu yaliyofuata.

Matokeo ya kiroho huko Durban katika siku hizi tano za mikutano ya ajabu yamewagusa maelfu ya wanaume na wanawake katika kila kiwango cha maisha. Afrika Kusini haijawahi kuona kitu kama hicho.

Ibada zilizofanywa kwa ajili ya Wazungu peke yao zilifanyika katika Ukumbi wa Jiji. Lilifurika tele likiwa na kusanyiko lililofikia watu 4,000, na mamia na mamia wakisimama nje wakisikiliza kupitia kwenye vipaza sauti. Licha ya mvua, wengi wao walikaa mpaka mwisho wa mikutano hiyo na huku mikono imeinuliwa juu, walijiunga na lile kundi kubwa lililokuwa ndani waliomkubali Kristo kama Bwana na Mwokozi wao.

Utukufu kwa Mungu Aliye Juu sana. Hakuna maneno ya mwandishi yanayoweza kuelezea shukrani za maelfu walioongozwa kwa Kristo katika uamsho huu pamoja na hiyo mingine.

UPONYAJI WA KIJUMLA

Moja ya mambo ya kushangaza sana ya miamsho hii ilikuwa ni uponyaji wa kijumla. Ndugu Branham mara nyingi aliwafundisha watu kuwekeana mikono wao kwa wao katika Jina lenye mamlaka la Yesu na wadai kuwekwa huru hao waliokuwa wakiugua miili. Maombi yake yenye upako yaliyofuata yaliwafanya watu kuwa na imani kwa Mungu. Waliponywa papo hapo magonjwa mbalimbali na mateso—viziwi walisikia, viwete walitembea na vipofu wakaona. *Ajabu sana!*

Jambo ambalo ni la ajabu jinsi iyo hiyo ni kwamba matukio ya kuponywa kwa ajabu sana yangali yanatukia—kulingana na shuhuda mwandishi huyu anazopata siku baada ya siku. Kwa unyenyekevu tunampa heshima zote, sifa na utukufu Bwana na Mwokozi wetu aliyefufuka.

"Amini tu, amini tu, yote yawezekana, amini tu" lilikuwa ndilo pambio la msingi la kila mkutano na ingawa miaka 1900 imepita tangu yalipotamkwa na Kristo wa Kalvari, maelfu

Picha ilipigwa na Lynn Acutt

Mvulana wa Kihindi ambaye aliponywa mara moja akiwa kwenye kusanyiko mguu mfupi na uliopooza.

ya watu wasiohesabika katika Afrika Kusini wamezinduka kwenye ukweli kwamba ni makamilifu na ya kweli leo kama tu wakati ule yalipotamkwa.

UAMSHO WA BRANHAM HUKO DURBAN

Imeandikwa na Mchungaji John F. Wooderson

"Kwa sababu hukutambua majira ya kujiliwa kwako... nyumba yako imeachwa kwako ukiwa..." Nikizungumzia kusanyiko langu mwenyewe Jumapili mbili kabla ya ule Uamsho wa Branham wa Uponyaji haujaanza Durban, nilijikuta mwenyewe, nilipokuwa nikizungumzia juu ya fungu la maneno yaliyonukuliwa, nikishurutishwa na Roho Mtakatifu kufanya tamshi hili: "Hivi karibuni tutakuwa na kile ninachoamini kitakuwa ni kujiliwa kwa kimbinguni na Mwenyezi Mungu kwenye jiji hili. Hebu na isisemwe kwa ye yote wenu, 'Hukujua siku ya kujiliwa kwako...' Ingia kwenye mstari wa baraka! Na kama Mungu akichagua kukutumia katika siku chache zifuatazo, jiweke kikamilifu chini ya mamlaka ya utumishi Wake."

Ziara ya Ndugu William Branham na wenzi wake, Ndugu Baxter na Ndugu Bosworth, kulihakikisha kwa kweli kuwa ni majira ya kujiliwa kwa jiji letu zuri na Mungu, SIKU TANO TU...bali ni siku tano ambazo kamwe hazitasahauliwa na maelfu kwa maelfu ya wanaume na wanawake. Haiwezekani kukisia hata sehemu ndogo sana ya yale yaliyotendeka katika kipindi hicho kidogo cha wakati. Kuweka jumla ya mambo yote—jiji hili lilipokea mabadiliko makubwa sana ya kiroho lililopata kuona.

Ingawa kulikuwako na matayarisho makubwa kwa majuma mengi kwa ajili ya mikutano hii...makaratasi makubwa ya matangazo yaliyobandikwa kote jijini, magari madogo kila mahali yakibeba maandishi kama njia ya matangazo...hata hivyo ilikuwa ni mpaka wakati ibada ya kwanza ilipofanyika katika Ukumbi wa Jiji Jumatano alasiri, tarehe 21 Novemba, ambapo wakazi wa Durban walitambua kitu fulani kisicho cha kawaida kilikuwa kikitukia. Ukumbi wa Jiji kujaa umati wa watu wasioweza kuingia kwenye ibada ya dini—na hiyo ilikuwa ni alasiri katikati ya juma, kulikuwa na jambo lisilo na kifani kabisa. Habari zilisambaa kama moto kwenye mbuga pana za manyasi! Jioni hiyo, licha ya watu waliokisiwa kuwa ni 4,000 waliokuwa *ndani* ya ukumbi huo, idadi iliyokadiriwa na magazeti ya mahali hapo kama ni 2,000 walisimama *nje* wakisikiliza ibada kupitia kwenye mfumo wa kupaza sauti. Na ingawa Durban ilipata dharuba mbaya sana ya radi usiku huo, wengi walibaki kwenye mvua iliyokuwa ikinyesha kwa nguvu, wamenaswa na nguvu za Neno la Mungu lililohudumiwa na Mwinjilisti W. J. Ern Baxter. Huu ulikuwa ni

Picha imepigwa na Lynn Acutt

Mabasi haya ni "Maalum" yakingojea kuurudisha umati nyumbani kutoka katika uwanja wa mashindano ya mbio za farasi. Durban ni jiji kubwa na lina mlolongo mkubwa wa mabasi ya Manispaa na ya watu binafsi bali hakukuwako na mabasi ya kutosha Durban nzima kuwahudumia watu wote.

mwanzo tu! Na kilichofuata ni vigumu kusimulia! Thibitisho la Neno la Mungu kwa ishara na maajabu, wakati wagonjwa walipoombewa katika ibada hiyo ya kwanza, kulisababisha msisimko unaofanana na ule uliotukia wakati wa huduma ya duniani ya Bwana Yesu.

Tangu mwanzo ilikuwa ni dhahiri kwa wote ya kwamba mkazo mkubwa ulikuwa ni juu ya wokovu wa nafsi. "Unaweza kwenda Mbinguni ukiwa na mwili mgonjwa, bali huwezi kwenda kule ukiwa na nafsi gonjwa," alisema mtumishi wa Mungu katika mahubiri yake ya kuweka Kweli, yenye nguvu, yanayovutia na kushawishi. Na bila kujali wadhifa, imani au rangi, wanaume kwa wanawake walifanywa kutambua ya kwamba kulikuwa na njia MOJA tu, na hiyo ilikuwa ni NJIA YA MUNGU...kwa imani katika Bwana Yesu Kristo... wapate kuokolewa. Ilikuwa si ajabu basi ya kwamba kila wakati nafasi ilipotolewa kuamua kwa Kristo, umati ulisimama kwa miguu yao na kwa shauku wakainua mikono yao wapate kadi ya uamuzi. Ni uamsho wa kujichunguza moyo wenye nguvu jinsi gani wa Roho wa Mungu uliotokea! Wengi wameshuhudia tangu wakati huo ukweli kwamba ingawa walikuja kwenye ibada wakiwa na mahitaji yao ya kimwili, haya karibu yalikuwa yasahaulike kabisa kwa kujua dhambi na hatia iliyowajilia. MUNGU ALIKUWA YUPO, nao WALIJUA JAMBO HILO! Nimewasiliana binafsi na watu wengi zaidi ya ninavyoweza kukumbuka ambao sasa ni "viumbe vipya katika Kristo

Yesu" . . . wameongoka kwa furaha sana na kuzaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu. Nilisimamishwa na mhariri mmoja wa habari mtaani na nikaambiwa yafuatayo: "Bw. Wooderson, ndugu yangu aliyekuwa kafiri wa kupindukia amebadilika kiajabu sana. Siwezi kujizuia, na kama Bw. Branham alikuja tu jijini kwa ajili ya kile kilichompata . . . ilifaa." NA SEHEMU HII YA UAMSHO WA BRANHAM imetuletea ujumbe wa kina kabisa wa shukrani kwa Mungu kwa ajili ya kujiliwa na watumishi Wake.

Bali je! sio HUDUMA YA KIMIUJIZA waliyopewa watu na Mungu katika siku hizi ambalo ndilo jambo muhimu sana na lenye nguvu sana katika uamsho wa kiroho wa nchi za ulimwengu? Je! hili silo jibu la Mungu kwa wakati wa hali ya kutojali, kutokuamini na kushuku? Chini ya huduma iliyoheshimiwa na Mungu ya Ndugu William Branham tamasha za kushangaza sana zilishuhudiwa. Mtu asingejizuia kukumbushwa siku za Agano Jipya. Wagonjwa walikuja kutoka kila mahali . . . wakiwa na mateso ya kila namna . . . wengine wakiwa na mikongojo, viti vya magurudumu, na machela. Ile karama ya ajabu sana iliyokuwa na mtumishi wa Mungu, iliyodhihirishwa katika kuyatambua magonjwa ya wanaume na wanawake, pamoja na unyenyekevu wake mkuu na huruma nyingi sana kwa ajili ya wanadamu wanaoteseka lilikuwa ni thibitisho linaloonyesha ukweli ya kwamba yeye alikuwa kweli ni "MTU ALIYETUMWA KUTOKA KWA MUNGU." Kamwe hatutasahau maombi hayo ambayo yalitoka katika kilindi cha ndani kabisa cha nafsi yake, wakati alipomsihi Mungu kwamba "uwahurumie maskini watu hawa na UWAPONYE." Na wakati alipokuwa akiomba, jibu lilikuja! Kila mahali katika makusanyiko hayo wanaume na wanawake walikombolewa kutoka katika nguvu za Shetani miilini mwao. Viungo vilivyopindika vilinyoshwa, vipofu waliona, viziwi walisikia. Kansa, vivimbe, magonjwa ya moyo yaliponywa katika jina la Yesu. Ndugu Branham kwa uaminifu alilielekeza kusanyiko lake kubwa kwenye chanzo pekee cha uponyaji, wala hakusita kamwe kukanusha wazo kwamba yeye alikuwa na uwezo wowote wa kuponya.

Mafundisho ya kujenga juu ya uponyaji wa Kiungu yaliyotolewa na Ndugu F. F. Bosworth, ambaye tunamchukua kama mtangulizi wa huduma ya kimiujiza ya karne ya 20, yalichochea na kuimarisha imani ya wengi. Imani yake jasiri katika maombi kwa viziwi bubu na matokeo yaliyofuata yalikuwa ni kichocheo kwa maelfu kumtumaini Mungu kwa ajili ya uponyaji wao.

Historia ilifanyika huko Durban Jumapili, tarehe 25 Novemba, siku ya kumalizia huo uamsho. Kile kilichoshuhudiwa kilikuwa zaidi ya matarajio ya wote kabisa. Katika Uwanja wa Mashindano ya Mbio za Farasi wa Greyville (tuliotunukiwa

kwa ukarimu tupate kuutumia tarehe 22 na 25 za Novemba) ibada za kimataifa zilizo kubwa kuliko zote zilizowahi kuendeshwa katika nchi hii zilifanyika. Kiongozi wa Uwanja huo wa Mashindano ya Mbio za Farasi anakadiria idadi ya chini umati wa karibu watu 40,000! Idadi hii haikujumlisha maelfu ya waliosimama nje, wasioweza kuingia. Maelfu na maelfu ya Wahindi na wenyeji walisimama siku nzima muda mrefu tangu kabla ya saa kumi na moja usiku chini ya hali iliyokuwa ngumu sana ya hali ya hewa. . . joto kali kupita kiasi asubuhi, upepo mkali alasiri, na mvua jioni. Lakini wao wala maelfu ya Wazungu hawakuijali hali ya hewa. Siku nzima kila mahali kwenye umati huu mkubwa mno wa watu Mungu alikuwa akiwaponya wagonjwa. Huko mbali katika sehemu ya wenyeji, ambako ilikuwa ni vigumu kumwona Ndugu Branham, miujiza ya kushangaza sana kuliko yote iliripotiwa. Upepo ulipokuwa ukivuma na mvua ikinyesha, wanaume na wanawake walisikiliza kwa shauku isiyopungua huduma ya kuchochea nafsi ya watumishi wa Mungu. Ni kitu gani kingaliweza kusababisha haya yote ila KUJILIWA KWA NGUVU NA MUNGU MWENYEWE KWA JIJI HILI! Kamwe kuimba kwa namna hiyo hakujapata kusikiwa kama kule kulikoijaza hewa wakati Ndugu Baxter alipoliongoza kusanyiko hilo kubwa mno katika kuimba kwa mtindo wake wa pambio tamu linalojulikana sana, "Yesu, Yesu, Yesu, Jina Tamu Sana ninalojua; Linajaza kila shauku yangu, Linanifanya daima kuimba nikitembea." Kumbukumbu za Mbinguni tu ndizo zitakazofunua kile kilichotukia kwenye siku hiyo ya kumbukumbu, isiyo na kifani. Maelfu walimkubali Kristo kama Mwokozi wao, wakionyesha jambo hilo kwa mkono ulioinuliwa, na idadi kubwa mno walipokea uponyaji kwa ajili ya miili yao. Kuimbwa kwa ule wimbo wa kale, "Kaa nami, ni usiku tena," kulikuwa ni kipeo chenye utukufu kwa ibada iliyo kuu sana iliyopata kufanyika Afrika Kusini.

Kesho yake tulikuwa kwenye hisia zilizochanganyikana tulipokusanyika kwenye uwanja wa ndege. Wakati Ndugu Branham na kundi lake walipokuwa karibu kupanda ndege walipewa ujumbe ufuatao kwenye vipaza sauti: "Zikipaza sauti. . . Kasisi Branham, Kasisi Baxter, Kasisi Bosworth na Billy Branham! Kamati ya Branham ya Durban, kwa niaba ya wakazi wa Durban, inataka kutoa shukrani zao nyingi sana kwa Mungu na kwenu, watumishi Wake, kwa ziara yenu kwenye jiji hili na baraka zilizoletwa kwa maelfu ya watu kwa ziara hiyo; na tunaomba ya kwamba Bwana atawapa rehema za safari na kuwarudisha kwetu." Na wakati tu tulipokuwa tukitafakari jinsi ziara ya watumishi Wake hasa imemaanisha nini kwa jiji hili, tunajisikia ya kwamba maneno yaliyotamkwa hapo juu hayatoshi kabisa.

Kikosi cha Branham kilikuwa kimeondoka. . . BALI KAZI ILIENDELEA! Kuzinduka kukuu zaidi katika matukio ya siku

tano zilizopita kulipambazuka mioyoni mwetu. Jiji lilikuwa limesukwasukwa! Kila sehemu ya jamii ilihisi matokeo ya kujiliwa huku kukuu na Mungu. Ilionekana kuwapo kwa mada moja ya mazungumzo. Wanaume na wanawake ambao hapo awali hawakuwa na wazo la Mungu ama haja ya Yeye walikuwa wadadisi wenye hangaiko. Kwa upande mwingine sauti ya wakinzani ilizidi kupazwa, na kama ilivyo kawaida, hawakujaribu kuficha dhihaka zao na kushuku kwao. Lakini pamoja na upinzani huu kulikuwako na mafuriko ya shuhuda zilizokuwa zikitiririka kutoka kila upande, za baraka za kimwili na za kiroho zilizopokelewa...mpaka, kama vile katika siku za Kristo, "kulikuwako na mgawanyiko kati ya watu"; wengine waliamini, wengine hawakuamini. Asiyeamini daima atapata kile kitakachoimarisha kutokuamini kwake, bali Bwana Yesu Kristo alisema: "Yote yanawezekana kwake aaminiye." Na wakati maelfu walipoimba maneno hayo ya pambio hiyo iliyopendwa sana, "Amini tu, amini tu, Yote yanawezekana, Amini tu"...WENGI waliinua mkono wa imani, "wakagusa upindo wa vazi Lake," na wakaponywa.

SIKU TANO ZA UAMSHO USIOWEZA KUSAHAULIKA

Imeandikwa na Mchungaji H. W. Oglivie

Loo, laiti ningalikuwa na kalamu ya mwandishi hodari! Katika kujaribu kusimulia Uamsho wa hivi majuzi wa Uponyaji wa Branham uliofanyika Durban kutoka November 21 hadi 25, 1951, mtu angetaka kuwa na maneno ya kimbinguni kuelezea huduma ya kimbinguni ya Bwana miongoni mwa watu. Kujiliwa huku kwa ajabu na Mungu, pamoja na umati wa kushangaza uliovunja rekodi ambao ulisongamana katika Ukumbi wa Jiji na Uwanja wa Mbio za Farasi wa Greyville, kulifanya ziara ya Ndugu Branham na wafanya kazi wenzake kutokusahaulika kamwe.

Inakadiriwa kwamba Wahindi, wenyeji na Wazungu 50,000 walihudhuria ibada ya Jumapili jioni—idadi kubwa kuliko zote ya watu iliyopata kukusanyika kwa ajili ya mkutano wa dini Afrika Kusini. Kundi la Uamsho lilikiri kwamba kamwe hawajapata kuona kitu kama hicho. "Mungu ni wa ajabu!" "Ni ajabu sana!" yalikuwa ndiyo matamshi yaliyosikika kila mahali. Ukumbi wa Jiji kwa jumla ulikuwa mdogo sana, na hata nafasi za ziada za kuketi hazikutosha. Kwa kweli maelfu walishindwa kupata ruhusa ya kuingia. Hata hivyo, vipazasauti vilikuwa vimewekwa kwa ajili ya msaada wa wale waliokuwa nje na lilikuwa ni tamasha la kutia moyo kuona wengi wao wakiinua mikono yao wakati wito ulipotolewa wa maamuzi kwa ajili ya Kristo.

Madhihirisho ya nguvu za Mungu za uponyaji yalikuwa ni makubwa na wengi wenye magonjwa yasiyotibika waliponywa bila kuwekewa mikono; viziwi walisikia, viwete waliponywa! Wengine walitoa magango ya feleji kutoka miguuni mwao na wengine tena walishika mikongojo yao mikononi mwao wakitembea huku na huko kudhihirisha uponyaji wao. Halafu kulikuwako na wale waliofurahia kuumbwa kupya kwa kiwambo cha sikio na wakadai wangeweza kusikia kunong'ona kuliko kudogo sana. Kweli, nguvu kuu za Mungu zimepita ufahamu wa binadamu. Haleluya!

Maelfu ya watu huko Durban na kwenye wilaya kamwe hawatakuwa vile walivyokuwa tena baada ya kuhudhuria ibada hizo muhimu sana. Mahubiri yenye nguvu ya Ndugu Baxter, mafundisho yanayopenya ya Ndugu Bosworth, na huduma iliyojaa upendo ya Ndugu Branham kumebadilisha maisha, kukavunja mioyo mikaidi, kukawarejesha waliorudi nyuma, kukaondoa ubaguzi, kukaamsha imani na ujasiri katika Mungu na katika Neno Lake. Wengi walioitumikia dhambi na kumtumikia Shetani sasa wanamtumikia Bwana. Wengi waliolikufuru jina la Yesu sasa wanaimba sifa Zake.

"Yesu, Yesu, Yesu,
Ni jina tamu kuliko yote nijuayo,
Linatosheleza kila shauku yangu,
Linanifanya niendelee kuimba ninaposafiri."

* * *

Tulipokuwa Afrika Kusini ibada nyingi zilichukuliwa katika kanda. Kanda hizi ziliachiwa Sidney Smith wa Durban aliyeziazimisha kwa mtu ye yote aliyetaka kuzitumia kwa mikutano ya Wazungu ama wasio Wazungu. Hapa nina nukuu la barua ambayo alinitumia nami nitanukuu: "Tulicheza urekodishaji wa kwanza wa ibada ya Branham jana usiku kwenye Kanisa la Full Gospel huko Wentworth, na ingawa ilikuwa ikinyesha sana nafikiri ulikuwa usiku wa ajabu sana ambao hilo kanisa lilipata kuwa nao. Hizi ibada zilizorekodiwa katika kanda ziliwakumbusha watu ya kwamba ingawa Ndugu Branham alikuwa ameondoka kwenda Marekani, hata hivyo sauti yake haikuwa imeondoka. Wangeweza kuja na kusikia maombi yenye nguvu ambayo Ndugu Branham alikuwa ameyatoa akiwaombea wagonjwa, kwa ajili ya mwili na nafsi pia."

Baada ya kufungwa kwa mikutano huko Durban, William Branham, Ern Baxter, na Billy Paul Branham waliruka kwa ndege hadi Salisbury, Rhodesia ya Kusini, na kufanya mikutano kule tarehe 28 na 29 Novemba. Ripoti za mikutano hiyo zilionyesha ya kwamba siku hizo mbili zilitokea kuwa ni baraka kuu kwa maelfu ya wengi. Mamia ya watu walikuja kutoka sehemu mbalimbali za Rhodesia ya Kusini na Kaskazini ambao hawakuweza kuhudhuria mikutano huku Afrika Kusini.

A Recording of a Complete Healing Service by

WILLIAM BRANHAM

(A Man Sent From God) will be given at the

Divine Healing Service

in the

FULL GOSPEL CHURCH WENTWORTH

(7 Brighton Road, Jacobs)

TO-NIGHT (SUNDAY)

7 p.m.

For those who did not hear Rev. Branham this is an opportunity to do so. Come and hear the mighty prayer that healed the sick, blessed the stricken and cast out all manner of evils.

NOTE: At the conclusion of the recording the Healing Ministry of the "Laying on of Hands" (Jms. 15.4) will be administered to the sick in Jesus's Name.

COME BELIEVING . . .
GO AWAY WITH HEALING!

67M2

Makala iliyokatwa kutoka gazetini ikitangaza Mkutano wa Branham kwa njia ya urekodishaji wa kanda.

Wakati uo huo, mimi pamoja na Ndugu Bosworth tuliendelea kwenda Pretoria, ambako yeye aliwahudumia watu, akihubiri mara tatu na mara nne kwa siku. Pretoria ndio makao makuu ya utawala wa Shirikisho hili na umekuwa na nafasi muhimu katika historia ya Afrika Kusini. Zaidi ya karne moja iliyopita ulikaliwa na Makaburu Wasafiri waliotoka Ghuba, wakisukumwa kaskazini na masetla wapya kutoka Ulaya. Karibu na Pretoria kuna mnara mkubwa na unaopendeza sana wa kumbukumbu unaojulikana kama Mnara wa Kumbukumbu wa Voortrekker. Ukanda wa kupendeza wa nakshi uliofanyizwa kwa marmar unasimulia historia ya Safari ndefu ya kutoka Koloni la Ghuba. Mtu asingeweza kujizuia bali ashangae sana na kupigwa na bumbuazi, akitambua gharama waliyolipia hawa watangulizi katika kulifungua bara la Afrika ya Kusini kwa ajili ya jamii ya

Sehemu ndogo sana ya umati kwenye ibada ya Jumamosi jioni.

kizungu. Mnara huu wa kumbukumbu umejengwa kwa mfano wa madhabahu zilizojengwa katika zama za Ibrahimu. Kuna kulinganisha kati ya kuondoka kwa Ibrahimu kutoka Uru wa Kaldayo na kutoka kwa hao Makaburu waliotoka Capetown wakaenda kutafuta nchi mpya. Hakuna mnara wa kumbukumbu ungaliweza kuwa na maana zaidi kwa watu wake kuliko kile mnara huu unachomaanisha kwa Makaburu wa Afrika Kusini.

Ndugu Branham, Ndugu Baxter, na Billy Paul walirudi kutoka Salisbury kwa wakati mzuri kuhudhuria ibada ya jioni huko Pretoria Jumamosi usiku. Matayarisho mazuri yalikuwa yamefanywa na kamati ya mahali hapo. Watu walikuwa wameelekezwa vizuri na kwa imani na matarajio walisikiliza kwa makini ujumbe wa Ndugu Baxter na halafu wa Ndugu Branham.

Maafisa wa polisi wa kienyeji waliouongoza umati kwenye mikutano ya wenyeji huko Pretoria.

Jumapili ilikuwa ni siku nyingine ambapo wengi walimpata Kristo kama Mwokozi wao na kujipatia uponyaji wa kimwili ambao ni sehemu ya Upatanisho wa Kristo. Mikutano yetu kwenye Uwanja wa Maonyesho huko Pretoria ilimalizikia Jumapili usiku, tarehe 2 Desemba, kukiwako na karibu watu 10,000 waliohudhuria.

Ifuatayo ni taarifa kutoka kwa Ndugu Gschwend kuhusu matokeo ambayo mikutano hii ilikuwa nayo miongoni mwa wenyeji.

"Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, wala usizisahau fadhili zake zote. Akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote, aukomboa uhai wako na kaburi, akutia taji ya fadhili na rehema, aushibisha mema uzee wako, ujana wako ukarejezwa kama tai." (Zaburi 103:2-5)

Ni kwa moyo uliojaa shukrani ambapo tunashuhudia juu ya baraka zilizopokelewa kupitia huduma ya Kikosi cha Branham. Hakika ilikuwa ni kujiliwa na Mungu kupitia watumishi Wake wenye vipawa. Ingawa huduma yao kwa jamii ya wenyeji ilikuwa na mpaka kwa wajibu wao kwa jamii za Kizungu tunamshukuru Mungu ya kwamba nguvu Zake hazikuwa na mpaka! Tuliongozwa kuanza na mikutano mikubwa ya hema tarehe 28 Novemba, ambayo kutoka mwanzo kabisa ilihudhuriwa vizuri sana. Kila asubuhi saa kumi na mbili mamia kadhaa ya wanaume na wanawake walikusanyika kwa ajili ya maombi. Mikutano ya alasiri na ya jioni ilihudhuriwa na umati mkubwa sana tuliopata kushuhudia katika sehemu hizi. Umati uliongezeka ukazidi watu 6,000 (ingawa wengine walikadiria idadi kuwa ni ya juu zaidi). Hema nne kubwa zilikuwa zimepigwa, mojawapo ilikaliwa na Wahindi na machotara wa Pretoria.

Alasiri ya kwanza kabisa ambayo Ndugu Bosworth alihudumu, Mungu aliibariki huduma ya mtumishi Wake mwaminifu katika njia ya ajabu sana. Kuhubiriwa kwa Neno kweli kulipata mlango wa kuingia katika mioyo ya wasikilizaji, kukiumba imani kwa ajili ya kuponywa kwa miili yao kwa Kristo Yesu. Baada ya kuomba pamoja na kundi la wagonjwa, ambao kati yao walikuwamo na wengine viziwi na bubu, wote waliponywa papo hapo isipokuwa mmoja ambaye, hata hivyo, tunaamini angali anaweza kuponywa. Jambo hili, hakika, lilifanya imani ya wasikilizaji kufikia kiwango cha juu zaidi. Halafu Ndugu Bosworth aligeuka kuuombea umati, akiwaambia waweke mikono yao kwa imani juu ya sehemu ya mwili wao iliyo na ugonjwa, na wakati walipoungana naye katika maombi, Mungu katika neema yake ya ajabu aliigusa miili mingi migonjwa na kuwaponya papo hapo.

Mwanamume mmoja kipofu kabisa aliyekuwa kipofu kwa muda wa miaka kumi na saba naye mgonjwa wa hospitali

ya vipofu ghafla alianza kumsifu Mungu akipiga makelele, "Kea bona, kea bona"—(Naweza kuona! Naweza kuona!) Na Mungu na ashukuriwe angali anaweza kuona leo hii. Msichana mmoja kiziwi na bubu mwenye umri wa kama miaka kumi alipokea kusikia kwake pamoja na kuzungumza kwake, ingawa kwa kuwa hakuwa amewahi kuzungumza hapo kabla ilibidi ajifunze kutamka maneno, bali alijifunza haraka sana. Mwanamke aliyekuwa amepooza upande mmoja kwa muda wa miaka arobaini, wala asingeweza kulala kwa upande huo, wala asingeweza kutumia mikono yake, alijikuta akilala na upande uliopooza kesho yake asubuhi baada ya kuponywa siku moja kabla, na pia akaweza tena kutumia mikono yake. Mmoja wa wainjilisti wetu alikuja amejaa furaha, akimsifu Mungu, akitwambia ya kwamba alikuwa amewaleta wagonjwa wanne, na wote waliponywa! Mmoja alikuwa ni kiziwi, mwingine kwa muda wa zaidi ya miaka kumi alikuwa amevimba shingo na koo, magonjwa ambayo yalimpa maumivu makali sana na kumzuia asiweze kuzungumza, bali hakuponywa kikamilifu, mbali na hao wengine waliokuwa na shida za ndani ya miili yao. Mmoja wa watumishi wetu wa kienyeji alikuwa na kivimbe kwenye tumbo lake la uzazi kwa miaka mingi, na wazazi wake walikuwa wamemlipa mchawi wanyama watatu kwa ajili ya uponyaji wake bila ya kupata msaada wo wote. Aliambiwa na madaktari Wazungu afanyiwe upasuaji, bali yeye alimtumainia Mungu. Sasa Mungu alikutana naye kwenye mkutano wa kwanza wa uponyaji wa Kiungu wakati kivimbe chake kilipotoweka, jambo ambalo kwalo tunamshukuru Mungu.

Mwanamke mzee aliyekuwa kipofu kabisa alipokea kuona kwake, hivi kwamba sasa anaweza kufanya kazi zake tena, akimsifu Mungu. Mwanamke mwingine alikuwa siku za karibuni amemlipa mmoja wa waganga wa kienyeji pauni thelathini na tano na maksai mweupe, bali akahofu kwamba matibabu yake yangemwua badala ya kumponya. Aliposikia juu ya hii mikutano ya kushangaza, alitoroka apate kuja na kusikiliza yale ambayo Mungu angeweza kufanya. Mungu alikutana naye na kuponya shida zake zote za ndani ya mwili, naye amepona kabisa. Mwanamke mmoja aliyekuwa kipofu katika jicho lake na kiziwi katika sikio lake la kushoto alinijia mimi na kuniambia jinsi ambavyo Mungu alikuwa amemponya jicho lake pofu hivi kwamba aliweza kuona vizuri sana, bali alitaka kujua ni kwa nini Mungu hakuwa amemponya sikio lake. Nilipomwangalia niliona hereni kubwa ikining'inia kutoka kwenye sikio lililokuwa ziwi, wakati hakuwa na hereni kwenye sikio lililo zima. Hili lilinifanya mimi kufahamu ya kwamba alikuwa ameweka hereni hiyo kama hirizi kwa ajili ya uponyaji wa sikio lake. Nikamwambia, "Ulimtumaini Mungu kwa ajili ya jicho lako, naye ameliponya jicho lako. Bali unaitumaini hiyo sanamu ya hereni kwenye sikio lako kuponya sikio lako, na bila shaka Mungu hawezi kukufanyia

jambo lo lote. Ondoa sanamu hiyo na umtumainie Mungu kwa ajili ya sikio lako kama vile ulivyotumaini kwa ajili ya jicho lako, Naye atakuponya." Baada ya kushawishiwa na wengine alimwondoa mungu wake wa uongo, ndipo Mungu kwa neema alikutana naye na kulifungua sikio lake. Hiki kilikuwa ni kizindua macho kwa wengi ambao wangali walikuwa kisiri wakitumainia madawa yao ya kishenzi na hirizi za wachawi.

Tulifurahi kuona wengi wakitupa miungu yao ya uongo ili kwamba Mungu aliye hai aweze kukutana nao. Pia tunamshukuru Mungu kwa kutenda kazi katika mioyo yao hivi kwamba hawakuwa tu wakitafuta kuponywa kwa miili yao, bali wokovu kwa ajili ya nafsi zao. Kwenye jioni mbili wengi walikuja mbele wakitupilia mbali sigara zao, viko vyao vya tumbaku, vijaluba vya ugoro, hirizi za kishenzi na madawa. Hata dadu walizotumia kucheza nazo kamari zililetwa jukwaani, nasi tulishangaa kuona baadhi ya "Tsotis" na "Amalites" (majambazi wa Kiafrika) wakileta visu vyao ambavyo walivitumia kuwachoma navyo watu. Ingawa hatukuwa tukihubiri dhidi ya mapambo ya nje ya wanawake, tulifurahi sana kuona wengi wao wakitoa hereni zao, bangili, nk., wakizisalimisha kwa Mungu, huku wakiitoa mioyo yao Kwake. Wakati ibada za uponyaji zikiendelea kila alasiri, Mungu pia aliendelea kufanya kazi na akawaponya wengi walioteseka kwa neema Yake ya ajabu. Mwanamke mmoja aliyepooza ambaye alitembea kwa shida, akiwa amepindwa kwa kuinamishwa chini na miaka ya mateso, alifunguliwa kutoka katika mateso yake na anaweza kutembea wima tena. Wengine ambao ilikuwa ni vigumu kwao kuishi kwa ajili ya pumu, TB, na magonjwa mengine waliponywa. Shuhuda zingali zinaingia za hao ambao wasingeweza kushuhudia kwenye mikutano, bali sasa wanaandika kutoka kwenye makazi yao mbalimbali wakituambia jinsi Mungu alivyokutana nao.

Tulisikitika sana kwamba huduma ya Ndugu yetu mpendwa Branham iliwekewa mipaka sana bali tunamshukuru Mungu kwa huduma yake fupi ya Jumapili alasiri, na ya kwamba Mungu kwa neema Yake aliikomboa kwa kugusa tena wengi walioteseka kwa nguvu Zake za kiungu. Mkono wa Mungu wa baraka ulikuwa juu ya mikutano hiyo sana hata Ndugu Bosworth aliitoa hiyo siku yake pekee aliyokuwa nayo ya mapumziko na kuhudumu tena Jumatatu usiku, ambayo ilikuwa ni siku kuu sana, uwepo wa Mungu ukidhihirishwa kwa ajabu sana katika mikutano mitatu iliyofanywa.

Habari za kutenda kazi kwa ajabu kwa Mungu zilisambaa upesi kote nchini hivi kwamba hata baada ya kumalizika kwa mikutano rasmi na mahema kung'olewa, makundi ya watu kutoka kote nchini yaliendelea kuja. Yalikuja hivi kwamba kwa juma zima kanisa letu jipya, ambalo ndio kwanza lifunguliwe miezi michache iliyopita

hapo Lady Selborne, lilijaa nafsi hitaji na wagonjwa ambao walimtazama Bwana kuwaponya. Mikutano mitatu hadi minne iliendeshwa kila siku kuvunja Mkate wa Uzima kwa ajili yao, kwani ingawa watumishi wa Mungu waliowekwa maalum hasa kwa karama walikuwa wameondoka tulitambua ya kwamba Mungu alikuwa yungali pamoja nasi, Naye alikuwa amelituma Neno Lake lipate kuwaponya, na Neno Lake linadumu pamoja nasi milele.

Ni vigumu kuelezea mikutano kama hiyo. Maombi ya bidii ya maelfu mengi, kuimba kwa ari, kuhubiriwa kwa ajabu kwa Neno la Mungu kwa nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu hakuwezi kuelezewa—kunaweza tu kushuhudiwa. Hatuwezi kumshukuru Mungu vya kutosha kwa ajili ya vile Yeye alivyotosheleza nafsi hitaji na miili migonjwa, na kwa ajili ya wengi ambao walikuwa wameponywa katika kusanyiko, hata zaidi ya wale ambao walioombewa kibinafsi. Hiki kilikuwa ni kizinduzi kwa watu wetu wenyeji. Lilikuwa ni jambo zuri kwa wenyeji wetu kuona ya kwamba Mungu aliweza kuwaponya watu bila ya kutumia maji yao matakatifu, majivu, kuvaa nguo rasmi ama mishipi, ama kushika vitu vingine vyovyote ambavyo vinatukumbusha mengi sana juu ya kazi za wachawi.

Tunamshukuru Mungu tena kwa ajili ya kujiliwa huku kwa ajabu na kutiwa moyo ambako kumewafanya Wakristo wetu wenyeji na wafanya kazi, mbali na kuwa somo kwa vielezo kwa wale wanaohudumia wagonjwa. Pia kujiliwa huku kumetutia moyo sana kuendelea kuomba hivi kwamba uwezo wa Mungu wa kuokoa, kuponya na nguvu za kutakasa kudhihirishwe kuliko ilivyowahi kuwa kwa ajili ya matayarisho ya kuja Kwake hivi karibuni.

* * *

Ndugu Bosworth alipokea barua kutoka kwa mmishenari mmoja na mke wake, ikiripoti baadhi ya uponyaji ambao walishuhudia katika mikutano ya Capetown. Barua hiyo imenukuliwa hapa chini kwa sehemu.

"Mimi na mume wangu tulikuwa wamishenari wa Assemblies of God ya Uingereza, huko India, na katika kipindi chetu cha mwisho baada ya vita katika Mkoa wa Hyderabad, tulikubali mwaliko kutoka kwa Makanisa ya Full Gospel huko Afrika Kusini ili kufanya huduma kule. Tulikuwa tukiongoza moja ya makanisa yao hapo Capetown wakati uamsho wa Branham ulipotukia. Lakini Mungu alikuwa akizungumza nasi kuhusu kurudi kwenye kazi yetu huko India, Naye akafungua njia kwetu kurudi Uingereza, ambako tulifika tarehe 11 Januari. Tunawazungukia Waassemblies katika kazi ya uwakilishi na tumekata tikiti kusafiri kwa meli kurudi India tarehe 16 Septemba, Mungu akipenda.

Sote wawili tungependa kukusimulia jinsi ilivyokuwa baraka kubwa na uvuvio kwetu kuwapo kwenye mikutano ile. Mimi binafsi nilipokea mguso mwilini mwangu (maumivu ya neva nyuma ya shingo) ama Jumapili usiku ama kesho yake asubuhi wakati tulipozungumza nawe na Ndugu Branham huko kwenye Bustani ya Kipentekoste.

Sijui kama ulijua ya kwamba kwenye kuombewa watu kwa pamoja na Ndugu Branham wagonjwa wote waliosalia kabla tu ya kuondoka jukwaani, mvulana mdogo mwenye umri wa kama miaka mitatu aliyezaliwa kipofu alipata kuona kwake?

Nilikuwa nimeketi tu nyuma, na wakati wa maombi yeye alianza kulia na kusugua macho yake. Nilipofungua macho niliona mama yake alikuwa akilia naye akaniambia ya kwamba mtoto wake aliyezaliwa kipofu ndio kwanza apokee kuona kwake. Pia, ndugu yake, mwenye umri wa miaka minane hivi alikuwa na makengeza mabaya sana, na katika wakati huo huo macho yake yalinyoshwa kabisa. Niliwaona watoto wawa hawa mimi mwenyewe, na maskini mtoto huyo mdogo alikuwa analia kwa sababu mwanga mkuu wa umeme uliyaumiza macho yake mapya ya kupendeza! Nilimwuliza mama yake kama alikuwa ni Mkristo, naye akasema alikuwa Mkristo na alikuwa wa Kanisa la Dutch Reformed. Nilimwambia arudi na kuwaambia watu mambo ambayo Mungu ametenda na amwishie Mungu maisha yake yote.

Watu kama watano katika kanisa letu dogo waliponywa katika uamsho ule, kijana mmoja mwanamume mwenye ugonjwa mbaya sana wa moyo aliponywa. Alikuwa mwongofu mpya; baada ya maisha ya uasherati, moyo wake ulikuwa katika hali mbaya, na uso wake ulikuwa daima una mpauko wa mauti, na alikuwa na kutokwa kubaya sana na damu puani, baada ya kuwa hospitalini kwa sababu hii kabla tu ya uamsho ule. Hata hivyo, alijitoa kwa Kristo, alibatizwa naye alikuwa amesimama nyuma ya Banda la Ndege kama bawabu. Ndugu Branham alimwelekezea kidole na kusema, 'Wewe uliye huko nyuma, ukiwa na shida ya moyo, Yesu anakuponya sasa.' Daudi alisema ya kwamba nuru inayong'aa ilimjia, akafumba macho yake ndipo nuru angavu ya kupendeza ikashuka ikaingia ndani ya moyo wake, ambao ulionekana ukivutwa na kugeuzwa, ndipo akayafumbua macho yake na nuru hiyo ikamrudia Ndugu Branham. Kesho yake uso wake ulkuwa umepoteza mpauko wake, akashuhudia uponyaji mkamilifu. Na juma moja ama mbili baadaye ilibidi achunguzwe na daktari kusudi apate kuomba kazi huko Rhodesia. Alituletea cheti ambacho kilimtangaza kwamba alikuwa ni mzima 100%. Mungu asifiwe.

Dada mmoja mzee kutoka kwenye Kanisa letu, mwanamke mzuri aliyejazwa Roho, aliketi moja kwa moja mbele kwenye mkutano wa mwisho wa Jumapili usiku, naye

alikuwa akilia na kuomba ya kwamba Mungu angemgusa. Alikuwa ameugua ugonjwa mbaya wa yabisi kavu kwa muda wa miaka ishirini na kitu, ambao ulikuwa unauma sana hata asingeweza kulala usiku. Wakati Ndugu Branham alipokuwa akiwaombea wagonjwa, mara alimwelekezea kidole akisema, 'Wewe, dada, pale uliyevaa gauni jekundu—kwa nini unalia? Tazama, Yesu ameiponya yabisi kavu yako.' Akaruka akasimama kwa miguu yake, huku ameinua mikono yake juu, akimsifu Bwana, naye alikuwa ameponywa. Alilala kama mtoto usiku huo na kushuhudia uponyaji wake kwenye mikutano yetu baadaye."

G. Stewart

Kutoka Pretoria tulirudi Johannesburg, tukiendesha uamsho mwingine kwenye Maskani ya Bustani ya Maranatha, ambako tulimalizia vyema kama tulivyoanza ziara yetu ya Afrika Kusini. Wakikumbuka yale waliyokuwa wameona katika hizo siku chache ambazo Ndugu Branham alikuwa Johannesburg, imani ya watu ilipanda, walipokuwa wakingojea kupokea uponyaji ambao Mungu alikuwa nao kwa ajili yao.

Uponyaji kutoka katika ibada ya mwisho ambao nitaukumbuka daima ulikuwa ni ule wa yule mama mmoja kipofu. Ndugu Branham alikuwa ameona ono la mama mmoja aliyekuwa ameketi huko katikati ya wasikilizaji ambaye alikuwa ameponywa. Alimwelekezea kidole na

Gazeti la Kiafrikaan lenye makala ya usaili wa Ndugu Branham.

kumwambia asimame na akubali uponyaji wake. Hakujibu. Wakati alipokuwa akimpa moyo asimame, bibi mwingine katika safu ile ile alisimama. Aligeuka akamwangalia kwa sekunde chache. Kisha akasema, "Kwa nini unasimama? Wewe ni wa dini ya Kiyahudi; wewe huamini ya kwamba Yesu ni Kristo. Wewe ni kipofu. Je! unafikiri ya kwamba Yesu Kristo angeweza kukurudishia kuona kwako?" Aliposikia maneno hayo alitikisa kichwa chake. "Lakini nisingeweza kumwomba awe Mponya wako bila ya kwanza kuwa Mwokozi na Bwana wako. Kama utamkubali kama Mwokozi wako, Masihi, Yeye atakuwa pia Mponya wako. Kama unamwamini, inua mkono wako." Aliinua mkono wake na mara aliweza kuona. Tulipokuwa kwenye uwanja wa ndege kesho yake asubuhi tukiwa tayari kurudi Marekani, mtu fulani alikuja akaripoti ya kwamba mama huyo aliweza kuona kikamilifu naye alikuwa ametoka kwenda kuwatembelea marafiki zake ambao hakuwa amewaona kwa miaka mingi.

Hivyo yakaisha majuma kumi huko Afrika Kusini, katika wakati ambapo watu walikuwa wameona na kusikia mambo makuu na ya ajabu yaliyofanywa na Bwana wetu mkuu na wa ajabu kupitia huduma ya mtumishi Wake, William Branham. Watu kamwe hawakujizuia kushangaa walipoona kile Kipawa kikitenda kazi kupitia kwa Ndugu Branham, wakati walipomwona akitambua magonjwa pamoja na mahitaji ya kiroho ya watu. Hawakuacha kushangilia wakati alipowageukia wasikilizaji na kumwelekezea kidole mtu fulani, akiyaelezea magonjwa yao pamoja na mambo mengine mbalimbali kwa utondoti, na kuwaambia ya kwamba Kristo alikuwa amewaponya. Wengi walilia walipoona viwete wakitembea, vipofu wakiona na viziwi wakisikia, na wengi waliondoka wakaenda zao wakisema kwa kweli Mungu amekuwa miongoni mwetu.

Tumeorodhesha miujiza michache kwa kukadiria miongoni mwa mingi ambayo ingeweza kutangazwa. Kwa watu wengi uponyaji wao ulimaanisha kuishi badala ya kifo. Kwa hao waliobadilika kuwa Wakristo, inamaanisha uzima tele zaidi na ushirika wa milele pamoja na Mungu. Kwa maelfu ya Wakristo ambao walihudhuria mikutano hiyo, wakimwona Mungu akitenda kazi na wakihisi uwepo Wake, ilimaanisha uvuvio mkuu kujitahidi kutembea karibu zaidi na Mungu. Yote haya yalikuwa ni matokeo ya kufafanuliwa kwa Neno na Ndugu Bosworth na Ndugu Baxter, thibitisho la Neno hili kwa kutenda kazi kwa kipawa cha Mungu kupitia Ndugu Branham na jitihada za dhati zilizotolewa na Wakristo wa Afrika Kusini.

Katika kufunga taarifa ya yale Mungu aliyofanya Afrika Kusini ningependa kuingiza ripoti zingine mbili ambazo

nimepokea. Moja ya hizi ni kutoka kwa Mwinjilisti mmoja, hiyo nyingine kutoka kwa Katibu wa Kamati ya Taifa ambayo ilifanya matayarisho yote ya uamsho huu.

* * *

TAARIFA KUTOKA KWA MWINJILISTI

Imeandikwa na J. H. Grobler

Nina furaha sana na ni mwenye shukrani kwa Mungu kwa nafasi hii kuelezea msimamo wangu na shukrani. Nachelea kwamba hakuna lugha ingetosha kuelezea maoni pamoja na ujuzi wangu.

Mimi ni Mwinjilisti ambaye pia amekuwa akihudumu uponyaji wa Kiungu wenye mafanikio makuu katika Afrika Kusini. Kusema kweli, nilikuwa ndiye Mwinjilisti pekee wa kudumu muda wote katika huduma ya Kipentekoste Afrika Kusini kwa miaka mingi ambaye alihudumu uponyaji wa Kiungu kwa umati wa watu. Nilikuwa na majaliwa ya kuona vipofu wakiona, viwete wakitembea, viziwi wakisikia na magonjwa yo yote yale mengine unayoweza kufikiria kuponywa katika Jina la Yesu katika huduma yangu.

Niliposikia habari za Kikosi cha Branham kinachokuja Afrika Kusini niliyakinia kwenda na kuchunguza mimi mwenyewe. Nilienda bila kuzingatia heshima ya mtu ama upendeleo nikiwa na kusudi la kufanya uchunguzi wa kinaganaga wa chochote nitakachoona na kusikia.

Jambo la kwanza lililonifurahisha lilikuwa ni kuhubiriwa kwa Neno, la kweli, imara, waziwazi na kwa nguvu. Ilikuwa ni wazi tangu mwanzo ya kwamba watu hawa walikuwa hawapo hapa ili kudhihirisha nguvu fulani kuwavuta watu wawatazame wao, bali ni kutangaza maagizo yote ya Mungu. Ilisisitizwa kabisa kila usiku ya kwamba wokovu wa nafsi ulikuwa ni muhimu zaidi ya uponyaji wa mwili. Si ajabu wingi wa watu walizaliwa katika Ufalme wa Mungu kila usiku. Ni nani ambaye asingefurahishwa na tamasha kama hilo, wakati mtu ukiwa na shauku kwa ajili ya nafsi za watu?

Kamwe sitasahau mhemuko usiku huo wa kwanza wakati Ndugu Bosworth alipotangaza kwa ujasiri sana ukweli kwamba uponyaji wa Kiungu ulihesabiwa katika ile Dhabihu na ya kwamba watu wangeweza kuponywa wakati wakisikiliza na kuamini Neno la Mungu. Jinsi hilo lilivyonivuvia! Wakati huyo mtumishi mpendwa wa Mungu alipoelezea ukweli huu moyo wangu ulifurahi sana na macho yangu yakajaa machozi yenye joto wakati nikijiambia, "Roho Mtakatifu yeye yule aliyenifundisha huku Afrika Kusini pia alimfundisha Ndugu Bosworth huko Marekani." Utukufu na sifa ni kwa Mungu.

Jambo lingine lilikuwa ni fundisho lenye nguvu, hata hivyo lililo wazi na rahisi la Ndugu Baxter juu ya maisha ya ushindi. Loo, jinsi lilivyofurahisha nafsi yangu sana! Jinsi nilivyoinuliwa kwa Mungu mpaka nikajisikia sikutaka kurudi tena bondeni, isipokuwa iwe ni kwa kuwasaidia wanadamu wanaoteseka. Loo, jinsi kweli hizo za thamani zilivyothibitisha huduma yangu mwenyewe. Zilipanua ono langu, ono ambalo limekuwa likinivutia kwa miaka mingi—yaani, kuketi pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho na kutoka huko kumtawala adui yetu na kuwa na mamlaka na kuyatumia juu ya nguvu zote za yule mwovu.

Jambo la kwanza lililoniingia moyoni kumhusu Ndugu Branham lilikuwa ni upendo wa Mungu ambao ungeweza kuonekana katika yale maneno yenye upendo sana "Habari za jioni, wapendwa," alipofika jukwaani kila usiku. Wakati alipozungumza, nilijua Mungu alikuwa pamoja naye. Katika huduma yake haikuwa ni miujiza ya uponyaji iliyonigusa kuliko yote, kwa kuwa nilikuwa nimeona hayo katika huduma yangu mwenyewe. Bali kile kilichonigusa kisichoweza kuelezewa kilikuwa ni kutenda kazi kwa zile Karama za neno la hekima, neno la maarifa na upambanuzi wa roho. Nilishikwa na butwaa wakati mtu mmoja baada ya mwingine walipokuja mbele zake jukwaani kila usiku na katika sekunde chache angeweza kutambua ugonjwa na kufunua siri za mioyo yao bila kukosea.

Niliangalia zoezi hilo kwa makini sana nami nikiwa mwaminifu kwa Mungu nilikuwa tayari kukubali kosa lo lote lililofanywa naye katika utekelezaji huo. Utukufu kwa Mungu, ninaweza kutangaza ya kwamba sikuona hata moja. Yalikuwa kweli asilimia mia moja. Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya jambo hili.

Tukio moja lililovutia sana lilikuwa ni wakati mtu fulani aliposimama kwenye kusanyiko na kupaza sauti, "Ndugu Branham, unafanya mambo haya kwa mamlaka gani?" Jibu lisilopangwa lilitoka kwenye kinywa chake katika kile kilichoonekana kuwa ni sauti ya mbinguni, sauti iliyokuwa ya tofauti sana na ile tunayosikia wakati ikiwashughulikia kwa upendo sana wagonjwa na wanaoteseka. Ilisikika yenye nguvu na kwa mamlaka kuu ya Kiungu wakati alipotangaza, "Kwa mtu yule ambaye unajua machache sana juu yake, Yesu Kristo." Jibu hilo liliwafurahisha sana wasikilizaji takriban elfu kumi hata wakaanza kupiga makofi. Wakati kushangilia kulipofifia alisema kwa unyenyekevu na uchaji katika sauti ile ya mwanzoni ya upendo, "Tafadhalini wapendwa, msishangilie, mtukuzeni Mungu." Wale waliokuwapo pale kamwe hawatasahau tukio hilo.

Mungu aligeuka akawa mkuu sana kwangu, halisi sana na wa thamani sana. Nilijisikia duni sana katika uwepo Wake nisingefanya lo lote ila kulia na kumpenda. Ninaweza

kuwahakikishia maisha yangu na huduma vimeimarishwa na huduma ya watumishi hawa wa Mungu. Kwangu mimi, Ndugu Branham hapana shaka kabisa kwamba ni nabii wa Mungu, Ndugu Baxter ni mwinjilisti, Ndugu Bosworth ni mwalimu waliotumwa na Mungu Afrika Kusini kujibu maombi mengi kwa ajili ya uamsho.

TUKIWA PAMOJA NA KIKOSI CHA BRANHAM AFRIKA KUSINI

Imeandikwa na W. F. Mullan

Ingekuwa karibu haiwezekani kuelezea shauku ya matarajio yaliyotapakaa Afrika Kusini tulipokuwa tukingojea kutembelewa na Kikosi cha Branham. Siku zilipita na majuma yalipita upesi tulipokuwa tukifanya matayarisho yote kwa ajili ya kuzuriwa huko. Matangazo ya awali yalifanikiwa zaidi kuliko tulivyotarajia. Mwitiko kutoka kwa watu wote ulipanuka kadiri tarehe ya ziara hiyo ilivyokaribia. Tulifikiwa na barua tele za kuulizia na simu ililia kwa mfululizo sana hata ilikuwa ni vigumu mtu kujua jinsi ya kupumzika

Hatimaye tulikuwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Palmietfontein, Johannesburg, tukiangalia hewani tupate ishara ya kwanza ya kuja kwa ndege ya Shirika la Ndege la Pan-American kutoka New York. Kiherehere kiliongezeka kadiri umati wa watu ulivyozidi na kuzidi kuongezeka. Doa dogo huko mbali hewani lilianza kupata umbo mpaka umati huo wa watu ukatulizwa kwa ukimya wa matarajio wakati walipoangalia yule ndege mkubwa wa kimitambo akiuzunguka uwanja wa ndege akijiandaa kutua.

Dakika chache baadaye na hiyo milango ya ndege ilifunguliwa na abiria wakaanza kushuka chini. Mwenyeketi na Katibu wa Kamati ya Taifa iliyohusika na matayarisho ya ziara ya Kikosi cha Branham Afrika Kusini, wakiwapo, A. J. Schoeman na W. F. Mullan, walipata kibali maalum kutoka kwa viongozi kuingia uwanjani kuwakaribisha washiriki wa Kikosi cha Branham. Kila kitu kilikuwa katika utaratibu; matangazo yalikuwa yameshughulikiwa kwa uangalifu na nchi ilikuwa ikiungojea wakati huu wenyewe.

Wakishuka kutoka kwenye ndege angeweza kuonekana Ndugu W. J. Ern Baxter, na Ndugu F. F. Bosworth wakifuatwa na mtu wa tatu. Walipokuwa wakikaribishwa Ndugu Baxter akasema, “Ndugu Branham hayuko pamoja nasi.” Ndipo akaeleza ya kwamba Ndugu Branham, ambaye ataambatana na mwanawe, Billy Paul, alikuwa amecheleweshwa kwenye uwanja wa ndege huko New York na atakuja kwenye ndege ifuatayo. Mshiriki wa tatu wa kundi hilo alikuwa ni Bw. Julius Stadsklev.

Wakati kundi hilo lilipokuwa likitoka kwenye uwanja wa ndege kuelekea kwenye Idara ya Forodha baadhi ya kundi lililokuwa likingoja waliuliza, "Ndugu Branham ni yupi?" Wakati washiriki wengine wa kundi hilo wakitangulia, Ndugu Mullan alielezea umati huo wa watu ya kwamba Ndugu Branham hakuwa pamoja na kundi hilo bali angefuata katika ndege ifuatayo. Sehemu hii ya taarifa karibu iwaache watu kuwa bubu. Kuwazia tu ya kwamba Ndugu Branham hakuwa pamoja na kundi hilo na mikutano ilikuwa ianze kesho yake na itachukua siku zisizopungua tatu kabla ndege inayofuata kuwasili. Kwa umati huo wa watu ilionekana kuwa kumetukia balaa kubwa sana na bughudha.

Mfululizo wa kwanza wa mikutano hiyo ulifanyikia Johannesburg, kilicho kituo kikubwa cha viwanda cha Afrika Kusini, na eneo lililo na watu wengi sana kuliko yote. Kwa kuwa walishindwa kupata mahali pa kukutanikia pa katikati kamati ya Johannesburg ilikuwa imekubali ukarimu wa fadhili za Misheni ya Imani ya Kimitume kutumia Mahali pao pa mikutano kwenye vitongoji vya kaskazini vya jiji. Lakini hata chumba chao kikubwa cha mikutano kingekuwa ni kidogo sana na kamati hiyo ikapata ruhusa kutoka kwao ya kupanua jengo hilo. Kazi hiyo ilianzishwa na ikamalizika katika muda mfupi sana na jumba hilo la mikutano likapanuliwa lipate kuwachukua watu wapatao 8,000. Kwa kuacha upande mmoja wa jengo hilo wazi ingewezekana kuwaketisha watu wengine elfu mbili mpaka tatu kwenye boma hilo ambapo wangeweza kuona na kusikia vizuri sana, na kwenye upande huo mwingine wa jumba hilo la mikutano watu wengine elfu tatu hadi elfu tano wangeweza kuketi kwa starehe na wangeweza kusikia bali wasingeweza kuona vizuri sana.

Ndugu Baxter na Ndugu Bosworth walikabiliana na jukumu gumu sana kwa ujasiri. Ilibidi wahudumie kundi ambalo lilikuwa limevunjika moyo kwa kutowasili kwa Ndugu Branham. Ndugu Baxter alianza mlolongo wa mikutano kwa huduma ambayo ilivutia usikivu wa watu na kuhakikisha ufanisi wa ziara yote. Huduma ya Ndugu Baxter ni ya kujenga imani. Ulimwengu kwa kiasi kikubwa umechanganya "imani" na "tumaini"! Ndugu Baxter alianza kazi yake kwa kuhudumu juu ya "Kipimo cha Imani" na huu ulifuatiwa na ujumbe motomoto juu ya "Jinsi Imani Inavyotenda Kazi." Siku hizi chache za kwanza za huduma tulipokuwa tukikungojea kuja kwa Ndugu Branham zilikuwa na manufaa sana. Neno la Mungu lilihudumiwa kwa nafsi zenye njaa na mwelekeo wa imani ulikuwa ukipanda juu kufikia kwenye kiwango kikubwa. Ndugu Bosworth alicheza nafasi kubwa sana katika mikutano wakati akiwatayarisha watu kwa maombi na kwa ujasiri mkuu na hakika tulivu ya imani akaita mtu ye yote aliyekuwa amepoteza kusikia kwa sikio moja kupitia upasuaji wa mfupa wa nyuma ya

sikio waje jukwaani kwa ajili ya maombi. Ndipo akawaombea na tena na tena mara nyingine tuliona nguvu kuu za Mungu zikidhihirishwa katika muujiza wa kuumbwa tena wakati masikio yasiyosikia yaliposikia tena licha ya ukweli kwamba ogani zote zilikuwa zimetolewa kwa upasuaji na isingewezekana kwa sikio hilo kusikia tena mbali na nguvu za Mungu.

Ndipo Ndugu Branham akawasili. Ndugu Schoeman alimlaki kwenye uwanja wa ndege na kumleta moja kwa moja kwenye mkutano uliojaa watu ambako kulikuwa na watu 10,000 wakingojea kwa shauku kuu ya matarajio. Ndugu Mullan alimkaribisha kwa niaba ya watu wa Afrika Kusini. Ulikuwa ni wakati uliokumbwa na wasiwasi na kiherehere cha matarajio. Baada ya kuzungumza na watu kwa muda mfupi Ndugu Branham aliwaombea "kwa pamoja" na mtu anaweza kusema kwa hakika kwamba miujiza ilitendeka usiku huo wa kwanza. Gazeti la *Sunday Tribune* la Durban baadaye liliripoti kisa cha mvulana mdogo, Ernest Blom, ambaye mguu wake mmoja ulikuwa mfupi kwa nchi kadhaa kuliko huo mwingine na ambaye aliponywa kwenye mkutano huo wa kwanza wakati Ndugu Branham alipoomba. Idadi ya waliohudhuria iliongezeka upesi sana. Jumapili alasiri umati ulifikia jumla ya watu 10,000 na Jumapili jioni 12,000. Kufikia Jumatano jioni umati wa watu ulifikia kiwango cha 14,000. Mikutano hiyo ilizungumzwa habari zake kila mahali. Kwa bahati mbaya ilibidi mikutano hiyo ifungwe mapema mno, kwa maana matayarisho yalikuwa yamefanywa kwamba Kikosi cha Branham kiende kwenye mfululizo wa mikutano mingine huko Klerksdorp, umbali wa maili mia moja. Kama mikutano ya Johannesburg ingaliendelea zaidi isingewezekana kukadiria matokeo hayo.

Katika kipindi cha majuma machache Kikosi cha Branham kilikuwa kimeizuru miji kumi na miwili ya Afrika Kusini. Nilijaliwa kuambatana nao kwenye mingi ya miji hii na nimeona mengi sana hata ni vigumu kwangu kutenganisha jambo moja kuu muhimu na lingine. Kila mahali umati wa watu ulikusanyika, na kama vile mwandishi mmoja katika gazeti la kila juma linalopendwa sana na watu alivyoandika, idadi kubwa zaidi ya watu waliohudhuria mikutano hiyo iliridhika ya kwamba walikuwa kwa kweli wameona "ishara na maajabu."

Katika kila kituo mikutano iliyo muhimu ilifanywa kati ya jamii ya Wazungu, lakini nafasi pia ilitolewa kwa ajili ya mikutano ya wasio Wazungu, pia. Katika Bloemfontein jioni moja Ndugu Baxter alizungumza juu ya somo, "Hakuna tofauti" (Warumi 3:22). Wakati wito ulipotolewa kwa ajili ya wanaume na wanawake kuamua kwa ajili ya Kristo kama Mwokozi wao takriban watu 2,000 walisimama kwa miguu yao. Lilikuwa ni jambo lenye utukufu. Katika sehemu nyingi itikio kwa wito wa ujumbe wa wokovu lilikuwa ni la kushangaza

sana. Kwa kweli mamia ya watu, na pahali pengine maelfu walisimama kuonyesha imani yao katika Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao.

Mikutano ya Branham iliendeshwa katika sehemu mbalimbali kwa kuwa hakuna ukumbi wo wote wa hadhara uliokuwa mkubwa vya kutosha kuukalisha umati. Tulitumia viwanja vya nje vya michezo, viwanja vya mpira wa miguu, viwanja vya mashindano ya riadha, viwanja vya maonyesho, uwanja wa mashindano ya mbio za farasi na banda la ndege. Kule East London jukwaa lilijengwa kwenye Uwanja wa Mpira wa Ragbi na viwanja vyenye safu za viti vilitumika kwa ajili ya kuwaketisha watu na pia vile vile uwanja wazi wa michezo. Lile jukwaa lililotumiwa kule East London lilikuwa ndilo jukwaa maalum lililotumiwa na familia ya kifalme kwenye ziara yao ya Afrika Kusini.

Kulikuwako na watu wasiopungua 10,000 wasio Wazungu waliokusanyika kwenye mikutano yao huko Bloemfontein na labda idadi ile ile huko East London. Huko Durban mikutano iliendeshwa kwenye uwanja wa mbio za farasi na mataifa yote ya watu waliweza kukusanyika kwa ajili ya mikutano hiyo. Hapa umati wa watu ulifikia watu 50,000 wa jamii zote Jumapili alasiri, ambapo maelfu walirudishwa, wasiweze kuingia ndani.

Ndugu Bosworth alitekeleza kwa uhodari kila kazi aliyopangiwa. Alihudumu Neno la Mungu kwa maelfu ya waliokusanyika na akawaombea wagonjwa wengi na Mungu akaibariki huduma yake. Aliwafanya watu wa Afrika Kusini wampende. Kila mahali Ndugu Baxter alishangiliwa kama mhubiri aliye mzuri sana na muda mrefu sana baada ya kila kitu kusahaulika, kama kweli mikutano kama hiyo ingeweza kusahaulika, huduma ya Ndugu Baxter ya Neno la Mungu itaendelea kuwa hai. Huduma yake iliwatia watu moyo kuamini Neno la Mungu, kutumia imani yao, na zaidi ya yote kumkubali Kristo kama Mwokozi na Bwana.

Tulimwona Ndugu Branham kuwa yote yaliyokuwa yameripotiwa kumhusu yeye. Alikuja kati yetu kama mtu mwaminifu, mnyenyekevu na ilikuwa ni dhahiri sana ya kwamba baraka ya Mungu ilikuwa pamoja naye. Tena na tena tulimwona Mungu akidhihirisha nguvu Zake kupitia Ndugu Branham. Watu walipomfikia Ndugu Branham yeye mara moja angetangaza maradhi ama ugonjwa waliokuwa wakiugua. Wakati alipoomba tulihisi huruma yake kuu sana juu ya wanaoteseka waliomzunguka. Wakati mwingine akisimama juu ya jukwaa angemchagua mtu fulani kati ya wasikilizaji na kutangaza ni ugonjwa gani walioteseka nao.

Zaidi ya mara moja wakati mikutano ilipopaswa kufanyikia nje tungeshangazwa sana kuwaona watu wameketi kwa utulivu na kusikiliza kwa makini hata wakati mvua

ilipoanza kunyesha. Hapa palikuwapo na ushahidi wa kutosha, endapo wo wote ulihitajika, kuthibitisha ya kwamba Mungu huwavuta watu Kwake wakati kweli yote inapohubiriwa kwa binadamu wenye njaa.

Nikiwa niliambatana na Kikosi cha Branham kwenye miji mingi ya Afrika Kusini iliyozuriwa ninaweza kusema ya kwamba ilikuwa ni dhahiri sana kwangu ya kwamba watu walioamini sana walipata mengi zaidi.

* * *

"Neno hili limetoka kwa BWANA; nalo ni ajabu machoni petu. Siku hii ndiyo aliyoifanya BWANA, tutashangilia na kuifurahia." (Zaburi 118:23-24)

Shuhuda

"Mpeni Bwana utukufu wa jina Lake . . . "

I Mambo ya Nyakati 16:29

Mlango huu una kama shuhuda mia moja za kwanza zilizokuja moja kwa moja kwangu mimi na kwa Ndugu Branham. Tunaelewa ya kwamba wingi wa hizo zilitumwa kwa wenyeketi wa mahali hapo na muda haukuturuhusu kuzipata.

Sijatoa jina kamili kwenye shuhuda hizi kwa kuwa sikuchukua wakati wa kupata ruhusa ya kutumia majina yao yote. Hata hivyo shuhuda hizi ziko kwenye faili na majina yao kamili na anwani zinaweza kupatikana. Shuhuda zilizo nyingi zimefupishwa kutoa tu kweli zilizo muhimu sana.

* * *

Mwalimu Aponywa Baridi Yabisi Na Vena Zilizovimba

Yapata miaka mitatu na nusu iliyopita ilibidi nikatize kazi yangu ya ualimu kwa kuwa nilikuwa nikiumwa sana na ugonjwa wa baridi yabisi na vena zilizovimba. Shida yangu ilianza kama miaka kumi na moja iliyopita. Hakuna kitu kilichoonekana kunisaidia sana. Tarehe 6 Okt. nilienda kwenye Uwanja wa Bustani ya Maranatha na kusimama kwa saa tatu. Nilipata shida ya kuingia ndani kwa kuwa ukumbi huo ulikuwa umejaa. Hatimaye niliruhusiwa kuingia ndani na nikasimama nikiegemea ukuta upande wa kushoto.

Ndugu Branham alikuwa ndio kwanza aje kutoka kwenye uwanja wa ndege na mtu angeweza kuona alikuwa amechoka sana baada ya safari ya kutoka Marekani. Alipendekeza kuombewa kwa pamoja kwa ajili ya wote walioteseka. Aliwaomba wawekeane mikono mmoja juu ya mwingine. Kisha akaelekeza kidole upande mmoja wa ukumbi huo nilikokuwa nimesimama na kusema ya kwamba kulikuwako na mwanamke aliyekuwa na yabisi kavu. Mimi nilikuwa ndiye mwanamke pekee aliyekuwa amesimama akiegemea ukuta. Sasa, hakukuwako na mtu ye yote katika umati huo mkubwa sana aliyejua ya kwamba nilikuwa na yabisi kavu, ila Dada Quinn wala yeye hakujua ya kwamba nilikuwa niko hapo. Lakini yeye na wengine wengi walikuwa wamemsikia Ndugu Branham akisema, "Kuna mwanamke aliye na yabisi kavu." Utukufu Haleluya! Tangu wakati huo na kuendelea nilijisikia nafuu zaidi sana. Nilihudhuria mikutano iliyofuata na kuona uponyaji mwingi, pamoja na kisa kingine cha yabisi kavu kibaya kuliko changu. Mama huyo aliletwa kwenye ambalanzi na baada ya kuombewa aliweza kuamka na kutembea huku

na huko. Pia kulikuwako na kisa cha msichana aliyekuwa amevunjika mgongo na akasimama, alipoambiwa afanye hivyo na Ndugu Branham, naye alikuwa mzima kabisa.

Mungu na ambariki Ndugu Branham na hao wote wanaohusika na mikutano ambao waliwezesha uponyaji huo wote kufanyika, pamoja na wangu.

E. S.

Uti wa Mgongo Ulio Mgonjwa Uliponywa Wakati Akimshukuru Mungu kwa ajili ya Yale Aliyowatendea Wengine

Baada ya kuugua kwa kipindi kirefu cha miezi 18, nilikuwa nimeachwa na uti wa mgongo mgonjwa wala nisingeweza kutembea pasipo kutumia msaada wa fimbo. Kwa siku kadhaa maumivu yake yalivumilika, siku zingine ni makali sana; hakuna maneno yanayoweza kuelezea. Katika kujaribu kutembea, uti wangu wa mgongo ungealika, ukiteguka kwa maumivu makali sana. Pia niliumwa sana vena kwa muda wa miaka 25, kuganda kwa damu kwenye mzunguko wa damu. Miaka minne iliyopita nililazimika kuifunga miguu yangu bendeji, vinginevyo nisingeweza kusimama kwayo.

Tarehe 7 Oktoba, 1951, dada yangu, Bibi Scott, alinipeleka kwenye mikutano ya William Branham huko kwenye Bustani ya Maranatha ambako nilishuhudia visa 56 vya uponyaji wa Kiungu wa magonjwa mbalimbali, dhihirisho la ajabu sana la nguvu za Mungu katika kuwakomboa maskini watu wanaoteseka. Nilifurahiwa sana kuwaona wakikombolewa hivi kwamba nililia na kulia kwa furaha. Baada ya ibada nilikuwa nimeketi kwenye gari nikitafakari juu ya maajabu niliyokuwa nimeona, nami nikajisahau kabisa kuhusu hali yangu, wakati nikimsifu Mungu kwa yale aliyokuwa amewafanyia wengine nilioshuhudia. Mara nikasikia nguvu za Mungu zikitenda kazi kwenye uti wangu wa mgongo. Nilivutwa juu na nguvu za Mungu, nikisimama kwa miguu yangu. Papo hapo Bwana mpenzi alirekebisha uti wangu wa mgongo na moja kwa moja maumivu yote yakaniacha. Nilienda nyumbani nikimsifu Mungu na kumshuhudia kila mtu niliyekutana naye. Jambo la kwanza nililofanya nilipofika nyumbani lilikuwa ni kuondoa bandeji kwenye miguu yangu; kwa neema ya Mungu sijayavaa tena. Ninaweza kufanya kazi zangu zote za nyumbani. Sijasikia maumivu tangu wakati huo wala sihitaji fimbo. Kwa sasa magoti yangu ni manyonge kidogo bali hayana maumivu. Ninamtumaini Mungu kwa cho chote ambacho hakina nguvu sana. Yeye ndiye Mwanzilishi na Mwenye Kukamilisha kazi zote njema, ambaye ninampa sifa zote na utukufu.

A. C. G.

Anathibitisha Uponyaji wa Dada Yake na Kusimulia Wake.

Hii ni kuunga mkono ushuhuda wa dada yangu, Bibi. A. C. Gribble. Ninamsifu Mungu kwa ajili ya yale aliyomfanyia. Aliletwa kwangu akiwa ni mgonjwa, sana sana. Ndugu Hugo anaweza kuthibitisha jambo hilo. Kwa muda wa miezi kumi na nane alikuwa chini ya uangalizi wangu.

Jioni hiyo hiyo, wakati wa maombi ya jumla, niliponywa tindi yangu ya mguu iliyoteguka na tumbo dhaifu. Tunampa Mungu sifa zote.

M. M. S.

* * *

Kaponywa Katika Kusanyiko

Ninamshukuru Mungu aliyeniponya maumivu ya mfululizo. Sikuwa kwenye mstari wa maombi bali nilikuwa mmoja tu miongoni mwa wasikilizaji ambao walimwamini Mungu wakati Ndugu Branham alipotuombea sisi sote. Ninamtukuza Bwana nimeponywa maumivu makali. Niliposikia mahubiri ya Ndugu Branham na jinsi alivyowaombea wagonjwa, nilianza kuwazia juu ya Bwana wetu Yesu Kristo wakati aliponena na Martha akisema, "Ukiamini, utauona utukufu wa Mungu."

H. K. M.

* * *

Niliponywa Jeruhi la Uti wa Mgongo

Ninaweka ndani marejeo mawili ya madaktari wangu ambao wamenipa matibabu kwa ajili ya mgongo wangu kabla ya kupokea uponyaji wa Kiungu kwenye ibada ya Ndugu Branham huko kwenye Bustani ya Maranatha. Madaktari hawa walinichunguza baada ya mimi kupokea uponyaji wa ajabu wa Mungu, nao walishangaa sana kuniona nimepona kabisa. Tulikuwa tumejiandaa kwa ajili ya upasuaji hatari wa uti wa mgongo.

Nilipokea uponyaji wangu tarehe kumi na moja Oktoba, mwaka wa elfu moja mia tisa na hamsini na moja. Nilikuwa mgonjwa mwaka mmoja kamili, na nilikuwa nimetibiwa kwa njia nyingi. Nilikuwa na hakika nimeponywa muda mfupi baada ya Ndugu Branham kuzungumza na mimi. Ndugu Branham aliniambia ya kwamba nilikuwa nimejeruhiwa mwaka mmoja uliopita na akaniambia vile hasa nilivyojisikia. Aliniambia ya kwamba alijua nina imani thabiti na ya kwamba Mungu angeniponya. Niliponywa mara moja.

Mwaka mmoja kabla sijapokea uponyaji wangu niliteleza kwenye sakafu ya saruji laini iliyosuguliwa jikoni mwetu, na kuvunja mfupa mdogo kwenye sehemu ya chini ya uti wa mgongo. Matokeo yake yalikuwa kwamba ningeweza kusimama tu kwa miguu yangu kwa shida sana baada ya kuketi ama kulala chini, nilikuwa na maumivu makali sana mgongoni mwangu karibu wakati wote, na ilikuwa ni udhia huko shuleni kwa kuwa nisingeweza kuketi wala kusimama kwa kipindi cho chote kile cha wakati. Uponyaji wangu umeifanya imani yangu kuwa thabiti zaidi, familia yangu inashukuru, wala hawawezi kukoma kunena juu ya nguvu za ajabu za Mungu.

Nina filamu za Eksrei zinazoonyesha huo mfupa uliovunjika, na nitafurahia kuzituma kwenu kama mkitaka nifanye hivyo.

H. J. N.

* * *

Kuponywa Kansa Nikiwa Katika Wasikilizaji

Ninataka tu kutoa ushuhuda wangu kifupi. Yesu alikutana na mimi katika njia ya ajabu. Niliugua kansa na madaktari walifanya waliyoweza. Nilifanyiwa upasuaji na hata hivyo hali yangu ikazidi kudhoofika, mpaka ugonjwa huu ukahamia ndani. Nilitaabika sana nyakati za usiku nikijua ya kwamba ilikuwa ni bure kutafuta msaada kutoka kwenye mkono wa binadamu, na kwa hiyo nikamwita Mungu.

Mungu alinena na mimi na nikaunyosha mkono wangu wa imani na kumshukuru Bwana, alisikia na akajibu mara moja pale kwenye kiti changu. Nilimsifu Bwana, na watu wote walisimama kwa mshangao kwa yale Yesu aliyokuwa amefanya.

Mungu na ashukuriwe kwa kutupa Mwokozi wa ajabu tuliye naye. Usiku huo Yesu alikuja mbele zangu msalabani, na sauti nyororo ikasema na mimi. Yesu hakusulibiwa msalabani kwa ajili ya dhambi zako tu bali pia kwa ajili ya maradhi yako.

Yesu ashukuriwe, alichukua maradhi yangu yote mara moja, kama tu alivyofanya kwa dhambi zangu.

J. K.

* * *

Kansa Imeondoka

Hapa napenda kushuhudia juu ya nguvu za ajabu katika damu ya Bwana wetu Yesu Kristo wa thamani. Yeye na apewe sifa na heshima milele!

Yesu aliniponya kansa chini ya huduma ya Ndugu yetu Branham.

Unaweza kuja na kuona. Ninazo picha zilizopigwa na pia taarifa ya daktari.

Jina Lake na lisifiwe!

N. J. O.

* * *

Hakuna Maumivu Tena Tumboni

Jumapili alasiri wakati Ndugu Branham alipokuwa huko nje Olando, nilipokea uponyaji wangu. Kwa miaka kadhaa nimekuwa na maumivu makali tumboni mwangu. Mwishoni mwa ibada Ndugu Branham alitwambia kuwekeana mikono na tuamini tupate kuponywa. Nilifanya jambo hili na, Mungu asifiwe, niliponywa. Tangu wakati huo, na sasa ni karibu miezi mitatu, sijawahi kusikia maumivu tumboni mwangu. Bwana asifiwe.

* * *

Upande wa Kushoto wa Uso Ulipooza Kabisa

Ninaandika haya kushuhudia jinsi Mungu alivyouponya uso wangu kutokana na kupooza kabisa upande mmoja. Nisingeweza kusogeza misuli yo yote ya upande wa kulia wa uso wangu na shingo yangu. "Kiharusi Kengele" ndivyo kinavyoitwa.

Majuma matatu kabla ya wakati mliotazamiwa kufika Afrika Kusini nilimwona daktari. Kwa kuwa mimi ninafanya Huduma kwenye Manispaa ilinibidi nichukue likizo ya ugonjwa na nilipelekwa nikachuliwe misuli kila siku na kutibiwa kwa umeme hospitalini. Jambo hili liliendelea kwa muda wa majuma mawili bila ya matibabu hayo kufanikiwa. Ndipo nikapewa vidonge fulani ambavyo vilikuwa na matokeo mazuri katika magonjwa mengine, kwa kuwa sasa inadhaniwa kuwa ni "kirusi" ndicho kinachosababisha kiharusi hiki.

Hii ilikuwa ni kabla tu ya uamsho wenu wa uponyaji ambao ulianzia huko kwenye Bustani ya Maranatha. Sikunywa vidonge hivi kwa kuwa nilitarajia uponyaji kutoka kwa Bwana. Nilimsihi Bwana aniguse kwa kuwa ilibidi niripoti hospitalini baada ya siku nne—kuhusu matokeo ya vidonge ambavyo sikuwa nikivinywa. Hii ilikuwa ni Alhamisi. Ijumaa tulikwenda kwenye mikutano yote miwili, pia Jumamosi. Jumamosi usiku nilijisikia vizuri zaidi mwilini mwangu bali uso ulikuwa ungali umepooza. Jumapili nilimkumbusha Bwana ya kwamba ilinibidi kwenda hospitali Jumatatu, kuhusu vidonge ambavyo sikuwa nikinywa. Wengi wa marafiki zangu walikuwa wakiomba pia. Jumapili tulihudhuria mikutano yote nami niliendelea tu kukubali uponyaji wangu

kutoka kwa Bwana kila wakati maombi yalipofanyika kwa ajili ya kusanyiko lote. Jumapili usiku niliweza kutabasamu na pande zote mbili za uso wangu na misuli hiyo mingine ikaanza kupata nafuu. Jumatatu asubuhi niliweza kupiga simu hospitalini na kuwaambia ya kwamba Bwana alikuwa amenigusa na ya kwamba sitaendelea tena na matibabu ila nitawaona mara tu baada ya ibada kwisha; jambo ambalo nilifanya nao, daktari na manesi, wote walishangaa sana kuniona, nami nilitangazwa kwamba nimepona.

J. P. P.

* * *

Kutapika Kusikodhibitiwa kwa Urahisi na Tezi

Niliugua ugonjwa wa kutapika kwa muda wa miezi mitano. Miezi miwili iliyopita ningeweza kunywa maji kidogo sana na kula chakula kidogo sana. Nilifanyiwa upasuaji mkubwa sana wa tumbo mara nne. Madaktari bingwa kadhaa walinishughulikia. Nilifanyiwa upasuaji mkubwa sana mara mbili katika muda wa miezi sita huko Kroonstad, mmoja baada ya mwingine. Hatimaye Dk. Dykman alikataa kunifanyia jambo lo lote zaidi. Nilikuwa huko Johannesburg katika Hospitali ya Kensington mara nyingi nikishughulikiwa na madaktari bingwa. Pia nilikuwa na tezi ambayo Bwana ameiponya kabisa.

Baada ya uponyaji wangu nilimwendea daktari naye akanipa cheti na kusema ya kwamba kimoja kinaweza pia kupatikana kutoka kwa hao wataalamu.

W. J. G.

Bibi J. G. amekuwa mgonjwa wangu kwa miaka kadhaa. Amefanyiwa upasuaji wa tumbo unaohusu kibofu nyongo na organi za kinena mara nne. Zaidi ya hayo alikuwa na tezi. Kwa karibu miezi mitano aliugua kutapika kusikotibika. Alishughulikiwa na wataalamu kadhaa huko Johannesburg. Sasa ni dhahiri yeye ni mzima kabisa.

Dk. H. J.

* * *

Mchungaji Anatoa Taarifa ya Uponyaji wa Wagonjwa Wanne

Tuliifurahia mikutano ya Branham iliyotumwa na Mungu pamoja na mahubiri yake yenye upako yaliyohubiriwa na washiriki-wenzi mbalimbali wa kikosi chake, bali kuhusu huduma ya kibinafsi ya Ndugu yetu mpendwa Branham hatuna maneno ya kuelezea shukrani zetu kwa Baba yetu wa Mbinguni kwa rehema ya kumtuma kwetu, sisi ambao tulipokea zaidi ya yanayoweza kusimuliwa. Mimi na mke wangu pamoja na kanisa letu kwa jumla tulivuviwa kwa uchaji sana na kutiwa moyo kiungu kwamba wengi walipokea uponyaji wao kwa kutazama

tu. Dada Fourie (mke wangu) aliugua kwa zaidi ya miezi tisa kutokana na kuzaliwa kwa mtoto wetu mchanga, ambaye yuko pamoja na Mungu sasa, bali wakati alipokuwa akisikiliza ujumbe wa kiungu wa uponyaji, alikubali ukweli wa jambo hilo naye akaponywa mara moja. Hayo yalitokea huko Klerksdorp.

Ndugu Ben Meyer wa kusanyiko letu alikuwa akiugua pua iliyokuwa imevimba vibaya sana, jicho lake pia liliathirika na likawa jekundu kwa damu na hatimaye likawa baya sana hivi kwamba baada ya miezi mitatu ilikuwa ni dhahiri kwa wote waliojua kansa ya kwamba ndugu huyo angekufa kifo kibaya sana. Nilimtia moyo ndugu huyo kuhudhuria mikutano huko Kimberley na nikamwelezea kuhusu tukio la dada huyo katika mji uliokwisha tajwa. Aliamua kwenda na akaponywa kwa namna hiyo hiyo wakati akimsikiliza Ndugu Branham akiwaambia wengine waamini. Yeye pia aliukubali kwamba ni wake binafsi na baada ya kusafiri kwa zaidi ya maili themanini usiku huo akienda nyumbani, kuvimba kwa pua kulitoweka na jicho likawa kawaida kama lilivyokuwa hapo kabla.

Kikosi hicho kilipokuwa kikipitia kwenye kijiji chetu kikielekea Kimberley kiliongozwa na Mungu kusimama nyumbani kwa mchungaji wetu kwani tulimwomba Mungu kumtuma ndugu huyo kwetu na awe na ujumbe wa kibinafsi na pia amtumie kwa ajili ya kuponywa kwa mtoto wetu mdogo Betty (mwenye umri wa miaka mitano) aliyekuwa akiumwa maumivu makali sana ya tumbo huku mishtuko ya ghafla ikifuata na pia dalili fulani iliyotutia wasiwasi sana. Wakati Ndugu Branham alipoingia sebuleni petu alimwona na akasema naye kwa namna ya utulivu na ya upendo sana ambayo niliwazia ilikuwa karibu sana na jinsi Bwana Yesu Mwenyewe angefanya. Yeye alimtaja Becky wake mpendwa na kwenye wakati huo huo nisingeweza kujizuia na nikasema: Betty daima husema ya kwamba kama Mjomba Branham akimwombea atapona. Kwa hiyo akasema, "Nitamwombea," naye akiweka mikono yake juu yake aliigusa Mbingu kwa ombi lake nyenyekevu na la uaminifu. Akimgeukia dada alisema: "Dada, usihofu tena, yeye ameponywa kabisa." Yeye pia alitwambia ugonjwa hasa aliokuwa akiugua na kwamba huo ulikuwa ndio mwisho wa mateso yake. Yeye ameponywa kabisa, Mungu mwenye enzi na asifiwe. Dalili hiyo pia imeondoka. Ninashukuru sana kusema ya kwamba wote hata wameponywa hivi sasa. Wakati huyo ndugu alipoondoka siku hiyo pia alisema: "Dada, Bwana Yesu anakupa shauku ya moyo wako." Jinsi tulivyo na furaha kujua ya kwamba Mungu angali anajibu maombi.

Bibi Wessels, Robyn Street, Christiana, alielekezewa kidole na Ndugu Branham katika mkutano wa Jumamosi (tarehe 20 Oktoba 1951) na kuambiwa ya kwamba alikuwa akiugua figo zake bali ameponywa na ilikuwa hivyo. Angali ameponywa.

Kuna wanaoshuku wachache mjini bali walio wengi wanaamini ya kwamba Ndugu Branham ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, na kuhusu wafuasi wetu wenyewe, sote tunajua jambo hilo na tumelikubali kwa mioyo yetu yote. Kadiri nijuavyo mimi mwenyewe ni kwamba nimemkaribia Mungu zaidi kuliko hapo awali. Niko mtu wa tofauti kabisa na Mungu anaibariki huduma yangu kuliko hapo awali.

Baraka kuu za Mungu na zidumu kwenye huduma yako.

D. P. F., Mchungaji

* * *

Sasa Ninatembea Kawaida Kabisa

Mishipa ya nguvu katika nyonga yangu ilichanika wakati nikikimbia. Nilikuwa nifanyiwe upasuaji hatari sana kwenye nyonga yangu. Baada ya kutoka hospitali bado nilichechemea lakini jana usiku nilijisikia ya kwamba Bwana alinigusa wakati Ndugu Branham alipokuwa akimwombea kila mtu.

Ninamshukuru Mungu kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu ya kwamba ninaweza kutembea kama kawaida kabisa.

J. B.

* * *

Kusoma Kuhusu Huduma ya Ndugu Branham Kulivuvia Imani Kwa Ajili ya Uponyaji Wake Mwenyewe

Kwa miaka kumi niliugua maradhi hatari ya "Ugonjwa wa Moyo." Madaktari walinikatia tamaa ya kupona kabisa na wakasema ya kwamba ilibidi niridhike kuishi maisha ambayo moyo wangu ungeniruhusu kuishi. Nilikuwa na mishtuko ya moyo ya mara kwa mara. Pia nilikimbizwa hospitalini kwa ajili ya oksijeni. Watoto wa Mungu walikuwa wakiniombea bali nilijisikia nilikuwa nikidhoofika polepole. Hakuna matumaini, hakuna matumaini, mpaka hatimaye tukapokea habari njema ya kwamba Ndugu Branham alikuwa anakuja Afrika Kusini.

Mara moja mume wangu, kwa telegramu ya haraka, aliagiza kitabu cha Ndugu Branham huko Durban na akanipa nikisome, akijua ya kwamba nitakapokisoma kitabu hicho imani yangu katika Mungu itaongezeka. Niliposoma hicho kitabu imani yangu katika Mungu ilizidi kupata nguvu zaidi na zaidi mpaka nikawa na hakika ya kwamba ningeweza kumtumaini Mungu kwa ajili ya uponyaji wangu. Nikijua Ndugu Branham alikuwa anakuja Afrika Kusini, nilitambua ya

kwamba maelfu watakuja kuombewa na nina matumaini gani ya kuingia katika mstari wa maombi. Mara nilianza kufunga na kuomba, nikimwomba Mungu aniweke kwenye mstari wa kwanza wa maombi, ili kwamba Ndugu Branham aweze kuzungumza na mimi kibinafsi.

Mungu alijibu maombi yangu. Mnamo tarehe 17 Oktoba, 1951, usiku wa kwanza wa uamsho wa Ndugu Branham huko Kimberley, nilipewa kadi na Billy Branham yenye namba 3 juu yake. Namba 1-15 ziliitwa kufanya mstari wa maombi na, Mungu asifiwe, nilikuwa wa pili kuombewa. Ndugu Branham alisema, "Habari za jioni, dada, wewe ni mwaminio. Uliumwa ugonjwa wa moyo. Uliponywa kwenye meza ya ushirika miezi michache iliyopita. Ulifunga na kuomba katika chumba chako cha kulala, ukimwomba Mungu akuweke kwenye mstari wa kwanza na hiyo ndiyo sababu uko hapa katika mstari wa kwanza wa maombi. Dada, nenda zako, Mungu amekuponya kabisa sasa."

Mungu asifiwe, nilipokea uponyaji wangu wakati uo huo na papo hapo nilikuwa na hakika ya kwamba Mungu alikuwa ameniponya. Sifa na haleluya ziliujaza ukumbi huo wa mji wakati Ndugu Branham aliponitangazia kwamba nimeponywa. Kila mtu aliyenijua alijua jinsi nilivyougua kwa muda wa miaka kumi na sasa wote walikuwa wakimsifu Mungu pamoja na mimi kwa ajili ya uponyaji wangu.

Ndugu Branham alitamka ya kwamba niliponywa kwenye meza ya ushirika. Hilo ni kweli. Asubuhi moja Jumapili mchungaji wa Kanisa la Full Gospel la Mungu la Kimberley pamoja na mume wangu waliniombea. Nilikuwa mahututi kabisa. Nilikuwa na shauku ya kushiriki meza ya Bwana asubuhi hiyo. Mchungaji akijua ya kwamba nilikuwa dhaifu sana alifikiri haiwezekani. Nilisisitiza, ndipo mchungaji akanipeleka kanisani. Asubuhi hii ilikuwa ni kuwekwa wakfu kwa viongozi. Halmashauri yote ya kanisa pamoja na wake zao waliombwa kuja mbele. Baada ya kuwekwa wakfu tulishiriki meza ya Bwana. Nilisimama karibu na mume wangu aliyekuwa akinishikilia. Nilikuwa ni mnyonge sana na nikipumua kwa shida. Kusanyiko lilikuwa limenikodolea macho yao likiwa halijui kitakachotukia. Ushirika ulihudumiwa na wakati nilipokuwa nikila Mkate (mwili wa Yesu) Mungu aliniponya na nikaondoka kanisani bila ya msaada wo wote na moyo wangu ulikuwa kawaida. Mungu asifiwe.

Baada ya Ndugu Branham kuniombea nilimwomba daktari anifanyie uchunguzi naye akasema: "Nenda na ushangilie wala usidhani kamwe umeishasumbuliwa na ugonjwa wa moyo." Mungu amenipa moyo mpya, na sasa mimi nina afya na ni mwenye nguvu, daima nikienda kote nikishuhudia na kuwaambia watu jinsi ambavyo Mungu ameniponya.

Vema, unaniuliza uponyaji wangu umekuwa na matokeo gani juu ya maisha yangu ya kiroho. Kwanza, ninamtukuza

Mungu kwa ajili ya kuniponya, lakini maneno aliyoyatamka Ndugu Branham, "Wewe ni mwaminio," yana maana zaidi kwangu. Daima nilitambua ya kwamba ninaweza kwenda Mbinguni nikiwa na mwili mgonjwa bali si na nafsi gonjwa. Hii ndiyo sababu maneno hayo yana thamani kuliko kitu cho chote kwangu. Pili, watu wanashangaa sana wanaponiangalia, wengine tena walisema, "Wewe ni mwujiza." Mimi na mume wangu sasa tunaingia katika huduma ya kudumu kuwaletea wengine Injili hii yenye utukufu ya wokovu na uponyaji. Mara nyingine tena, jiungeni pamoja na mimi na mseme "Bwana asifiwe." Hebu na tuseme tena, Bwana asifiwe.

V. O. N.

* * *

Uponyaji wa Polepole Kutokana na Maumivu Tumboni

Nilikuwa nikiumwa maumivu kwenye ubavu wangu wa kulia na tumboni mwangu. Baada ya Ndugu Branham kuniombea huko Kimberley nilipata nafuu polepole mpaka sasa ninajisikia kama mtu mpya. Daktari anashangazwa kuona jinsi nilivyopata nafuu. Shukrani, kwa kuwa kwa Mungu yote yanawezekana.

E. J.

* * *

Huru Katika Kila Hali Kutokana na Magonjwa Mbalimbali

Kwa muda wa miaka ishirini na mitatu nilikuwa nikiugua na kutibiwa yabisi kavu, kansa, shinikizo la damu la juu na jeraha la upasuaji ambalo lisingepona. Kwenye tarehe 21 Oktoba, huko Kimberley, Ndugu Branham aliongea na mimi. Alisema ya kwamba nilikuwa na kansa na magonjwa mengine, na ya kwamba Mungu pekee ndiye angeweza kuniekoa na kaburi. Baada ya kuniombea alisema ya kwamba ningeweza kwenda nyumbani kwa kuwa nilikuwa nimeponywa.

Uponyaji wangu ulikuja polepole bali katika majuma matatu maumivu yote yalikuwa yamekwisha na nilikuwa huru kwa kila hali. Mchungaji wangu wa Dutch Reformed alifurahi kusikia kuhusu habari hiyo na baada ya kufanyiwa uchunguzi daktari wangu alinipa taarifa iliyosema ya kwamba hakukuwako na kansa wala yabisi kavu mwilini mwangu. Mungu asifiwe imemfanya Bwana kuwa halisi sana kwangu.

W. J. B.

Historia ya W. J. B., Andalusia, umri wa miaka 54.

Alikuwa ametolewa kibofu nyongo na baadaye upasuaji mwingine wa minato. Alipakwa marhamu ya kansa kwa ajili ya uvimbe kwenye mkono wa kulia kwa zaidi ya miaka kumi

na mitano. Pia ana marhamu kwenye ziwa la kushoto kwa ajili ya uvimbe kwenye ziwa. Pia alikuwa na shida ya maumivu mgongoni mwake. Sasa alipochunguzwa alionekana kuwa mnene bali vinginevyo ni mwanamke anayeonekana mwenye afya. Hakuna mpauko wala homanyongo. Kovu kubwa kwenye mkono wa kuume na ziwa la kushoto, makovu yote yana afya ya kawaida. Hakuna uvimbe kwenye ziwa. Hakuna mtoki kwapani, shingoni, wala po pote pale. Makovu ya tumboni hayana shida—ini liko kawaida—kifua, mapafu, na moyo viko kawaida. Anajisikia mzima wala hana dalili za magonjwa.

Dk. R. N.

* * *

Uvimbe Usoni Umekwisha

Ninaweza kushuhudia ya kwamba Mungu angali ana nguvu za kuponya. Wakati wa ziara ya Kasisi Branham hapo Kimberley niliponywa papo hapo tarehe 21 Oktoba, 1951. Jioni hiyo hiyo nilipofika nyumbani, niliangalia kwenye kioo changu na ningeweza kuona ushahidi wa mwujiza alioutenda Mungu.

Kwa muda wa miezi 3½ nilikuwa nikiugua uvimbe upande wa kushoto wa pua yangu, hivi kwamba tundu la pua langu upande huo lilikuwa limeziba karibu wakati wote. Nilihofu ya kwamba uvimbe huo umekua ukawa kansa. Tumaini langu pekee lilikuwa ni kumfikia nabii wa Mungu, ili kwamba mimi kama mtoto wa Mungu nipate kuponywa. Mungu asifiwe, uponyaji wangu umekamilika na ni wa kudumu.

B. P. M.

* * *

Kuponywa Ugonjwa wa Tumbo

Ninataka kumsifu Bwana kwa maana Yeye ameniponya ugonjwa wa tumbo ambao umenisumbua maishani mwangu mwote. Kwa karibu miaka ishirini nimekuwa pia nikiugua kwa sababu ya ini gonjwa. Nimetumia karibu mapato yangu yote katika matibabu ambayo yamenipa tu msaada wa muda. Nilipata uponyaji wa mara moja wa ugonjwa wangu wa tumbo, ila ini langu lilipona polepole mpaka lenyewe, pia, sasa ni zima kabisa. Leo mimi ni mtu mwenye afya na ninamsifu Bwana kwa kuwa amenifanya mtu mpya.

N. W.

* * *

Kuugua Ugonjwa wa Ini

Wakati Kikosi cha Branham kilipokuwa kikifanya mikutano ya uponyaji wa Kiungu huko Kimberley, nilipokea uponyaji wangu mara moja. Kwa muda wa miaka miwili

nilikuwa nikiugua ugonjwa wa ini. Sasa ni zaidi ya majuma sita yaliyopita tangu mikutano hiyo ilipomalizika na tukio hili limeiimarisha imani yangu na kunileta karibu zaidi na Mungu.

R. S.

* * *

Kuponywa Mkamba na Damu Kuvilia

Ninataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya uponyaji ambao niliupokea huko Kimberley baada ya kuugua ugonjwa wa mkamba na kuvilia damu kwa zaidi ya miaka 20. Nilikuwa nimeketi ibadani, nikiwa ninahisi sana uwepo wa Roho Mtakatifu. Hata Ndugu Branham wala mtu mwingine ye yote hakuzungumza nami wala kuniombea, bali nilinyosha mkono wa imani na Mungu akaniponya. Mwezi mmoja sasa umepita tangu wakati huo na hadi sasa hakuna dalili ya mateso hayo.

B. A. J.

* * *

Natembea Tena

Kwa muda wa miaka minne nilishindwa kutembea. Ndugu Branham aliniambia nisimame na kutembea na sasa nimeponywa kabisa.

Ninampa Mungu sifa zote, heshima na utukufu.

J. J.

* * *

Mwingine Anatembea Tena

Wakati mmoja siku zilizopita nilishikwa na kiharusi kilichopoozesha upande wote wa kushoto wa mwili wangu. Akili zangu pia zilikuwa zikiniruka. Nilikuwa kilema kabisa kwa kama miezi mitano.

Usiku mmoja Ndugu Branham alisema ya kwamba wale walioamini wangeponywa na pia akawaambia wale wote waliokuwa na imani kwa ajili ya uponyaji wao wasimame na kutembea. Nilisimama na kutembea.

Bibi N.

* * *

Hali ya Damu Sasa Ni ya Kawaida

Binti yangu alikuwa mgonjwa tangu alipokuwa na umri wa miaka minane. Kwanza alitolewa kidole tumbo na halafu akaendelea kuwa na hali mbaya zaidi na zaidi mpaka daktari

wa Kimberley akampeleka Johannesburg, ambako aliwekwa katika Hospitali Ndogo ya Binafsi ya Norman kwa majuma kumi na matatu. Alidungwa sindano tatu tofauti za aina mbalimbali kila baada ya saa tatu, usiku na mchana, bali aliendelea kukonda zaidi na zaidi na hatimaye niliamua kumleta nyumbani kwa ndege kwa kuwa asingaliweza kustahimili safari ya garimoshi.

Ndipo nikamtumaini Mungu tu. Baadaye kidogo (1950) Marlene alitolewa wengu wake na damu yake ikabadilishwa (wengu wake ulikuwa mrefu mara kumi na tano kuliko kawaida). Kuvuja damu kukaanza. Baada ya upasuaji angali alitapika damu. Alinuka mdomo hali ambayo daktari alisema inatokana na ugonjwa huo wa damu. Amepata kuwekewa damu mara nyingi, na alipaswa kupata painti moja ya damu mwezi wa Novemba, bali sasa si jambo la lazima.

Tulimwandikia Ndugu Branham kabla hajakuja Afrika Kusini na Ndugu Bosworth akatuma leso iliyotiwa mafuta ambayo yeye sasa anaivaa. Tumekuwa tukija kila usiku na tunaweza kweli kumshukuru Mungu yeye ameponywa kabisa na nina hakika Mungu hata ameweka wengu mpya ndani yake.

M. W.

* * *

Uvimbe wa Nyuzinyuzi

Ndugu Branham aliniombea Jumatano usiku na akaniambia ya kwamba nilikuwa na uvimbe wa nyuzinyuzi katika kifuko cha mayai na ya kwamba, katika saa 72 kutoka wakati huo ningepokea uponyaji wangu.

Jumamosi usiku nilipokuwa nimeketi kati ya wasikilizaji na Ndugu Branham, yule nabii, alikuwa akiwahudumia wagonjwa, karibu saa 72 baada ya kuombewa naye, Bwana alinionyesha ono la msalaba kwenye kilima kidogo. Jambo lililonigusa lililokuwa ni la kushangaza sana lilikuwa ni kwamba pande zote za msalaba kulikuwa na giza. Mara kando ya huo msalaba, kana kwamba ilikuwa ni hewani, kulitokea kitu ambacho ninaweza tu kukielezea kama uvimbe nyuzinyuzi. Ninamshukuru Bwana kwa kuniponya.

N. M. C

* * *

Uvimbe

Kabla hatujaitwa kwenye mstari wa maombi tayari nilijisikia ya kwamba jambo fulani lilikuwa limetukia.

Ninaweza tu kushuhudia ya kwamba ninajua nimeponywa na ya kwamba Bwana amefanya kazi hiyo. Nilikuwa nikiugua uvimbe katika ogani zangu za kike kwa muda wa mwaka mmoja na miezi minne.

H. Van E.

* * *

Moyo Wenye Baridi Yabisi kwa Miaka Ishirini

Nilikuwa na umri wa miaka mitatu niliposhikwa na homa ya baridi yabisi na hii ilisababisha moyo wenye baridi yabisi ambao kutokana na huo nimekuwa nikiugua kwa miaka ishirini. Nilikuja kwa Ndugu Branham naye akaniombea nami nikaponywa. Marafiki zangu na jamaa zangu wana furaha sana kuona ya kwamba nimepona.

Ulimi wangu ni mfupi sana kumshukuru na kumsifu Bwana kwa kuniponya.

J. L. O.

* * *

Yabisi Kavu Imekwisha

Nilikuwa na maumivu makali sana mwilini mwangu. Tangu Juni, niliposhikwa na ugonjwa wa mvilio wa damu moyoni, daktari aliniambia nitulie kabisa. Wakati wote katika ibada hizi nilijisikia ya kwamba Mungu ataniponya. Jana usiku nilipokea uponyaji wa papo hapo nilipoondoka kwenye ukumbi. Nisingeweza kusogeza mkono wangu wa kushoto hadi jana usiku. Nilikuwa na yabisi kavu kwenye mikono yangu yote miwili, bali sasa ninaweza kuisogeza. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya yale aliyonitendea na ninaahidi kudumu mwaminifu mpaka atakaponipeleka nyumbani katika ile Nchi Iliyo Bora Zaidi.

W. M.

* * *

Maumivu Kwenye Ziwa na Bega Yamekwisha

Nilikuwa nikiugua kwa muda wa miaka miwili kwenye ziwa langu la kulia na pia nilikuwa ninaumwa sana kwenye bega langu la kulia. Madaktari walinifanyia upasuaji miaka mitatu iliyopita bila mafanikio. Nilimwendea Daktari K. wa Petersburg naye akaniambia ya kwamba kama mambo yakiendelea namna hiyo, karibuni itakuwa ni kansa. Niliamua kumtumainia Bwana.

Uamsho wa Ndugu Branham wa uponyaji ulianzia kwenye tarehe 24 Oktoba, 1951, huko Bloemfontein na usiku wa kwanza nilipokea kadi kutoka kwa Billy, mwana wa Ndugu

Branham. Niliitwa kwenda jukwaani nikaombewe. Nikiwa nimesimama mbele ya Ndugu Branham, aliniangalia na kusema, "Wewe ni mwana wa Mungu. Walikufanyia upasuaji." Nikajibu, "Ndio," na halafu akasema, "Kitu fulani kinatoka kwenye ziwa lako sasa, na Bwana amekuponya. Nenda zako nyumbani." Yeye hakunigusa wala kuniombea, bali alinizungumzia tu. Tangu saa iyo hiyo niliponywa.

Niliposimama karibu na Ndugu Branham, hisia takatifu ilikuja juu yangu nami nilisikia mitetemo ya baridi. Ndugu Branham ni mtumishi halisi wa Mungu, mtu ambaye hunifanya niwazie juu ya Yesu.

Ninajisikia kama mtu mpya. Maisha yangu ya kiroho yamejengeka. Ninaomba zaidi na ninajisikia kama kushuhudia kwa ajili ya Bwana wangu kila mahali niendapo. Kikombe changu kinafurika kwa furaha. Ninajisikia kama kumwishia Yesu wangu kabisa kwa kuwa amenifanyia mengi. Sina maumivu tena katika ziwa langu wala kwenye bega langu la kulia. Ninalisifu jina Lake kwa ajili hiyo.

S. S.

* * *

Kuteswa na Henia

Pamoja na Mtunga Zaburi katika Zaburi 103, tunaweza kupaza sauti kwa nguvu "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi Jina Lake takatifu."

Moyo wangu umejaa hata kufurika kwa shukrani kwa Bwana kwa ajili ya yale aliyonitendea. Yeye alijua kuhusu shida yangu yote, na jinsi nilivyokuwa nimeteseka na henia kwa muda wa miaka 27. Nilipitia maumivu makubwa, bali niliendelea kumtumainia Mungu kwa ajili ya uponyaji. Nilikuwa nimesoma katika gazeti la "Mfariji" ya kwamba mikutano ya huko Bloemfontein ingeanza tarehe 24 Oktoba na nikaamua kwenda kule.

Nilipofanya yale Ndugu Branham aliyoniambia nilijisikia kana kwamba mzigo mkubwa ulikuwa umeondolewa kwangu. Niliona jambo hilo hasa wakati nilipotembea; tumbo langu lilisikika ni jepesi sana.

Sijawahi kuweza kulala kwa njia nyingine yo yote ila ile ya mkono wangu

wa kushoto kuishikilia hiyo henia. Sasa jambo hili halihitajiki tena. Mizigo yangu na masumbufu yote yameondolewa mbali. Ninaweza tu kusema, "Upendo wa Yesu ni wa ajabu, ajabu," nami ninampa Mungu utukufu wote.

J. M. H.

Imetiwa sahihi pia na Mchungaji: J. J. G.

* * *

Ugonjwa wa Figo na Moyo

Ninataka kushuhudia kwa ajili ya rafiki yangu ambaye ana umri wa miaka kumi na miwili. Mtoto huyu alikuwa mgonjwa kwa muda wa miaka saba. Alikuwa na ugonjwa wa baridi yabisi alipokuwa na umri wa miaka mitano na alikuwa akilazwa kitandani mara kwa mara kwa ugonjwa wa moyo, na mambo mengine. Tulikuja tukiwa na imani kubwa kwenye mikutano hii, tukiamini ya kwamba Ndugu Branham alikuwa anaweza kuomba na Yesu angemponya kabisa. Alipata kadi ya maombi bali hakuitwa kwenye mstari wa maombi, naye alivunjika matumaini, ninajua. Bali alimwita msichana huyu kutoka katikati ya wasikilizaji. Wakati alipokuwa akinena habari za ugonjwa wa figo yake, niliwazia, Loo! yeye hatauombea ugonjwa wake wa moyo. Lakini alifanya hivyo. Aliuona huo, pia. Yesu alionyesha ya kwamba msichana huyo pia alikuwa na ugonjwa wa moyo, na ameponywa yote mawili. Haleluya! Bwana asifiwe.

S. R.

* * *

Shida ya Tumbo na Henia

Ninataka tu kushuhudia ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele, akiwa angali anafanya ishara na maajabu. Yeye habadiliki.

Nimeugua kwa muda wa miaka minne kwa sababu ya tumbo langu. Nimekesha siku nyingi usiku bila kulala usingizi. Daktari aliagiza nitumie poda bali hazikufaa kitu sana. Wakati Ndugu Branham alipokuwa huko Bloemfontein, tuliamua kwenda kule na kuombewa. Wakati alipokuwa akiwaombea wagonjwa wote Bwana alinigusa na kuniponya. Mke wangu pia aliponywa henia jioni hiyo hiyo. Mungu atukuzwe kwa ajili ya rehema Zake.

H. C. H.

Imetiwa sahihi pia na Mchungaji J. J. G.

* * *

Ugonjwa wa Moyo

Nimeugua ugonjwa wa moyo kwa muda wa miaka kadhaa. Sikuweza kujitahidi kutumia nguvu hata kidogo bila ya

kuhisi athari yake, bali Mungu asifiwe, nimeponywa! Wakati nikihudhuria mikutano hiyo huko East London, tarehe 18 Novemba, nilikubali uponyaji wangu kutoka kwa Bwana. Chini ya huduma ya Ndugu Branham Bwana alinigusa na kuniponya kabisa. Wakati wa mikutano hiyo ambayo ilifuata uponyaji wangu, nilisaidia kuwabeba wagonjwa kupanda na kushuka kwenye vipandio bila ya kusikia athari yo yote. Nisingeweza kufanya hivyo isipokuwa nimeponywa na Mungu.

J. H. P.

* * *

Kuugua Ugonjwa wa Angina

Huu ni wakati wa furaha sana maishani mwangu. Jumatano asubuhi nisingeweza kutembea kwa mwendo mzuri wa kawaida urefu wa uwanja wa mpira wa miguu bila ya mpapatiko wa moyo, kukosa pumzi na maumivu makali mkononi mwangu, jambo ambalo kila mtu ambaye ameugua angina anajua. Wakati mtu huwezi kutembea na licha ya hilo huwezi kuinama na kulima bustani kidogo, wala mtu usingethubutu kuchukua ndoo ya kunyweshea, wala kuchuma maua machache, basi mambo si mazuri. Na basi Jumatano nilikuwa nimekuja kwenye mkutano nikiwa na imani kabisa ya kwamba kwa namna fulani ningempata Mungu katika baraka Zake kamilifu.

Ndugu Branham alianza kuzungumza, naye alizungungumza kwa bubujiko kubwa sana la imani. Uvuvio huu wa ajabu ulibubujika mwilini mwangu mwote na kutokea kwenye mikono yangu kama umeme. Nilijua basi niliponywa, ingawa sikuthubutu kusema jambo hilo. Nilifikiri ningengojea mpaka kesho, lakini nilijua kabla sijafika nyumbani kwamba mwili wangu ulikuwa na hali nzuri zaidi kwa sababu kutembea hadi kwenye gari langu kulikuwa ni rahisi sana. Kesho yake asubuhi nilitembea kwenye Ufuko wa Mashariki pamoja na mke wangu na kurudi tena dhidi ya upepo mkali. Nililima bustani kidogo na kulima kidogo kwa jembe, na leo nilitembea ili kuondoa kukakamaa kwa maana kamwe sijapata kutembea vizuri namna hii maishani mwangu. Bwana asifiwe.

S. C. H.

* * *

Kijana Aponywa Maumivu Makali Sana ya Kichwa

Baada ya kuwa mgonjwa na kutibiwa kwa muda wa miaka mitano, nilipokea uponyaji wangu huko Bloemfontein tarehe 24 Oktoba. Ndugu Branham aliniambia ya kwamba nilikuwa ninateseka na maumivu makali sana ya kichwa, jambo ambalo lilikuwa ni kweli, lakini niliponywa mara moja baada ya yeye kuniambia ya kwamba Yesu alikuwa amekwisha kuniponya

na ya kwamba ningeweza sasa kuufurahia uponyaji ambao ulikuwa ni wangu. Nina umri wa miaka kumi na minne na kwa sababu ya yale Yesu Kristo amenifanyia nimeyatoa maisha yangu Kwake.

A. S.

* * *

Polio na Kansa

Niliugua ugonjwa wa polio kwa zaidi ya miaka ishirini na saba. Hivi majuzi nimeshikwa na kansa ya ndani, bali niliponywa mara moja baada ya maombi ya pamoja ya tarehe 24 Okt. huko Bloemfontein.

Daktari wangu anasema ni mwujiza hasa na ana furaha sana ya kwamba nimeponywa. Uponyaji wangu umemleta mume wangu na watoto wangu kwa Bwana. Jina Lake takatifu lisifiwe.

G. E. D.

* * *

Watu Watatu wa Familia Moja
Wanapokea Uponyaji Katika Jioni Moja

Kwangu mimi ni majaliwa makubwa kuweza kushuhudia juu ya baraka na uponyaji niliopokea wakati wa uamsho wa Branham huko Bloemfontein. Nilipokea uponyaji wangu tarehe 27 Oktoba huko Bloemfontein na siwezi kumshukuru Bwana vya kutosha kwa ajili ya ukombozi wangu. Kwa muda wa miaka mitano niliugua baridi yabisi kila mwaka na mwaka wa sita, nilipokuwa na umri wa miaka kumi, neva zangu ziliharibika. Kwa miezi sita nilikuwa kwenye Hospitali Kuu huko Bethlehemu. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili goti langu la kushoto lilianza kuvimba. Miaka ya kwanza miwili ama mitatu halikuwa na hali mbaya sana lakini baadaye hali hiyo ilizidi kuwa mbaya zaidi. Juzijuzi, baada ya kujasiria kutembea maili moja, mguu wangu ungesikia maumivu sana hivi kwamba kwa siku tano ama sita ningeshindwa kutembea.

Nilitaka ushauri kutoka kwa madaktari kumi na wawili mbalimbali. Hata tulifikia kiwango cha kuwataka ushauri wachawi bali hakuna hata mmoja angaliweza kufanya jambo lo lote kunisaidia.

Madaktari na wataalamu mabingwa wa Bloemfontein waliwaambia wazazi wangu ya kwamba wasingeweza kufanya kitu cho chote wala kufanya ubainishaji sahihi.

Daktari Visser wa Bloemfontein alisema ya kwamba nilikuwa nina matatizo ya goti na kwamba lingerudia hali yake ya kawaida

kwenye umri wa miaka 24 ama 25 hivi. Juma moja tu kabla ya hapo Dk. Scheepers wa Johbg. alibaini gegedu lililokwanguliwa ambalo lingerekebishwa kwa kufanyiwa upasuaji.

Kwa kuwa tulikuwa tunakaa O.F.S. upasuaji ulipaswa kufanyiwa Bloemfontein. Juma lililofuata wataalamu huko Bloemfontein walikataa kufanya upasuaji na ndipo nikarudi nyumbani usiku uo huo nimevunjika moyo sana na kusikitishwa.

Hali yangu ikawa mbaya zaidi na goti langu halikuwa tu limevimba bali kwa wakati huu mguu wangu wote mzima na kifundo cha mguu na wayo pia. Nilidungwa sindano ya tofauti kwa kuwa daktari alifikiri nilikuwa na ugonjwa wa jongo. Usiku wa pili sikulala kamwe. Kesho yake tulimtaka shauri daktari mwingine. Dk. Kellerman na Daktari Jordaan walinifanyia uchunguzi vizuri sana nao waliamini ya kwamba misuli iliyo juu ya goti ilikuwa imedhoofika sana kuweza kudumisha kibandiko cha goti juu vya kutosha katika mahali pake pa kawaida, hivyo kusababisha maji kukusanyika.

Dk. Kellerman aliniandikia kwamba ninapaswa kubaki kitandani kwa juma moja na kufanya mazoezi fulani ya goti. Alhamisi ya juma lililofuata mkono na kiganja changu cha kulia pia vilianza kuvimba. Nililala kwa muda wa siku tatu usiku na mchana na daktari akahofu ya kwamba huenda nilikuwa nikishikwa na "malale." Tuliposikia juu ya mtu aliyetumwa na Mungu kuwaponya wagonjwa kwa njia ya maombi, wazazi wangu mara moja waliamua ya kwamba wangenipeleka kwake kwa ajili ya uponyaji.

Ilikuwa ni ajabu sana kuona viwete wakiinuka kutoka kwenye vitanda vyao na machela na kuona magari ya wagonjwa yakiondoka kwenye mikutano yakiwa matupu.

Mimi pamoja na shangazi zangu wawili tulipokea uponyaji wetu Alhamisi jioni. Tangu siku hiyo sina maumivu tena mguuni na mkononi mwangu na nimeweza kufanya kazi ya kutarizi kwa mkono huo na kutembea kwenda po pote pale nitakapo bila ya matokeo yoyote ya ugonjwa.

Nilikuwa mfuasi wa Kanisa la Dutch Reformed la Bethlehemu. Mimi, pamoja na wazazi wangu na familia nzima, tu wenye shukurani kwa Bwana kwa ajili ya uponyaji ambao amenitunukia, baada ya kuteseka kwa karibu miaka kumi na mbili.

J. D.

* * *

Maumivu ya Figo na Shinikizo la Damu la Juu

Tangu nilipokuwa na umri wa miaka miwili, nimesumbuliwa na ugonjwa wa figo. Miaka michache iliyopita mikono na miguu yangu imekuwa imevimba na nimekuwa nikiugua ugonjwa

wa shinikizo la damu la juu. Wakati wa mikutano ya huko Bloemfontein, Ndugu Branham alinielekezea kidole na kuniambia ya kwamba nilikuwa nikiugua kwa sababu ya ugonjwa wa figo. Aliniuliza kama jambo hili ni sahihi, nami nikainamisha kichwa changu. Ndipo akaniuliza kama nilimwamini Mungu na kama nilimwamini Mungu angeniponya, hapo tena nilijibu kwa kuitikia. Alijibu kwa kuniambia ya kwamba Mungu alikuwa tayari ameniponya. Kesho yake asubuhi kuvimba kote kulikuwa kumeondoka, shinikizo la damu lilikuwa ni la kawaida, na figo zangu hazijanipa shida yo yote tangu tarehe 24 mwezi wa Oktoba, wakati Ndugu Branham aliposema na mimi. Ninataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya tukio hili kwa sababu limenileta karibu zaidi na Yesu pia mimi na wazazi wangu tunajisikia kuwa na furaha sana juu ya jambo hilo.

A. P.

* * *

Polio, Ugonjwa wa Kidole Tumbo, na Kuumwa Tumbo

Nilikuwa nikiugua tangu kuzaliwa kwangu. Nina umri wa miaka kumi na tatu. Niliugua ugonjwa wa polio. Nisingeweza kula cho chote vinginevyo ningeanza kutapika. Nilikuwa nimevimba chini ya ziwa, na niliumwa na tumbo baada ya kula chakula. Nilienda toka kwa daktari mmoja hadi kwa mwingine bila mafanikio. Nilitumia aina yo yote ya dawa bali hakuna kitu kilisaidia. Nimekonda sana na ni mdogo sana kuliko umri wangu na ninaonekana kama mtoto wa miaka minane. Tarehe 26 Oktoba niliitwa kwenda jukwaani nikaombewe. Nilisimama mbele ya Ndugu Branham. Akasema, "Kipenzi, je! unaamini?" Nikasema, "Ndiyo." Akasesma, "Una ugonjwa wa kidole tumbo na shida kubwa ya tumbo." Akaniwekea mikono na kuniombea. Nilijisikia kama niliinuka kutoka sakafuni na nikasisimkwa mwili mzima. Nilijua kutoka wakati huo nilikuwa nimeponywa. Sasa ninaweza kula, kuruka, kukimbia na kufanya kila kitu nisichoweza kufanya hapo kabla. Bwana mpenzi amenifanyia mambo makuu sana.

V. S.

* * *

Mke na Mume Wote Wanaponywa

Mungu asifiwe, mimi na mume wangu tulipokea uponyaji wetu jioni moja. Ndugu Branham alinigeukia na kusema, "Wewe uliye kwenye machela ya mwisho ni mwanamke

anayekufa na usipotoka kwenye kitanda chako hutapona kamwe. Ni ini lako, sivyo? Umeponywa." Niliamka mara moja na tangu wakati huo kamwe sijaangalia nyuma. Bwana asifiwe. Nimekuwa kitandani kwa muda wa miezi mitano nikiwa na ini lenye usaha lakini tangu jioni hiyo nimekuwa mzima kabisa.

G. K.

* * *

Ugonjwa wa Mbweta

Nilipokea uponyaji wangu huko Capetown. Nilikuwa nikiugua ugonjwa wa mbweta lakini katika juma moja baada ya kuombewa hakukuwa na dalili yo yote yake. Mungu asifiwe nimekombolewa.

R. J. K.

* * *

Kiziwi Kwenye Sikio Moja Tangu Kuzaliwa

Nilipokea uponyaji wangu tarehe 4 Novemba huko Capetown. Nilikuwa kiziwi kwenye sikio langu la kushoto tangu nilipozaliwa bali sikio langu la kulia lilikuwa ni zima. Ndugu Bosworth aliniombea nami nikapokea uponyaji wangu kwenye sikio hilo la kushoto mara moja. Shukurani kwa Mungu. Wako mwaminifu,

G. A.

* * *

Magonjwa ya Pumu na Mkamba Yameondoka

Tangu nilipokuwa na umri wa kama mwezi mmoja nilikuwa nikiugua mashambulizi ya pumu na mkamba, na takriban, miezi miwili iliyopita nilikuwa kitandani nikiugua nimonia. Baada ya kuruhusiwa na daktari kuamka nilikuwa nimeachwa na maumivu makali sana mapafuni mwangu.

Ilikuwa ni kwa bahati sana kwamba nilihudhuria mkutano wenu wa pili, ikiwa ni tarehe 11 Novemba, 1951. Niliombwa na Bibi Van Dar Westhuizen kama ningepata wakati wa kumchukua baada ya mkutano huu kwisha kwenye kama saa 4 usiku huo. Nikamchukua, nikiwasili Wingfield kwenye saa 3:40 usiku. Niliwahi tu kusikiliza mwisho wa mkutano huo. Ulionekana kunipasha habari fulani, kwamba ni nini, sikujua hasa, nami nikaamua kuhudhuria mkutano mzima usiku uliofuata.

Nilikuwa nimevutiwa sana na ibada kwa sababu imani yangu katika Yesu ilikuwa ikikua moja kwa moja kwenye mkutano huo. Kabla hata sijaondoka kwenye eneo hilo,

nilijisikia ya kwamba maumivu kifuani mwangu yalikuwa yameanza kupungua na katika siku mbili hadi tatu maumivu yalikuwa yameondoka, yote ila tu kuchomwa kwa mara kwa mara. Tangu wakati huo nimeondoa nguo za ziada ambazo nilikuwa nikivaa, kwa kuona kwamba hazihitajiki. Sijaona kwamba ni lazima kuvaa nguo hizi tangu wakati huo wala sijakuwa na dalili zo zote za shida ya kupumua.

L. W. H.

* * *

Kuvuja kwa Moyo na Maumivu Makali Sana ya Kichwa

Niliponywa huko Capetown tarehe 31 Oktoba, 1951. Tangu nilipokuwa mtoto daima ilinibidi kunywa dawa za toniki kwa kuwa nilikuwa mdhaifu sana. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita wazazi wangu walinipeleka kwa daktari naye akasema kwamba nilikuwa na moyo unaovuja. Daima nilijisikia mchovu sana. Ndipo nikashikwa na homa ya baridi yabisi nilipokuwa na umri wa miaka kumi na saba, na hii pia iliniathiri moyo wangu. Kadiri nilivyopata umri mkubwa, ndivyo moyo wangu ulizidi kunyong'onyea. Majuma machache kabla Ndugu Branham hajafika, nilisikia nikiwa ninanyong'onya polepole. Niliomba angaa nipate kuishi mpaka Ndugu Branham atakapowasili, kwa kuwa nilikuwa na uhakika ya kwamba Yesu angeniponya.

Usiku wa kwanza wa mikutano ya Ndugu Branham, baada ya yeye kuwaombea wagonjwa jukwaani, alitwambia sisi sote tuamini, nami niliponywa papo hapo. Nilijisikia kama mtu mpya tangu wakati uo huo.

Pia, niliumwa sana na neva za kichwa. Nisingeweza kukaa kwenye makundi ya watu. Baada ya mikutano mikubwa kichwa changu kilikuwa katika hali ambayo kwamba nisingeweza kuyafungua macho yangu. Kwenye Ijumaa hiyo jioni (Tarehe 2 Nov.), mara nilitambua hapo mkutanoni ya kwamba Bwana alikuwa ameniponya na huo pia. Sijapata kuumwa na kichwa tangu Jumatano hiyo usiku.

Ninamtukuza na kumshukuru Yesu kwa kuniponya kupitia huduma ya Ndugu Branham. Itakuwa ni majuma matatu kesho. Siwezi kujizuia kumwambia kila mtu kuhusu nguvu za uponyaji zilizoko katika damu ya Yesu. Jina Lake lisifiwe.

E. S.

* * *

Kuponywa Ugonjwa wa Pumu ya Mkamba

Loo, haleluya! Utukufu kwa Mungu kwa kuwa kuna nuru ya jua nafsini mwangu leo. Yesu amekuja kuishi maishani mwangu, akiligeuza giza kuwa nuru ya mchana, na huzuni kuwa furaha. Loo, ni Yesu mtenda maajabu wa jinsi gani.

Kwa muda wa miaka kumi na tano nilikuwa nikiugua ugonjwa wa pumu ya mkamba. Wakati Ndugu Branham na kikosi chake walipokuwa wakifanya uamsho wa uponyaji huko Wingfield, Capetown, Afrika Kusini, nilimwomba Bwana asinipite bila ya kuuponya mwili wangu. Kila asubuhi niliondoka nyumbani kwangu kabla ya saa nne nipate kuwa na hakika ya kupata kiti kwa ajili ya ibada ya jioni. Mnamo tarehe 1 Novemba, 1951, wakati Billy alipokuwa akisambaza kadi za maombi alivuka kiti changu bila kunipa moja. Ndipo Billy Paul akarudi kwenye kiti changu tena na kunipa kadi ya maombi. Moyoni mwangu nilimshukuru Bwana wangu mpendwa kwa kuwa nilijua Bwana alikuwa amejibu maombi yangu na ataniponya. Wakati mstari wa maombi ulipoitwa jioni hiyo, Ndugu Branham alisema, "Ni wale tu wenye kadi za maombi F50 hadi F60 wanaopaswa kuja jukwaani." Niliangalia nyuma ya kadi yangu. Ilikuwa ni F54. Loo, jinsi nilivyomshukuru Bwana wangu mpendwa kwa kujibu maombi. Nilipokuwa nimesimama chini ya jukwaa, mwili wangu ulianza kutetemeka. Ilikuwa vigumu kwangu kuandika jina langu na anwani nyuma ya kadi. Nilipopanda kwenda kwa Ndugu Branham aliniangalia na kusema, "Dada yangu, umeponywa pumu yako; uliponywa wakati ulipokuwa ungali umesimama huko chini ya jukwaa." Loo, jinsi ninavyomsifu Bwana wangu kwa kuniponya.

M. H.

Taarifa za Daktari

24/10/45

Hii ni kushuhudia ya kwamba Bibi M. H. anaugua ugonjwa wa pumu ya mkamba.

Imetiwa sahihi na Dk. R.
8/11/51

Hii ni kuthibitisha ya kwamba nimemchunguza Bibi M. H. wala siwezi kupata dalili yoyote sasa changanuzi ya kubaini pumu.

Imetiwa sahihi na Dk. I. J. W.

* * *

Moyo Unapata Kuwa na Nguvu Tena

Kwenye tarehe 4 Novemba, 1951, katika jiji la Port Elizabeth nilipokea uponyaji wangu kutokana na moyo mdhaifu. Ndugu Branham alinielekezea kidole na kuniambia ya kwamba nilikuwa nimekwisha kuponywa na ya kwamba ningeweza kwenda nyumbani. Nilipata hakikisho la jambo hili siku chache baadaye wakati nilipoweza kuona dalili ya waziwazi ya nafuu katika hali ya moyo wangu. Mungu asifiwe.

M. M.

Ugonjwa Hatari Sana wa Wasiwasi

Ninapenda kumsifu Bwana kwa ajili ya uponyaji niliopokea huko Port Elizabeth. Tangu kuzaliwa kwa mtoto wangu wa mwisho, ambako kulikuwa ni miaka sita iliyopita, nimekuwa nikiugua ugonjwa wa wasiwasi na huo umeathiri moyo wangu. Pia mwezi uliopita nimekuwa nikiumwa vibaya sana na miguu ambayo iliniwezesha kutembea kidogo sana. Nimewaona madaktari kadhaa lakini hakuna ye yote angaliweza kunisaidia kwa kweli. Hiyo alasiri niliyopokea uponyaji wangu, maumivu yote yalitoweka miguuni mwangu. Sasa ninaweza kula kitu cho chote, jambo ambalo nisingeweza kufanya kabisa katika hali yangu ya wasiwasi hapo nyuma. Nimeongezeka ratili kumi na tano katika muda wa yale majuma matatu tangu kikosi cha Branham kilipokuwapo hapa Port Elizabeth. Ninamshukuru Mungu kwa yale amenifanyia na nitafurahi sana kama mtamwomba Mungu anifanye nuru inayoangaza kama ninavyojua ninapaswa kuangaza, bali mimi ni mnyonge sana kufanya hivyo mimi mwenyewe. Nawatakia heri.

D. M. P.

* * *

Kiwambo Kipya cha Sikio Chaumbwa

Ningependa kushuhudia ya kwamba Bwana ameniponya kabisa. Katika mwaka wa 1932 nilifanyiwa upasuaji muhimu wa uvimbe wa mfupa wa nyuma ya sikio lakini, Mungu asifiwe, wakati Ndugu Bosworth aliponiombea, Bwana alinipa sikio jipya kabisa na sasa ninaweza kusikia vizuri kabisa. Bwana asifiwe!

C. A. D.

* * *

Kawekwa Huru kutokana na Kansa Pia na Magonjwa ya Akina Mama

Ninapenda hapa kushuhudia ya kwamba Mungu aliniponya wakati wa ziara ya Ndugu Branham huko Port Elizabeth, mnamo Jumatano, tarehe 7 Novemba, 1951.

Nilikuwa nikiugua kutokana na ogani zangu za kike kwa muda wa miaka tisa. Nilikwenda toka kwa daktari mmoja hadi kwa mwingine, bali bila mafanikio. Mwanzoni mwa mwaka uvimbe ulianza shingoni mwangu. Daktari alinishauri nikubali huu uondolewe, bali jambo hili lilifanya tu mambo kuwa mabaya zaidi. Miezi mitatu baada ya huo kuondolewa, niliamua kumwona daktari bingwa wa kansa, kwa kuwa kuwashwawashwa na kuwangwa kulikuwa kunaogopesha sana. Ubainishaji wa daktari ulikuwa kwamba nilikuwa na kansa. Aliitoa hiyo kansa, ambayo ilikuwa kubwa kuliko thumuni, lakini tezi zilikuwa tayari zimeathirika.

Kulikuwa na uvimbe kwenye mkono wa kuume wa shingo yangu, na maumivu na kuwangwa kulikuwa kunanitesa sana. Nilijisikia daima mchovu, na nilikuwa nikiumwa na kichwa mfululizo. Niliumwa kwa muda wa miezi minne, na hali ya mambo ilikuwa ikizidi kuwa mbaya zaidi. Mwezi wa Oktoba nilimtaka ushauri mtaalamu bingwa mmoja, naye akanishauri ya kwamba nifanyiwe matibabu ya radiamu. Nilipaswa niende hospitali tarehe 24 Oktoba, bali niliamua kumtumaini Mungu kwa ajili ya uponyaji wangu. Niliomba na kuamini ya kwamba Mungu angeyasikia maombi yangu.

Mnamo tarehe 7 Novemba, mkutano wa kwanza wa ile iliyokuwa ifanyikie Port Elizabeth ulianza. Nilikuwa kwenye maumivu makali mno, bali nilienda mkutanoni nikiamini ya kwamba Mungu angeniponya. Hata sikupewa kadi, bali ile sauti nyororo ilisema, "Si suala la mtu ukiwa na kadi kwamba utaponywa." Ndipo mara moja nilimwazia Bwana Yesu amening'inia msalabani, na kutambua ilikuwa si kwa ajili tu ya dhambi zetu, bali alikufa pia kwa ajili ya magonjwa yetu.

Wakati Ndugu Branham alipotuombea sisi sote kwa pamoja mara alisema, "Yupo mama hapa mbele yangu," nami nikaomba kwa bidii, "Bwana, hebu huyo awe ni mimi." Ndugu Branham akaendela, "Ni mama mmoja anayeugua kansa na organi zake za kike, mponye, Bwana."

Wakati aliposema "kansa" ilikuwa ni kana kwamba kisu kilikuwa kikichomekwa kwenye bonge hilo gumu, nami niliomba ya kwamba Mungu Mwenyewe angefanya upasuaji huo. Papo hapo maumivu yaliondoka, na ugumu ubavuni mwangu ulitoweka.

Nikiwa njiani kuelekea nyumbani usiku huo nilianza kutapika vitu vigumu, na mara nikajisikia mzima kabisa. Asubuhi hiyo mume wangu na jamaa zangu walishangaa kuniona jinsi nilivyoonekana mzima. Ninamsifu Mungu na kumpa utukufu wote. Ninamshuhudia kila mtu ninayekutana naye. Baadhi yao wanafurahi pamoja nami, lakini wengine hawataniamini. Ninamshukuru sana Mungu kwa mwujiza alioufanya.

H. K.

* * *

Sikio Moja Ziwi Kabisa kwa Miaka Arobaini na Mitano

Nilipoteza kiwambo cha sikio cha moja ya masikio yangu kutokana na mlipuko ambao ulitukia wakati nilipokuwa mvulana wa miaka kumi. Hilo lilikuwa ni miaka arobaini na mitano iliyopita na sikio hili limekuwa ni ziwi kabisa.

Wakati Ndugu Bosworth alipoliombea, kusikia kwangu kulinirudia kikamilifu. Bwana asifiwe!

D. J. D.

Macho Yenye Makengeza Yananyoshwa

Jambo la ajabu limetukia nyumbani mwetu. Maskini msichana wetu mwenyeji mwenye umri wa miaka kumi na miwili aliyekuwa akitufanyia kazi katika miezi michache iliyopita alikuwa ana makengeza mabaya mno. Alikuwa na makengeza mabaya sana hivi kwamba ilikuwa ni vigumu kabisa mtu kuona kwamba alikuwa na macho. Macho yake yalionekana kuangalia chini juu ya pua yake na kuwa yamefichwa nusu pembeni. Watu wangemwangalia wakati alipokuwapo chumbani na alipokuwa ameondoka wangesema, "Hivi ninyi watu hamjisikii kuwa na mkosi wa kutisha sana kuwa na msichana kama huyo akiwafanyia kazi? Ninajisikia vibaya sana kila ninapomwangalia." Sisi, wenyewe, tungemtetea na kumkinga kwa kusema ya kwamba kwa kweli lingekuwa ni jambo ovu sana kwetu kama ingalitulazimu kumpa taarifa ya kuacha kazi ati kwa sababu tu alikuwa na makengeza. Kusema kweli, Mungu alikuwa ametubariki katika njia nyingi tangu alipokuja nyumbani mwetu.

Ndipo tukasikia ya kwamba Ndugu Branham alikuwa akija Port Elizabeth. Tulikuwa tumeambiwa juu ya uponyaji mwingi wa ajabu ambao ulikuwa umetukia kwenye mikutano yake. Tuliwazia sisi wenyewe, "Kama Ndugu Branham anaweza kuwaombea watu wengine nao wanaweza kuponywa kwa maombi yake, kwa nini asiweze kuyaombea macho ya msichana wetu mdogo wa kienyeji?" Tulimwambia juu ya kuja kwake, naye akaamini ya kwamba kama angelikuwa na imani angeponywa. Mapema Jumapili iliyopita asubuhi alienda kwenye Ukumbi wa Soko la Unyoya ambako mkutano ulikuwa ufanyikie. Mara ya kwanza alivunjika moyo sana kwa maana hakuchaguliwa kuingia katika mstari wa maombi. Lakini mwishoni mwa mkutano, Ndugu Branham aliwaambia wote wale waliotaka kuponywa wasimame wakati akiomba maombi ya pamoja kwa ajili ya wote. Yeye alikuwa ni mmoja wa wengi waliosimama.

Alienda nyumbani na amevunjika moyo wakati alipokuta kwamba macho yake yalikuwa yangali yana makengeza, bali aliamua kuendelea kuamini bila kujali alichoona.

Wazia furaha yetu kuu wakati siku mbili baadaye tuliona ya kwamba jicho lake la kushoto lilikuwa limenyoka na ni zima kabisa, na, Mungu asifiwe, siku mbili baadaye jicho lake lingine, pia, lilikuwa limenyoka na ni zima kabisa. Bwana asifiwe! Hapo siku zilizopita alitazama vitu na dunia ilonekana kama shaghalabaghala, bali sasa anaweza kuona kikamilifu kabisa. Bwana apewe sifa!

D. G.

Pumu kwa Muda wa Miaka Kumi na Mitano

Nina furaha kuwatumia ushuhuda wangu wa vile ambavyo Yesu aliniponya kwa nguvu kuu za Kiungu. Bwana asifiwe.

Tangu niliporudi kutoka kwenye mkutano wa uponyaji ninajisikia vizuri sana. Sikuwa nikifanya kazi zo zote ngumu, ambazo zilikuwa na athari kwa kifua changu, kwa kuwa nilikuwa na shida ya pumu kwa muda wa miaka kumi na tano. Ninaweza kufanya kazi yo yote sasa bila ya hofu. Ninamshukuru Yesu kwa kuniponya.

D. M.

* * *

Kuponywa Henia

Ninamshukuru Mungu kwa kuniponya! Mnamo jioni ya tarehe tisa Novemba, 1951, wakati nikiwa huko Port Elizabeth, Mungu aliniponya papo hapo nikiwa kwenye moja ya ibada za Ndugu Branham. Mimi sikuitwa kwenda kuombewa, bali Ndugu Branham alisema, "Yote yanawezekana kwa hao waaminio." Niliamini Mungu angeniponya, naye akaniponya.

Niliugua miaka minane baada ya kufanyiwa upasuaji wa kidole tumbo ugonjwa ambao baadaye uligeuka kuwa henia. Nisingeweza kamwe kufunga gidamu za viatu vyangu wala hata kuinama, bali Mungu na ashukuriwe jioni hiyo hiyo niliponywa. Niliweza kuinama na kufanya kila kitu nilichofanya miaka minane iliyopita. Ninampa Bwana sifa zote.

A. J. R.

* * *

Kuponywa Henia Yenye Ukubwa wa Mpira wa Soka

Baada ya kuzaliwa kwa mwanangu katika mwaka wa 1926, niliachwa na henia ya kitovu ukubwa wa mpira wa soka. Madaktari walinifanyia upasuaji bali hawakufanikiwa.

Jioni hiyo hiyo Ndugu Branham alimwelekezea kidole mume wangu na kumwambia kile alichokuwa anaumwa, na ya kwamba aliponywa, na mimi pia nilielekezewa kidole. Ndugu Branham aliniambia nisimame. Baada ya kuniambia juu ya henia, aliniambia pia kukubali uponyaji wangu. Mungu ahimidiwe! Mara hiyo henia ikaondoka mwilini mwangu wala hakuna dalili ya henia hii ambayo ilikuwa na ukubwa wa mpira wa soka. Mungu na ashukuriwe kwa sababu Yeye aliniponya na kuugusa mwili wangu.

M. G.

Pafu Lililokauka kwa Miaka Thelathini na Minne, Linafanya Kazi Kawaida

Wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia, niliathiriwa na gesi huko kwenye Mbuga za Flanders, na kwa zaidi ya miaka thelathini na minne nimekuwa nikitumia pafu moja tu kwa kuwa hilo lingine lilikuwa limekauka kabisa. Moyo wangu pia ulikuwa katika hali mbaya sana. Madaktari walikuwa wamenikatia tamaa kama nisiyeponyeka na wala asiyeweza kuishi muda mrefu zaidi.

Tarehe 7 Novemba, 1951, nilienda kwenye Ukumbi wa Soko la Unyoya nikiwa nina matumaini kabisa ya kwamba Bwana angeweza kuniponya. Wakati Ndugu Branham alipomwelekezea kidole mke wangu, ambaye alikuwa ameketi karibu na mimi, na kusema, "Umeponywa," nikasema, "Bwana, mimi pia; usiniache nyuma, tafadhali, Bwana." Ndipo Ndugu Branham akaniambia, "Simama!" Aliniambia shida yangu, akibaini magonjwa yangu kikamilifu na akaniambia nimeponywa. Mara nikaanza kupumua kirahisi zaidi na ninaweza kumsifu Mungu ya kwamba nimeponywa kabisa wala hapajakuwa na dalili yo yote ya athari za kuathiriwa na gesi tangu mikutano ya Port Elizabeth.

F. G.

* * *

Kiziwi kwa Muda wa Miaka Kumi na Mitatu

Kwa muda wa miaka kumi na mitatu sikuweza kusikia hata kidogo bali ninamsifu Bwana ya kwamba Yeye aliniponya kabisa. Ninaweza sasa kusikia mnong'ono ulio mdogo sana. Mungu asifiwe kwa ajili ya mguso Wake wa ajabu.

G. F.

* * *

Maumivu Mgongoni na Tumbo la Uzazi Lililoshuka

Ninataka kutuma shukrani zangu za furaha kwa ajili ya uponyaji nilioupokea kwenye mkutano wa Alhamisi, tarehe nane. Niliugua kwa miaka mingi maumivu ya mgongo na tumbo la uzazi lililoshuka. Nilipokuwa nimeketi mkutanoni nilipokea uponyaji wa papo kwa papo ambao kwa huo ninamshukuru Baba yetu wa Mbinguni.

E. C. H.

* * *

Uvimbe Kwenye Ubongo

Nina furaha sana kuweza kushuhudia yale ambayo Bwana amenitendea. Miaka miwili na nusu iliyopita nilianza kuugua kutokana na uvimbe kwenye ubongo. Kwa kipindi cha mwaka

wa 1950 nilikuwa kwenye Hospitali ya Johannesburg mara tatu ambako nilitibiwa na daktari hodari. Asingeweza kufanya kitu chochote na ndipo basi akanishauri kurudi katika miezi kumi na miwili ijayo ili aone jinsi ulivyokuwa umekua. Yote aliyoweza kufanya wakati huo ilikuwa ni kuagiza matibabu ya radiamu. Nilitibiwa mara moja tu, ambapo baada ya matibabu hayo madaktari walitangaza wasingeweza kunifanyia jambo lo lote. Kivimbe hicho kilisababisha maumivu makubwa sana kwangu na pia kiliharibu uwezo wangu wa kuona. Wakati mtu aliposimama mbele zangu ningeweza tu kutambua uso peke yake bali si kitu kingine tena.

Usiku wa kwanza nilipokuwa huko nilikwenda kukaa kwenye nafasi yangu katika eneo lililotengwa kwa ajili ya wagonjwa. Niliamini na kujua ya kwamba ningeweza kuponywa. Baada ya Ndugu Branham kuwaombea watu wapatao watano, aliangalia upande nilikokuwa na akanena nami. Wakati huo huo nilihisi kitu fulani kikitukia kwangu na giza lililokuwa mbele ya macho yangu lilitoweka. Wakati aliposema nami sikuwa nikimwangalia, bali mara nikamwelekezea uso wangu na ningeweza kumwona na maumivu yalikuwa pia yametoweka.

Sasa ni siku tatu wala sijasikia maumivu yo yote na ninaweza kuona vizuri sana. Sasa ninaishi na kulala bila kutumia dawa na ninajua ni matokeo ya yale Bwana amenifanyia. Kamwe sitaacha kumshukuru.

N. P.

* * *

Wasiwasi na Kuumwa na Tumbo

Maishani mwangu mwote nimekuwa nikiugua wasiwasi na tumbo lililotokeza mbele. Mungu alikuwa mwema kwangu na mke wangu katika kuturuhusu kuingia kwenye mstari wa maombi. Nilipofika kwa Ndugu Branham alisema, "Wewe ni nusu kiziwi, una wasiwasi na unaumwa na tumbo lililotokeza. Yote yameponywa sasa." Amani kuu ilishuka juu yangu na nimeacha kunywa dawa kwa ajili ya tumbo langu. Limefanya kazi kawaida tangu wakati huo. Kusikia kwangu ni bora zaidi, pia.

Daima nimeishi karibu na Muumba wangu bali inafurahisha sana kuwazia ya kwamba Yeye amekuja na kunigusa. Sijaacha kumshukuru Yesu kwa kuniponya. Rafiki yangu aliniazima kitabu kinachoitwa "Kristo Mponyaji" na kilikuwa ni cha kusisimua kwangu kujua kwamba mauti ya Bwana wetu msalabani yalikuwa pia ni kwa ajili ya uponyaji wa mwili pamoja na wokovu wa nafsi.

A. L.

Sketi Inapwaya Sana Baada ya Kuponywa Ini Lililotanuka

Nimekuwa nimelazwa kitandani kwa muda wa miaka mitano na miezi tisa. Moyo wangu na ini langu vilikuwa vimetanuka, ini kwa kipimo cha inchi kumi na moja na nusu. Wakati wa kipindi cha ibada moja ya alasiri nilikuwa nikimwomba Mungu aniponye, na kimya kimya moyoni mwangu niliendelea tu kuamini. Niliposimama kwenda nyumbani, nilisikia sketi yangu ikianguka chini juu ya nyonga zangu. Ilibidi niifunge kwa pini kwa kuwa nisingeweza kufunga mwanya wa kando wakati nilipokuja mkutanoni. Sasa kulikuwako na kupungua kwa ghafla kwa kiuno changu hivi kwamba hizo pini ziliacha mwanya mkubwa sana. Hadi kufikia wakati nilipofika nyumbani hakukuwa na uvimbe hata kidogo. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya uponyaji wangu.

H. R.

* * *

Mgonjwa wa Kiti Chenye Magurudumu Aponywa Magonjwa Mengi

Niliponywa kwenye jiji la Grahamstown mnamo tarehe 13 Novemba, 1951, baada ya kuugua pumu kwa muda wa miaka kumi na mitano. Kamwe sitasahau siku hiyo ya shangwe na furaha. Nimegharimia mamia ya pauni kwa madaktari na dawa. Hazikunifaa kitu na hatimaye moyo wangu ukanyong'onya. Daktari wangu alishauri sindano za rikosini kuimarisha misuli ya moyo wangu bali ilisaidia kidogo sana.

Niliposikia ya kwamba Ndugu Branham alikuwa anakuja Grahamstown niliamua ya kwamba yabidi kuhudhuria huo mkutano wake mmoja na wa pekee kule kwa vyo vyote vile. Kwa muda wa siku kumi na tano nililala kitandani nikihesabu siku na saa. Wakati mwingine nilikuwa mgonjwa sana hivi kwamba nilidhani nitaaga dunia kabla ya tarehe 13. Nilikuwa mdhaifu sana hivi kwamba ilibidi nisukumwe kwenye kiti chenye magurudumu. Tuliwasili kwenye ukumbi huo saa nne asubuhi, na kukaa humo mpaka saa tano usiku.

Ndugu Branham alikuja kwa utulivu sana jukwaani yapata saa tatu. Aliwaombea watu kadhaa waliokuja jukwaani na pia wengine kati ya wasikilizaji. Yapata saa 3:30 alinielekezea kidole na kusema, "Wewe

uliye kwenye kiti hicho cha magurudumu, uliye na pumu yako, moyo mdhaifu na magonjwa mengine mengi, umeponywa." Mungu asifiwe, wapendwa, ni wale tu ambao wameteseka kama nilivyoteseka wanaweza kuwazia furaha na shukrani za moyoni mwangu. Tangu wakati huo nilianza kupata nafuu. Licha ya kuwa mdhaifu mwilini mwangu na miguuni nilitembea nikatoka katika huo ukumbi. Ninamshukuru Mungu kwa rehema na ukombozi Wake kutokana na mateso yangu na ninamsifu kwa kumtuma Ndugu Branham maili elfu kumi katika kuyajibu maombi yangu kwa ajili ya uponyaji. Usiku huo nilienda kulala na nikaondolea mbali hilo tita la mito, nikaacha mitatu tu. Kwa kawaida ilibidi kuweka angalau dazani moja. Nilikuwa na usingizi mtulivu sana na wa amani mpaka saa 12:30 kesho yake asubuhi.

Habari zilienea ya kwamba nilikuwa nimeponywa kwenye mkutano wa Ndugu Branham. Marafiki walikuja kuniona, mchungaji alikuja, bali ilikuwa ni vigumu kwake kuamini mabadiliko waliyoona kwangu, kutoka mtu mwenye uso uliopauka aliyelala kitandani kubadilika kuwa mtu mwenye uso mzuri zaidi akitembea kila mahali. Daktari alinitembelea kwa ghafla, akachukua mapigo yangu ya moyo na kusema, "Jamani, ni mtu tofauti wa jinsi gani. Nimefurahi sana kukuta moyo wako katika hali hii nzuri." Daktari mwingine alikuja kuniona. Alikuwa amenishughulikia kwa zaidi ya miaka mitatu lakini alikuwa amenikatia tamaa kwa ajili ya moyo wangu. Akasema ya kwamba pumu ilikuwa imeuharibu na ya kwamba hapakuwapo na tiba kwa ajili yangu. Alikuwa amesikia kuhusu kuponywa kwangu naye akaja kuniuliza kama nilikuwa nimeenda kwa "Mponyaji wa Imani." Nikasema, "Mungu asifiwe, nimeponywa." Pia alielezea jinsi nilivyokuwa nikionekana mwenye afya nzuri.

Uponyaji huu umeigusa familia yangu pamoja na mimi mwenyewe kiroho. Daima nimesema ya kwamba kama ningelikuwa na afya yangu jinsi gani ningeweza kufanya kazi ya Mungu vizuri zaidi. Imekuwa ni wito kwetu sisi sote. Tumehudhuria mikutano kadhaa kushuhudia juu ya uponyaji wangu.

P. E. H.

* * *

Kifafa Kwa Muda wa Miaka Kumi na Mitano

Siwezi kamwe kuacha kumsifu na kumshukuru Mungu kwa ajili ya uponyaji wa ajabu niliopokea huko kwenye Ukumbi wa Jiji la Grahamstown mnamo tarehe 13 Novemba, 1951. Nilipokea uponyaji wa kiroho pamoja na uponyaji wa kimwili, Bwana asifiwe. Haipiti siku bila mimi kumwambia mtu fulani juu ya uponyaji wangu wa ajabu na baadhi

ya marafiki zangu tangu wakati huo wamehudhuria mikutano hiyo huko East London na wao pia wamepokea uponyaji. Kesho ndugu yangu na binti yake mdogo wanaondoka kwenda Johannesburg kwenda kwenye mkutano tarehe 5 Desemba, kwa kuwa wao pia wanataka kuponywa, jambo ambalo ninajua wataponywa wakiamini.

Nilikuwa nikiugua kifafa kwa muda wa miaka kumi na mitano. Nimekwenda kwa mabingwa. Hatimaye nilipelekwa huko Port Alfred nikawe huko pwani na pia kamwe sikukaa bila vidonge ambavyo ilinibidi kuvinywa kila siku. Daima nilihofu ya kwamba nitaanguka barabarani ama kazini na kuzimia, jambo ambalo lilitukia mara nyingi, na nilihofu kuachwa peke yangu.

Kama majuma mawili kabla ya Ndugu Branham kuja Grahamstown, nilianza kuumwa maumivu makali sana nyuma ya kichwa changu. Hakuna kitu kingaliweza kunisaidia nami nilihofu kila dakika ya kwamba nitashikwa na kifafa. Kitu fulani kiliendelea kunishawishi niende mikutanoni, jambo ambalo nilifanya. Nilipokuwa nimeketi miongoni mwa mamia ya wengine, Ndugu Branham alinielekezea kidole nami nikajisikia kana kwamba sumaku ilikuwa ikinivuta. Ilikuwa ni hisia ya ajabu nami nilitaka tu kuruka na kupaza sauti, "Bwana asifiwe," kwa kuwa nilijua mara moja ya kwamba nilikuwa nimeponywa. Wakati Ndugu Branham aliposema, "Bibi aliye na kofia nyeupe—kivuli cheusi kinakuja juu yako; una ugonjwa wa kifafa." Nilipoashiria kwa kichwa na kuinua mkono wangu, yeye alisema, "Bwana asifiwe, umeponywa." Loo, ni hisia ya ajabu jinsi gani—ningeweza tu kuendelea na kuendelea nikimwelezea kila mtu ninayemwona aamini na kuwa na imani nao pia watapokea uponyaji.

T.V.

* * *

Pumu kwa Muda wa Miaka Ishirini na Minne

Ningependa kumsifu Bwana kwa ajili ya nguvu Zake za uponyaji wa ajabu ambao ulitukia kwenye mkutano wa Branham huko East London tarehe 15 Novemba. Nilikuwa nimeugua pumu kwa muda wa miaka ishirini na minne, tangu umri wa miaka mitatu. Bali ninamsifu na kumshukuru Bwana ya kwamba si kwamba tu aliniponya kimwili bali na kiroho pia.



Uponyaji wangu ulitukia usiku wa kwanza wa ziara ya Ndugu Branham. Imani yangu ilitiwa nguvu sana hata niliponywa bila ya huyo Ndugu kuniombea. Roho wa Bwana alikuwa na nguvu sana miongoni mwetu hivi kwamba yote yaliyonibidi kufanya ni kuomba.

Usiku wa mwisho wa uamsho wa Branham nilimwomba Bwana amfanye Ndugu Branham aniambie kitu fulani. Aliniambia. Alisema ya kwamba nilikuwa nikiugua ugonjwa wa pumu na kwamba Bwana alikuwa tayari ameniponya. Ninafurahi sasa katika Bwana na kuahidi kumtumikia hata mwisho.

G. R.

* * *

Kansa Ilitoweka

Yapata miaka kumi na sita iliyopita niliugua sana na daktari akaitwa aje. Baada ya kunichunguza aliniambia niende kwenye chumba cha kufanyiwa upasuaji kwa ajili ya uchunguzi wa viungo vya ndani. Alinifanyia uchunguzi kwenye chumba chake cha kufanyia upasuaji na kuniambia ya kwamba nilikuwa na uvimbe wa ndani, ambao ulikuwa ukinyonya nguvu zangu na damu yangu haikuwa ikizunguka vizuri, na ya kwamba ninapaswa kufanyiwa upasuaji kuondoa uvimbe huu. Uvimbe huo hatimaye ulianza kutokeza, na kwa miezi sita iliyopita ilikuwa ni vigumu kwangu kuketi, na wakati wote maumivu yaliyo makali sana yalipita upande wa chini wa tumbo langu na kwenye muundo wa mifupa ya mgongo wangu.

Usiku wa pili wa uamsho wa Branham huko East London mnamo tarehe 15 Novemba, 1951, nilikuwa nimeketi kwenye sehemu ya wagonjwa, nikiomba kwamba nipate kadi ya maombi. Wakati Billy Branham aliponipita, alinipa moja, na wakati namba zilipoitwa, nilikuwa wa pili mstarini. Wakati nilipofika jukwaani, Ndugu Branham aliniambia, "Ninaona wewe ni Mkristo. Una uvimbe unaotoa seli na unazidi kuwa mkubwa. Ni kansa. Siku zingine una wingu jeusi linaloning'inia juu yako, na unajisikia umechoka. Umeponywa kansa yako." Mara alipotamka hili, nilipata hisia kwamba nilikuwa nimepona, na wakati niliporudi kwenye kiti changu nilijihisi ya kwamba uvimbe ule ulikwisha toweka. Nilipofika nyumbani nilijichunguza, na Bwana asifiwe, ule uvimbe ulikuwa umetoweka.

Nina hisia nzuri sana kiroho, na ninajisikia mtu wa tofauti sana kuwahusu watu wengine. Nina mwelekeo tofauti sana, wala siwezi kukoma kujisikia mwenye shukrani kwa Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji huu wa ajabu sana.

E. M.

* * *

Taarifa ya Mtu Aliyekuwa Anakufa na Matokeo ya Kumwamini Mungu Kwa Muda wa Miezi Minne Bila Kujali Dalili

Ningependa kuwapa shuhuda za wawili hapa East London. Mtu huyo alikuwa katika hali ya kufa akiwa na tyubu mwilini mwake mwote. Ndugu Branham alimwambia ya kwamba kulikuwako na giza nyuma yake lakini basi alimwona malaika wa Bwana na akamwambia ndugu huyu ya kwamba Mungu alikuwa ameyasikia maombi yake na ya kwamba hana budi kwenda nyumbani kwa kuwa alikuwa ameponywa. Mara aliamka, akaondoa tyubu zote mwilini mwake na akaenda nyumbani. Haleluya. Yeye sasa yuko katika afya nzuri.

Mwanamke mmoja ambaye Ndugu Branham alimwombea aliendelea kuwa na hali mbaya zaidi na zaidi bali alimwamini Mungu na baada ya miezi minne ya maumivu makali sana aliamka asubuhi moja amekombolewa na laana ya kansa.

A. G.

* * *

Bawasiri ya Ndani na Ugonjwa wa Akina Mama

Ninataka kumshukuru Mungu kwa kumtuma nabii Wake, Ndugu William Branham, kuizuru Afrika Kusini kutoa ujumbe wa uponyaji wa Kiungu, na kwamba niliombewa na yeye.

Nilipokea uponyaji wangu huko East London, jioni ya tarehe 15 Novemba, 1951. Nilikuwa mgonjwa tangu kuzaliwa kwa mwanangu, na nilikuwa nikiumwa sana wakati mwingine. Nilitibiwa wakati mmoja, wakati nilipokuwa mgonjwa sana na nikiwa katika maumivu, bali niliponywa tu kwa muda kidogo tu halafu nikateseka zaidi.

Baada ya ile jioni niliyoombewa, polepole nilipata hakikisho ya kwamba nilikuwa nimeponywa kwa kuwa ule ugonjwa haukurudi kamwe tena. Jioni hiyo hiyo, Ndugu Branham alizungumza na mimi na kusema, “Nenda zako nyumbani na upone, wala usisahau ahadi yako kwa Mungu kuishi maisha yako yote kwa ajili Yake.” Chanzo cha ugonjwa wangu ulikuwa ni bawasiri ya ndani na matatizo ya akina mama. Sasa sina maumivu tena wala sina shida tena na bawasiri. Mchungaji wangu na wengine wote pamoja na familia yangu wanashukuru kwa ajili ya uponyaji wangu.

Mimi pia nina furaha kushuhudia ya kwamba mimi ni mwana wa Mungu na ninataka kumtumikia Yeye maishani mwangu mwote, kwa sababu nisingeweza kamwe kupata rafiki mzuri zaidi na wa kweli kuliko Yesu, ambaye daima huelewa na haja zangu na hunisaidia kwenye njia ngumu ya maisha.

Nilishuhudia miongoni mwa marafiki zangu na kwa mume wangu ambaye hajaokoka, na Mungu na ajalie ya kwamba nafsi hiyo moja tu, kwa ushuhuda wangu, ijaliwe kuipata njia yake ya kuelekea Kalvari.

Mungu na akubariki, Ndugu Branham.

M. C.

* * *

Mgongo Uliodumaa Sasa ni Mzima

Mimi ni mmoja wa wagonjwa waliopokea uponyaji kupitia kazi ya Yesu Kristo. Ninamsifu Bwana kwa maana ameosha dhambi zangu. Nilipokea uponyaji wangu huko Sehemu za Ukingo wa Mashariki. Ilikuwa ni tarehe 18 Novemba nami nilikuwa mgonjwa kwa muda wa miaka kumi na saba. Mgongo wangu ulikuwa umedumaa tangu nilipokuwa na umri wa miaka mitatu lakini sasa ni mzima. Wakati Ndugu Branham alipokuwa akiwaombea watu wote, aliwaambia waweke mikono yao kwenye sehemu ya mwili wao iliyokuwa inaumwa. Niliweka mkono wangu mgongoni mwangu. Wakati wa maombi nilisikia kitu fulani kikiuinamisha mgongo wangu kwa nyuma. Nilimwomba ndugu yangu aliyekuwa karibu nami auangalie mgongo wangu. Alishangaa alipougusa na kuniambia nilikuwa nimeponywa. Mgongo wangu ulikaa sawa na hata uko vivyo hivyo leo. Niliponywa mara moja kabla Ndugu Branham hajafunga maombi yake. Mhudumu wangu, N. Bengu, alifurahiwa kwa sababu alikuwa ameniombea mara nyingi. Watu wa kanisa langu wanafurahi pamoja na mimi kwa sababu Yesu amekuwa ni wa ajabu sana kwangu. Wako mwaminifu,

E. M.

* * *

Kiziwi Kabisa na Magonjwa Mengine

Niliposikia ya kwamba Ndugu Branham alikuwa anakuja Afrika Kusini, niliamua ya kwamba ningeenda East London na nifanyiwe maombi kwa sababu nilikuwa mgonjwa mahututi na kiziwi kabisa. Sikupata nafasi ya Ndugu Branham kuniombea, bali hata hivyo nilipokea uponyaji wangu. Usiku wa kwanza nilipokuwa hapo niliona baadhi ya watu wakisogea mbele. Nilikuwa kiziwi na sikuwa

nimesikia nani alikuwa ameitwa, kwa hiyo nilisogea mbele pamoja nao. Mhudumu mmoja aliniuliza nilichotaka, ama kitu kama hicho. Nilimwambia nilikuwa kiziwi na kwa kuwa sikuwa nimesikia kilichosemwa, nilimwomba aandike kile alichosema. Aliandika na kuniambia ya kwamba namba yangu haikuwa imeitwa na ya kwamba ninapaswa kutafuta mahali pa kuketi chini. Wazia kuvunjika kwangu moyo kukubwa. Nililia kwelikweli wakati niliporudi kwenye kiti changu. Wakati Ndugu Branham alipowaombea wagonjwa, mimi pia niliomba kwa bidii sana ya kwamba Mungu angeniponya. Vema, hakuna kitu kilichotukia, bali nilisikia mguso wa Kiungu wakati mitetemo baridi na ya joto ikipitia mwilini mwangu na moyo wangu kudunda kwa haraka.

Jumapili asubuhi nilikuwa mgonjwa kwelikweli kwa vile niliugua kwa miaka saba mapafu mabovu, yabisi kavu miguuni mwangu, na ugonjwa wa kibofu nyongo. Nilikuwa na huzuni na nikaiambia familia yangu ya kwamba afadhali niende nyumbani kuliko kukaa na kujaribu kuingia kwenye mstari wa maombi. Binti yangu alinisihi kuendelea kukaa mpaka Jumatatu. Baada ya chakula cha mchana nilisikia kelele kidogo katika masikio yangu, kwa hiyo nikasema tu, "Asante, Mungu. Ninajua na ninaamini ya kwamba unaniponya." Sikuwaambia watoto wangu lo lote juu ya jambo hilo. Nikiwa njiani kuelekea kwenye ibada nilimsikia binti yangu wa kwanza akimwambia dada yake ya kwamba kama Mama angekuwa na imani angeweza kuponywa. Nilijibu nikamwambia ya kwamba nilikuwa na imani na ya kwamba nilikuwa nimeponywa. Walishangaa sana sana kusikia ya kwamba nilikuwa nimesikia mazunguzo yao. Nikasema, "Naam, Mungu asifiwe, nimeponywa na nilisikia yale mliyosema." Nilipokea kusikia kwangu papo hapo bali nilipokea uponyaji wa yabisi kavu na magonjwa mengine polepole. Sasa, Mungu ashukuriwe, ninajisikia mzima kabisa. Mchungaji wangu alifurahi na akamsifu Mungu pamoja na mimi, ya kwamba Mungu alikuwa ameuponya mwili wangu. Jambo hilo limetuvuta sote karibu zaidi kwa Bwana. Mungu ashukuriwe kwa ajili ya Ndugu Branham na huduma yake.

M. M. N.

* * *

Kifafa kwa Muda wa Miaka Minne

Binti yangu mdogo alipokea uponyaji huko East London wakati William Branham alipomwombea mnamo tarehe 18 Novemba. Alikuwa akiugua kifafa kwa zaidi ya miaka minne. Tulimpeleka akachunguzwe na madaktari kadhaa. Wataalamu wawili wa maungo pia walikuwa wamempa matibabu. Hakuna hata mmoja angaliweza kumponya mtoto huyo. Januari

iliyopita tukiwa huko Johannesburg alishikwa na kifafa mara tatu katika muda wa saa tatu. Tuliita daktari fulani siku hiyo na ilibidi aingie kwenye hospitali ndogo ya binafsi kuchunguzwa. Daktari huyo aliwasiliana na mtaalamu. Alifanyiwa Eks-rei ya kichwa, ambayo ilionyesha hakuna mifupa iliyovunjika alipoanguka. Ilibidi pia afanyiwe uchunguzi mwingine kwenye Hospitali Kuu. Baada ya majuma matatu waliniambia hakukuwa na tiba yo yote, hatuna budi kuendelea tu kumpa dawa.

Tulisoma hadithi ya maisha ya Ndugu Branham kabla hajafika katika mji wetu. Nilikuwa na hakika kabisa kwamba Mungu angemponya mtoto wetu kupitia kwa Ndugu Branham. Tulikuwa na shauku sana ya kumwona.

Jumapili, ule mkutano wa mwisho, tuliingia kwenye mstari wa maombi. Ndugu Branham akasema, "Mama, je! utaamini? Ninajua mtoto wako ana shida gani." Nikasema, "Nitaamini." Akasema, "Yeye ana kifafa." Niliinua mkono wangu wa kuume na nilitaka kulia vibaya sana. Ndugu Branham aliomba kwa bidii sana. Mimi pamoja na msichana wangu tulisikia tumejaa shukrani sana kwa Mungu Baba yetu na Ndugu Branham, nabii Wake. Ndipo Ndugu Branham akasema, "Mama, je! unaamini ya kwamba mtoto wako ameponywa?" Nikasema, "Kwa moyo wangu wote." Ndipo akanipa mkono na kusema, "Atakuwa mzima, nenda nyumbani wala usihofu." Tukarudi kwenye viti vyetu katika ukumbi huo na kuomba na kumshukuru Mungu.

Nilitambua wakati wa uamsho wa Branham ya kwamba nilikuwa nikiomba vibaya. Daima nilimwamini Mungu na niliamini maombi, bali nilikuwa nikiomba na kusihi wala sikuwa nimekubali ahadi iliyotolewa na Mungu kama ambayo tayari imetukia. Hiyo mikutano ya ajabu ilitufundisha sisi sote jambo fulani ambalo hatukuwa tumejua hapo awali.

P. B.

* * *

Kuponywa Kifua Kikuu

Hata siwezi kuelezea kwa kalamu na wino ushuhuda huu. Nililazwa kwenye Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza tarehe 20 Agosti kwa ajili ya kifua kikuu. Mhudumu wangu aliniletea ushirika wa meza ya Bwana hospitalini. Nilimwomba kama ningeweza kwenda kwenye mkutano wako. Alikubali kwa furaha na akasema tunapaswa

kuwekea mikono zaidi. Aliniambia jinsi alivyokuwa amemwekea mikono mtoto mchanga aliyekuwa amekonda sana aliyekuwa karibu na kufa, na maskini nafsi hiyo ikapona kabisa ugonjwa wa kifua kikuu. Daktari alinipa ruhusa na kunitakia heri na fanaka.

Wakati wewe, Ndugu Branham, ulipokuja jukwaani, niliomba kwa bidii sana kwamba utatufanyia jambo fulani sisi wagonjwa waliolazwa vitandani. Nilikuwa nikihisi ya kwamba maombi yangu yalikuwa yakikuzuia kufanya jambo fulani. Ndipo ukasema, "Wekeaneni mikono." Tulifanya hilo kwa furaha nawe ukaomba vizuri sana na kusema, "Mnaweza kuondoka mwende zenu mmeponywa." Nilisikia kitu fulani kikitenda kazi mwilini mwangu mwote kama waya wenye umeme. Nilipatwa na hisi tulivu sana na nikarudi hospitalini nikimsifu Mungu. Nilingojea mpaka Eksirei yangu ilipokuja, na daktari akanionyesha ilikuwa imefanikiwa. Ningeweza kuona tofauti wakati ile Eksirei ya zamani na ile mpya zilipolinganishwa. Ninamsifu Mungu kwa ajili ya jambo hili. Daktari akasema ningeweza kwenda nyumbani na kuripoti kwake tena katika muda wa miezi miwili.

S. S. K.

* * *

Jamaa Inaokoka kwa Ajili ya Uponyaji

Sijui niseme nini, kwa maana maneno yanashindikana kwangu kupata lugha inayofaa ya kumsifu Mungu kwayo.

Nimekuwa mwaminio aliyezaliwa mara ya pili kwa muda wa miaka ishirini na mitano na Mungu amenibariki katika njia nyingi. Kwa muda wa miaka mitano nimekuwa nikiteseka kwa maumivu yaliyokuwa ndani ya mwili kutokana na jeraha la kujifungua mtoto. Hili lilifanyika kuwa donda ndugu na tumbo langu la uzazi lilitoa usaha na kusumishwa hata daktari wangu wa Port Shepstone akanishauri nifanyiwe upasuaji. Aliondoka kwenda Uingereza nami nikaenda kwenye Hospitali ya Addington, ambako nilifanyiwa upasuaji mwanzoni mwa mwaka wa 1950. Upasuaji huo ulifanikiwa bali tumbo langu la uzazi lilikuwa limejaa toksini na sumu.

Nikiwa hospitalini mambo yalianza kuniendea vibaya zaidi katika siku ya tisa baada ya upasuaji. Hatimaye niliondoka hospitalini na nikawasili nyumbani nikiwa mnyonge katika mwili wala sikuwa nimepona. Yapata mwezi mmoja baadaye nilipooza kutoka kwenye nyonga zangu kwenda juu, pamoja na sehemu moja ya mguu wangu wa kushoto. Nilishikwa na mipapatiko mibaya sana ya moyo kila siku, mingine ikidumu mara kadhaa kwa saa moja. Nilikuwa na shida katika kupumua pamoja na kula

na nikawa nimechoka sana hata nikajisikia ya kwamba ningekufa. Nililazwa kitandani kwa kama miezi tisa, nikikonda sana na kuwa mdhaifu.

Baada ya majuma kadhaa katika hali hii huku madaktari wawili wa Port Shepstone wakishindwa kuuelewa ugonjwa wangu nilianza kumsihi Mungu kwa maombi ya bidii. Nilijua nafsini mwangu ya kwamba mwanadamu akikata tamaa Mungu hupata nafasi, kwa hiyo nilimwomba Mungu kuliingilia; niliomba msamaha, kusafishwa, na kuponywa na kwa imani kwa dhati kabisa nilivyojua kuomba. Nilikuwa tayari nimekisoma kitabu cha Ndugu Branham mara chache, na pia nilikuwa nikipokea gazeti lake la uponyaji kutoka Marekani. Wakati kila kitu kilipokuwa kimeshindikana, Mungu katika rehema Yake alimtuma mwanamke mmoja mwananchi, ambaye sikumjua wala sijapata kumwona tangu wakati huo, kuniombea na mara nikaanza kupata nafuu. Kesho yake kiharusi kilikuwa kimekwisha wala hakijapata kurudi. Nilikuwa nimepokea uponyaji kwa sehemu. Katika hali ya udhaifu sana nilisindikizwa na akina mama wawili kurudi Durban kwa ajili ya matibabu ya umeme na kusingwa. Matibabu yalianza tarehe 24 Octoba, 1950, na yakaendelea hata kwenye juma la pili mwezi wa Aprili, 1951, na yalitolewa na msingaji mwanaume anayejulikana sana aliyeishi kwenye Barabara ya Umbilo, Durban. Alikuwa ameniambia nilikuwa mmoja wa watu wagonjwa sana aliopata kuwatibu uvimbe wa misuli. Mtu huyu alishuka akaja Port Shepstone kuniona wakati nilipokuwa mgonjwa mahututi. Baada ya miezi mitano na nusu ya matibabu hapa nilianza kupata nguvu na nikaruhusiwa kwenda nyumbani. Hata hivyo, niliendelea kupatwa na maumivu makali sana ya mara kwa mara ya kichwa na mipapapatiko ya moyo, na pia maumivu kutokana na uvimbe wa misuli. Nilishangaa ni kwa nini Mungu hakuwa amenipa uponyaji mkamilifu.

Huko Durban nikiwa nimefika kwenye mafundisho yenye nguvu ya Kikosi cha Branham, Roho alinisadikisha ya kwamba yote hayakuwa sawa maishani mwangu. Mara, kwa unyenyekevu lakini kwa furaha, niliyatoa mapenzi yangu yote kwa Bwana, na Alhamisi, tarehe 22 Novemba, 1951, wakati nikiwa nimeketi huko juu sana kwenye safu za viti katika Uwanja wa Mashindano ya Mbio za Farasi wa Greyville, Durban, nilihisi mguso wa Mungu wa uponyaji na nikajua ya kwamba nilikuwa nimeponywa. Nilisikia hisi yenye joto na msisimko ukipitia mwilini mwangu mwote na nikajua ya kwamba hii ilikuwa ni Mungu akinipa uponyaji wangu. Ninajisikia mwenye hali njema na mzima sasa na ninaendesha gari letu ambalo sijaligusa kwa muda wa miaka miwili.

Moyo wangu wote na nafsi vimechochewa kufikia kwenye kilindi chake, nami nimejazwa na kicho kikuu na mshangao kwa upendo na uvumilivu wa Mungu kwa ajili ya mwanadamu

mwenye dhambi. Siwezi kamwe tena kutilia shaka ahadi zo zote za Mungu. Naomba anifungulie kila moja ya hizo. "Bwana, ninaamini."

Wakati wa uamsho wa Branham, Mungu alinipa furaha ya kuona ndugu zangu wawili, wake zao na watoto wao wakipokelewa katika familia ya Mungu baada ya miaka kadhaa ya kuwaombea. Haleluya! Mungu asifiwe kwa ajili ya wokovu. Mungu asifiwe kwa ajili ya uponyaji.

A. D. C. J.

* * *

Mkatoliki Apokea Ukombozi Kutokana na Kisukari na Mavune ya Miguu

Ninataka kumshukuru Mungu kwa sababu ameniponya na magonjwa yangu. Wakati nilipokuwa nikihudhuria mmoja wa mikutano yako niliketi na kusikiliza kwa sababu nilitaka kupokea kila kitu ambacho Mungu alikuwa nacho kwa ajili yangu. Mimi si Mprotestanti. Nililelewa kama Mkatoliki. Bali ulituhakikishia ya kwamba tuliponywa kwa imani nami nilimwamini Mungu.

Niliugua kukakamaa kwa magoti na miguu yangu na kwa muda wa miaka mitano nimekuwa nikinywa insulini kwa ajili ya kisukari. Kwanza nilipokea dalili kwamba Mungu alikuwa akiyasikia maombi yangu na kuikubali imani yangu wakati kusanyiko liliposimama kuimba ule wimbo, "Kusimama kwenye Ahadi za Mungu." Mimi, pia, nilisimama bali nilisikia kizunguzungu na kuangusha miwani yangu. Inaonekana, ninapoangalia nyuma sasa, kwamba nilikuwa nimezirai karibu wakati huo wote wa ibada kwa sababu ya vile nilivyojisikia wala sikumbuki cho chote kilichotukia. Lakini nilipokuwa nikiamka kwenda nyumbani baada ya ibada niliona ya kwamba ukavu wote miguuni na magotini ulikuwa umeondoka. Sikuhitaji fimbo tena. Nilienda nyumbani nimesisimkwa sana hata nilikuwa nimesahau kuhusu kisukari changu.

Kesho yake asubuhi nilipima na kuona kwamba hakukuwa na sukari. Hapakuwa na haja ya kunywa insulini. Nilipima mara nyingi siku nzima bila ya dalili yo yote ya sukari. Kesho yake nilienda kwa daktari naye akaniambia ya kwamba yeye pia alikuwa amesikia juu ya taarifa zingine, ila kwamba inanipasa kuwa mwangalifu na kuendelea kupima kisukari. Mungu asifiwe, hakuna dalili ya kisukari mwilini mwangu na kule kukakamaa kwenye magoti yangu ambako niliugua kwa miaka mingi kumetoweka. Mungu ashukuriwe, Yeye ameyasikia maombi yangu.

Bibi B.

Huru na Ugonjwa wa Moyo

Utukufu wote na apewe Mungu kwa kuniponya ugonjwa wa moyo. Nilisikia mguso wa mkono wa uponyaji wa Mungu wakati Ndugu yetu mpenzi Branham aliponiambia nisimame kwa miguu yangu wakati malaika aliponielekezea kidole kwake. Ambapo hapo awali mikono na miguu yangu na mwili mzima vyote vilijisikia vimefungwa, sasa ninajisikia huru.

L. E. H.

* * *

Kuponywa Ugonjwa wa Akina Mama

Niliponywa huko Durban tarehe 22 Novemba, 1951. Nilikuwa mgonjwa kwa mwaka mmoja. Nilienda kwa madaktari wengi na hata nilikaa kwenye hospitali moja kwa siku nyingi bali haikuniletea nafuu yoyote katika hali yangu. Kwa msaada wa Bwana wetu Yesu, niliponywa. Ndugu Branham aliniuliza kama nilimjua. Nikasema "La," naye akasema yeye hakunijua. Akasema, "Mungu anakujua." Ndipo Ndugu Branham akawaambia watu ya kwamba angependa kuzungumza na mimi bila maikrofoni. Kila neno Ndugu Branham alilosema nami lilikuwa ni kweli. Alifanya jambo hilo kwa msaada wa Mungu. Nilipata imani nilikuwa nimeponywa wakati nilipotoka jukwaani. Uponyaji huo ulikuwa ni wa papo hapo. Nilikuwa na ugonjwa wa akina mama. Matokeo ya uponyaji wangu yameniongoza kwenye maisha ya kweli ya Kikristo.

S. C.

* * *

Aponywa Ugonjwa wa Kansa

"Nawasalimu katika Jina la Bwana wetu Yesu. Utukufu na apewe Mungu, mambo makuu ameyafanya."

Ni kwa furaha kuu ambapo ninaandika ushuhuda wangu wa kuponywa kwangu ugonjwa wa kansa. Nilipokea uponyaji wangu katika Ukumbi wa Jiji la Durban, tarehe 21 Novemba, 1951.

Nimekuwa na shida ya tumbo la uzazi kwa miaka minne iliyopita na nimetibiwa na madaktari na hospitali mbalimbali. Kwa miaka miwili iliyopita nimekuwa nikiumwa sana, na nimefanyiwa upasuaji mara nne na kutokwa na damu kubaya sana mara tatu, pamoja na kutokwa na damu kidogo mara kadhaa.

Yapata miezi saba iliyopita nilishauriwa na daktari kufanyiwa upasuaji mwingine ili kuiondoa hiyo kansa. Ni mwaka mmoja kamili tangu niliposhuku ya kwamba nilikuwa

na kansa na nilipowauliza madaktari wawili tofauti katika nyakati mbili mbalimbali, niliambiwa ya kwamba hilo ndilo walilohofia.

Nilipata uhakika wa uponyaji wangu usiku ule ule wakati Ndugu Branham alipomkemea pepo wa kansa atoke ndani yangu. Nilisikia tumbo langu likisogea juu kwenye kifua changu mara mbili, na mara ya tatu nilisikia gesi ikitoka moja kwa moja kinywani mwangu. Ndipo niliweza kupumua vizuri tena. Ndugu Branham aliniambia ya kwamba nilikuwa ninaumwa kansa, kwamba nilikuwa nimefanyiwa upasuaji, na kwamba nilikuwa ni mama mzazi anayeteseka. Kila kitu alichoniambia kilikuwa ni kweli. Nilisikia nguvu kuu za kimbinguni zimenizunguka, na ilionekana kwangu kana kwamba niko nusu kwenye njozi. Rafiki zangu na jamaa zangu baadaye walisema ama walinikumbusha kuhusu baadhi ya mambo ambayo sikuyasikia. Ndugu Branham pia alisema ya kwamba ningekuwa mgonjwa kwa saa sabini na mbili. Usiku huo nilipoenda kitandani, nilitokwa na damu. Baada ya saa sabini na mbili, nilikoma na nimekuwa mzima mpaka kwenye dakika hii ya sasa. Nilikuwa nikisikia maumivu makali sana kwenye tumbo langu la uzazi, kwenye mgongo na kutokea kwenye uti wa mgongo hadi kwenye kichwa changu. Kuumwa na kichwa kulikuwa ni kipandauso, na ilibidi nitengenezewe miwani moja ambayo nilikuwa nimevaa kwa miezi kumi iliyopita. Lakini niliivua baada ya kuondoka kwenye jukwaa la ukumbi huo wa jiji, na sijapata tena yo yote ya mashambulizi hayo makali sana ya kikatili. Amina! Mimi ni kiumbe kipya.

Nilikwenda kumhoji daktari wangu juma moja lililopita, naye akasema ya kwamba nilikuwa ni mwanamke mgonjwa sana miezi michache iliyopita na kumekuwako na badiliko kuu na halisi tangu wakati huo. Alifurahia sana badiliko hilo. Marafiki zangu wote wameona badiliko kubwa katika sura yangu. Familia yangu inafurahi katika Bwana. Jirani zangu wamevutiwa sana na wanakungojea kurudi kwa Mchungaji Branham kwa hamu.

Mungu ashukuriwe kwa ajili ya mikutano mikubwa sana ya ufufuo ambayo Durban limepata kuwa nayo.

F. H. G.

* * *

Ugonjwa wa Uti wa Mgongo Umetoweka

Ninataka kumtukuza Mungu kwa ajili ya kazi Zake za ajabu. Jana usiku chumbani mwangu nilipokea uponyaji wa mgongo wangu. Nimesumbuka kwa muda mrefu na shida ya

uti wa mgongo, tangu kuzaliwa kwa mtoto wangu mchanga. Sasa ninamsifu Mungu kwamba jana usiku nilihisi nguvu za Mungu kupanda na kushuka kwenye uti wangu wa mgongo na tangu wakati huo sijapata hata chembe ya maumivu. Ninamsifu na kumshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo.

W. M.

* * *

Kuponywa Vidonda na Pepo Mchafu

Nilipokea uponyaji wangu kwenye Uwanja wa Michezo ya Mbio za Farasi wa Greyville, huko Durban, tarehe 22 Novemba, 1951. Nilikuwa mgonjwa kwa miaka miwili iliyopita. Nilikwenda kwa daktari na kwa majuma matano yaliyopita nilikuwa hospitalini. Nilipata uhakika ya kwamba nilikuwa nimeponywa mara Ndugu Branham aliponigusa na kunibariki katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Ndugu Branham aliniambia ya kwamba nilikuwa na vidonda na pepo mchafu ambaye alikuwa akinisumbua usiku. Aliniambia niende nyumbani na nile kitu cho chote nilichotaka. Uponyaji ulikuwa ni wa papo hapo.

Ilikuwa kwenye wakati fulani uliopita wakati mara nilijikuta kwamba nisingeweza kula cho chote hata kidogo, na wakati nikijitahidi kujilazimisha kula, nilisikia maumivu makali kifuani na nikaanza kutapika. Nilipoteza ratili ishirini na tano za uzito katika majuma mawili ya kwanza na ratili zingine ishirini na tatu. Nilishindwa kusimama sawasawa kwa miguu yangu na kama ilinibidi kunywa maziwa, nilikuwa nikitapika.

Marafiki zangu wote na wazazi, walisema ya kwamba Bwana Yesu Kristo kweli aliyajibu maombi yangu na aliniponya na kunipa maisha mapya kwa sababu ya imani yangu Kwake. Hawakunitarajia kuishi wakati walipoona jinsi nilivyokuwa mgonjwa mahututi hospitalini. Niliponywa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo wala hakuna kitu kasoro kwangu. Maumivu yangu na kutapika vyote vimetoweka. Kule kuona vitu vya ajabuajabu usiku kama vile vitu viovu kote kumetoweka. Ninamshukuru Bwana Yesu Kristo kuniponya na kunipa uzima mpya.

B. R.

* * *

Sasa Anaweza Kusoma

Alhamisi iliyopita usiku nilikuja kwenye mkutano uliofanyika kwenye Uwanja wa Mbio za Farasi huko Durban. Nilihitaji uponyaji kwa ajili ya macho yangu. Baada ya mkutano mzuri sana Ndugu Branham alipotuombea sisi wote, sikusikia kuponywa hata kidogo, bali nilishawishika inanipasa kupiga hatua ya imani na kumtumainia Bwana kuniponya.

Ijumaa usiku nilienda kwenye mkutano uliokuwa kwenye Ukumbi wa Jiji bali nikaja nyumbani nimehuzunika sana. Jumapili nilinunua picha ya ukumbusho ya Ndugu Branham na wakati nikingojea mkutano uanze, nilifungua ndani kuangalia yale maelezo yalikuwa ndani ya hiyo karatasi. Ningali sikuwa nimevaa miwani. Kwa mshangao wangu na furaha kuu, niliona niliweza kusoma maandishi hayo vizuri sana. Niliendelea kusoma na kusoma, na wakati nilipofikia ile nakala ya barua iliyoandikwa ikithibitisha uhalisi wa ile negativu, niljikuta hata nikiweza kusoma hizo herufi ndogo sana. Kwa furaha tupu sikutaka kuacha kusoma.

J. M.

* * *

Tumbo Lenye Kiwewe kwa Muda wa Miaka Ishirini na Moja

Nimekuwa mgonjwa kwa muda wa miaka ishirini na moja na hivi majuzi neva zangu zilipoteza nguvu. Tumbo langu lilikuwa dhaifu sana na likafanya vurugu hata nisingeweza kula. Mnamo tarehe 24 Novemba, katika Ukumbi wa Jiji la Durban Ndugu Branham aliniombea na mara nikaanza kupata nafuu. Nilienda nyumbani na nikakuta kwamba niliweza kula chochote bila ya kitu hicho kutoka nje. Sasa mimi ni mzima kabisa.

S. R.

* * *

Moyo Mgonjwa kwa Muda wa Miaka 27

Nilipokea uponyaji wangu huko Durban, tarehe 23 Nov., 1951. Kwa muda wa miaka ishirini na saba nilikuwa na moyo mgonjwa sana. Ulikuwa ukizidi kuwa dhaifu zaidi wakati wote na hatimaye daktari wangu akasema kwamba hakuna kitu cha zaidi ambacho angaliweza kunifanyia. Nisingeweza kuinama. Nilikuwa naumwa sana hivi kwamba nilipokuwa nimeketi na kumsikiliza William Branham akihudumu nilitaka kufa.

Ndugu Branham aliwachagua wengine kutoka kwenye viti vyao na kuzungumza nao. Hatimaye akanigeukia, yule mama aliyevaa gauni lenye rangi nyeusi na nyeupe, na akasema ya kwamba yule malaika alikuwa yuko juu yangu. "Umeugua kwa sababu ya ugonjwa wa moyo bali sasa umepona," Ndugu Branham akasema. Niliweza kusikia badiliko likija juu yangu. Nilisimama kwa miguu yangu na kumsifu Bwana. Ninashukuru kwa ajili ya uponyaji ambao Bwana amenipa.

H. B.

Insulini Haihitajiki Tena

Ninataka kumsifu Bwana kwamba nilipokea uponyaji wangu wakati wa mkutano uliofanyika Durban. Kwa muda wa miaka mitatu iliyopita nimekuwa nikisumbuliwa na ugonjwa wa kisukari na nimekuwa nikinywa vipimo arobaini na tano kwa siku. Nilikubali uponyaji wangu kwa imani, wakati Ndugu Branham aliponielekezea kidole na kusema, "Dada, je! unaamini ya kwamba mimi ni nabii wa Mungu? Nenda zako nyumbani na ukaponywe." Tangu wakati huo sijahitaji kunywa insulini na nimemwona daktari wangu kwa ushauri na yeye, pia, hakuweza kuona dalili yo yote ya sukari. Ninamshukuru Mungu kwa yale aliyonifanyia.

L. L.

* * *

Daktari Anaripoti Moyo ni Mzima

Nina furaha kuwajulisha ya kwamba nimepona kabisa kutokana na ugonjwa mbaya sana wa moyo niliokuwa nao. Mwezi mmoja baada ya wewe kuniombea nilikwenda kwa daktari wangu. Alishangazwa na kukaa kwangu kwa muda mrefu bila matibabu ya dawa. Katika kujibu nilimwambia ya kwamba kwa rehema za mwenyezi Mungu ninajisikia vizuri zaidi.

Baada ya kunifanyia uchunguzi, daktari huyo aliniambia ya kwamba sikuwa tu na nafuu, bali niko mzima kabisa. Haleluya!

R. S.

* * *

Sikio Ziwi Linasikia

Ninataka kushuhudia ya kwamba sikio langu la kushoto lilikuwa ziwi kwa muda wa miaka sita mpaka nilipoponywa huko Pretoria. Wakati Ndugu Bosworth aliposema ya kwamba watu wenye sikio moja lililo ziwi kabisa na moja ambalo ni zima waje mbele, nilikuwa mtu wa tatu kusimama. Baada ya maombi Ndugu Bosworth alizungumza kwenye sikio langu la kushoto na akahesabu kuanzia moja hadi kumi. Aliniuliza kama niliweza kusikia ama singeweza kusikia. Nikasema, "Naam." Ndipo akahesabu mpaka tano na akaniambia kurudia namba hizo. Nikafanya hivyo. Wakati huu wote ilinibidi kufunga sikio lililokuwa zima vizuri kabisa nilivyoweza. Nilikuwa na furaha sana. Nilipofika nyumbani nilienda kwenye simu na kumpigia shemeji yangu na dada yangu kuwaambia ya kwamba sasa ningeweza kusikia. Nilisikiliza na sikio lililokuwa ziwi.

M. J. S. de B.

Maumvivu kwenye Ubavu wa Kulia

Ilikuwa ni baraka kwa nafsi yangu kuweza kuhudhuria uamsho wa uponyaji Pretoria huko Lady Selbourne tarehe 2 Des., 1951.

Niliumwa kutokana na maumivu upande wangu wa kulia wa ubavu tangu Desemba, 1947. Nimewaendea madaktari, bali nilipata vitulizo vya muda mfupi. Mwaka uliopita mwezi wa Mei nilichukuliwa Eksirei, bali hakukuwa na ubainishaji wa kuridhisha.

Tarehe 2 Desemba, 1951, alasiri wakati ulipowaombea wagonjwa, nilisikia maumivu makali sana ubavuni mwangu. Niliweka mkono wangu penye maumivu ulipoomba. Mungu na ashukuriwe tangu wakati huo sikusikia maumivu hayo ubavuni mwangu tena. Mungu asifiwe. Nimeweza kufanya shughuli zangu za kila siku kwa urahisi. Kwa kweli, Yesu ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Haleluya.

Nilimchukua binti yangu, mwenye umri wa miaka 12, pamoja nami. Alikuwa ana shida ya mishtuko baada ya mazoezi magumu, lakini Mungu na ashukuriwe, tangu kurudi kwetu yeye hufanya mazoezi kwa urahisi na hulala usingizi mzito. Jinsi tunavyotamani kwamba ungekuja tena hivi karibuni.

W. G.

* * *

Kuvuja Kwa Moyo, Pua Hutoka Damu na Maumivu Mgongoni

Nilikuwa na ugonjwa wa moyo kuvuja, pua kutoka damu ambayo mara nyingi yalikuwa ni vigumu sana kuyakomesha na maumivu makali mgongoni mwangu. Ninaamini ya kwamba niliponywa wakati Ndugu Branham alipowaombea watu wote wakati wa kufungwa kwa ibada Jumamosi jioni. Jumapili jioni Ndugu Branham alizungumza nami na akaniambia ya kwamba nilikuwa na moyo uliokuwa ukivuja na nilikuwa na ugonjwa mbaya wa pua kutoka damu. Aliniambia ya kwamba nilikuwa mfuasi wa kanisa la Presbiteri. Yote aliyoniambia yalikuwa ni kweli. Tangu mikutano hiyo kamwe pua yangu haijatoka damu wala sijapata kamwe maumivu yo yote mgongoni mwangu. Mungu asifiwe. Jambo hili limekuwa na matokeo makubwa juu ya mama yangu, pia.

M. C.

Macho Mabovu Yanakuwa Mazima

Kwa zaidi ya miaka mitatu iliyopita binti yangu wa pekee alikufa kwenye siku yake ya arusi. Mungu ashukuriwe, alikuwa ameokoka. Mshtuko huo uliathiri macho yangu sana hata nisingeweza kusoma hata neno moja, hata kwenye mwangaza wa jua, wala nisingeweza kuandika barua.

Jioni hiyo ya Jumapili ya kutosahaulika kamwe huko Johannesburg wakati nilipoona wagonjwa wakiponywa wakiwa kwenye viti vyao, niliamua ya kwamba hii ilikuwa ndiyo nafasi yangu. Nikasema, "Bwana, sasa wakati ndio huu. Ninachukua uponyaji kwa Neno Lako." Nilienda kulala usiku huo nikiamini ya kwamba jambo fulani lingetukia.

Nilipokuwa nimelala nilisikia kitu kama mshtuko ukipita kwenye macho yangu ndipo nikaamka na makelele ya sifa na ushindi. Kesho yake asubuhi niliweza kusoma bila ya miwani. Sijaivaa tena na ninasoma kila kitu mwenyewe, kuandika na kushona na macho yangu yanaendelea kuwa na nguvu zaidi. Ninampa Mungu utukufu wote.

J. H. G.

* * *

Hakuna Jambo Lililo Gumu Sana kwa Mungu

Ni majuma mawili tu yaliyopita ambapo kikosi cha Branham kiliondoka nchini mwetu bali baraka zinazotokana na mikutano hiyo zinalundikana kila siku, wala hatuwezi kumshukuru Bwana wetu Yesu vya kutosha kutuma kikosi cha Branham huku Afrika Kusini. Tunatazamia ziara ya kurudi ya kikosi hicho.

Shirikisho la Afrika Kusini kamwe halijawahi kutikiswa kwa kiwango hicho na dini. Kuna uamsho mpya wa ukweli wa dini ya Mungu.

Katika familia yetu tungali kila siku tunamtolea Mungu shukrani kwa kuwa alimtuma Ndugu Branham A.K. kwa maana kama asingalimtuma, nina hakika baba yangu asingekuwa anaishi leo. Mnamo tarehe 24 Agosti, 1951, baba yangu kwa ghafla alishikwa na ugonjwa na akazirai katika hali ya kukosa fahamu mpaka Jumapili. Katika siku hizi tatu madaktari wawili wa mahali hapo walishindwa kubaini ugonjwa wa ghafla wa baba yangu. Daktari bingwa aliitwa naye akasema ya kwamba mirija ya nyongo ilikuwa imepasuka na upasuaji wa dharura ulihitajika usiku uo huo. Uhai wake ulikuwa mashakani sana siku nne zilizofuata kwa kuwa mwili wake mzima ulikuwa ni mdhaifu sana.

Hali ya hatari hatimaye ilipita na katika juma la pili la Septemba baba yangu aliruhusiwa kuja nyumbani. Kwa juma moja aliendelea vizuri sana. Tulikuwa na furaha sana,

na ndipo maafa yakapiga. Kwa ghafla sana aliugua tena. Alikimbizwa hospitalini na kwa sababu ya hali mbaya aliyokuwa nayo madaktari waliamua wasimfanyie upasuaji mpaka Jumanne.

Mara nyingine tena uhai wake ulikuwa katika hatari kubwa. Katika juma moja alifanyiwa upasuaji mara mbili na daktari akamwambia mama yangu ya kwamba angeishi tu siku chache. Hata hivyo hatukukata tamaa. Tuliendelea kuomba. Hali ilikuwa ni ya huzuni na ilionekana hakuna matumaini. Tulimwomba Mungu kwa bidii ya kwamba angempa Kasisi Branham ono ili kwamba angeweza kumwombea baba yangu naye angeponywa.

Jumatatu jioni, tarehe 8 Oktoba, daktari alisema ya kwamba mwisho ulikuwa umewadia. Hata hivyo tulimpeleka kwenye Bustani ya Maranatha. Jioni iliyofuata tulimpeleka tena. Wakati watu wa gari la wagonjwa walipompeleka kwenye hiyo Maskani alikuwa akiumwa sana na uvimbe wa ngozi ya tumbo. Alibebwa akaingizwa akiwa ni mtu anayekufa.

Wakati wote katika mkutano huo watoto wa Mungu walikuwa wakimwombea, kwa kuwa alikuwa ni mchungaji aliyejulikana sana. Tulijisikia ya kwamba angepokea uponyaji wake usiku huo. "Amini tu, yote yawezekana, amini tu."

Wakati wa ibada Ndugu Branham aliwageukia wasikilizaji, macho yake yakimwangukia baba yangu. Akasema, "Umefanyiwa upasuaji mmoja, upasuaji mara mbili, la, upasuaji mara tatu." Haleluya. Tulikuwa tumeomba kwamba Ndugu Branham azungumze na baba yangu na Mungu alikuwa amejibu maombi yetu. Ndugu Branham alimwombea baba yangu na akamwambia asimame. Alisimama, mara ya kwanza katika majuma matano. Huku machozi yakitiririka usoni mwake alikuwa akimsifu Mungu. Usiku huo Mungu alidhihirisha nguvu Zake katika ishara za ajabu sana na wengi walipokea uponyaji wao.

Baada ya ibada baba yangu alitembea akarudi kwenye gari la wagonjwa bila kusaidiwa. Mungu asifiwe. Kesho yake alijisikia vizuri zaidi wala hakupigwa sindano ya kuzuia maumivu. Jana yake alikuwa amepigwa sindano ishirini za kutuliza maumivu. Jumamosi iliyofuata alikuja nyumbani kutoka hospitali na amekuwa akiendelea vizuri kila siku.

V. R.

"Ni neno jema kumshukuru Bwana, . . ."

Zaburi 92:1

Naam, msomaji mpendwa, ni neno jema kumshukuru Bwana. Bwana anapenda kusifiwa. Shuhuda hizi ambazo umesoma, zinawakilisha sehemu ndogo tu ya maelfu ya walioponywa kwenye uamsho wa Afrika Kusini. Kama vile ambavyo umesoma yale Kristo alivyowafanyia wengine, naomba wewe pia, umwamini Mungu kwa ajili ya shida yako binafsi. Pia kumbuka, una haki kama mwana wa Mungu, kudai uponyaji ambao ni wako kwa uwezo wa Upatanisho. Sisi daima tuna furaha kupokea shuhuda zenu na labda zitawachochea wengine kumwamini Mungu pia.

Katika Matendo 19:11-12 tunasoma: "Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida; hata wagonjwa wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake, magonjwa yao yakawaondokea, pepo wachafu wakawatoka."

Kuna zaidi ya jumbe 1179 asili za Kiingereza za Ndugu William Marrion Branham zilizorekodiwa na zinapatikana katika vielelezo vya kusikia. Nyingi za jumbe hizi zinapatikana katika vitabu. Kuna maofisi na maktaba za kuazimisha katika mataifa kote ulimwenguni ambamo jumbe hizi zinapatikana kwa urahisi katika lugha nyingi.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Kwa maelezo zaidi ama kupata jumbe za
Ndugu Branham waombwa kuwasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org